

# 2012/2013

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI



**RIPOTI KUU YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA  
HESABU ZA SERIKALI KUHUSU TAARIFA YA FEDHA ZA SERIKALI  
KUU KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2013**

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,  
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi  
Mtaa wa Samora /Ohio,  
S. L .P 9080,  
Simu: +255 (022) 2115157/8,  
Nukushi: +255 (022) 2117527,  
Barua pepe: [ocag@nao.go.tz](mailto:ocag@nao.go.tz),  
Tovuti: [www.nao.go.tz](http://www.nao.go.tz),  
Dar es Salaam.

*Ripoti hii imejumuisha; Wizara, Idara na Wakala 60, Sekretarieti za  
Mikoa 25 na Balozi 32*



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI



---

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Barabara ya Samora, S.L. P 9080,  
DAR ES SALAAM. Simu ya upepo: "Ukaguzi" Dar es Salaam, Simu: 255(022)2115157/8,  
Nukushi: 255(022)2117527, Barua pepe: [ocag@nao.go.tz](mailto:ocag@nao.go.tz), Tovuti: [www.nao.go.tz](http://www.nao.go.tz)

---

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na.FA.27/249/01/2012/2013

Tarehe: 28 Machi, 2014

Mh. Dkt. Jakaya M. Kikwete,  
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,  
S.L.P. 9120,  
Ikulu,  
Dar es Salaam.

**Yah: Kuwasilisha Ripoti Kuu ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa mwaka ulioishiatarehe 30 Juni, 2013**

Kwa mujibu wa Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (iliyorekebishwa 2005) na Kifungu cha 34 (1)(c) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008.

Ninayo heshima kubwa kuwasilisha ripoti kuu ya ukaguzi ya mwaka inayohusu taarifa za fedha za serikali kuu za mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2013 kwa taarifa na hatua zako muhimu.

Katika ripoti hiyo, nimetoa mapendekezo yenye lengo la kujenga ambayo kama yatatekelezwa yanaweza kupunguza matukio ya ukiukwaji wa taratibu na kwa kiasi kikubwa kuboresha uwajibikaji wa watendaji wa Serikali katika masuala ya fedha.

Nawasilisha.

Ludovick S. L. Utouh  
**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

## YALIYOMO

<b>ORODHA YA MAJEDWALI .....</b>	<b>vii</b>
Mdhibiti Na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,.....	x
Dira, Dhimana vigezo vya msingi.....	x
<b>DIBAJI .....</b>	<b>xii</b>
<b>SHUKRANI.....</b>	<b>xvii</b>
<b>VIFUPISHO .....</b>	<b>xix</b>
<b>MUHTASARI WA MAMBO MUHIMU KATIKA RIPOTI YA UKAGUZI WA TAARIFA ZA FEDHA ZA SERIKALI KUU KWA MWAKA 2012/2013.....</b>	<b>xxi</b>
<b>SURA YA KWANZA .....</b>	<b>1</b>
1.0 UTANGULIZI WA MAMBO YA JUMLA .....	1
1.1 Mamlaka na umuhimu wa kufanya ukaguzi .....	1
1.2 Viwango na taratibu zinazotumika kutoa taarifa .....	4
1.3 Idadi ya wakaguliwa na mpangilio wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa hesabu za Serikali.....	5
1.4 Wajibu wa Kisheria wa Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa .....	7
<b>SURA YA PILI.....</b>	<b>9</b>
<b>MAANA YA HATI ZA UKAGUZI, AINA ZAKE, MASUALA YANAYOPELEKEA KUTOLEWA HATI HIZO NA MATOKEOHALISI YA UKAGUZI.....</b>	<b>9</b>
2.0 KUHUSU HATI ZA UKAGUZI .....	9
2.1 Aina za hati za ukaguzi .....	10
2.2 Vigezo vya hati za ukaguzi pamoja na matokeo halisi ya ukaguzi uliofanyika.....	10
2.3 Mwelekeo wa Hati za Ukaguzi .....	20
2.4 Taasisi zilizokaguliwa na kupata; hati yenye shaka na hati isiyoridhisha na sababu za kupewa hati.....	24
<b>SURA YA TATU .....</b>	<b>53</b>
<b>UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJIWA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI KWA MIAKA ILIYOPITA.....</b>	<b>53</b>
3.0 Utangulizi.....	53
3.1 Majibu ya taarifa za kila fungu kutoka kwa Afisa .....	53
Masuuli. ....	53
3.2 Majibu kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) . ....	56
3.3 Ufuatiliaji wa mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Hesabu za Serikali Kuu (PAC) .....	66
<b>SURA YA NNE .....</b>	<b>79</b>
<b>MAKUSANYO YA MADUHILI NA MCHANGANUO WA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO.....</b>	<b>79</b>

4.1	Mapitio ya Ufanisi wa Mapato .....	79
4.2	HESABU ZA TAIFA .....	91
4.3	USIMAMIZI WA MATUMIZI .....	118
<b>SURA YA TANO .....</b>		<b>131</b>
<b>TATHMINI YA UDHIBITI WA NDANI NA UTAWALA BORA .....</b>		<b>131</b>
5.0	Utangulizi.....	131
5.1	Mapungufu ya Kiutendaji katika Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani .....	131
5.2	Mapungufu katika Kamati za Ukaguzi.....	132
5.3	Mapungufu katika Udhibiti wa Vihatarishi .....	133
5.4	Mapungufu katika Mazingira ya Usimamizi wa Teknolojia ya Habari .....	134
5.5	Mapungufu katika kuzuia udanganyifu .....	135
5.6	Mapungufu katika matumizi ya mfumo wa kahasibu (IFMS/Epikor).....	136
<b>SURA YA SITA.....</b>		<b>138</b>
<b>USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU NA MISHAHARA .....</b>		<b>138</b>
6.0	UTANGULIZI .....	138
6.1	Masuala muhimu yaliyojitokeza katika ukaguzi wa rasilimali watu katika Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa .	139
6.2	Kukosekana au kuwepo kwa mfumo duni wa kupima utendaji wa watumishi wa umma .....	142
6.3	Madai ya watumishi .....	143
6.4	Uhaba wa rasilimali watu .....	144
6.5	Mikopo kwa watumishi isiyodhibitiwa .....	144
6.6	Matatizo yanayohusiana na matumizi ya mfumo wa taarifa za watumishi wa umma .....	145
6.7	Kuchelewa kurejesha mishahara isiyolipwa Hazina na makato ya mishahara kwa taasisi za fedha .....	146
6.8	Kukosekana Afisa utalii katika ubalozi wa Tanzania- Berlin.	148
<b>SURA YA SABA.....</b>		<b>149</b>
<b>MAPITIO YA TARATIBU ZA MANUNUZI .....</b>		<b>149</b>
7.0	UTANGULIZI .....	149
7.1	Mapungufu yaliobainika katika ukaguzi wa Manunuzi .....	149
7.2	Manunuzi yaliyofanyika bila ushindani.....	150
7.3	Mali zilizonunuliwa na kuachwa bila ya kutumika .....	151
7.4	Malipo yaliyozidi Kiwango cha Mkataba/ bei .....	152
7.5	Manunuzi kinyume na Mpango wa Manunuzi wa Mwaka.....	153
7.6	Manunuzi yaliyofanyika bila idhini ya Bodi ya Zabuni .....	154
7.7	Manunuzi kwa kutumia Masurufu.....	155
7.8	Vifaa vilivyoununuliwa havikuingizwa vitabuni .....	157
7.9	Mapungufu yaliyobainishwa na PPRA .....	158

7.10	Ufuatiliaji wa Sheria ya Manunuzi ya umma ya mwaka, 2004na Kanuni zake za mwaka, 2005. ....	158
7.11	Usimamizi Dhaifu wa Mikataba .....	159
7.12	Utunzaji wa kumbukumbu za Manunuzi. ....	159
7.13	Tathimini ya Mfumo wa Utunzaji wa taarifa za Manunuzi (PIMS).....	159
7.14	Mapendekezo yaliyotolewa na PPRA.....	160
7.15	Mapungufu katika manunuzi na utunzaji wa bohari/stoo katika taarifa ya Kurugenzi ya Uhakiki mali zaSerikali. ....	161
<b>SURA YA NANE .....</b>		<b>164</b>
<b>USIMAMIZI MALI NA MADENI .....</b>		<b>164</b>
8.0	<b>UTANGULIZI .....</b>	<b>164</b>
8.1	Mapungufu katika utunzaji wa taarifa sahihi za mali katika rejista ya mali za kudumu.....	164
8.2	Mali ambazo zimeegeshwa bila matengenezo.....	167
8.3	Kutothaminishwa kwa baadhi ya Majengo, Mitambo na Vifaa..	167
8.4	Ukosefu wa nyaraka za umiliki wa Majengo, Mitambo na Vifaa (PPE) .....	168
8.5	Utambuzi usiofaa wa mali zisizoshikika .....	169
8.6	Ukosefu wa vifaa vya ufuatiliaji (CCTV kamera) katika vituo vya mizani .....	170
8.7	Uhamisho wa fedha za maendeleo kwenda katika taasisi zilizo chini ya wizara kuonyeshwa kama mali za wizara katika taarifa za fedha za wizara .....	171
8.8	Mapungufu katika usimamizi wa meno ya tembo na nyara .... nyingine za taifa.....	172
8.9	Masurufu hayakuonyeshwa katika taarifa ya fedha kama ni wadaiwa .....	174
8.10	Madeni ambayo hayajalipwa .....	175
<b>SURA YA TISA.....</b>		<b>177</b>
9.0	<b>UKAGUZI MAALUM .....</b>	<b>177</b>
9.1	Utangulizi.....	177
9.2	Ukaguzi maalum uliofanywa kwenye hospitali teule za rufaa za Wilaya na hospitali binafsi kwa mwaka wa fedha2010/2011 na 2011/2012 .....	177
9.3	Ukaguzi maalum wa Wizara ya Ujenzi kuhusu ununuzi wa kivuko cha Misungwi .....	179
9.4	Ukaguzi maalum wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kuhusu Mfumo wa Pembejeo za kilimo wa Taifa .....	181
9.5	Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuhusu matumizi mabaya ya fedha za ada katika Chuo cha Uuguzi Mkomaindo .	184
<b>SURA YA KUMI .....</b>		<b>185</b>

MASUALA MENGINE .....	185
10.0 UTANGULIZI .....	185
10.1 Tathmini ya Wakala wa Serikali .....	185
10.2 Ulipaji wa kodi ya kupanga ofisi .....	190
10.3 Changamoto zilizopo huduma ya magereza Tanzania.....	192
10.4 Jukumu la Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali katika kukagua miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP).....	197
10.5 Masuala yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi wa hesabu za Vyama vya Siasa .....	204
<b>SURA YA KUMI NA MOJA.....</b>	<b>207</b>
11.0 MAJUMUISHONAMAPENDEKEZO .....	207
11.1 Kutotekelezwa kwa baadhi ya mapendekezo yangu ya mwaka uliopita .....	207
11.2 Usimamizi wa Manunuzi .....	208
11.3 Kutofanyiwa kazi kwa changamoto ya upungufu wa nguvukazi katika Wizara na Sekretarieti za Mikoa.....	210
11.4 Malipo ya mishahara kwa watumishi hewa .....	210
11.5 Usimamizi wa Matumizi.....	211
11.6 Utendaji katika Balози zetu. ....	213
11.7 Uendeshaji wa Hospitali Teule .....	214
11.8 Vocha za Pembejeo za Kilimo (NAIVS).....	215
11.9 Utayari na utekelezaji wa IPSAS .....	216
11.10 Ufuatiliaji na tathmini ya miradi inayotekelezwa kwa fedha za mikopo .....	219
11.11 Kukosekana kwa Ofisi ya Usimamizi wa Madeni.....	220
11.12 Kubadilisha Hati za Ukwasi kugharamia nakisi ya bajeti ....	220
11.12 Kutolewa migao ya fedha mwishoni mwa mwaka wa fedha	221
11.13 Usimamizi wa Forodha na maghala ya mali (customs bonded warehouses) ambazo hazijalipiwa kodi.....	221
<b>12. VIAMBATISHO .....</b>	<b>223</b>

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 1:	Idadi ya Wakaguliwa.....	5
Jedwali 2:	Idadi ya wakaguliwa waliopata hati inayoridhisha ...	11
Jedwali 3:	Orodha ya taasisi zilizopata hati safi yenye masuala mengine .....	14
Jedwali 4:	Taasisi ilizopata hati mbaya na sababu zilizopelekea hati hiyo.....	17
Jedwali 5:	Mwelekeo wa Hati za Ukaguzi .....	21
Jedwali 6:	Wizara, Idara na Wakala zilizopata hati yenye mashaka na sababu zilizopelekea .....	26
Jedwali 7:	Orodha ya taasisi ambazo zimepata hati isiyoridhisha pamoja na sababu zilizopelekea hati hiyo .....	52
Jedwali 8:	Ufuatiliaji wa Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali ...	57
Jedwali 9:	Mapendekezo ya kamati ya hesabu za Serikali kuu ..	66
Jedwali 10:	Makadirio na mapato halisi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2012/2013 na 2011/2012.....	80
Jedwali 11:	Uwiano wa bajeti ya matumizi wa kawaida, fedha zilizotolewa na matumizi halisi.....	82
Jedwali 12:	Uwiano wa bajeti ya matumizi ya maendeleo, fedha zilizotolewa na matumizi halisi.....	84
Jedwali 13:	Ulinganisho wa fedha zilizotolewa kwa matumizi ya kawaida na matumizi halisi .....	85
Jedwali 14:	Ulinganisho wa fedha zilizotolewa kwa matumizi ya maendeleo na matumizi halisi .....	86
Jedwali 15:	Muhtasari wa mapato yasiyotokana na kodi .....	87
Jedwali 16:	Uwiano wa madaai na bajeti kutoka mwaka 2010/11 hadi 2012/13 unaoneshwa kwenye .....	90
Jedwali 17:	Masuala ya Mamlaka ya Mapato yaliyosalia .....	102
Jedwali 18:	Mapato yaliyokusanywa - Tanzania Bara .....	103
Jedwali 19:	Mapato yaliyokusanywa - Zanzibar .....	104
Jedwali 20:	Makusanyo ya mapato Tanzania bara .....	104
Jedwali 21:	Mwelekeo wa Makusanyo ya Mapato - Zanzibar .....	105
Jedwali 22:	Muhtasari wa misamaha ya kodi kwa Taasisi mbalimbali.....	106
Jedwali 23:	Mwelekeo wa Misamaha ya Kodi kwa miaka, 2011/12-2012/2013.....	107
Jedwali 24:	Uwiano wa mapato baada ya misamaha ya kodi	

dhidi ya pato la taifa .....	108
Jedwali 25: Taarifa ya Matumizi ya Serikali .....	112
Jedwali 26: Fedha iliyotolewa kwa kila robo ya mwaka .....	113
Jedwali 27: Masurufu yaliyokaa muda mrefu bila kurejeshwa ...	118
Jedwali 28: Masurufu yasiyorejeshwa kwa ufupi.....	119
Jedwali 29: Mwenendo wa malipo katika vifungu visivyostahili .	120
Jedwali 30: Malipo yaliyozidi kiwango stahiki .....	120
Jedwali 31: Malipo ya zaidi ya kiwango stahiki .....	121
Jedwali 32: Matumizi nje ya bajeti iliyoidhinishwa .....	121
Jedwali 33: Mtiririko wa malipo yenye nyaraka pungufu kwa miaka mitatu .....	122
Jedwali 34: Malipo yasiyo na stakabadhi za kawaida na kielectroniki (EFR) .....	124
Jedwali 35: Kukosekana kwa mchanaganuo wa matumizi .....	125
Jedwali 36: Orodha ya Wizara na idara ambazo hati za .....	127
Jedwali 37: Mwenendo wa miaka mitatu (3) wa matumizi yasiyo na hati za malipo .....	127
Jedwali 38: Orodha ya malipo ya madeni ya miaka ya nyuma ...	128
Jedwali 39: Orodha ya Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa yenye Mishahara isiyolipwa na kurejeshwa hazina .....	139
Jedwali 40: Malipo kwa watumishi ambao hawapo kwenye utumishi wa Umma .....	140
Jedwali 41: Makato yasiyoruhusiwa kisheria kutoka kwa waliokuwa watumishi wa Serikali .....	141
Jedwali 42: Kukosekana au kuwepo kwa mfumo duni wa kupima utendaji wa watumishi wa umma.....	142
Jedwali 43: Madai ya watumishi .....	143
Jedwali 44: Makato yaliyofanyika kwa watumishi zaidi ya theluthi mbili (2/3) pato la mshahara.....	145
Jedwali 45: Adhabu kwa kuchelewa kupeleka makato ya watumishi .....	147
Jedwali 46: Manunuzi yasiyo kuwa na ushindani.....	150
Jedwali 47: Mali ambazo hazijatumika.....	152
Jedwali 48: Malipo yaliyozidi bei tajwa kwenye Ankara .....	153
Jedwali 49: Orodha ya Wizara, Idara na sekretarieti za mikoa zilizo fanya Manunuzi nje ya mpango wa manunuzi wa mwaka.....	154

Jedwali 50: Manunuzi yaliyofanyika bila idhini ya Bodi ya Zabuni .	155
Jedwali 51: Manunuzi kwa kutumia Masurufu .....	156
Jedwali 52: Vifaa havikuizingizwa vitabuni.....	157
Jedwali 53: Taarifa ya Mhakiki Mali .....	161
Jedwali 54: Wizara, Wakala, idara na Sekretarieti za Mikoa zilizobainika kuwa na mapungufu katika utunzaji wa rejista ya mali za kudumu .....	166
Jedwali 55: Orodha ya Wizara, Wakala, Idara na Sekretarieti za Mikoa ambazo hazina nyaraka za umiliki .....	168
Jedwali 56: Hamisho la fedha za maendeleo kwenda katika taasisi zilizo chini ya wizara.....	171
Jedwali 57: Masurufu yasioonyeshwa katika taarifa wadaiwa ...	174
Jedwali 58: Upungufu wa fedha .....	187
Jedwali 59: Upungufu katika makusanyo .....	188
Jedwali 60: Ulipaji wa kodi ya pango katika Wizara na Idara za Serikali .....	190
Jedwali 61: Bajeti finyu .....	193
Jedwali 62: Upungufu wa fedha zilizotolewa .....	194
Jedwali 63: Ongezeko la madeni kutoka kwa wauzaji na madai ya wafanyakazi.....	195

**Mdhibiti Na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,  
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,  
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

***Ilianzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano***

Madaraka na wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yameelezwa kwenye Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (iliyorekebishwa 2005) na kufafanuliwa zaidi katika Kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008.

**Dira**

Kuwa kituo cha ufanisi katika Ukaguzi wa Hesabu za Serikali na Taasisi za Umma.

**Dhima**

Kutoa huduma ya ukaguzi wa hesabu yenye tija ili kuimarisha uwajibikaji nathamani ya fedha katika kukusanya na kutumia rasilimali za umma.

**Katika kutoa huduma zenye ubora, ofisi hii inaongozwa na vigezo vya msingi vifuatavyo:**

- ✓ **Uadilifu:** sisi ni asasi adilifu inayotoa huduma kwa namna isiyo na upendeleo.
- ✓ **Ubora:** sisi ni wanataaluma wanaotoa huduma zenye ubora kwa kuzingatia viwango kubalifu vya Ukaguzi
- ✓ **Uaminifu:** tunahakikisha kuwa na kiwango cha juu cha uaminifu na kuzingatia utawala wa sheria.
- ✓ **Mtazamo wa watu:** tunatazama na kukazia zaidi katika matarajio ya wadau wetu kwa kujenga utamaduni mzuri wa kuhudumia mteja na kuwa nawatumishi wataalamu na wenye motisha ya kazi.
- ✓ **Uvumbuzi:** sisi ni asasi ambayo wakati wote inahamasisha utamaduni wakupokea na kuendeleza mawazo mapya kutoka ndani na nje ya asasi.
- ✓ **Matumizi bora ya rasilimali:** sisi ni asasi inayothamini na kutumia rasilimali za umma ilizokabidhiwa kwa umakini mkubwa.

**Tunaifikia adhama yetu kwa kufanya yafuatayo:**

- Kuchangia usimamizi bora wa fedha za umma kwa kuhakikisha kwamba wateja wetu wanawajibika kwa rasilimali walizokabidhiwa;
- Kusaidia kuboresha ubora wa huduma za jamii na kusaidia ubunifu katika kufanya matumizi bora ya rasilimali za umma;
- Kutoa ushauri wa kiufundi kwa wateja wetu juu ya mapungufu yaliyoko katika mifumo ya uendeshaji wa shughuli zao
- Kufanya ukaguzi shirikishi baina yetu na wateja wetu katika mchakato mzima wa ukaguzi; na
- Kuwapatia mafunzo sahihi wakaguzi wetu, vitendea kazi vya kutosha na motisha ili kuhakikisha uhuru wakati wakitekeleza majukumu yao.

© Taarifa hii ni nia ya kutumiwa na Mamlaka za Serikali. Hata hivyo, baada ya Spika kuipokea ripoti hii na mara baada ya kuiwasilisha Bungeni, ripoti hii itakuwa ni mali ya umma na usambazaji wake hautadhibitiwa.

## DIBAJI



*Bw. Ludovick S.L. Utouh (CAG)*

Huu ni mwaka wa kwanza Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa kuandaa taarifa za fedha kwa kutumia Viwango vya kimataifa vya kahasibu katika sekta vya umma kwa msingi wa fedha usio taslimu. Naipongeza Serikali kupitia Mhasibu Mkuu kwa jitihada za makusudi kuanza kutumia Viwango vya kimataifa vya kahasibu katika sekta ya umma vya msingi wa fedha usiyo taslimu<sup>1</sup>.

Mbali na changamoto zilizopo, sina shaka ninapolinganisha namsingi wa fedha taslimu<sup>2</sup>; msingi wa fedha usio taslimu unatoa taarifa za kina za fedha ambazo ni muhimu katika kusaidia menejimenti na watumiaji wengine wa taarifa za fedha kufanya maamuzi huku wakiwa na taarifa za kina. Wakati ninaipongeza Serikali pia ninaishauri, kupitia kwa mhasibu mkuu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa mpango uliopo wa kuelekea kutekeleza msingi wa fedha usio taslimu kikamilfu.

Ripoti hii ya Ukaguzi inawasilishwa kwa Mheshimiwa Rais kwa mujibu wa Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kifungu 34(1)(c) cha Sheria Na.11 ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka, 2008.

---

<sup>1</sup>IPSAS- Accrual Basis

<sup>2</sup>IPSAS - Cash Basis

Kwa mujibu wa Ibara 143 (2) (c) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anatakiwa angalau mara moja kila mwaka kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa Hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano, hesabu zinazosimamiwa na watumishi wote wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, hesabu za Mahakama zote za Jamhuri ya Muungano na hesabu zinazosimamiwa na Katibu wa Bunge.

Chini ya Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anatakiwa kuwasilisha kwa Rais kila ripoti anayotoa chini ya Ibara 143(2)(c). Baada ya kupokea ripoti hizo, Rais ataagiza wanaohusika waziwasilishe ripoti hizo mbele ya Kikao cha kwanza cha Bunge ndani ya siku saba baada ya kuanza kwa kikao.

Uhuru wa kiutendaji wa ofisi yangu kwa kiasi kikubwa umeimarika baada ya kuanza kutumia sheria ya Ukaguzi wa Umma Na 11 ya mwaka 2008. Hata hivyo kulingana na viwango vya kimataifa maboresho zaidi yanahitajika hasa kwa upande wa kupanga mishahara na ajira za watumishi wa ofisi yangu ili kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya kikatiba kwa ufanisi zaidi.

Ni vyema kutambua kuwa wakati ofisi yangu inatoa taarifa kuhusu ukiukwaji wa sheria, taratibu na kanuni mbalimbali na udhaifu katika mifumo ya udhibiti wa ndani kwenye taasisi za Umma na hasa Serikali Kuu, lakini wajibu wa kuhakikisha kuwepo kwa mifumo thabiti ya udhibiti wa ndani ni jukumu la Maafisa Masuuli.

Bunge na watanzania kwa ujumla wanatarajia kupata uhakikisho kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikalikuhusiana na taarifa za fedha na usimamizi wa rasilimali katika Serikali Kuu pia ufanisi na ubora na usimamizi wa mipango iliyowekwa. Kwa njia ya ukaguzi, ofisi inachangia katika kutoa mapendekezo kuhusu uimarishaji na uboreshaji wa sekta ya Umma. Kwa msingi huu, Serikali Kuu na Ofisi yangu kila mmoja ana mchango katika kujenga imani kwa umma katika usimamizi wa rasilimali za umma.

Ingawa majukumu ya ofisi yangu na yale ya taasisi za umma yanatofautiana, hata hivyo matarajio ya usimamizi bora wa rasilimali yanafanana.

Ili kukidhi matarajio ya Wabunge na Umma wa watanzania kwa mapana zaidi, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imeendelea kufanya uchambuzi wa njia bora zaidi za kufanya ukaguzi na kuongeza wigo wa masuala yanayokaguliwa na hivyo kuimarisha utendaji wa uwajibikaji katika sekta ya Umma. Aidha, tunahakikisha ukaguzi wetu unalenga kuyapa kipaumbele maeneo muhimu ili kuchangia maendeleo katika sekta ya Umma. Kwa kuwa kazi ya ukaguzi ni chachu katika usimamizi wa fedha, tutaendelea kujadili masuala yanayoathiri utawala/uongozi katika sekta ya umma, hasa katika utoaji wa taarifa za usimamizi wa fedha na masuala ya utawala bora.

Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali Kuu (PAC), moja kati ya kamati za Kudumu za Bunge, inafanya kazi kwa karibu na kwa ushirikiano na Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa. Pamoja na jitihada hizo, naamini Serikali kuu inalo jukumu muhimu la kuhakikisha kwamba kamati inajengewa uwezo ili kuhakikisha kuwa Maafisa masuuli wanatekeleza maoni ya kamati. Kamati itumie nguvu ambayo inayo ili kuhakikisha maoni ya kamati yanatekelezwa.

Napenda kutambua mchango wa wafanyakazi wa Ofisi yangu kwa utaalamu, juhudi kubwa walioonesha katika kutimiza malengo tuliyojipangia licha ya kufanya kazi katika mazingira magumu ambayo ni pamoja na kukosa fedha za kutosha, kukosa vitendea kazi, mishahara duni na upungufu wa watumishi, na wakati mwingine kufanya kazi maeneo ya vijijini ambayo sio rahisi kufikika.

Napenda pia kutambua kazi iliyofanywa na Mamlaka ya Ununuzi wa umma na Kitengo cha Usimamizi wa Mali za Serikali kilicho chini ya Wizara ya Fedha kwa kuandaa na kuwasilisha taarifa ya uhakiki wa mali uliofanyika kwenye baadhi ya Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa kwa mwaka wa fedha 2012/13 na kuonyesha mambo mengi

ambayo kwa kiasi kikubwa yalijitokeza kwenye ripoti yangu ya mwaka. Napenda kutambua kazi iliyofanywa na ofisi hizi ambayo nimeona ni vyema nikaijumuisha kwenye ripoti yangu.

Natarajia kuwa Bunge litaona taarifa hii kuwa ni muhimu katika kuiwajibisha Serikali kwa jukumu lake la usimamizi wa fedha za Umma na utoaji wa huduma kwa Watanzania. Hivyo, nitafurahi kupata maoni kutoka kwa watumiaji wa ripoti hii jinsi gani nitaweza kuboresha taarifa yangu kwa siku zijazo.

Ludovick S. L. Utouh

---

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,  
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,  
S.L.P. 9080,  
Dar es Salaam.

**Machi, 2014**



## SHUKRANI

Napenda kutoa shukrani zangu za kipekee kwa kila mtumishi katika ofisi yangu kwa kufanya kazi kwa juhudi bila kuchoka kulikowezesha kukamilisha taarifa ya ukaguzi kwa wakati.

Pia, napenda kuwashukuru wajumbe wa kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuu, kwa maoni yao mazuri, maelekezo na mapendekezo wakati wa mijadala na Maafisa Masuuli. Bunge kupitia kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuu inajukumu la kutoa uhakika na uthibitisho wa namna fedha za umma zilivyotumika. Tunalipa umakini mkubwa jukumu la kamati katika kusimamia uwajibikaji katika kuwezesha uelewa wa pamoja wa mamlaka ya mdhibiti na mkaguzi mkuu wa hesabu za Serikalimiongoni mwa wadau wote wa ndani na nje ya nchi.

Natoa shukrani zangu za dhati kwa wafadhili hasa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Sweden, Serikali ya Sweden kupitia Shirika la Kimataifa la Misaada la Maendeleo la Sweden, Benki ya Dunia kupitia Mradi wa Kusimamia na Kuboresha Sekta ya Fedha za Umma (PFMRP), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Shirika la Misaada la Ujerumani (GIZ), Shirika la Misaada la Marekani (USAID), Serikali ya China na wale wote wanaotutakia mema ambao wamechangia kwa kiasi kikubwa katika kuboresha Ofisi yangu. Michango yao katika kukuza rasilimali watu, mifumo ya teknolojia ya habari na mali (vitendea kazi) imekuwa na manufaa makubwa katika kufanikisha shughuli zetu.

Nina kila sababu ya kuwashukuru wadau wetu wengine ikiwa ni pamoja na Waziri wa Fedha, Mlipaji Mkuu wa Serikali, Maafisa Masuuli wotewa Wizara, Balozi, Wakala, Idarana Sekretarieti za Mkoa; kitengo cha Mhakiki Mali Mkuu na Mamlaka ya Ununuzi wa Umma walio chini ya Wizara ya Fedhakwaushirikiano nautoaji wataarifa muhimuzilizohitajikakwa ajili ya maandaliziya ripoti hii. Pia napenda kumshukuru Mpiga chapa mkuu wa

Serikalikwa kuharakisha uchapaji wa ripoti hii na kuweza kuiwasilisha kwa wakati.

Kwakumalizia, napenda kuwashukuruwadau wetu woteikiwa ni pamoja nawatumishi wa umma, vyombo vya habari, wanaharakatinaumma kwa ujumla bilakuwasahau walipa kodiwa nchi hii ambao ripoti hiiimetolewa mahususi kwaajili yao. Mchango wao mkubwa katika ujenzi wa taifa hili unathaminiwa sana.

Mwenyezi Mungu awabarikiwote huku sisi tukiahidi kuendelea kuchangia katika kukuza uwajibikaji katika matumiziya rasilimali za ummakatikanchi hii.

## VIFUPISHO

<b>ISSAIs</b>	Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi wa Taasisi za Umma
<b>INTOSAI</b>	Shirika la kimataifa la Taasisi kuu za Ukaguzi
<b>AFROSAI</b>	Shirika la Taasisi Kuu za Ukaguzi Kanda ya Afrika
<b>AFROSAI-E</b>	Shirika la Taasisi Kuu za Ukaguzi kwa nchi zinazooonea kiingereza
<b>NAOT</b>	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi
<b>IPSAS</b>	Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa hesabu katika Sekta za Umma
<b>PAC</b>	Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali Kuu
<b>CAG</b>	Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali
<b>TRA</b>	Mamlaka ya Mapato Tanzania
<b>PPRA</b>	Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma
<b>AGR</b>	Ripoti Kuu Ya Mwaka Ya Mdhibiti Na Mkaguzi Mkuu Wa Hesabu Za Serikali
<b>CG</b>	Serikali Kuu
<b>MDAs</b>	Wizara, Idara na Wakala
<b>RS</b>	Sekretariat ya Mkoa
<b>RAS</b>	Katibu Tawala Mkoa
<b>DDH</b>	Hospitali Teule za Wilaya
<b>NAIVS</b>	Mpango wa Taifa wa Pembejeo za Kilimo
<b>CCTV</b>	Kamera na Runinga za Ulinzi
<b>PPE</b>	Mali, Mitambo na Vifaa
<b>TANROAD</b>	Wakala wa Barabara Kuu za Tanzania
<b>IFAC</b>	Shirikisho la Wahasibu la Kimataifa
<b>TPDF</b>	Jeshi la Ulinzi la Tanzania

<b>TBA</b>	Wakala wa Ujenzi wa Nyumba Tanzania
<b>MTEF</b>	Mkakati wa Matumizi wa Muda wa Kati
<b>VT</b>	Fungu
<b>PMU</b>	Kitengo cha Usimamizi wa manunuzi
<b>PE</b>	Taasisi inayofanya Manunuzi
<b>PPRA</b>	Mamlaka ya Udhubiti wa manunuzi ya Umma
<b>MSD</b>	Bohari ya Madawa
<b>REA</b>	Wakala wa Umeme Vijijini
<b>PSPF</b>	Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma
<b>NSSF</b>	Mfuko wa Taifa wa hifadhi za jamii
<b>CDA</b>	Mamlaka ya Ustawi wa Mji wa Dodoma
<b>IT</b>	Teknolojia ya Habari
<b>IFMS</b>	Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha
<b>JKT</b>	Jeshi la Kujenga Taifa
<b>PFA</b>	Kanuni za Fedha za Umma
<b>PMG</b>	Mlipaji Mkuu wa Serikali
<b>PAA</b>	Sheria ya Ukaguzi wa Umma
<b>SUMA</b>	Shirika la Uchumi na Maendeleo

## **MUHTASARI WA MAMBO MUHIMU KATIKA RIPOTI YA UKAGUZI WA TAARIFA ZA FEDHA ZA SERIKALI KUU KWA MWAKA 2012/2013**

Ripoti hii ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inatoa muhtasari wa matokeo ya mwisho ya ukaguzi wa taarifa za fedha za Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2013. Ukaguzi wa taarifa za fedha za Serikali ni uchunguzi huru wa hesabu unao lenga kutoa maoni ya kitaalamu ambayo ni hati ya ukaguzi na hakikisho kwamba taarifa za fedha zilizowasilishwa na mkaguliwa kwa kiwango kikubwa ni sahihi na za kuaminika kwa ajili ya kufanya maamuzi ya Serikali kama vile Serikali kutathmini kama fedha zilizotengwa kwa ajili ya Wizara/Idara/Wakala na Sekretarieti za Mikoa zimetumika kwa manufaa ya Umma na ripoti za fedha zimeandaliwa kulingana na mwongozo wa uandaaji taarifa.

Sehemu hii ya muhtasari, inatoa maelezo ya jumla juu ya matokeo ya ukaguzi ikifuatiwa na mambo muhimu niliyoyabaini wakati wa ukaguzi na mapendekezo yake kwa muhtasari.

### **Mwenendo wa Jumla wa hati za ukaguzi**

Ukaguzi wa kisheria wa taarifa za fedha ulifanyika kwa Wizara na idara za Serikali sitini (60), Sekretarieti za Mikoa ishirini na tano (25) na Balozi thelathini na mbili (32) kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2013. Muhtasari wa matokeo muhimu ya ukaguzi yamejumuishwa katika taarifa hii na taarifa za kina kwa menejimenti ambazo zilitumika kutengeneza taarifa hii zimetolewa kwa barua kwa Maafisa Masuuli wote husika. Matokeo na hati za ukaguzi zilizotolewa ni kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini:

## Mwenendo wa Hati za Ukaguzi kwa kipindi cha miaka minne :

Hati	Hati Zinazoridhisha		Hati zenye Mashaka		Hati zisizoridhisha		Hati Mbaya		Jumla ya wakaguli wa
	Years	Jumla	Asili mia	Jumla	Asili mia	Jumla	Asili mia	Jumla	
2012/13	85 <sup>3</sup>	72	30	26	1	1	1	1	117
2011/12	103 <sup>4</sup>	95	5	5	0	0	0	0	108
2010/11	99	93	8	7	0	0	0	0	107
2009/10	78	76	21	21	2	2	1	1	102

Hati isiyoridhisha ilitolewa kwa Ubalazi wa Tanzania nchini Muscat na Hati mbaya ilitolewa kwa taarifa ya Hesabu Jumuifu za Fedha za Taifa.

Kwa ujumla, Hati Safi zimeshuka kwa kiasi kikubwa huku hati zenye mashaka zikiongezeka ikilinganishwa na miaka miwili iliyopita. Taasisi zilizopata Hati Safi zimeshuka kutoka 46 hadi 26 sawa na upungufu wa asilimia 48 ikilinganishwa na mwaka jana, wakati ambapo kuna ongezeko la Hati zinazoridhisha zenye masuala ya msisitizo kutoka 57 hadi 59 ikilinganishwa na mwaka jana. Taasisi zilizopata Hati zenye mashaka zimeongezeka kutoka taasisi 5 hadi 30 ambapo ni mara sita ya mwaka jana. Pia katika kipindi cha mwaka huu taasisi moja(1) imepata Hati mbaya na taasisi moja(1) ilipata hati isiyoridhisha ambapo hapakuwepo hati hizo katika ukaguzi wa mwaka jana.

<sup>3</sup> Kati ya Hati 85, 26 ni hati Zinazoridhisha na 59 ni Hati zinazoridhisha zenye masuala ya msisitizo

<sup>4</sup> Kati ya Hati 103, 46 ni hati zinazoridhisha na 57 ni Hati zinazoridhisha zenye masuala ya msisitizo

Matokeo haya ya ukaguzi si mazuri ikilinganishwa na mwaka jana, yanaashiria kwamba, taarifa za fedha hazikukidhi mahitaji ya viwango vya uhasibu vya kimataifa, kwa maana ya viwango vya uhasibu vya kimataifa visivyo na misingi ya taslimu (IPSAS Accrual). Hii ina maana kwamba, kulikuwa na baadhi ya maeneo katika taarifa za kifedha ambayo hayakuripoti ukweli na uhalisia wa shughuli za utendaji wa taasisi zilizokaguliwa. Sababu ya uwezekano wa vikwazo hivi inaweza kuwa ni kutokana na sababu zifuatazo;

- a) Kuhama kwenda viwango vya uhasibu vya kimataifa visivyo vya taslimu (IPSAS Accrual) kutoka vile vya taslimu (IPSAS Cash) walivyokua wakitumia kabla, ambavyo vina namna tofauti za kuonesha hesabu kama; matumizi katika kipindi cha mwaka, utambuzi wa ruzuku pokelewa katika taarifa ya mtiririko wa fedha, kutambua mali zote na usuluhishi kati ya kitabu cha fedha na taarifa za kibenki.
- b) Udhaifu katika Mfumo wa kompyuta wa kiuhasibu (IFMS-Epicor), ambapo muundo huohuo uliotumika katika viwango vya uhasibu vya kimataifa vilivyo vya taslimu umetumika pia kwa vile visivyo vya taslimu. Matokeo yake, miamala ya kiuhasibu kama vile masurufu yanayo onyeshwa katika mfumo kama matumizi, pia mfumo huu hautambui miamala isiyofanywa kwa pesa taslimu, mengine ni kutotambua madeni na madai n.k.
- c) Taasisi na idara nyingi zilizokaguliwa hazijawajengea uwezo watumishi wake wahasibu na wasio wahasibu wanaohusika na uandaaji na ufungaji wa hesabu kwa kuwapatia mafunzo stahiki.
- d) Muundo wa kuandaa taarifa za fedha upo katika msingi isiyo ya taslimu (non cash basis) wakati msingi wa bajeti/Makadirio bado upo katika msingi fedha taslimu, hili limesababisha kuwepo dhana mchanganyiko jinsi ya kutolea taarifa masuala mbalimbali katika taarifa za fedha; mfano matumizi yasiyo ya taslimu

hayakujumuishwa katika taarifa ya utendaji wa kifedha.

- e) Kuanza kutumika viwango vya kimataifa vya uhasibu visivyo na msingi wa taslimu kabla ya marekebisho ya sheria zilizopo, kwa mfano Sheria ya Fedha za Umma namba 6 ya mwaka 2001 (ilifanyiwa marekebisho 2004) ambayo inapingana na viwango vya kimataifa vya uhasibu visivyo na msingi wa taslimu vinavyotumika kuandaa taarifa za fedha za serkali kuu.

### **Mambo muhimu katika ukaguzi wa mwaka huu kwa muhtasari**

Wakati wa ukaguzi, nilibaini tena mapungufu kadha wa kadha ambayo yameelezwa kwa kina kwenye sura zinazofuata kwenye taarifa hii. Udhaifu ulijitokeza hasa ni juu ya kutofuatwa kwa sheria na kanuni zilizopo, ukosefu wa mifumo sahihi ya udhibiti wa ndani na pale penye mifumo hiyo kutofuatwa kwa kiasi kikubwa. Dosari kubwa na mapungufu yaliyoonekana wakati wa ukaguzi wangu yameelezwa kwa kifupi hapa chini.

#### **a) Utekelezaji wa mapendekezo ya kaguzi zilizopita**

Katika taarifa zangu za miaka iliyopita, nilitoa mapendekezo kadhaa ambayo yalihatiji kufanyiwa kazi na Serikali. Katika ukaguzi wa mwaka jana, taarifa yangu ilikuwa na masuala Ishirini na nane (28) ambayo yalihatiji majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali. Nimepokea majibu kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali ambapo hoja tano (5) zimefungwa huku hoja ishirini na tatu (23) bado zinasubiri majibu.

Nimefanya ufuatiliaji juu ya utekelezaji wa mapendekezo yangu katika taarifa za Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara za Serikali na Sekretarieti za Mikoa. Katika Wizara na Idara za Serikali, kulikuwa na hoja 960. Kasi ya utekelezaji wa mapendekezo niliyotoa sio ya kuridhisha. Kati ya hoja 960, hoja 401 (42%)

zilitokelezwa kikamilifu, 276 (29%) zilitokelezwa kwa sehemu na 283 (29%) hazikutekelezwa. Kwa Sekretarieti za Mikoa, kulikuwa na hoja 578 kutoka miaka ya nyuma, kati ya hizo hoja 272 (47%) zilitokelezwa kikamilifu. Hoja 105 (18%) zilitokelezwa kwa sehemu na hoja 201 (35%) hazikutekelezwa.

Uchambuzi unaonyesha kwamba utekelezaji wa mapendekezo niliyotoa ni chini ya asilimia 50. Hii si kasi nzuri katika kuboresha shughuli za Serikali na uwajibikaji kwa umma. Kushindwa kutekeleza mapendekezo ya ukaguzi husababisha kujirudia kwa madhaifu hayo katika siku za baadaye.

**b) Mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali Kuu**

Kulingana na Sheria ya Ukaguzi wa Umma, 2008 kinaeleza kwamba Mlipaji Mkuu wa Serikalianatakiwa kuandaa majibu na mpango wa utekelezaji wa taarifa ya Mdhubiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kuzingatia mapendekezo ya Kamati za Hesabu za Bunge. Mwaka jana Kamati ya Bunge ya hesabu za Serikali ilikaa na kujadili taarifa yangu ya ukaguzi katika Wizara, Idara za Serikali na Sekretarieti za Mikoa. Kamati hii ilitoa jumla ya mapendekezo kumi na moja (11) kwa Serikali kwa utekelezaji. Taarifa ya Kamati ya Bunge inayosimamia Hesabu za Serikali Kuu (PAC) iliwasilishwa Bungeni tarehe 7 Desemba, 2013, Hadi wakati wa kuandika taarifa hii, sikuweza kupata majibu kutoka kwa Serikali kuhusu utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali Kuu lakini natarajia kufanya ufuatilia wa utekelezaji katika ukaguzi ujao.

**c) Makisio/ Bajeti na Fedha iliyotolewa**

Kumekuwepo ucheleweshaji mkubwa wa fedha kutoka hazina na pengine kutoka kwa washirika wa maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hii

imesababisha kuchelewa kwa utekelezaji wa miradi au kutotekelezwa kabisa kwa miradi kusudiwa na kuongezeka kwa gharama za mradi pamoja na kiasi kikubwa cha fedha kutotumika. Katika kipindi cha mwaka husika, fedha za maendeleo kiasi cha Sh.997,940,092,853 hakikutolewa na fedha iliyotolewa

kiasi cha Sh.44,428,749,202 hakikutumika. Akaunti ya matumizi ya kawaida ilikuwa kiasi cha Sh.315,463,083,291 ambacho hakikutolewa na kiasi cha Sh.35,141,163,606 cha fedha iliyotolewa hakikutumika.

**d) Usimamizi wa matumizi**

Nimegundua udhaifu katika mifumo ya udhibiti wa malipo, ukosefu wa nyaraka za malipo, matumizi yasiyo na manufaa, matumizi yasiyoidhinishwa, kukosekana

kwa hati za malipo, masurufu yasiyorejeshwa na udhibiti dhaifu wa bajeti, fedha kutumika kwa sababu zisizokusudiwa. Taarifa hizi zimeelezwa kwa kina katika sura ya nne.

**e) Kukosekana kwa Ofisi ya Usimamizi wa Madeni**

Kuendelea kukosekana kwa Ofisi ya Usimamizi wa Madeni inapelekea kuwepo na usimamizi hafifuwa madeni ya umma katika nchi. Muundo wa sasa ambao unahusisha Wizara ya Fedha, Tume ya Mipango, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Benki Kuu ya Tanzania ni mbaya kwa usimamizi wa deni la Taifa kutokana na ukweli kwamba kila mshirika muhimu ana majukumu ya msingi mbali na deni la Taifa. Katika hali hiyo, utendaji na uwazi ambao ni muhimu katika usimamizi wa madeni, ni hatua ya mbali kufikia hivyo kuathirika uwajibikaji kwa kiwango kikubwa.

Katika usimamizi wa madeni, uratibu wa wadau ambao ni Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Tume ya Mipango, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Idara ya mikopo ya nje na Msajili wa Hazina hili ni suala muhimu ambalo

utekelezaji wake haujawekwa bayana huku ikizingatiwa kuwa wote hawa wana majukumu yao ya kuanzishwa kwao tofauti najukumu la usimamizi wa Deni la Taifa;

Hivyo, ukosefu wa ofisi inayojitegemea ya Usimamizi na uratibu wa Madeni (DMO) imepelekea kutoyashughulikia madhara ya madeni ya fedha za mikopo kwa ajili ya miradi na hivyo kudhoofisha uratibu na usimamizi wa deni la taifa.

**f) Maandalizi ya Serikali kutumia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma visivyo na msingi wa fedha taslimu (IPSAS accrual basis)**

Kuhusu uandaaji wa hesabu kwa kutumia Viwango vya kimataifa vya uhasibu katika sekta ya Umma visivyo na msingi wa taslimu (IPSAS accrual), nilibaini kuwa Serikali bado inakabiliwa na changamoto kuhusu utekelezaji wa masuala kadhaa kama vile malimbikizo

ya kazi za nyuma, ukosefu wa uratibu wa kutosha wa zoezi lenyewe, hatarizinazohusu mali/majengo, mitambo na vifaa, na mfumo wa bajeti ya Serikali, taratibu za kifedha, na sera bado zipo katika msingi wa fedha taslimu.

Nilipokuwa napitia Taarifa Jumuifu za kifedha za Serikali, nilibaini kuwa hapakuwa na taarifa jumuifu za mapato, matumizi, mali na madeni ya Serikali za Mitaa (LGAs) na mashirika ya umma na Taasisi za Serikali ambazo zote kwasasa zinatumia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma visivyo na msingi wa fedha taslimu (IPSAS accrual basis). Hii ni kinyume na mwongozo IPSAS 6 ambayo inahitaji Serikalikutoa taarifa Jumuifu ya fedha ambayo inajumuisha Taasisi/idara/mamlaka zote za Serikali na mashirika yote yaliyo chini ya Serikali ndani na nje ya nchi.

Nimebaini pia kuwa, Serikali haijafanya uthamini wa mfuko wa mafao ya uzeeni na Pansheni kwawatumishi

wa umma yaani wastaafu wanaolipwa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kinyume na IPSAS 25. Bila kufanya tathmini ya uwezo wa mfuko huo kulipa mafao ya wastaafu imepelekea Serikali kushindwa kutambua kiasi cha deni la wastaafu katika mfuko huo linalotakiwa kulipwa kila mwezi baada ya kustaafu, gharama za uendeshaji wa mfuko, faida au hasara ya mfuko na huduma zinazopaswa kutolewa kwa sasa na mfuko huo.

**g) Tathmini ya mfumo wa udhibiti wa Ndani**

Wakati wa ukaguzi, nilibaini kuwa kamati ya Ukaguzi na Vitengo vya ukaguzi wa Ndani vilifanya kazi chini ya kiwango kutokana na uhaba wa watumishi, rasilimali na mapungufu katika muundo wa kamati za ukaguzi. Nilibaini kwamba Wizara/Idara za Serikali na Sekretarieti za mikoa hazikuwa na Sera inayoongoza matumizi ya Teknolojia ya Habari iliyoandikwa na kutolewa kwa watumiaji wote wa vifaa vya kompyuta, pia nilibaini kutokuwepo mpango wa kufufua huduma

iwapo maafa yakijitokeza. Maelezo ya kina kuhusu udhibiti wa ndani yanapatikana sura ya tano ya taarifa hii.

**h) Usimamizi wa Rasilimali watu na taarifa za mishahara**

Rasilimali watu ni kiungo muhimu cha rasilimali nyingine kwa hiyo, inahitaji uangalizi maalumu. Usimamizi wa Rasilimali watu, nilibaini kutokuwepo kwa taarifa kamili za watumishi, udhaifu katika mfumo wa kupima utendaji wa watumishi wa umma na kuchelewa kuwasilishwa kwa makato ya mishahara. Maelezo ya kina na mapendekezo yake yanapatikana katika sura ya sita ya taarifa hii.

**i) Manunuzi na Usimamizi wa mikataba**

Kuhusu ununuzi na usimamizi wa mikataba, napenda kutambua juhudi zinazofanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) katika mpango wa

kujenga uwezo ambao kwa kiasi kikubwa umechangia katika kuimarisha manunuzi kwa vyombo vya Serikali na kuvifanya kufuata sheria ya Manunuzi ya Umma Na.21 ya mwaka 2004 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2005. Hata hivyo, bado kuna baadhi ya Wizara, Idara za Serikali na Sekretarieti za Mikoa ambazo hazifuati kikamilifu mahitaji yaliyomo katika sheria ya Ununuzi wa Umma katika kuidhinisha zabuni, utendaji wa vitengo vya manunuzi, uteuzi wa kamati ya tathmini, kamati ya ukaguzi bidhaa na kamati mapokezi. Maelezo ya kina kuhusu mikataba na manunuzi ya bidhaa na huduma yanapatikana sura ya saba ya taarifa hii.

**j) Usimamizi Mali na dhima**

Usimamizi Mali ni kazi muhimu kuhakikisha Wizara na Sekretarieti za Mikoa zinafikia malengo kwa ufanisi ili kukuza kiuchumi. Matatizo makubwa ni ukosefu wa uthibitisho wa umiliki halali wa mali na vifaa, kutokuwepo na daftari la kuandikisha mali za kudumu, mali za kudumu zilizoachwa muda mrefu bila kufanyiwa matengenezo, njia isiyofaa ya kutambua mali za kudumu zisizogusika, uhamisho wa fedha kuonekana kama ununuzi wa mali za kudumu na madeni yasiyolipwa. Maelezo ya kina yanapatikana sura ya tisa ya ripoti hii.

**k) Ukaguzi Maalum**

Ofisi yangu chini ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka, 2008 kifungu cha 29 yakisomwa pamoja na Kanuni ya 79 (1) Kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka, 2009 inaruhusu kufanya ukaguzi maalum. Katika mwaka 2012/2013 nimefanya kaguzi maalum nne (4). Taarifa zimeadaliwa na kutolewa kwa Maafisa Masuuli wanao husika. Hata hivyo, maelezo ya ukaguzi maalum uliofanywa yanapatikana katika sura ya kumi na moja ya taarifa hii. Muhtasari wa Masuala ya msingi kutokana ukaguzi maalum ni kama unavyosomeka hapa chini:

- Ukaguzi maalum juu ya mishahara na madai mengine katika hospitali za rufaa, hospitali teule za wilaya na hospitali mashirika ya hiari kwa miaka 2010/2011 na 2011/2012, nilibaini malipo ya mishahara kwa watumishi hewa kiasi cha Sh.754,992,183 mishahara isiyolipwa ambayo haikurejeshwa hazina na kubaki katika hospitali Sh.3,047,574,792 na kutumika kwa shughuli nyingine zisizo idhinishwa.
- Ukaguzi maalum juu ya ununuzi wa kivuko cha MV Misungwi nilibaini usimamizi duni na ufuatiliaji usioridhisha wa mkataba kati ya Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Sinnautic International. Hati ya makabidhiano haikuandaliwa hivyo MV Misungwi haikukabidhiwa rasmi kwa Wizara ya Ujenzi na vipuri vya thamani ya Euro 41,140 vya MV Misungwi havikuletwa na M/S Sinnautic International.
- Ukaguzi maalum kwenye vocha za pembejeo za kilimo nilibaini, watu ambao hawakuwepo katika orodha ya walengwa wa kupokea vocha za pembejeo za kilimo walipewa vocha bila kufuata taratibu rasmi, Usimamizi duni wa maafisa wa Ugani kuhusu mbegu zilizotolewa na wafanyabiashara na kutokaguliwa kwa mbegu na mbolea, kuchelewa katika ununuzi na usambazaji wa vocha za pembejeo za kilimo, kutokuwepo kwa mwongozo wa mfumo wa uendeshaji, taarifa juu ya mbolea na usambazaji wa mbegu katika nchi. Wakulima kutoelewa mpango wa Taifa wa Pembejeo za Kilimo.
- Ukaguzi maalum kuhusukituo cha mafunzo ya uuguzi Mkomaindo nilibaini utunzaji mbaya wa kumbukumbu na matumizi mabaya ya makusanyo ada hivyo kusababisha upotevu wa ada za wanachuo.

## **I) Masuala mengine**

Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka, 2008 na Kanuni za ukaguzi za mwaka 2009, zinanipa nguvu ya kutolea taarifa mambo ambayo naona ni vyema kuyasemea. Kanuni ya 34 ya Ukaguzi wa Umma, 2009 inatoa uwezo wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kutoa mapendekezo kwa Serikali kwa ajili ya jambo lolote ambalo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anafikiria kuwa bora kwa ajili ya usimamizi bora wa fedha za umma, maghala ya Serikali, dhamana, mihuri na masuala mengine ya rasilimali za umma. Katika sura ya kumi na mbili nimetoa mapendekezo yangu kuhusu masuala yafuatayo:-

- Uendeshaji wa Wakala wa Serikali
- Malipo ya kodi ya kupanga ofisi za Wizara mbalimbali
- Masuala yanayohusu usimamizi wa huduma za Magereza.
- Jukumu la Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu katika ukaguzi wa hesabu za miradi inayosimamiwa kwa Ushikiano baina ya Serikali na Sekta Binafsi (PPP).
- Masuala ya yaliyojitokeza katika ukaguzi wa vyama vya siasa.

### **Muhtasari wa Mapendekezo**

Serikali inatakiwa kufanyia kazi mapendekezo ya Mkaguzi kwa umakini na kwa wakati. Ni wajibu wa Maafisa Masuuli kuhakikisha uwepo wa mfumo thabiti wa uthibiti wa ndani kwenye shughuli zote za Fungu ili kupunguza mapungufu mbalimbali yanayosababishwa na ukosefu wa mfumo thabiti wa udhibiti wa ndani. Kwa kuzingatia masuala tajwa hapo juu, yafuatayo ni mapendekezo yangu ya jumla:

### **Kutotekelezwa baadhi ya mapendekezo ya mwaka uliopita**

Serikali inapaswa kuweka juhudi za makusudi ili kuhakikisha kuwa mapendekezo yanafanyiwa kazi ipasavyo. Hazina inatakiwa kutoa maagizo kwa Maafisa Masuuli kuchukua hatua muhimu ili kuboresha utunzaji wa nyaraka, ambayo ni moja ya sababu kuu zinazochangia

kukosekana kwa nyaraka na kwa hiyo kushindwa kujibu baadhi ya hoja za ukaguzi.

Maafisa Masuuli wanatakiwa kutengeneza mpango kazi wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi. Mpango kazi huo wa utekelezaji uwe maalum kwa ajili ya masuala ambayo hayawezi kufanyika ndani ya kipindi cha muda mfupi. Msisitizo wa kuwa na daftari la kutunza taarifa za hoja za ukaguzi kwa kila Afisa Masuuli ni utaratibu mwingine muhimu. Kuwa na daftari la kumbukumbu ni chombo kizuri cha kufuatilia masuala ya ukaguzi yasiyojibiwa ikiwa ni pamoja na maendeleo yaliyopatikana hadi sasa.

### **Makisio/Bajeti na Fedha iliyotolewa**

Ili kukabiliana na changamoto ya fedha zilizoidhinishwa kutotolewa kwa wakati, nashauri Serikalikuandaa makisio ya matumizi ya mwaka yanayoendana na makusanyo ya mapato ili kuzuia kutolewa kwa kiasi kikubwa cha fedha mwishoni mwa mwaka wa fedha. Kwa kufanya hivyo, inatarajiwa kwamba shughuli zilizopangwa zitatekelezwa kama zilivyopangwa.

Serikali kupunguza utegemezi wa misaada ya nje kwa ajili ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya taifa, nashauri Serikali ijitahidi kuchunguza vyanzo vya mapato mbadala vya ndani. Maelezo zaidi kuhusu hili yameelezwa katika sura ya nne ya taarifa hii.

### **Ukosefu wa Ofisi ya Usimamizi wa Madeni**

Haja ya kuwepo Ofisi ya Usimamizi Madeni ni moja kati ya masuala muhimu ambayo nilishauri yafanyike katika taarifa ya mwaka wa fedha 2010/2011. Nashauri Serikali ifanye mchakato wa kuanzishwa kwa Ofisi ya usimamizi wa madeni ili kuweza kukabiliana kikamilifu na kwa ufanisi kutekeleza majukumu ya usimamizi wa madeni. Pia, hatua makini kuchukuliwa na Serikali ikiwa ni pamoja na kujiepusha na kubadilisha karatasi ukwasi (liquidity paper) mara kwa mara ili kugharamia bajeti, kuboresha

ukusanyaji wa mapato ya Serikali kwa njia ya TRA, nidhamu ya matumizi na makadirio ya halisi ya bajeti.

### **Maghala ya bidhaa zisizolipiwa Ushuru wa forodha (Customs bonded warehouses)**

Serikali inashauriwa kuhakikisha udhhibiti wa kutosha kwenye uendeshaji wa maghala ya ushuru wa forodha, bidhaa zinazokaa katika maghala yasiyolipiwa ushuru wa forodha na kukusanya madeni yote yatokanayo na kutokukusanywa kwa ushuru wa forodha. Aidha, Mamlaka ya Mapato Tanzania izingatie na kusimamia sheria zilizopo.

### **Utekelezaji wa mwongozo wa kimataifa wa hesabu katika sekta ya umma na Usimamizi wa Mali**

Kwa kuwa Serikali ina kipindi cha mpito cha miaka mitano kama mtumiaji wa mara ya kwanza wa Viwango ya Kimataifa vya Uhasibu visivyo vya msingi wa taslimu (IPSAS Accrual Basis), naishauri Serikali kufanya mambo yafuatayo ili kutumia kwa ufanisi kipindi hiki cha mpito:-

- Kutenga rasilimali za kutosha ikiwa ni fedha na rasilimali watu ili kurahisisha utendaji wa zoezi hili.
- Nashauri Serikali kuzingatia kikamilifu Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika sekta ya Umma Na.25 (Mafao ya Watumishi) kwa mipango mizuri ya Mafao ya Watumishi ili kuamua dhima yake ya awali ikizingatiwa kuwa huu ni mwaka wa kwanza wa kutumia viwango hivyo vikiwa katika misingi isiyo ya taslimu.
- Kuanzisha Kamati ya Taifa ya kuratibu yenye wataalamu wa fani mbalimbali ambao watakuwa wasimamizi kwa miaka mitano na kuwa na mkakati wa kuhakikisha kila hatua inachukuliwa kwa umakini na kwa wakati.
- Kurugenzi ya Serikali Usimamizi wa Mali wanapaswa kufanya kazi kwa karibu na wadau ili kufanikisha utekelezaji wa mpango wa kuingia katika viwango vya kimataifa vya uhasibu visivyo na msingi wa taslimu kwa ukamilifu kama ilivyowekawa wazi na 'IPSAS' 17.

- Nashauri Serikali kuanza kujumuisha taarifa za fedha za Serikali za Mitaa na taasisi nyingine za Serikali katika Hesabu Jumuifu za fedha za Jamhuri ya Muungano.
- Kubadili mfumo wa pamoja wa usimamizi wa fedha (IFMS-EPICOR) na mfumo ya bajeti iweze kukidhi mahitaji ya viwango vya kimataifa vya uhasibu kwa sekta ya umma visivyo vya msingi wa taslimu.

### **Usimamizi wa Manunuzi**

Kama awali nilivyosema, manunuzi yanachukua sehemu kubwa ya rasilimali za Serikali ili kutekeleza shughuli zake kama zilivyopangwa. Hivyo, Serikali inatakiwa kuboresha mfumo wa manunuzi ili kuepuka kujirudia kwa hoja. Yafuatayo yanahitaji kuzingatiwa ili kuboresha manunuzi.

- Serikali kupitia PPRA inatakiwa kuendesha semina kadhaa kwa lengo la kujenga uwezo wa wasimamizi wa vitengo vya manunuzi (PMU), Bodi za Zabuni, Maafisa Masuuli na watumiaji kuhusu umuhimu wa kutekeleza Sheria ya Manunuzi ya Umma na kanuni zake.
- Pia ni muhimu kuwa na Mfumo wa Usimamizi wa Manunuzi (PIMS) katika uendeshaji wenye ufanisi. Mfumo huu unamilikiwa na Mamlaka ya kudhibiti Manunuzi ya Umma (PPRA). PPRA inatakiwa kuhakikisha kwamba mfumo huu ni mfumo rafiki kwa watumiaji wa Wizara/Idara za Serikali na Sekretarieti za Mikoa na unaweza kutumika kwa urahisi ili kuboresha shughuli za manunuzi ya umma.

### **Usimamizi wa rasilimali watu na mishahara**

Ninaishauri Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma (PO- PSM) ipitie upya ikama za Wizara, Idara za Serikali na Tawala za Mikoa na kuja na mapendekezo halisi ya idadi ya watumishi wanaohitajika. Taasisi zote zilizobainika kuwa na upungufu wa rasilimali watu, zinatakiwa kujaza nafasi hizo ili kuboresha huduma kwa jamii. Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara za Serikali na Tawala za Mikoa wanapaswa kufuatilia kwa bidii kuhakikisha kwamba wana idadi ya watumishi wa kutosha na wenye sifa stahiki. Nashauri pia wawe na mpango unaotekelezeka kwa ajili ya motisha kwa wafanyakazi na

sera ya kuwafanya wadumu kazini. Uhaba wa wafanyakazi unapaswa kutolewa taarifa kwa mamlaka husika ikiwa ni pamoja na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma (PO- PSM).

### **Mishahara iliyolipwa kwa watumishi hewa**

Ili kuepuka hasara kama hii kwa siku zijazo, Maafisa Masuuli katika Wizara/Idara na Mikoa wanapaswa kuangalia taarifa za mishahara ya watumishi wao mara kwa mara na kuthibitisha uhalali wa watumishi wote kabla ya malipo. Pia, mawasiliano lazima kuimarishwa ili kuhakikisha kwamba majina ya wastaafu, watoro/walioacha kazi au walioachishwa kazi yanafutwa katika taarifa za wafanyakazi mara moja. Mbali na hayo, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuhakikisha mishahara isiyolipwa kwa watumishi ambao muda wao wa utumishi umekoma kwa sababu moja au nyingine iwe inarejeshwa Hazina kwa wakati. Zaidi ya hayo, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuhakikisha kuwa Mfumo wa kutunza taarifa za watumishi (HCMIS-LAWSON) unafanya kazi na unatumika kikamilifu ili kupata thamani ya fedha tarajiwa.

### **Usimamizi wa Matumizi**

Hili ni moja ya eneo ambalo lina changamoto nyingi. Changamoto hizi husababishwa na kuwepo kwa udhibiti wa ndani usiosimamiwa kwa usahihi au maafisa wenye dhamana kukiuka taratibu kwa makusudi. Maafisa Masuuli wa Wizara/Idara, Mikoa na Balozi wanapaswa kuhakiki hati za malipo na nyaraka zote na kuthibitisha uhalali na usahihi kulingana na matakwa ya Kanuni ya 95 (4) ya Kanuni za Fedha za Umma ya 2001 inavyosema. Mifumo ya udhibiti wa ndani ni lazima iboreshwe ikiwa ni pamoja na ukaguzi wa awali (Pre-Audit).

### **Usimamizi na uendeshaji wa Balozi za Tanzania**

Utafiti unaendelea katika eneo hili; hata hivyo, kutokana na kile nilichobaini wakati wa ukaguzi, nina mapendekezo ya jumla kama ifuatavyo:-

- Balozi husika zikishirikiana na Wizara ya Mambo ya nje na Ushirikiano wa Kimataifa (MFAIC) zinatakiwa

kusitisha malipo ya posho ya ya watumishi waliostaafu walioko nje ya nchi na kufanya utaratibu wa kuwarudisha nyumbani haraka pindi utumishi wao unapokoma. Napendekeza mamlaka husika kuangalia ni jinsi gani zitakavyoweza rudisha fedha zilizolipwa maafisa wa zamani wa ubalozi wakikwa hawako katika utumishi.

- Usimamizi wa Balozi uwasiliane na Wizara (MFAIC) kwa ajili ya kuwarejesha majumbani watumishi waliomaliza utumishi wao ambao bado wanaendelea kuishi ubalozini na wale ambao wamekaa kituo kimoja muda mrefu wabadilishwe. Hii itakuwa na athari chanya katika utoaji wa huduma kwa balozi zetu.
- Uongozi wa Wizara ya Mambo ya nje na Ushirikiano wa Kimataifa (MFAIC) uangalie uwezekano wa kuanzisha mfuko katika bajeti yao kwa ajili ya kufanya shughuli za diplomasia ya kiuchumi na kukuza vivutio vya utalii. Hii ni kazi muhimu kwa uchumi wa nchi.

### **Kaguzi maalum**

- Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Hazina inatakiwa kuboresha mawasiliano na Menejimenti za Hospitali husika kuhakikisha watumishi waliostaafu, kufa, kuacha kazi na watoro wa muda mrefu wanafutwa haraka katika taarifaza utumishi ili kuepuka tatizo la kulipa mishahara hewa. Hospitali Teule za Wilaya na zile za Shirika hiari kuzingatia makubaliano ya mkataba kati yao na Wizara ya Afya na Usitawi wa Jamii.
- Hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya maafisa wa umma walioshindwa kusimamia utekelezaji wa mkataba wa ununuzi kivuko cha Misungwi na hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya mzabuni M/S Sinnautic international ambaye alishindwa kutekeleza kazi zote za kuleta vipuri vya thamani ya Euro 41,140 zakivuko cha Misungwi kwa mujibu wa mkataba.
- Kuhusu mpango wa Taifa Pembejeo za Kilimo kwa kutumia vocha (NAIVS), orodha ya walengwa ipitiwe upya ili kutathmini uwepo wao na kama kweli wanakidhi vigezo vilivyoainishwa. Maafisa Ugani, Wakala wa Mbegu na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo

wanapaswa kushirikiana katika mapitio na tathmini ya mbegu na mbolea inayotolewa nchini. Ununuzi na usambazaji wa vocha lazima ufanyike kwa wakati na Wizara inapaswa kutenegeza toleo la mwongozo katika lugha ya kiswahili ili kufanya zoezi liwe rahisi.

- Kuhusu ukaguzi maalum uliofanywa katika kituo cha mafunzo ya uuguzi Mkomaindo, nashahuri uongozi wa kituo kuimarisha mfumo wa udhibiti wa ndani ikiwa ni pamoja na kuboresha utunzaji wa kumbukumbu.

## SURA YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI WA MAMBO YA JUMLA

#### 1.1 Mamlaka na umuhimu wa kufanya ukaguzi

##### 1.1.1 Mamlaka ya kufanyaukaguzi

Taarifa hii inatolewa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kifungu cha 10 cha Sheria ya Ukaguzi wa umma Na. 11 ya mwaka 2008, kwa mujibu wa rejea hii inatakiwa kufanya ukaguzi wa hesabu na kumbukumbu nyingine za Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa.

Kutokana na Ibara ya 143(2) (C) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ninapaswa kukagua na kutoa taarifa ya hesabu za fedha angalau mara moja kwa mwaka katika Ofisi zote za Umma, Mahakama, Mamlaka zote za Serikali ya Muungano wa Tanzania na Bunge.

Kwa upande mwingine, Kifungu 10(2)(a) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya 2008, kinanitaka kujiridhisha kuwa Taarifa za Fedha zimeandaliwa kulingana na viwango vya uhasibu vinavyokubalika. Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa zinapaswa kuandaa taarifa za hesabu kulingana na Viwango vya kimataifa vya kiasibu katika sekta ya umma (IPSAS) kwa misingi ya fedha isiyo taslim naviwango vya kimataifa vya taarifa za fedha (IFRS).

Taarifa za fedha za Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa zilizowasilishwa zimeandaliwa kwa kuzingatia Viwango vya kimataifa vya kiasibu katika sekta ya umma (IPSAS) kwa misingi ya fedha isiyo taslim na kifungu 25(4)(a) na (b) cha Sheria ya Fedha ya Umma Na. 6 ya Mwaka 2001 inayowataka Maafisa Masuuli kuwasilisha kwa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali taarifa za fedhaziliyoandaliwa kwa kuzingatia Viwango vya uhasibu vinavyokubalika na kuzingatia maelekezo yaliyoidhinishwa na Katibu Mkuu wa Hazina na kutolewa na Mhasibu Mkuu

wa Serikali yanayoelekeza msingi wa uandaaji wa taarifa za hesabu ambao Maafisa Masuuli wanatakiwa kutumia. Waraka wa Kihisibu Na. 11 wa mwaka 2012/2013 uliotolewa na Mhasibu Mkuu wa Serikali unawataka Maafisa Masuuli kuandaa taarifa za hesabu kwa kutumia Viwango vya kimataifa vya kihisibu katika sekta ya umma (IPSAS) kwa misingi ya fedha isiyo taslim.

Taarifa kamili za fedha zilizoandaliwa kwa mujibu wa viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma (IPSAS) kwa misingi ya fedha isiyo taslim inajumuisha taarifa zifuatazo:

- (a) Mizania ya Hesabu;
- (b) Taarifa ya mapato na matumizi;
- (c) Taarifa kuhusu mabadiliko ya mtaji;
- (d) Taarifa ya mtiririko wa fedha;
- (e) Taarifa ya uwiano wa bajeti na kiasi halisi cha matumizi;
- (g) Sera za uhasibu na maelezo ya taarifa za fedha

Kifungu Na. 34 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 na kanuni namba 88 ya Kanuni za ukaguzi wa umma za mwaka 2009 zinamtaka Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali baada ya kukagua taarifa za hesabu kuandaa na kuwasilisha taarifa ya ukaguzi. Ripoti ya taarifa za fedha za mwaka zinatakiwa kuwasilishwa na Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mheshimiwa Rais kabla ya tarehe 31 Machi kila mwaka na itawasilishwa na Waziri husika kwa Bunge ndani ya siku saba baada ya kikao cha Bunge kinachofuata kuanza.

## **1.1.2 Umuhimu wa kufanya ukaguzi**

### **1.1.2.1 Lengo la ukaguzi**

Lengo kuu la kufanya ukaguzi ni kumwezesha Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutoa maoni ya ukaguzi huru kuhusiana na hesabu za Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka ya Mapato Tanzania na Hesabu Jumuiifu za Taifa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2013. Pia kubainisha

endapo kama zimetayarishwa kwa kuzingatia Viwango vya kimataifa vya kihesabu katika sekta ya umma (IPSAS) kwa misingi ya fedha isiyo taslim au viwango vya kimataifa vya taarifa za fedha (IFRS).

#### **1.1.2.2 Mbinu za ukaguzi**

Mbinu za kuangalia vihatarishi vilivyopo ndiyo iliyotumika katika ukaguzi wa Taarifa za fedha. Mbinu hii ya ukaguzi inasisitiza haja ya kuelewa kwa kina mazingira, ikiwa ni pamoja na mifumo ya udhibiti wa ndani, kutathimini vihatarishi ili kuweka mategemeo inapowezekana kwenye udhibiti wa ndani uliowekwa na menejimenti. Mbinu za ukaguzi za ofisi zinatekelezwa kwa kutumia mwongozo wa utaratibu wa ukaguzi na programu ya kutunza kumbukumbu za ukaguzi ujulikanao kama *Teammate*.

Ili kuhakikisha mbinu za ukaguzi zinaenda na wakati, menejimenti ya ofisi kupitia kitengo cha huduma za kiufundi hufanya maboreshokila mwaka kwenye mbinu za ukaguzi. Maboreshohayo yanahusisha mabadiliko yote muhimu katika fani ya ukaguzi na uhasibu, pamoja na mabadiliko katika mifumo ya sheria.

#### **1.1.2.3 Mawanda ya Ukaguzi**

Ukaguzi ulifanyikakwa mujibu waviwango vya kimataifavya Taasisi Kuu za Ukaguzi (ISSAls) ili kutoa uhakika kama taarifa za fedha hazina dosari. Taratibu za ukaguzi zinajumuisha chunguzi wa kumbukumbu za taarifa mbalimbali, mifumo ya udhibiti wa ndani, mifumo ya taarifa na mahitaji ya kutoa taarifa zinazohitajika kisheria.

Taarifa za fedha za Serikali kuu kwa mwaka 2012/13 zinaonyesha kwa muhtasari matokeo ya ukaguzi yaliyofanyika kwa misingi ya sampuli, kwa hiyo, matokeo ya ukaguzi kwa kiasi kikubwa yalitegemea kumbukumbu za taarifa, na nyaraka tulizomba na kuwasilishwa kwa ajili ya kufanya ukaguzi.

## **1.2.0 Viwango na taratibu zinazotumika kutoa taarifa**

### **1.2.1 Viwango vinavyotumika wakati wa Ukaguzi**

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni mwanachama wa Shirika la Kimataifa la Taasisi Kuu za Ukaguzi (INTOSAI), Shirika la Taasisi kuu za Ukaguzi Kanda ya Afrika (AFROSAI) na Shirika la Taasisi Kuu za Ukaguzi Kanda ya Afrika kwa nchi zinazoongea kingereza (AFROSAI-E). Ushirikiano na Taasisi nyingine kuu za Ukaguzi (SAI) unaruhusu Ofisi ya Taifa ya ukaguzi wa hesabukubadilishana maarifa nataarifa kuhusunjia bora namaendeleokatika sekta ya ukaguzi wa umma.

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inafanya kazi za ukaguzi kwa mujibu wa viwango vya Shirika la Kimataifa la Asasi Kuu za Ukaguzi (ISSAI) vilivyotolewa na Shirika la Kimataifa la Asasi Kuu za Ukaguzi (INTOSAI) na viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA) vilivyotolewa na Shirikisho la Wahasibu la Kimataifa (IFAC).

### **1.2.2 Taratibu zinazotumika katika kutoa taarifa**

Ufanisi waukaguzi wanguhutegemea sanamawasiliano mazuri namenejimenti ya wakaguliwa. Mawasilianonimuhimukatikamchakato mzima wa ukaguziambao unahusishahatua zifuatazo:

- (i) Kutoa barua ya kushiriki ukaguzi kwa mkaguliwa kabla ya kuanza kazi ya ukaguzi inayoeleza madhumunina mawanda ya ukaguzi, maeneo yanayotarajiwa kufanyiwa ukaguzi na kuelezea majukumu ya Mkaguzi na mkaguliwa.
- (ii) Kuandaa mkakati wa ujumla wa ukaguzi unaoonyesha mwelekeo mzima wa ukaguzi, vigezo vitakavyotumika katika hatua za mwanzo za kutathmini Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa zinazokaguliwa.
- (iii) Kufanya kikao cha kwanza na uongozi wa Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa inayokaguliwa kabla ya kuanza ukaguzi.
- (iv) Kutoa ripoti ya ukaguzi wa mwanzo kwa menejimenti ambayo itakuwa inaonyesha kilichoonekana wakati

wa ukaguzi na kuwapa nafasi uongozi kuweza kujibu ripoti hiyo.

- (v) Kutoa rasimu ya ripoti ya ukaguzi kwa menejimenti inayoelezea hoja za ukaguzi zilizobainishwa na kutoa muda kwa menejimenti kuweza kujibu hoja hizo.
- (vi) Kufanya kikao cha mwisho na mkaguliwa baada ya kumaliza ukaguzi cha kupitia kwa pamoja hoja zilizojitokeza wakati wa ukaguzi.
- (vii) Kutoa ripoti ya mwisho kwa uongozi wa Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa inayoonyesha matokeo ya ukaguzi ikiwa ni pamoja na hoja za ukaguzi na kutoa nafasi kwa uongozi wa mkaguliwa kuweza kujibu hoja hizo.
- (viii) Kutoa ripoti ya ukaguzi kwa menejimenti inayoonyesha hati ya ukaguzi aliyopata mkaguliwa kuhusiana na taarifa za fedha.

### 1.3.0 Idadi ya wakaguliwa na mpangilio wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa hesabu za Serikali

#### 1.3.1 Idadi ya wakaguliwa.

Katika mwaka wa fedha 2012/2013, nilikagua ofisi 116 za Serikali zilizojumuishwa wizara, Idara, Wakala wa Serikali 25; Sekretarieti za Mikoa 25 na Balozi za Tanzania nje ya nchi 32. Kila ofisi ilipewa ripoti yake ya ukaguzi. Mgawanyo waUwiano wawakaguliwani kama inavyoonekanakatikajedwali hapachini:

#### Jedwali 1: Idadi ya Wakaguliwa

Mkaguliwa	Jumla	Asilimia
Wizara, Idara na Wakala	59	51
Sekretarieti za mikoa	25	21
Balozi	32	28
<b>Jumla</b>	<b>116</b>	<b>100</b>

Mbali naukaguzi wa Wizara, Idara, Wakala, Sekretarieti za mikoa na balozi, ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa hesabu za


Serikali pia inakagua, hesabu jumuiifu za taifa, mafao ya wastaafu kabla ya malipo na Mamlaka ya mapato Tanzania.

### 1.3.2 Mpangilio wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

Ofisi inafanya kazi zake kwa mpangilio wa timu za ukaguzi, mfumo ambao unajaribu kuwaweka karibu wakaguliwa waofanana katika kusaidia ofisi kutekeleza majukumu yake kitaalamu na kikamilifu katika nyanja mbalimbali za ukaguzi. Timu za ukaguzi zinaongozwa na Wakaguzi Wakazi wakisaidiwa na viongozi wa timu na wakaguzi wengine. Wakaguzi wakazi husimamiwa na Wasaidizi wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Tuliona ni vyema kugawa wakaguliwa wetu katika Kanda ambazo zinaongozwa na Wasaidizi wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambao wanaripoti kwa Manaibu wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu. Kwa mujibu wa Muundo wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Manaibu wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wanawajibika moja kwa moja kwa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama inavyoonekana katika kizidua cha muundo wa ofisi hapa chini:

**Kielelezo Na.1 Muundo wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi(kizidua)**



#### **1.4.0 Wajibu wa Kisheria wa Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa**

##### **1.4.1 Kuandaa na kuwasilisha taarifa za hesabu**

Kifungu cha 25(4)(a)na(b) cha sheria ya Fedha ya Umma inahitajiMaafisa Masuulikuwasilishataarifa za fedha zilizoandaliwa kwa mujibu wa Viwango vya uhasibu vinavyokubalikana kwa kuzingatia maelekezo yaliyoidhinishwa na Katibu Mkuu wa Hazina na kutolewa na Mhasibu Mkuu wa Serikali.Taarifa za Fedha zinatakiwa kuonyesha msingi uliotumikawakati wa uandaaji wa taarifa za fedha.

Waraka wa Kihisibu Na. 11 wa mwaka 2012/2013 uliotolewa na Mhasibu Mkuu wa Serikali unazitaka Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa kuandaa taarifa za hesabu kwa kuzingatia kifungu cha 25 cha Sheria ya Fedha za umma na pia kwa kutumia Viwango vya kimataifa vya kihisibu katika secta ya umma (IPSAS) kwa misingi ya fedha isiyo taslim. Serikali kuu ilihama kutoka misingi ya fedha taslim kwenda misingi isiyokuwa ya fedha taslim katika mwaka wa fedha 2012/2013 ili kuboreshaUtawala Bora na Uwajibikajikatika usimamizi warasilimali za umma. Hata hivyo, Serikali kuu ipo katika kipindi cha mpito cha muda wa miaka mitano.Serikali kuu itakuwa inatekeleza Viwango vya kimataifa vya kihisibu katika sekta ya umma (IPSAS) kwa misingi ya fedha isiyo taslim kikamilifumwaka 2016/2017.

Uongozi wa Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa unatakiwa kuanzisha na kusimamia mifumo ya udhibiti wa ndani ili kuhakikisha taarifa za fedha na rekodi za kumbukumbu za fedha zinaandaliwa vizuri, kikamilifu na zinafuata sera, taratibu na kunakuwa ufanisi katika utendaji wa kazi na utunzaji mzuri wa kumbukumbu na kulinda mali na rasilimali.

Aidha,Kanuni Na.71 (1) ya Kanuni ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2009 inahitajiAfisa Masuulikuandaa na kuwasilishataarifa za fedhakwaMdhibiti na Mkaguzi

Mkuuwa Hesabu za Serikalindani ya muda wa miezi mitatubaada ya kumalizika kwamwaka wa fedhahusikapamoja na hayo, Kanuni Na. 71 (2) ya Kanuni ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka, 2009 inahitajiMhasibu Mkuu wa Serikalikuandaa na kuwasilisha hesabu jumuiifu za TaifakwaMdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Serikalindani yakipindicha miezi minnebaada yakumalizika kwa mwaka wa fedha.

#### **1.4.2 Kuandaa na kuwasilisha majibu ya hoja**

KanuniNa.86(1) -(3) ya Kanuni ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2009 inamtakaMdhibili na MkaguziMkuu wa Hesabu za Serikali kuandaa na kuwasilisha ripoti ya ukaguzi kwa menejimenti ya wakaguliwa inayoonyesha mapungufu yaliyojitokeza. Menejimenti ya Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa unatakiwa kutoa majibu ya hoja hizo ndani ya siku ishirini na moja toka tarehe ya kupokea ripoti ya ukaguzi. Endapo uongozi utashindwa kutoa majibu ndani ya siku ishirini na moja hoja hizo zitajumuishwa kwenye ripoti ya mwisho ya ukaguzi kwa menejimenti kwa mwaka husika.

Pamoja na hayo,Kanuni ya93 ya Kanuni ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2009 inataka kilaAfisaMasuuli kuandaa na kuwasilisha majibu ya hoja ndani yasiku ishirini na mojatokatarehe ambayo taarifa ya fedha jumuiifu ya Serikali kuu imewasilishwa bungeni.Pia kanuni ya 94 inawataka Maafisa Masuulikuwasilisha majibu kwa kamati ya hesabu za Serikali na nakala kwa Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

## SURA YA PILI

### MAANA YA HATI ZA UKAGUZI, AINA ZAKE, MASUALA YANAYOPELEKEA KUTOLEWA HATI HIZO NA MATOKEO HALISI YA UKAGUZI

#### 2.0 KUHUSU HATI ZA UKAGUZI

Kama nilivyoeleza kwenye sura zilizopita, serikali kuu imefanya maamuzi mazito ya kuhamia katika mfumo mwingine wa kuandaa taarifa za hesabu za mwaka kwa kuzingatia mwongozo wa kimataifa wa uhasibu katika sekta ya umma kwa msingi usio wa fedha taslimu (IPSASs accrual accounting basis) kuanzia tarehe 1 Julai, 2012. Huu ni uamuzi unaostahili kusifiwa kwa serikali katika kuboresha utoaji wa taarifa za fedha za umma. Hivyo basi, kwa mara ya kwanza taarifa hizi zitakaguliwa kwa kuzingatia mwongozo wa kimataifa wa uhasibu kwa msingi usio wa fedha taslimu. Pia maelezo ya kina yaliyotolewa kwenye taarifa kwenye tanbihi namba 8 kuhusu kipindi cha mpito yamezingatiwa katika kutoa hati za ukaguzi.

Hata hivyo, kuhamia katika mfumo mwingine wa utoaji taarifa umekuwa na changamoto katika kutoa hati za ukaguzi, kwa sababu, tofauti na mwaka uliopita, mwaka huu idadi ya taasisi zilizopata hati safi zimepungua na zilizopata hati zenye shaka zimeongezeka. Pia, ubalozi wa Maskati umepata hati isiyoridhisha na hesabu jumuiifu za Taifa imepata hati mbaya.

Lengo kuu la kufanya Ukaguzi huu ni kutoa maoni huru juu ya ukaguzi uliofanyika kwenye taarifa za fedha za wakaguliwa, kama taarifa hizo zimeandaliwa kulingana mifumo iliyokubalika ya uandaaji wa taarifa za fedha. Kwa kuwa Ukaguzi huu imehusisha sekta ya umma, lengo hili limepanuliwa ili kutathmini utiifu wa sheria na kanuni mbalimbali pamoja na ufanisi wa wa mifumo ya udhibiti wa ndani wa wakaguliwa.

Hati ya ukaguzi ni maoni yanayotolewa na mkaguzi wa nje kwa njia ya ripoti iliyosainiwa (hati) kama taarifa za fedha

zilizoandaliwa na kukaguliwa zinaonyesha hali halisi ya shughuli zilizofanyika; yaani matokeo ya mapato na matumizi na hali ya kifedha ya taasisi zilizokaguliwa. Ripoti hiyo inawapa watumiaji wa taarifa za fedha juu ya mambo yaliyoripotiwa kwenye taarifa hizo ili kufanya maamuzi sahihi.

## **2.1 Aina za hati za ukaguzi**

Kutokana na mazingira au hali halisi ya ukaguzi, aina hizi za hati zinaweza kutolewa; angalia **Kiambatisho 'A'**

- i. Hati inayoridhisha
- ii. Hati isiyoridhisha
- iii. Hati yenye shaka
- iv. Hati mbaya

Katika hali ya kawaida, nimeainisha masuala muhimu ambayo hayakuathiri maoni na hati za ukaguzi ambayo kwa maoni yangu nimeona ni vyema kuwa ya muhimi kwa wale watumiaji wa taarifa za fedha. Katika hili nimeweka aya zifuatazo:

- Aya yenye masuala ya msisitizo
- Aya yenye masuala mengine

## **2.2 Vigezo vya hati za ukaguzi pamoja na matokeo halisi ya ukaguzi uliofanyika**

### **2.2.1 Hati inayoridhisha**

Aina hii ya hati inatolewa pale ambapo nimejidhihirisha kuwa kutokana na kiwango na usahihi wa ushahidi wa kiukaguzi nilioupata, hesabu zilizoandaliwa zimekidhi viwango, yaani taarifa zilizoandaliwa zinatoa picha halisi ya shughuli zilizofanywa na wakaguliwa. Hii inamaanisha kuwa; sera za kiuhasibu zilizotumika zinaendana na matakwa ya IPSAS accrual na zimetumika kwa mfululizo (mwaka hadi mwaka) kwenye kuaanda hesabu hizo, sheria na kanuni husika zimefuatwa na pia kuna taarifa za kutosha ambazo zinazifanya hesabu kujieleza zenyewe na hivyo kueleweka kirahisi kwa watumiaji wa taarifa hizo.

Kwa mwaka huu wa 2012/13; jumla ya wakaguliwa 26<sup>5</sup> kwa upande wa serikali kuu wamepata hati safi kati ya wakaguliwa wote 117<sup>6</sup>, ambapo ni asilimia 22%. Hili ni punguzo la 43% ukilinganisha na ukaguzi wa mwaka jana. Jedwali lifuatalo linaonesha orodha ya wakaguliwa waliopata hati safi.

**Jedwali 2: Idadi ya wakaguliwa waliopata hati inayoridhisha**

S/N	Fungu Na.	Jina la Mkaguliwa
1.	8	Tume ya Kurekebisha Katiba
2.	9	Bodi ya Mishahara ya Watumishi wa Umma
3.	12	Tume ya Mahakama
4.	13	Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu
5.	20	Ofisi ya Rais Ikulu
6.	25	Ofisi ya Waziri Mkuu
7.	26	Ofisi ya Makamu wa Rais
8.	27	Msajili wa Vyama vya Siasa
9.	30	Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri
10.	31	Ofisi ya Makamu wa Rais
11.	33	Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Maadili
12.	34	Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa
13.	39	Jeshi la Kujenga Taifa
14.	47	Sekretarieti ya Mkoa wa Simiyu
15.	57	Wizara ya ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa
16.	58	Wizara ya Nishati na Madini
17.	59	Tume ya Marekebicho ya Sheria
18.	62	Wizara ya Uchukuzi
19.	67	Sekretarieti ya Ajira
20.	84	Sekretarieti ya Mkoa wa Singida
21.	94	Tume ya Utumishi wa Umma

<sup>5</sup>Wizara, Idara & Wakala 21, Sekretarieti za mikoa 2 na Balozi 3

<sup>6</sup>Wizara, Idara na Wakala 60, sekretarieti za mikoa 25, Balozi 30 na wawakilishi wa kudumu 2

S/N	Fungu Na.	Jina la Mkaguliwa
22.	97	Wizara ya Afrika Mashariki
23.	98	Wizara ya Ujenzi
24.	2012	Ubalozi wa Tanzania Ottawa; Canada
25.	2018	Ubalozi wa Tanzania Washington
26.	2027	Ubalozi wa Tanzania Abu Dhabi

*Chanzo: Ripoti ya CAG ya wizara husika kwa mwaka 2012/2013*

### 2.2.2 Masuala ya msisitizo/na masuala mengine.

Kutokana na taarifa zilizoandaliwa na wakaguliwa, nimelazimika kuweka aidha masuala yenye msisitizo au masuala mengine kwenye ripoti zangu kwa wakaguliwa ili kuelezea mambo ambayo kitaalamu nimeona ni ya muhimu kwa watumiaji wa taarifa za fedha zilizoandaliwa ili waweze kuzielewa vizuri.

Nimeweka aya ya mausala ya msisitizo kwenye ripoti zangu kwa wakaguliwa ili kuwaeleza masuala ambayo, ingawaje yameripotiwa sahihi kabisa kwenye taarifa zao ni ya muhimu sana na ni ya msingi kwa watumiaji kuzielewa taarifa hizo. Aya hii kwa kawaida huwekwa baada ya aya ya hati ya Ukaguzi.

Kulingana na mahitaji ya Viwango vya Kimataifa vya Taasisi Kuu za Ukaguzi (ISSAIs<sup>7</sup>), mambo yafuatayo yanapelekea kuwa na aya ya masuala ya msisitizo kwenye ripoti ya ukaguzi ambayo ndiyo niliyoyatumia kupelekea aya hiyo;

- i. Uwalakini juu ya uwezo wa wakaguliwa kuendelea kutoa huduma bora ili kutimiza malengo yaliyokusudiwa,
- ii. Kutokuwa na mwendelezo (mwaka hadi mwaka) wa matumizi ya Kanuni za Uhasibu zilizokubaliwa,
- iii. Uwalakini kutokana na madai ya kisheria ambapo haijulikani matokeo ya madai hayo,

---

<sup>7</sup>ISSAI 1706: Kuweka aya ya masuala ya msisitizo na ya masuala mengine kwenye ripoti huru ya wakaguzi

- iv. Pale ambapo mkaguliwa ametumia kiwango kipya cha uandaaji hesabu kabla ya muda wake rasmi kufika, na
- v. Pale ambapo kuna kiasi kikubwa cha kutooana au kuchanganyana kati ya yaliyomo kwenye ripoti ya mwaka ya wakaguliwa na taarifa za fedha, au kati ya ufafanuzi uliopo kwenye taarifa za fedha na taarifa zenyewe za fedha ambapo yalihatiji kurekebishwa lakini uongozi wa taasisi husika haukufanya hivyo.

Kwa mwaka husika, kati ya taasisi 117 zilizokaguliwa; taasisi 54<sup>8</sup> zilipata hati zinazoridhisha zenye masuala ya msisitizo sawa na asilimia 46% ya taasisi zote. Orodha ya taasisi hizo ni kama inavyooneka kwenye kiambatisho 'B'.

### **2.2.3 Masuala mengine**

Aya ya masuala mengine imewekwa kwenye ripoti za ukaguzi ili kuwaeleza watumiaji wa taarifa za fedha mambo mengine ukiachana na yale yaliyopo kwenye taarifa za fedha zilizoandaliwa na kukagulia ambayo kwa mtizamo wangu nimeona ni ya muhimu kwa watumiaji wa taarifa hizo kuelewaukaguzi, wajibu wa wakaguzi na ripoti ya wakaguzi. Aya hii huwekwa mara tu baada ya aya ya maoni ya ukaguzi na masuala ya msisitizo kama yapo kwenye ripoti ya ukaguzi.

Kutokana na viwango vy ukaguzi vya kimataifa, mambo yafuatayo yanapelekea kuwa na aya ya mambo mengine kwenye ripoti ya ukaguzi na ndiyo yaliyotumika kuwa na aya hizo kwenye ripiti zangu za ukaguzi.

1. Endapo kumegundulika kiasi kikubwa cha udanganyifu kwenye taarifa nyingine za mwaka (other information in the annual report) ambapo ilihatiji kurekebishwa lakini uongozi wa taasisi husika haukufanya hivyo.
2. Masuala yanayohusiana na kutokuwepo na; kamati makini na zenye ufanisi za ukaguzi au kamati hizo

---

<sup>8</sup> Wizara, Idara & Wakala 24, Sekretarieti za Mikoa 6 na Balozzi 24

kutokuwepo kabisa, vitengo vya ukaguzi wa ndani kutokidhi haja au kutokuwepo kabisa na kutokuwepo vitengo vya manunuzi makini na vyeye ufanisi,

3. Hali ya kutozingatia sheria na kanuni ambazo zimeleta athari ndogo<sup>9</sup>

Kwa mwaka 2012/12, kati ya wakaguliwa 117; watano (5)<sup>10</sup> wamepata hati safi yenye masuala mengine sawa na (4%) ya wakaguliwa wote. Jedwali lifuatalo hapa chini linaonesha orodha ya wakaguliwa waliopata hati safi yenye masuala mengine.

### Jedwali 3: Orodha ya taasisi zilizopata hati safi yenye masuala mengine

Na.	Fungu	Jina la taasisi
1	16	Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali
2	65	Wizara ya Kazi
3	78	Sekretarieti ya Mkoa wa Mbeya
4	2007	Ubalozi wa Tanzania nchini Zambia
5	2032	Ubalozi wa Tanzania nchini Malasia

Chanzo: Ripoti ya CAG ya wizara husika kwa mwaka 2012/2013

#### 2.2.4 Hati yenye shaka

Aina hii ya hati hutolewa baada ya kujidhihirisha kuwa, kulingana na ushahidi wa kiukaguzi;

- i. Taarifa za fedha zilizoandaliwa zina makosa makubwa lakini siyo muhimu<sup>11</sup>, makosa hayo yakichukuliwa moja moja au kwa ujumla wake kwenye taarifa za fedha, au
- ii. Pale ambapo nimeshindwa kupata nyaraka za kutosha ili niweze kutoa hati ya Ukaguzi, na nimejidhihirisha kuwa madhara yanayoweza

---

<sup>9</sup>Angalizo: Kutozingatiwa kwa sheria na kanuni kunapelekea athari kubwa hivyo kutoa hati yenye shaka au isiyoridhisha kulingana na ukubwa wa madhara yenyewe.

<sup>10</sup>Wizara, Idara & Wakala 2, Sekretarieti 1 na Balozi 2

<sup>11</sup>Hii inamaanisha kuwa; kukwazwa kwa mawanda ya Ukaguzi au kutokukubaliana na uongozi wa taasisi kaguliwa kumejikita kwenye eneo fulani la taarifa za fedha lakini maeneo mengine ya kwenye taarifa hizo yameripotiwa kama inavyotakiwa.

kutokea kwenye taarifa za fedha kutokana na makosa ambayo sijaweza kuyagundua kutokana na ukosefu wa nyaraka hizo ni makubwa lakini sio ya muhimu.

Hii inamaanisha kuwa, kwenye taarifa zilizoandaliwa kuna aidha;

- i. Kukwazwa kwa mawanda ya ukaguzi kunakotokana aidha na uongozi wa taasisi husika au na hali ambayo ipo nje ya uwezo wa mkaguzi na endapo kukwazwa huko kuna madhara makubwa lakini sio muhimu; au
- ii. Kuna kiasi kikubwa cha kutokukubaliana na uongozi wa taasisi kaguliwa aidha kutokana na kuwa na taarifa ambazo hazijitoshelezi kwenye taarifa za fedha au kurekodi vitu kwenye taarifa za fedha kinyume na inavyotakiwa.

Kutokana na viwango vya kimataifa vya uhasibu, mambo yafuatayo yamezingatiwa kupelekea kutoa hati yenye shaka kwa wakaguliwa;

- i. Kuwepo kwa makosa makubwa ambayo sio muhimu kwenye taarifa za fedha zilizoandaliwa,
- ii. Kuwepo kwa kiasi kikubwa cha mapato na matumizi yasiyokuwa na nyaraka muhimu,
- iii. Kutokuzingatiwa kwa sheria na kanuni mbalimbali ambako kunapelekea madhara makubwa ambayo siyo muhimu kama vile;
  - Matumizi yaliyofanyika bila ya kuwa na kibali halali au matumizi ya mapato ambayo hayakuhalalishwa kutumiwa;
  - Kuwa na vitu ambavyo vilitakiwa kuripotiwa kwenye taarifa za fedha lakini havikuripotiwa,
  - Kutofuatwa kwa sheria na kanuni za manunuzi,
  - Upotevu wa bidhaa za stoo na rasilimali za kudumu,
  - Kutokuwa na rejista ya vifaa vya stoo na ile ya rasilimali za kudumu, au kuwa na vifaa vya stoo

na rasilimali za kudumu ambazo hazijarekodiwa kwenye rejista husika,

- Kufanya matumizi ambayo hayakuzaa matunda kwa taasisi husika
- Kutokufanyika kwa usuluhisho wa benki hali inayopelekea kushindwa kupata usahihi wa salio la fedha mwishoni mwa mwaka wa fedha.

Wakati natoa hati hii, pia nimetilia maanani matakwa ya ISSAI 1706<sup>12</sup>.

Kwa mwaka 2012/13, jumla ya taasisi 30<sup>13</sup> zilipata hati yenye shaka kati ta taasisi 117 zilizokaguliwa sawa na 26%. Jedwali katika **kiambatisho 'C'**lifuatalo hapa chini linaonesha orodha ya taasisi zilizopata hati yenye shaka;

#### 2.2.5 Hati isiyoridhisha

Hati hii inatolewa pale ambapo nimejidhihirisha kuwa, taarifa zilizoandaliwa na kukaguliwa zina makosa makubwa na ya muhimu, likiangaliwa kosa moja moja au kwa ujumla wake. Makosa hayo yanaweza yakawa yametokea kutokana na; kutokukubaliana na uongozi wa taasisi husika aidha kwa kuwa na taarifa ambazo hazijitoshelezi kwenye hesabu (inadequate disclosures) au kurekodi vitu kwenye taarifa za fedha kinyume na inavyotakiwa (inappropriate accounting treatment). Kutokukubaliana huko kunapelekea taarifa za fedha kupoteza uhalisia wake na hivyo kutoaminiwa kwa ujumla wake. Kwa hali hiyo mkaguzi anahitimisha kuwa taarifa zilizoandaliwa hazionyeshi hali halisi ya shughuli zilizofanywa na hivyo hazikuzingatiwa viwango vya kimataifa vya uandaaji wa taarifa hizo.

Kwa mwaka 2012/13, taasisi moja<sup>14</sup>ilipata hati isiyoridhisha kati ya taasisi 117 zilizokaguliwa sawa na 1%.

---

<sup>12</sup>Kuweka aya ya masuala ya msisitizo/na masuala mengine kwenye ripoti ya ukaguzi

<sup>13</sup>Wizara, Idara na Wakala 12, Sekretarieti 16 na balozi 2

<sup>14</sup>Ubalozi wa Tanzania Muscat

### 2.2.6 Hati Mbaya

Hati mbaya hutolewa pale ambapo nimeshindwa kupata nyaraka za kutosha wakati wa ukaguzi ili kuweza kutoa hati sahihi na nimejidhihirisha kuwa, madhara yanayoweza kutokea kutokana na mapungufu ambayo sijaweza kuyagundua yanaweza yakawa makubwa na ya muhimu sana<sup>15</sup>. Katika hali hii mkaguzi anakataa kutoa hati ya ukaguzi.

Kwa mwaka 2012/13 hesabu jumuifu za taifa zilipata hati mbaya sababu zilizopelekea kushindwa kutoa maoni ni kama zilivyobainishwa katika jedwali hapa chini:

#### Jedwali 4: Taasisi ilizopata hati mbaya na sababu zilizopelekea hati hiyo

S/N	Jina la taasisi
1.	<b>Hesabu jumuifu za taifa</b> <b>Kutoingizwa taasisi zote zilizoko chini ya himaya ya serikali katika Hesabu jumuifu za taifa</b>  Aya ya 20 inaeleza kwamba Hesabu jumuifu za taifa lazima zijumishe taasisi zote zinazomilikiwa na mkaguliwa, isipokuwa zilizotajwa aya 21. Aya 21 imeeleza kwamba taasisi amabzo hazitajumuishwa ni zenye uthibitisho kwamba umiliki wake ni wa muda mfupi na zimechukuliwa na kuhifadhiwa kwa ajili ya kuuzwa/kutolewa ndani ya kipindi cha miezi kumi na mbili tangu zilipochukuliwa na pia manajimenti inatafuta mnunuzi.  Kinyume na aya hii, hesabu jumuifu hazikujumuisha mamlaka ya serikali za mitaa na taasisi zingine za serikali zinazojiendesha kibiashara kulingana na aya 20 IPSAS 6. Sababu za kutojumuisha hesabu zote zimeelezwa kwenye tanbihi namba 2 kwamba serikali za mitaa zinandaa hesabu kwa kufuata mwongozo

<sup>15</sup>Madhara yanayoweza kutokea yatapotosha kwa ujumla wake taarifa za fedha zilizotolewa na kukaguliwa

wa kimataifa (IPSASs) wakati serikali ndio kwanza imeanza kuandaa hesabu kwa IPSAS kwa msingi usio wa taslimu.

Nimeona kwamba sababu zilizotolewa hazikidhi haja ya aya 21 IPSAS 6 na wala matakwa ya kipindi cha mpito kama ilivyo kwenye aya 21 IPSAS 6. Kwa taasisi zingine kwamba hazitakiwa kujumuishwa kwa vile zinatoa gawio kwa serikali. Hii pia ni kinyume na matakwa ya aya ya 27 ya IPSAS 6 inayoeleza bayana kwamba taasisi iliyo chini ya udhibiti wa serikali haitajumuishwa kwa sababu ya tofauti za shughuli zake na zile za wengine katika uchumi, kwa mfano, kujumuisha taasisi katika bajeti na maelezo mahususi yanatolewa katika hesabu jumuiifu kuhusu aina ya taasisi zilizo chini ya udhibiti na maelezo ya ziada katika hesabu jumuiifu kuhusu aina tofauti za kazi za taasisi.

Kwa kutojumuisha hesabu za mamlaka za serikali za mitaa na taasisi nyingine zenye udhibiti wa serikali zinazojiendesha kibiashara kunazifanya hesabu jumuiifu za taifa kutokuwa kamilifu, na hivyo kuonyesha hesabu jumuiifu zinazoishia tarehe 30 Juni 2013 kutokuwa sahihi.

**Kutumia vibaya vifungu katika kipindi cha mpito kama msingi wa kuuandaa taarifa za fedha.**

Kulingana na aya 65 na 66 ya IPSASs inayotoa kipindi cha mpito kwa taasisi zilizoko chini ya udhibiti wa serikali ambazo zimehamia na kutumia mwongozo wa kimataifa wa uhasibu (IPSASs) unaozingatia msingi usio wa taslimu kwa mara ya kwanza wenye matakwa ya kuondoa miamala katika taasisi, bakaa, maduhuli na matumizi (kama inavyojieleza aya ya 45 ya IPSAS 6) kwa kipindi cha miaka mitatu. Pamoja na hayo, aya 67 inaeleza kwamba taasisi zitaje kwamba siyo bakaa, miamala, maduhuli na matumizi yameondolewa.

Kama inavyoelezwa kwenye tanbihi namba 2, msingi wa kuandaa taarifa za hesabu jumuiifu za taifa kwa msingi wa kipindi cha mpito IPSAS 17 inayohusu mali, vifaa, mitambo ardhi na majengo(PPE) inataja kwamba seti nzima ya hesabu jumuiifu itakamilika ndani ya kipindi cha miaka mitano. Hii ni kupoteza ukweli, kwani IPSAS 17 haitoi kipindi cha mpito kuandaa hesabu jumuiifu bali inahusu mali, vifaa, mitambo ardhi na majengo(PPE).

#### **Kutokuonyesha miamala kwa usahihi**

Kulingana na aya 62(a) ya IPSAS 6, kati ya mambo mengi, hesabu jumuiifu zinatakiwa zionyesha orodha ya taasisi zote zilizoko chini ya udhibiti. Kinyume na aya hii, hesabu jumuiifu za taifa hazikuonyesha orodha nzima kwani mamlaka za serikali za mitaa na taasisi nyingi hazikuorodheshwa.

#### **Kutosuluhisha tofauti za miamala**

Ukaguzi wa taarifa za suluhisho za benki, umebaini kuwepo kwa tofauti ya Shilingi 12,724,073,618 kati ya bakaa ya benki na bakaa ya daftari la fedha. Tofauti hii haikuonyeshwa kwenye taarifa ya suluhisho za benki.

#### **Hundi zilizochacha**

Ukaguzi imebaini hundi zilizochacha za kiasi cha shilingi 168,047,718.73 katika suluhisho za benki ambazo hazijasafishwa kwenye daftari la fedha kati ya miaka miwili na miaka kumi.

#### **Mpango wa mikopo na dhamana ya kuuza bidhaa nje ya nchi**

Katika kupitia mpango wa mikopo na dhamana wa kuuza bidhaa nje tumebaini mikopo ya kiasi cha shilingi 8,129,556,449.15 iliyokaa muda mrefu ikiwa na dhamana ya serikali ambayo wahusika wameshindwa kulipa kwa sababu ya kukosa uwezo wa kulipa mkopo; hata hivyo serikali haijatekeleza wajibu wake licha ya kukumbushwa mara nyingi na taasisi za fedha.



### **2.3 Mwelekeo wa Hati za Ukaguzi**

Chati zifuatazo hapa chini zinaonesha mwelekeo wa hati za Ukaguzi kwa miaka minne mfululizo iliyopita. Pia zimechambua mwelekeo wa hati za Ukaguzi kwa miaka miwili mfululizo iliyopita kwa; Wizara, Idara na Wakala, Sekretarieti za Mikoa na Ofisi za Balizi

## Jedwali 5: Mwelekeo wa Hati za Ukaguzi

Mwelekeo wa hati za ukaguzi kwa miaka minne mfululizo iliyopita																								
	2009/2010					Jumla	2010/2011					Jumla	2011/2012					Jumla	2012/2013					Jumla
	Hati safi	Hati safi yenye masuala ya msisitizo/masuala mengine	Hati yenye shaka	Hati isiyoridhisha	Hati mbaya		Hati safi	Hati safi yenye masuala ya msisitizo/masuala mengine	Hati yenye shaka	Hati isiyoridhisha	Hati mbaya		Hati safi	Hati safi yenye masuala ya msisitizo/masuala mengine	Hati yenye shaka	Hati isiyoridhisha	Hati mbaya		Hati safi	Hati safi yenye masuala ya msisitizo/masuala mengine	Hati yenye shaka	Hati isiyoridhisha	Hati mbaya	
Wizara Idara na Wakala	7	30	12	1	0	50	13	35	6	0	0	54	28	24	3	0	0	55	21	27	11	0	1	60
Sekretarieti za Mikoa	3	9	7	1	1	21	0	19	2	0	0	21	7	14	0	0	0	21	2	7	16	0	0	25
Ofisi za Baloz	8	21	2	0	0	31	3	29	0	0	0	32	11	19	2	0	0	32	3	26	2	1	0	32
<b>Jumla</b>	<b>18</b>	<b>60</b>	<b>21</b>	<b>2</b>	<b>1</b>	<b>102</b>	<b>16</b>	<b>83</b>	<b>8</b>	<b>0</b>	<b>0</b>	<b>107</b>	<b>46</b>	<b>57</b>	<b>5</b>	<b>0</b>	<b>0</b>	<b>108</b>	<b>26</b>	<b>59</b>	<b>29</b>	<b>1</b>	<b>1</b>	<b>117</b>
<b>Jumla %</b>	<b>18%</b>	<b>59%</b>	<b>21%</b>	<b>2%</b>	<b>1%</b>	<b>100%</b>	<b>15%</b>	<b>78%</b>	<b>7%</b>	<b>0%</b>	<b>0%</b>	<b>100%</b>	<b>43%</b>	<b>53%</b>	<b>5%</b>	<b>0%</b>	<b>0%</b>	<b>100%</b>	<b>23%</b>	<b>50%</b>	<b>25%</b>	<b>1%</b>	<b>1%</b>	<b>100%</b>
%Wizara Idara na Wakala	7%	29%	12%	1%	0%		12%	33%	6%	0%	0%		26%	22%	3%	0%	0%		18%	23%	9%	0%	1%	
% Sekretarieti za Mikoa	3%	9%	7%	1%	1%		0%	18%	2%	0%	0%		6%	13%	0%	0%	0%		2%	6%	14%	0%	0%	
%Ofisi za Baloz	8%	21%	2%	0%	0%		3%	27%	0%	0%	0%		10%	18%	2%	0%	0%		3%	22%	2%	1%	0%	

## Kielelezo Na.2: Mwelekeo wa hati za ukaguzi kwa miaka minne mfululizo



## **2.4 Taasisi zilizokaguliwa na kupata; hati yenye shaka na hati isiyoridhisha na sababu za kupewa hati**

Kama ilivyoenezwa mwanzoni mwa sura hii, jumla ya taasisi 117 za serikali kuu zilikaguliwa kwa mwaka 2012/2013. Kati ya taasisi hizo, taasisi 30 ziliporomoka kwa kupata hati yenye shaka ukilinganisha na taasisi tano zilizopata mwaka jana ambapo ni kama mara sita. Pia, taasisi moja (1) imepata hati isiyoridhisha ambapo mwaka jana hakukuwa na taasisi iliyopata hati isiyoridhisha.

Kwa ujumla, matokeo haya ya Ukaguzi sio mazuri kwani inaonesha kuwa kuna maeneo kwenye taarifa za fedha zilizoandaliwa na kukaguliwa ambayo yalikuwa hayatoi picha halisi ya yaliyofanywa na taasisi hizo na hivyo taarifa hizo hazikukidhi kikamilifu matakwa ya viwango vya kimataifa vya uandaaji wa taarifa hizo.

Kuporomoka huku kunaweza kukawa kumechangiwa na haya yafuatayo;

1. Kuhamia kwenye mfumo wa uandaaji wa taarifa za fedha kwa kutumia viwango vya kimataifa vya uhasibu ambapo muamala na matukio mengine hutambulika na kuonyeshwa pale ambapo umetokea na sio hadi fedha zipokelewe au kulipwa (IPSAS accrual basis of accounting). Hii imechangia kwa kiasi kikubwa kwani kulikuwa na miamala iliyohusu taarifa za fedha ambazo hazikuonyeshwa ipasavyo hasa kwenye maeneo haya yafuatayo;

- i. Gharama zilizotumika ndani ya mwaka husika ambapo malipo yake hayakufanyika, hayakuonyeshwa na kuingizwa kwenye hesabu,
- ii. Baka la mwisho la vifaa ambavyo havikuwa vimetumika vilionyeshwa kama matumizi kwenye taarifa za fedha na hivyo kufanya kiasi cha matumizi kuonekana kikubwa kuliko hali halisi,

- iii. Taarifa ya mtiririko wa fedha kutoandaliwa ipasavyo. Kwa mfano fedha zote zilizopokelewa (za matumizi ya kawaida na zile za matumizi ya maendeleo) kuonyeshwa kama fedha kutoka kwenye shughuli za kawaida (cash flows from operating activities) na hivyo kufanya sehemu ya fedha zilizopokelewa kwa ajili ya kuongeza mitaji (cash flows from financing activities) kutoonyeshwa kwenye taarifa hizo.
  - iv. Thamani ya mali zisizoshikika (intangible assets) kujumuisha mchanganuo ambao haukuwa na vigezo vya kuitwa hivyo.
  - v. Kutoandaliwa kwa taarifa za usuluhisho wa benki hali iliyopelekea wakaguzi kushindwa kuthibitisha usahihi wa bakaa ya mwisho ya fedha zilizoonyeshwa kwenye taarifa za fedha.
2. Kasoro zilizotokana na mfumo funganifu wa taarifa za fedha (IFMS) ambapo muundo wa mfumo huo uliokuwa unatumika kabla serikali haijahamia kwenye IPSAS kwa msingi usio taslimu ndio huo huo unaotumika baada ya kuhamia. Matokeo yake, baadhi ya miamala ya kahasibu iliyotakiwa ifanyike kwenye mfumo baada ya kuhamia imeshindwa kufanyika kwenye mfumo na hivyo kutokuwa sehemu ya taarifa zilizoandaliwa. Kwa mfano, masurufu yalikuwa yanalipwa moja kwa moja kama matumizi pale yanapotolewa na hivyo masurufu ambayo hayajarejeshwa hayakuwa sehemu ya wadaiwa wa taasisi husika. Pia madeni na malipo yaliyofanyika kabla huduma au bidhaa hazijapokelewa havikuingia kwenye mfumo, n.k.
3. Mafunzo kutotolewa kikamilifu kwenye idara zote za wakaguliwa ikiwepo idara za fedha ambazo zinakusika moja kwa moja kwenye kuandaa taarifa za fedha. Pia idara nyingine ambazo zinachangia kwa kiasi kikubwa kuhifadhi taarifa mbalimbali muhimu ambazo zinatumiwa kuanda taarifa zinazoendana na viwango vinavyotakiwa.

4. Kutokufuatwa kikamilifu mpango wa jinsi ya kutekeleza maandalizi ya kuhamia kwenye 'IPSAS accrual' ulioandaliwa na Wizara ya fedha. Kwa mfano, Wizara ya fedha ilitakiwa iwe imeboresha sera za uhasibu, mwongozo wa uhasibu na kuandaa kielezo (template) cha hesabu kufikia Machi 2012. Kufikia sasa maboresho hayo bado hayajakamilika. Pia, kulikuwa na changamoto ya kubainisha madai ya likizo ya mwaka na malipo mengine yanayohusu ajira ambapo ni wakaguliwa wachache sana ndio waliojitahidi kuzionyesha kwenye hesabu zao.

Undani wa taasisi zilizokaguliwa na kupata hati yenye shaka na hati isiyoridhisha na sababu zilizopelekea hati hizo ni kama inavyooneka kwenye **Jedwali la '6'**: Orodha ya taasisi zilizopata hati yenye shaka na sababu zilizopelekea hati hiyo:

**Jedwali 6: Wizara, Idara na Wakala zilizopata hati yenye mashaka na sababu zilizopelekea**

<b>Na.</b>	<b>Jina la Taasisi iliyokaguliwa</b>
<b>1</b>	<b>Kitengo cha Zimamoto</b>
	<b>Matumizi kuripotiwa pungufu kwa kiasi cha Sh.500,162,825</b> Katika kipindi cha mwaka 2012/13; Kitengo cha Zimamoto kilinunua bidha na huduma za kiasi cha shilingi 500,162,825 ambapo fedha hizo hazikuwa zimelipwa. Hata hivyo kiasi hiki hakikuripotiwa kwenye taarifa za fedha kama matumizi na hivyo kusababisha matumizi yaliyoripotiwa kuwa pungufu kwa kiasi hicho.
<b>2</b>	<b>Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknologia</b>
	<b>Mapungufu katika taarifa ya Mali za kudumu kiasi cha Sh.737,827,680</b> Kufikia tarehe 30 Juni 2013; wizara iliripoti mali zisizoshikika za kiasi cha shilingi 737,827,680. Maelezo ya ziada ya mali hizo yalionesha mchanganuo wa mali hizo hauna vigezo vya kuitwa

Na.	Jina la Taasisi iliyokaguliwa
	<p>mali za kudumu kulingana na IPSAS 31 kwani vilikuwa ni ripoti na nyaraka mbalimbali na hivyo kusababisha mchanganuo wa mali zisizoshikika kutokuwa sahihi.</p> <p><b>Mapungufu katika taarifa ya Matumizi kiasi cha Sh.162,073,744</b> Kwa mwaka 2012/13; wizara ilikuwa na matumizi ya shilingi 162,073,744 ambapo hayakuwa yamelipwa. Kiasi hiki hakikuingizwa kama matumizi kwenye taarifa za fedha na hivyo matumizi yaliyoripotiwa yalikuwa upungufu kwa kiasi hicho na hivyo kupelekea wizara kutokuwa na faida wala upungufu/nakisi. Kama matumizi hayo yangeingizwa yangesababisha wizara kubaki na nakisi.</p> <p><b>Kutokuandaa taarifa za usuluhisho wa benki</b> Wizara haikufanya usuluhisho wa benki kinyume na matakwa ya kanuni ya 162 ya fedha za umma ya mwaka 2001. Hii ilituwia vigumu kuthibitisha usahihi wa kiasi cha Shilingi 23,389,759 kilichoonyeshwa kwenye mizania ya hesabu na taarifa ya mtiririko wa fedha kwa mwaka ulioishia Juni 2013.</p>
<b>3</b>	<b>Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika</b>
	<p><b>Mapungufu katika taarifa ya mali za kudumu kiasi cha Sh.6,374,281,432</b> Kufikia tarehe 30 Juni 2013; wizara iliripoti mali zisizoshikika za kiasi cha shilingi 6,374,281,432. Maelezo ya ziada kuhusu mali hizo yalionesha mchanganuo ambao haukukidhi vigezo vya kuitwa mali za kudumu kulingana na IPSAS 31 kwani vilikuwa ni ripoti na nyaraka nyingine na hivyo kusababisha taarifa ya mali kutokuwa sahihi.</p> <p><b>Kutokuandaa taarifa za usuluhisho wa benki</b> Wizara kilimo haikufanya usuluhisho wa benki</p>

Na.	Jina la Taasisi iliyokaguliwa
	<p>kinyume na matakwa ya kanuni ya 162 ya fedha za umma ya mwaka 2001. Hii ilituwia vigumu kuthibitisha usahihi wa kiasi cha Shilingi 5,648,305,420 kilichonyeshwa kwenye mizania ya hesabu na taarifa ya mtiririko wa fedha kwa mwaka ulioishia Juni 2013</p> <p><b>Kukosekana kwa nyaraka za madeni ya wizara/wadai, shilingi 2,162,343,978</b>  Hatukuweza kuthibitisha usahihi na uhalali wa madeni ya wizara ya kiasi cha shilingi 2,162,343,978 kati ya deni lote lililoonyeshwa la kiasi cha shilingi 44,739,685,558.75 kutokana na madeni hayo kutokuwa na nyaraka za kuyathibitisha.</p>
<b>4</b>	<b>Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi</b>
	<p><b>Kukosekana kwa nyaraka za madeni ya wizara Sh.344,799,155</b>  Madai ya watumishi yanayofikia kiasi cha Sh.344,799,155 hayakuwa na nyaraka muhimu za kuthibitisha usahihi na uhalali wake.</p> <p><b>Kutothibitisha mapokezi ya kiasi cha Sh.752,736,291</b>  Wizara iliamisha kiasi cha Sh.10,091,081,130 kwenda Chuo cha Utafiti wa Uvuvi na Wakala wa Maabara ya Mifugo Tanzania. Kati ya kiasi hicho; kiasi cha Sh.752,736,291 hakuna stakabadhi ya kukiri mapokezi.</p> <p><b>Salio la akaunti ya amana kutokuwa na nyaraka, Sh.756,274,215</b>  Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2013 kiasi cha Sh.756,274,215 kimeonyeshwa kama salio kwenye akaunti ya amana. Hata hivyo kiasi hicho hakikuwa na nyaraka za kuthibitisha usahihi wake.</p>
<b>5</b>	<b>Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania</b>

Na.	Jina la Taasisi iliyokaguliwa
	<p><b>Vifaa ambavyo havikutumika vimeonyeshwa kama matumizi, Sh.222,013,632</b>  Vifaa vya thamani ya Sh.222,013,632 ambavyo havikutumika kufikia tarehe 30 June 2013 vimeonyeshwa kwenye taarifa ya fedha kama matumizi ambapo ni kinyume na mahitaji ya aya ya 44 ya IPSAS 12.</p> <p><b>Malipo yenye nyaraka pungufu Sh. 79,607,500</b>  Malipo ya kiasi cha Sh.79,607,500 yalikuwa na nyaraka kama vile; risiti ya kukiri mapokezi ya fedha zilizotumwa na nyaraka za kurejesha masurufu. Kukosekana kwa nyaraka hizi ni vigumu kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.</p> <p><b>Taarifa zilizohitilafiana</b></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Kulikuwa na kuhitilafiana kati ya kiasi cha fedha zilizopokelewa kutoka hazina ambapo taarifa ya ufafanuzi kwenye taarifa za fedha (commentary) kwenye ukurasa wa 14 na taarifa ya fedha zilizopokelewa (statement of exchequer received) ukurasa wa 56 zilionesha kiasi cha Sh.9,167,936,780 kama fedha iliyopokelewa wakati 'statement of vote account', ukurasa wa 47 unaonyesha kiasi kilichopokelewa kuwa ni Sh.9,691,811,644, na hivyo kusababisha tofauti ya kiasi cha Sh.523,874,864,</li> <li>• Taarifa ya fedha inaonyesha kuwa Tume iliiza magari chakavu matatu (3) kwa kiasi cha Sh.31,800,000 na samani kwa Sh.4, 231,000. Ilibainika kuwa magari yaliyouzwa hayakutolea kwenye jedwali la mwenendo wa mali za kudumu na hivyo kiasi taarifa inaonyesha mali zaidi ya inavyostahili. Vile vile, kiasi cha Sh.127,787,101 kilitolewa kwenye samani badala ya Sh.4,231,000 ambacho ndicho kiasi kilichoonyeshwa katika maelezo.</li> </ul>

Na.	Jina la Taasisi iliyokaguliwa
6	<b>Wizara ya Mambo ya Ndani</b>
	<p><b>Kukosekana kwa nyaraka za madeni ya wizara/wadai shilingi Sh.84,295,595</b>  Wizara ilionyesha kwenye taarifa zake kuwa ilikuwa inadaiwa kiasi cha Sh.84,295,595. Hata hivyo hatukuweza kuthibitisha usahihi na uhalali wake kwa kuwa hakukuwa na nyaraka za kuthibitisha kama vile hati za madai, hati za kuleta vifaa, hati zakutolea vifaa na hati ya kupokelea vifaa.</p> <p><b>Kushindwa kuthibitisha manunuzi na matumizi ya mafuta ya Sh 83,000,000</b>  Wakati wa ukaguzi wa vifaa, ilibaini kuwa, kiasi cha Sh.83,000,000 kililipwa na Wizara kwa GPSA kwa ajili ya manunuzi ya mafuta. Hata hivyo, hatukuweza kuthibitisha manunuzi hayo na jinsi mafuta hayo yalivyotumika kutokana na kukosekana kwa nyaraka.</p>
7	<b>Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi</b>
	<p><b>Mapungufu katika taarifa ya mali za kudumu kiasi cha Sh.1,582,518,051</b>  Kufikia tarehe 30 Juni 2013; wizara iliripoti mali zisizoshikika za kiasi cha shilingi 1,582,518,051. Maelezo ya ziada kuhusu mali hizo yalionesha mchanganuo ambao haukukidhi vigezo vya kuitwa mali za kudumu kulingana na IPSAS 31 kwani vilikuwa ni ripoti na nyaraka nyingine na hivyo kusababisha taarifa ya mali kutokuwa sahihi.</p> <p><b>Mapungufu katika taarifa za mtiririko wa fedha</b>  Kiasi cha Sh.1,451,862,356 kilipokelewa na wizara kwa ajili ya mali za kudumu ambazo ni mtaji. Kiasi hicho hakikuonyeshwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha kwa ajili ya kuongeza mtaji (cash flows</p>

Na.	Jina la Taasisi iliyokaguliwa
	<p>from financing activities).</p> <p><b>Kutokuandaa taarifa za usuluhisho wa benki</b> Wizara haikufanya usuluhisho wa benki kinyume na mahitaji ya kanuni ya 162 ya fedha za umma ya mwaka 2001. Hii ilituwia vigumu kuthibitisha usahihi wa kiasi cha Shilingi 5,734,804,409 kilichoripotia kwenye mizania ya hesabu na taarifa ya mtiririko wa fedha kwa mwaka ulioishia Juni 2013.</p> <p><b>Utata uliojitokeza kwenye fidia ya kiwanja Na. 2003, kitalu cha 1 eneo la Kurasini at Kurasini chenye thamani ya Sh.3,242,000,000</b> Wizara ilinua kumfidia mmiliki wa kiwanja Na.12 kitalu Na.65 kilichopo Kariakoo kwenye kiwanja Na. 65 na kiwanja na 2009, kitalu Na.2 chenye ukubwa wa 371 eneo la mraba lenye thamani ya Sh.970,000,000 kilichopo maeneo ya Kurasini. Bila ya kuwepo na maelezo ya ziada, lengo hili lilibadilishwa na badala yake mmiliki huyo alifidiwa kiwanja Na. 2003 kwenye kitalu Na. 1 chenye ukubwa wa 131,000 eneo la mraba chenye dhamani ya Sh.3,240,000,000 kilichopo maeneo ya viwanda.</p> <p>Pia, iligundulika kuwa taarifa zilizokuwa zimetolewa kwa Wizara kuhusu Kiwanja Na.12 kitalu Na.65 zilikuwa za uongo kwani ukubwa halisi wa kiwanja hicho ni eneo la mraba 371 na sio 750 iliyokuwa imedaiwa.</p> <p><b>Hati za kumiliki ardhi zilizotolewa lakini kutokuingizwa kwenye mfumo wa utunzaji kumbukumbu za ardhi wa Wizara.</b> Ilibainika kuwa, kati ya hati 263,000 za kumiliki ardhi zilizokuwa zimetolewa kwa kanda ya Mashariki, ni kiasi cha hati 22,740 tu sawa na asilimia 9 ndicho kilikuwa kimeingizwa kwenye</p>

Na.	Jina la Taasisi iliyokaguliwa
	mfumo wa utunzaji kumbukumbu za ardhi wa Wizara. Vile vile viwanja 59,660 kati ya 187,896 vilivyokuwa vimefanyiwa tathmini kwenye jiji la DSM na kuidhinishwa na mkurugenzi wa ramani na utafiti havikuwa vimeingizwa kwenye mfumo huo. Matokeo yake, hatukuweza kugundua kiasi cha kodi ya ardhi kilichotakiwa kiwe kimekusanya ambacho hakikukusanywa.
8	<b>Ofisi ya Waziri Mkuu</b>
	<p><b>Mapungufu ya kuandaa taarifa za mtiririko wa fedha</b> Kiasi cha Sh.2,750,989,763 kilipokelewa na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ajili ya kununua mali za kudumu. Kiasi hicho hakikuonyeshwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha kama fedha iliyopokelewea kwa ajili ya kuongeza mtaji (cash flows from financing activities) kinyume na mahitaji ya aya ya 18 ya IPSAS 2.</p> <p><b>Fedha zilizolipwa zaidi kwa mkandarasi Sh.25,947,276</b> Ofisi ya Waziri Mkuu ilimlipa mkandarasi Stefnat Engineering and Technical Services Ltd kiasi cha Sh.58,902,066 kama malipo ya kandarasi aliyopewa ya kukarabati jengo lililopo Oyster bay. Kiasi hiki ni zaidi ya kilichotakiwa kulipwa cha Sh.32,954,790 kama kilivyoonyesha kwenye ripoti ya tathmini ya mkataba kwa kiasi cha Sh.25,947,276.</p>
9	<b>Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii</b>
	<p><b>Vocha za malipo kutokuwa na nyaraka Sh.889,209,329</b> Vocha za malipo zilizokuwa na thaman ya Sh.889,209,329 zilikuwa hazina nyaraka muhimu za kutuwezesha kuthibitisha uhalali wa malipo yaliyofanyika kinyume na mahitaji ya kanuni ya 95 (4) ya fedha za umma.</p>

Na.	Jina la Taasisi iliyokaguliwa
	<p><b>Malipo ya matibabu kwenye ofisi za balozi kutokuwa na nyaraka, Sh.500,114,305</b> Kiasi cha Sh.500, 114,304 kilitumwa kwenye ofisi mbalimbali za balozi kwa ajili ya matibabu lakini hatukuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo kwa kuwa hayakuwa na nyaraka za kutuwezesha kufanya hivyo.</p> <p><b>Mishahara iliyolipwa kwa wafanyakazi waliokwisha kustaafu Sh.87,157,948</b> Kiasi cha Sh.87,157,948 kililipwa kama mishahara kwa watumishi ambao walisha kustaafu kinyume na kanuni za kudumu za utumishi.</p>
10	<b>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi</b>
	<p><b>Mapungufu katika kuandaa taarifa za mtiririko wa fedha</b> Kiasi cha Sh.60,553,424,907 kilipokelewa na Wizara kwa ajili ya kununua au ketengeneza mali za kudumu. Hata hivyo, kiasi hicho hakikuonyeshwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha kama fedha iliyopokelewea kwa ajili ya kuongeza mtaji (cash flows from financing activities) kinyume na mahitaji ya aya ya 18 ya IPSAS 2</p> <p><b>Mapungufu katika taarifa ya maduhuli Sh.7,978,228,228,186</b> Wizara ya Elimu ilikusanya kiasi cha Sh.7,991,535,515 kama inavyoonekana kwenye aya ya 10 na 11 kwenye taarifa za fedha. Hata hivyo, kiasi kilichoonekana kwenye taarifa ya utendaji wa fedha (statement of financial performance) kilikuwa ni Sh.13,307,329 ambapo ni pungufu kwa Sh. 7,978,228,186.</p> <p><b>Mapungufu katika mali za muda mfupi kiasi cha Sh.1,641,690,000</b> Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ililipa kiasi</p>

Na.	Jina la Taasisi iliyokaguliwa
	<p>cha \$1,000,000 sawa na Sh.1,641,690,000 kwa Wizara ya Elimu CUBA kwa ajili ya usambazaji wa vifaa vya kufundishia. Kufikia Januari, 2014 vifaa hivi vilikuwa bado havijawasilishwa Wizarani. Hata hivyo, malipo ambayo yalikuwa yameshafanyika kabla ya vifaa hivyo kusambazwa hayakuonyeshwa kwenye mizania ya hesabu kama mali za muda mfupi (current assets).</p> <p><b>Bakaa la fedha taslim ambalo halikufanyiwa usuluhisho, Sh.692,955,176</b> Takwimu za tangu mwaka 2008 kati ya kumbukumbu za Wizaya ya Elimu na kumbukumbu za amana za Hazina zimeonyesha kuwa kufikia June 2013 kulikuwa na kiasi cha Sh.692,955,176 ambapo ni mapato yaliyokuwa kwenye daftari la fedha ya amana ya Wizara ambayo hayakuwemo kwenye kumbukumbu za Hazina. Vile vile, usuluhisho wa benki hesabu za majumuisho wa akaunti ya amana kwa mwaka 2012/13 haukutolewa na Hazina kwa ajili ya ukaguzi</p> <p><b>Fedha zilizohamishwa kwenda kwenye taasisi nyingine kuonyeshwa kama mali za kudumu (PPE), Sh.26,797,695,648</b> Wizara iliamisha kiasi cha Sh. 26,797,695,648 kwenda kwenye taasisi mbalimbali zilizoko chini yake ambapo kiasi hicho kilionyesha kama mali za kudumu kwenye mizania ya hesabu. Hii imepelekea mali hizo kuonyeshwa taarifa ya hesabu zaidi ya hali halisi.</p> <p><b>Mapungufu katika taarifa ya Mali zisizoshikika kiasi cha Sh.11,978,566,813</b> Kufikia tarehe 30 Juni 2013; wizara ilionyesha mali zisizoshikika za kiasi cha Sh.11,978,566,813. Maelezo ya ziada ya mali hizo yalionyesha kuwa hazikuwa na vigezo vya kuitwa mali za kudumu kulingana na IPSAS 31 na hivyo kusababisha</p>

Na.	Jina la Taasisi iliyokaguliwa
	<p>kuonyeshwa kimakosa.</p> <p><b>Gharama za mafunzo kuonyeshwa zaidi kwa kiasi cha Sh.16,369,208,367</b>  Kwa mwaka 2012/13, Wizara ilionyesha kiasi cha Sh. 25,098,228,598 kama gharama za mafunzo. Wakati wa ukaguzi ilibainika kuwa gharama hizo zilikuwa ni kiasi cha Sh. 16,369,208,367 ambazo zilikuwa ni fedha zilizopelekwa kwenye Taasisi za elimu ya juu na hivyo kupelekea gharama za mafunzo zilizoripotiwa kuwa zaidi kwa kiasi hicho.</p> <p><b>Hati zenye nyaraka pungufu Sh.2,637,856,858</b>  Hati zenye malipo ya kiasi cha Sh.2,637,856,858 hazikuwa na nyaraka muhimu za kutuwezesha kuthibitisha uhalali wa malipo yaliyofanyika kinyume na kanuni ya 95 (4) kanuni za fedha za umma ya mwaka 2001.</p>
11	<p><b>Idara ya Huduma za Magereza</b></p> <p><b>Kutokuwasilishwa kwa mikataba ya ujenzi wa majengo na ununuzi wa magari kutokana na mihadi iliyokuwepo ya Sh.1,542,000,000</b>  Kufikia tarehe 30 Juni 2013, Idara ya Magereza ilikuwa na mihadi ya Sh.1,542,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa majengo na manunuzi ya magari ambapo kiasi cha Sh.242,000,000 kilikuwa ni kwa ajili ya ujenzi wa majengo na Sh.1,300,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa magari. Hata hivyo mikataba inayohusu mihadi hizo haikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi na hivyo hatukuweza kuthibitisha; uwepo, uhalali na usahihi wa mihadi hizo.</p> <p><b>Matumizi yaliyofanyika kwa mwaka 2012/13 kutokuingizwa kwenye taarifa za fedha; Sh.19,020,339,744</b>  Ilibainika kuwa, kwa mwaka 2012/13, Idara ya Magereza ilifanya matumizi ya Sh.19,020,339,744 ambapo kufikia mwishoni mwa mwaka huo,</p>

Na.	Jina la Taasisi iliyokaguliwa
	<p>hayakuwa yamelipwa. Kinyume na aya ya saba (7) ya IPSAS 1, matumizi hayo hayakuizingizwa kwenye taarifa za fedha zilizoandaliwa na hivyo kupelekea Idara kutoonyesha faida wala hasara. Kama matumizi hayo yangeonyeshwa kungekuwa na upungufu kwa kiasi hicho.</p> <p><b>Malipo yenye nyaraka pungufu Sh.557,243,558</b> Idara ya Magereza ilifanya malipo ya Sh.557,243,558 kwa watoa huduma mbalimbali; makao makuu na ofisi za mikoa. Hata hivyo ilibainika kuwa, malipo hayo hayakuwa na nyaraka za kutosha kama vile; ristiti za kukiri mapokezi ya fedha, risiti za kupokelea fedha, hati za madai, n.k kinyume na kanuni ya 95 (4) ya Kanuni za Fedha za Umma za umma ya mwaka 2001.</p> <p><b>Kukosekana kwa hati za madai za Sh.126,090,620</b> Wakati wa ukaguzi, hati za madai za Sh.126,090,620 za magereza mkoani Kilimanjaro hazikuwasilishwa na hivyo hatukuweza kuthibitisha uhalali na usahihi wa malipo yaliyofanyika kwenye hati hizo.</p>
12	<b>Deni la Taifa</b>
	<p><b>Kutokufanyika kwa tathmini ya mfuko wa mafao ya uzeeni</b> Ukaguzi wa mafao ya wastaafu, ulibaini kuwa tathmini ya mfuko wa mafao ya uzeeni kwa watumishi wa umma yanayolipiwa kupitia katika mfuko mkuu wa serikali haikufanyika. Hii ni kinyume na IPSAS 25 inayotaka tathmini hiyo kufanyika ili kubaini madai ya mwanzo wa mafao hayo kufuatia kuanza kutumika kwa mfumo wa IPSAS</p>

Na.	Jina la Taasisi iliyokaguliwa
	<p><b>Kuwepo kwa hundi za muda mrefu zilizochacha za Sh.146,173,387,027</b>            Ukaguzi wa taarifa za fedha ulibaini kuwepo kwa hundi zilizochacha za Sh.146,173,387,027 ambazo hazikufanyiwa marekebisho kwenye taarifa hizo za fedha kwa miaka kumi na mbili(12) sasa. Hundi hizo zililipwa kutoka kwenye; akaunti ya deni la taifa, akaunti ya amana na akaunti ya mfuko mkuu wa serikali.</p>

### Sekretarieti za Mikoa

Na.	Jina la Sekretarieti na mambo yaliyopelekea kupata hati yenye mashaka
1	<p><b>Sekretarieti ya mkoa wa Katavi</b></p>
	<p><b>Mapungufu katika taarifa ya matumizi Sh.100,333,200</b>            Kwa mwaka 2012/13, Sekretarieti iliingia matumizi ya Sh.100,333,200 kama posho ya kukaimu ambapo ilikuwa haijalipwa kufikia mwisho wa mwaka. Hata hivyo, kiasi hicho hakikuonyeshwa kama matumizi kwenye taarifa ya utendaji wa kifedha, na kwa hali hiyo, matumizi yalikuwa pungufu kwa kiasi hicho.</p> <p><b>Matumizi ya matengenezo ya gari ambayo hayakuwa na tija, Sh.9,905,321</b>            Kiasi cha Sh.9,905,321 kililipwa na Sekretarieti kwa ajili ya matengenezo ya gari namba DFP 8524 Toyota Hilux D4D lililokuwa limepata ajali licha ya kuwa gari hilo lilikuwa na bima ambapo ingetumika kulitengeneza.</p> <p><b>Kukosekana kwa maelezo katika marekebisho ya mtaji Sh.1,244,973,625</b>            Kwa mwaka 2012/13, Sekretarieti ya mkoa ilionyesha kiasi cha Sh.1,244,973,624.71 kama marekebisho ya mtaji wa wananchi (taxpayers fund/equity). Hatukuweza kudhibitisha usahihi na uhalali wake kwa kuwa</p>

	<p>nyaraka za kufanya hivyo hazikuwepo kwa ajili ya ukaguzi.</p> <p><b>Kutokuandaa taarifa za usuluhisho wa benki</b>          Sekretarieti haikufanya usuluhisho wa benki kinyume na mahitaji ya kanuni ya 162 ya fedha za umma ya mwaka 2001. Hii ilituwia vigumu kuthibitisha usahihi wa kiasi cha Shilingi 59,381,779.59 kilichoripotia kwenye mizania ya hesabu na taarifa ya mtiririko wa fedha kwa mwaka ulioishia Juni 2013.</p>
2	<p><b>Sekretarieti ya Mkoa wa Njombe</b></p>
	<p><b>Malipo yenye nyaraka pungufu Sh.9,030,000</b>          Malipo ya kiasi cha Sh. 9,030,000 hayakuwea kuthibitishwa usahihi na uhalali wake kwa kutokuwa na nyaraka za kutosha.</p> <p><b>Matumizi yaliyofanyika kwa mwaka 2012/13 kutokuingizwa kwenye taarifa za fedha; Shs. 164,424,716</b>          Ilibainika kuwa, kulikuwa kuna matumizi ya Shs.164,424,716 yaliyofanyika kwa mwaka 2012/13, lakini matumizi hayo hayakuingizwa kwenye taarifa za fedha zilizoandaliwa kinyume na mahitaji ya aya ya saba (7) ya IPSAS 1. Hii imepelekea matumizi yaliyoonyeshwa kuwa pungufu kwa kiasi hicho.</p> <p><b>Kutokuandaa taarifa za usuluhisho wa benki</b>          Sekretarieti haikufanya usuluhisho wa benki kinyume na mahitaji ya kanuni ya 162 ya fedha za umma ya mwaka 2001. Hii ilituwia vigumu kuthibitisha usahihi wa kiasi cha Shs.49,180,305 kilichoonyeshwa kwenye mizania ya hesabu na taarifa ya mtiririko wa fedha kwa mwaka ulioishia Juni 2013.</p>

	<p><b>Mapungufu katika kuandaa taarifa za mtiririko wa fedha</b>  Kiasi cha Sh.180,122,269 kilipokelewa na Sekretarieti ya Mkoa kwa ajili ya kununua mali za kudumu. Hata hivyo, kiasi hicho hakikuonyeshwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha kama fedha iliyopokelewea kwa ajili ya kuongeza mtaji (cash flows from financing activities) kinyume na mahitaji ya aya ya 18 ya IPSAS 2.</p>
<b>3</b>	<p><b>Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga</b></p> <p><b>Mapungufu katika taarifa ya mali zisizoshikika Sh.36,880,000</b>  Kufikia tarehe 30 Juni 2013; sekretarieti iliripoti mali zisizoshikika za kiasi cha Sh.36,880,000. Maelezo ya ziada ya mali hizo yalionesha kuwa mchanganuo wa mali hizo haukuwa na vigezo vya kuitwa mali zisizoshikika kulingana na IPSAS 31 na hivyo kusababisha kilichoonyeshwa kutokuwa sahihi.</p> <p><b>Mapungufu katika taarifa ya matumizi Sh.1,139,615,661.39</b>  Ilibainika kuwa, kulikuwa na matumizi ya Sh.1,139,615,661.39 yaliyofanyika kufikia mwishoni mwa mwaka yalikuwa hayajalipwa. Kiasi hicho hakikuingizwa kwenye taarifa za fedha zilizoandaliwa kama matumizi kinyume na mahitaji ya aya ya saba (7) ya IPSAS 1. Hii imepelekea matumizi yaliyoonyeshwa kuwa pungufu kwa kiasi hicho.</p> <p><b>Kutokuandaa taarifa za usuluhisho za benki</b>  Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga haikufanya usuluhisho wa benki kinyume na mahitaji ya kanuni ya 162 ya fedha za umma ya mwaka 2001. Hii ilituwia vigumu kuthibitisha usahihi wa kiasi cha Sh.310,789,801.65 kilichoonyeshwa kwenye mizania ya hesabu na taarifa ya mtiririko wa fedha kwa mwaka ulioishia Juni 2013.</p>

	<p><b>Mapungufu katika kuandaa taarifa za mtiririko wa fedha</b> Kiasi cha Sh.63,972,465 kilipokelewa na Sekretarieti ya Mkoa kwa ajili ya kununua mali za kudumu. Hata hivyo, kiasi hicho hakikuonyeshwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha iliyopokelewea kwa ajili ya kuongeza mtaji (cash flows from financing activities) kinyume na mahitaji ya aya ya 18 ya IPSAS 2.</p> <p><b>Fedha za bohari kuu ya madawa</b> Wizara ya Afya na Usitawi wa Jamii ilipeleka kiasi cha Sh.260,036,084 bohari kuu ya madawa kwa ajili ya kununua madawa pamoja na vifaa vingine vya Hospitali ya mkoa wa Tanga. Kiasi hicho hakikuonyeshwa kwenye taarifa za fedha za Sekretarieti ya mkoa wa Tanga kama mapato ya Sekretarieti.</p>
<b>4</b>	<b>Sekretarieti ya Mkoa wa Simiyu</b>
	<p><b>Mapungufu katika taarifa ya matumizi Sh.208,920,427</b> Ilibainika kuwa, kulikuwa na matumizi ya Sh.208,920,427 yaliyofanyika kwa mwaka 2012/13 ambapo hadi kufikia mwisho wa mwaka yalikuwa hayajalipwa. Kiasi hicho hakikuingizwa kwenye taarifa za fedha zilizoandaliwa kama matumizi kinyume na mahitaji ya aya ya saba (7) ya IPSAS 1. Hii imepelekea matumizi yalionyeshwa pungufu.</p>
<b>5</b>	<b>Sekretarieti ya Mkoa wa Kigoma</b>
	<p><b>Mapungufu katika mali zisizoshikika Sh.76,228,380</b> Sekretarieti ya Mkoa wa Kigoma ilionyesha mali zisizoshikika za kiasi cha Sh.76,228,380. Maelezo ya ziada kuhusu mali hizo yalionesha kuwa mchanganuo wa mali hizo haukuwa na vigezo vya kuitwa mali zisizoshikika kulingana na IPSAS 31 na hivyo kusababisha kilichotolewa maelezo kutokuwa sahihi.</p>

	<p><b>Kutokuandaa taarifa za usuluhisho wa benki</b> Sekretarieti ya Mkoa wa Kigoma haikufanya usuluhisho wa benki kinyume na kanuni ya 162 ya kanuni za fedha za umma ya mwaka 2001. Hii ilituwia vigumu kuthibitisha usahihi wa kiasi cha Sh.198,206,741 kilichoonyeshwa kwenye mizania ya hesabu na taarifa ya mtiririko wa fedha kwa mwaka ulioishia Juni 2013.</p> <p><b>Mapungufu katika kuandaa taarifa za mtiririko wa fedha</b> Kiasi cha Sh.151,190,140 kilipokelewa na Sekretarieti ya Mkoa kwa ajili ya kununua mali za kudumu. Hata hivyo, kiasi hicho hakikuonyeshwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha kama fedha iliyopokelewea kwa ajili ya kuongeza mtaji (cash flows from financing activities) kinyume na aya ya 18 ya IPSAS 2.</p> <p><b>Fedha za bohari kuu ya madawa kutoingizwa kwenye taarifa za fedha</b> Kwa mwaka 2012/13, Wizara ya Afya ilipeleka kiasi cha Sh.253,166,245 bohari kuu ya madawa kwa ajili ya kununua madawa pamoja na vifaa vingine vya Hospitali ya mkoa wa Kigoma. Kiasi hicho hakikuonyeshwa kwenye taarifa za fedha za Sekretarieti ya mkoa kama mapato.</p>
<b>6</b>	<b>Sekretarieti ya Mkoa wa Kagera</b>
	<p><b>Kutokuonyesha vifaa vilivyo ghalani Sh.75,971,420</b> Vifaa vilivyokuwepo ghalani vyenye thamani ya Sh.75,971,420 havikuonyeshwa kwenye hesabu za sekretarieti na hivyo kupelekea kiasi cha mali za muda mfupi kuonyeshwa pungufu kwa kiasi hicho.</p> <p><b>Malipo yenye nyaraka pungufu Sh.31,320,000</b> Sekretarieti ya Mkoa wa Kagera ilifanya matumizi ya kiasi cha Sh.31,320,000 lakini hatukuweza kudhibitisha uhalali na usahihi wa malipo hayo</p>

	<p>kutokana na kutokuwa na nyaraka za kutosha.</p> <p><b>Mapungufu katika taarifa ya matumizi Sh.523,895,425</b>        Ilibainika kuwa, kulikuwa na matumizi ya kiasi cha Sh.523,895,425 yaliyofanyika mwaka 2012/13 yayokuwa hayajalipwa. Kiasi hicho hakikuingizwa kwenye taarifa za fedha zilizoandaliwa kama matumizi kinyume na mahitaji ya aya ya saba (7) ya IPSAS 1. Hii imepelekea matumizi yaliyoonyeshwa kuwa pungufu.</p> <p><b>Kutokuandaa taarifa za usuluhisho wa benki</b>        Sekretarieti haikufanya usuluhisho wa benki kinyume na mahitaji ya kanuni ya 162 ya fedha za umma ya mwaka 2001. Hii ilituwia vigumu kuthibitisha usahihi wa kiasi cha Sh.17,724,509 kilichoripotia kwenye mizania ya hesabu na taarifa ya mtiririko wa fedha kwa mwaka ulioishia Juni 2013.</p>
<b>7</b>	<b>Sekretarieti ya Mkoa wa DSM</b>
	<p><b>Mapungufu katika kuandaa wa taarifa za mtiririko wa fedha</b>        Kiasi cha Sh.58,081,340 kilipokelewa na Sekretarieti ya Mkoa kwa ajili ya kununua au ketengeneza mali za kudumu. Hata hivyo, kiasi hicho hakikuonyeshwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha kama fedha iliyopokelewea kwa ajili ya kuongeza mtaji (cash flows from financing activities) kinyume na mahitaji ya aya ya 18 ya IPSAS 2.</p> <p><b>Kutokuandaa taarifa za usuluhisho wa benki</b>        Sekretarieti haikufanya usuluhisho wa benki kinyume na mahitaji ya kanuni ya 162 ya fedha za umma ya mwaka 2001. Ni vigumu kuthibitisha usahihi wa kiasi cha Sh.1,395,251,823 kilichoonyeshwa kwenye mizania ya hesabu na taarifa ya mtiririko wa fedha kwa mwaka ulioishia</p>

	<p>Juni 2013.</p> <p><b>Mapungufu katika matumizi Sh.182, 882,717</b>  Ilibainika kuwa, kulikuwa na matumizi ya Sh.182, 882,717 yaliyofanyika kwa mwaka 2012/13 ambapo kufikia mwishoni mwa mwaka yalikuwa hayajalipwa. Kiasi hicho hakikuingizwa kwenye taarifa za fedha zilizoandaliwa kama matumizi kinyume na aya ya saba (7) ya IPSAS 1. Hii imepelekea matumizi yaliyoripotiwa kuwa pungufu kwa kiasi hicho.</p> <p><b>Mapungufu katika taarifa ya mali zisizoshikika Sh.114,000,000</b>  Sekretarieti ya Mkoa wa Dar es Salaam ilionyesha mali zisizoshikika za kiasi cha Sh.114,000,000.Maelezo ya ziada kuhusu mali hizo yalionesha kuwa mchanganuo wa mali hizo haukuwa na vigezo vya kuitwa mali zisizoshikika kulingana na IPSAS 31 na hivyo kusababisha kilichoonyeshwa.</p>
<b>8</b>	<b>Sekretarieti ya Mkoa wa Iringa</b>
	<p><b>Mapungufu katika taarifa ya Matumizi Sh.144,940,737</b>  Ilibainika kuwa, kulikuwa na matumizi ya Sh.144,940,737yaliyofanyika kwa mwaka 2012/13 ambapo kufikia mwishoni mwa mwaka yalikuwa hayajalipwa. Kiasi hicho hakikuingizwa kwenye hesabu zilizoandaliwa kama matumizi kinyume na aya ya saba (7) ya IPSAS 1. Hii imepelekea matumizi yaliyoonyeshwa kuwa pungufu kwa kiasi hicho.</p> <p><b>Malipo yenye nyaraka pungufu Sh. 19,286,800</b>  Sekretarieti ya mkoa ilifanya malipo ya Sh.19, 286,800ambayo hatukuweza kuthibitisha uhalali wake kutokana na kukusekana kwa nyaraka muhimu. Hii ni kinyume na kanuni ya 95(4) ya kanuni za fedha za umma ya mwaka 2001.</p>

<b>9</b>	<b>Sekretarieti ya Mkoa wa Ruvuma</b>
	<p><b>Mapungufu katika taarifa ya mali zisizoshikika Sh.194,545,500</b>  Sekretarieti ya Mkoa ilionyesha mali zisizoshikika za kiasi cha Sh.194,545,500. Maelezo ya ziada kuhusu mali hizo yalionesha kuwa mchanganuo wa mali hizo haukuwa na vigezo vya kuitwa mali zisizoshikika kulingana na IPSAS 31 na hivyo kusababisha mali zilizoonyeshwa kutokuwa sahihi.</p> <p><b>Mapungufu katika matumizi Sh.687,324,501.31</b>  Ilibainika kuwa, kulikuwa na matumizi ya Sh.687,324,501.31 yaliyofanyika kwa mwaka 2012/13 ambapo kufikia mwishoni mwa mwaka wa fedha yalikuwa hayajalipwa. Kiasi hicho hakikuingizwa kwenye hesabu zilizoandaliwa kama matumizi kinyume na aya ya saba (7) ya IPSAS 1. Hii imepelekea matumizi yaliyoonyeshwa kwenye taarifa kuwa pungufu kwa kiasi hicho.</p> <p><b>Mapungufu katika kuandaa taarifa za mtiririko wa fedha</b>  Kiasi cha Sh.345, 019,149 kilipokelewa na Sekretarieti ya Mkoa kwa ajili ya kununua mali za kudumu. Hata hivyo, kiasi hicho hakikuonyeshwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha kama fedha iliyopokelewa kwa ajili ya kuongeza mtaji (cash flows from financing activities) kinyume na aya ya 18 ya IPSAS 2</p> <p><b>Kutokuandaa taarifa za usuluhisho wa benki</b>  Sekretarieti haikufanya usuluhisho wa benki kinyume na mahitaji ya kanuni ya 162 ya fedha za umma ya mwaka 2001. Ni vigumu kuthibitisha usahihi wa kiasi cha Sh.62,262,362 kilichoonyeshwa kwenye mizania ya hesabu na taarifa ya mtiririko wa fedha kwa mwaka ulioishia Juni 2013</p>

	<p>Hakukuwa na usuluhisho wa kiasi cha Sh.180,522,758 kikiwa ni tofauti iliyogundulika kati ya thamani ya vifaa vya ghalani kama ilivyo kwenye karatasi ya kuchukulia taarifa za vifaa, Sh.210,168,538 na kiasi kilichopo kwenye hesabu zilizoandaliwa Sh.29,645,780.</p>
<b>10</b>	<b>Sekretarieti ya Mkoa wa Rukwa</b>
	<p><b>Malipo yenye nyaraka pungufu Sh.11,697,050</b>        Ilibainika kuwa, Sekretarieti ilifanya malipo ya Sh.11,697,050 ambayo hayakuwa na nyaraka sahihi za kuthibitisha uhalali wake kinyume na kanuni ya 95 (4) ya kanuni za fedha za umma za mwaka 2001.</p> <p><b>Mapungufu katika kuandaa taarifa za mtiririko wa fedha</b>        Kiasi cha Sh.338,903,914 kilipokelewa na Sekretarieti ya Mkoa kwa ajili ya kununua au ketengeneza mali za kudumu. Hata hivyo, kiasi hicho hakikuonyeshwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha kama fedha iliyopokelewea kwa ajili ya kuongeza mtaji (cash flows from financing activities) kinyume na aya ya 18 ya IPSAS 2.</p> <p><b>Mapungufu katika taarifa ya marekebisho ya mtaji Sh.1,645,021,768</b>        Kwa mwaka 2012/13, Sekretarieti ya mkoa ilionyesha kiasi cha Sh.1,645,021,768 kama marekebisho ya mtaji wa wananchi (taxpayers fund/equity). Hatukuweza kudhibitisha usahihi na uhalali wa marekebisho hayo kwa kuwa nyaraka za kufanya hivyo hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.</p> <p><b>Mapungufu katika Matumizi Sh.356,771,074</b>        Ilibainika kuwa, kulikuwa na matumizi ya Shs.356,771,074 yaliyofanyika kwa mwaka 2012/13 ambapo kufikia mwishoni mwa mwaka fedha yalikuwa hayajalipwa. Kiasi hicho hakikuingizwa</p>

	<p>kwenye hesabu zilizoandaliwa kama matumizi kinyume na aya ya saba (7) ya IPSAS 1. Hii imepelekea matumizi yaliyoonyeshwa kwenye taarifa kuwa pungufu kwa kiasi hicho.</p> <p><b>Kutokuandaa taarifa za usuluhisho wa benki</b> Sekretarieti haikufanya usuluhisho wa benki kinyume na mahitaji ya kanuni ya 162 ya fedha za umma ya mwaka 2001. Ni vigumu kuthibitisha usahihi wa kiasi cha Sh.157,532,432.49 kilichoonyeshwa kwenye mizania ya hesabu na taarifa ya mtiririko wa fedha kwa mwaka ulioishia Juni 2013.</p>
<b>11</b>	<b>Sekretarieti ya Mkoa wa Mara</b>
	<p><b>Upungufu wa Vifaa ghalani kiasi cha Sh.101,942,400</b> Sekretarieti ya Mkoa wa Mara ilionyesha kwenye hesabu zake vifaa vilivyokuwa ghalani mwishoni mwa mwaka kuwa na thamani ya Sh.130, 493,400. Thamani hiyo inatofautiana na ile iliyopatikana wakati wa kuhesabu vifaa hivyo ambapo vilikuwa na thamani ya Sh.232,435,800 na hivyo kuwa pungufu kwa Sh.101,942,400.</p>
<b>12</b>	<b>Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha</b>
	<p><b>Mapungufu katika taarifa ya Mali zisizoshikika Sh.246,398,410.45</b> Sekretarieti ya Mkoa ilirionyesha mali zisizoshikika za kiasi cha Sh.246,398,410.45. Maelezo ya ziada kuhusu mali hizo yalionyesha kuwa mchanganuo haukuwa na vigezo vya kuitwa mali zisizoshikika kulingana na IPSAS 31 na hivyo kusababisha kilichoonyeshwa kwenye taarifa kutokuwa sahihi</p> <p><b>Mapungufu katika matumizi Sh.617,865,810</b> Matumizi ya kiasi cha Sh.617,865,810 yaliyofanyika kwa mwaka 2012/13 hayakuingizwa kwenye hesabu zilizoandaliwa kama matumizi kinyume na aya ya</p>

	<p>saba (7) ya IPSAS 1. Hii imepelekea matumizi yaliyoonyeshwa katika taarifa kuwa pungufu kwa kiasi hicho.</p> <p><b>Kutokuandaa taarifa za usuluhisho wa benki</b>  Sekretarieti haikufanya usuluhisho wa benki kinyume na mahitaji ya kanuni ya 162 ya fedha za umma ya mwaka 2001. Ni vigumu kuthibitisha usahihi wa kiasi cha Sh.157,514,999.42 kilichoonyeshwa kwenye mizania ya hesabu na taarifa ya mtiririko wa fedha kwa mwaka ulioishia Juni 2013.</p> <p><b>Fedha zilizopelekwa bohari kuu ya madawa kutoingizwa kwenye taarifa za fedha; Shs.228,532,794</b>  Kwa mwaka 2012/13, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ilipeleka kiasi cha Sh.228,532,794bohari kuu ya madawa kwa ajili ya kununua madawa pamoja na vifaa vingine vya Hospitali ya mkoa wa Arusha. Kiasi hicho hakikuonyeshwa kwenye taarifa za fedha za Sekretarieti ya mkoa kama mapato.</p>
<b>13</b>	<b>Sekretarieti ya Mkoa wa Shinyanga</b>
	<p><b>Kutokuandaa taarifa za usuluhisho wa benki</b>  Sekretarieti haikufanya usuluhisho wa benki kinyume na kanuni ya 162 ya kanuni za fedha za umma ya mwaka 2001. Ni vigumu kuthibitisha usahihi wa kiasi cha Sh.253,147,996.19 kilichoonyeshwa kwenye mizania ya hesabu na taarifa ya mtiririko wa fedha kwa mwaka ulioishia Juni 2013</p> <p><b>Malipo yenye nyaraka pungufu Sh.59,634,367.99</b>  Ilibainika kuwa, Sekretarieti ilifanya malipo ya Sh.59,634,367.99ambayo hayakuwa ya nyaraka za kuthibitisha uhalali wake kinyume na kanuni 95 (4) ya kanuni za fedha za umma za umma za mwaka, 2001.</p>

14	Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro
	<p><b>Mapungufu katika kuandaa taarifa za mtiririko wa fedha</b>  Kiasi cha Sh.987,691,895 kilipokelewa na Sekretarieti ya Mkoa kwa ajili ya kununua mali za kudumu. Hata hivyo, kiasi hicho hakikuonyeshwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha kama fedha iliyopokelewea kwa ajili ya kuongeza mtaji (cash flows from financing activities) kinyume na aya ya 18 ya IPSAS 2</p> <p><b>Fedha zilizopelekwa bohari kuu ya madawa kutoingizwa kwenye taarifa za fedha; Sh.272,233,978</b>  Kwa mwaka 2012/13, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ilipeleka kiasi cha Sh.272,233,978bohari kuu ya madawa kwa ajili ya kununua madawa pamoja na vifaa vingine vya Hospitali ya mkoa wa Kilimanjaro. Kiasi hicho hakikuonyeshwa kwenye taarifa za fedha za Sekretarieti ya mkoa kama mapato.</p> <p><b>Matumizi ya mafuta kutoka GPSA ambayo hayakuthibitishwa Sh.27,275,000</b>  Sekretarieti ililipa GPSA kiasi cha Sh.27,275,000kwa ajili ya kununua mafuta ya magari. Katika kupitia nyaraka za GPSA hatukuweza kupata kumbukumbu za malipo hayo na pia hatukuweza kupata mchanganuo wa jinsi mafuta hayo yaliyodaiwa kununuliwa yalivyotumika. Kwa kukosekana taarifa hizo hatukuweza kuthibitisha uhalali wa malipo na matumizi ya mafuta hayo.</p> <p><b>Kukosekana kwa vitabu sita (6) vya risiti za mapato</b>  Sekretarieti ilipokea vitabu vitano vya stakabadhi za halmashauri vyenye jumla makusanyo ya Sh.2, 500,000 na kitabu kimoja cha Stakabadhi za Serikali. Vitabu hivi havikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi na hivyo</p>

	<p>hatukuweza kuthibitisha jinsi vilivyotumika.</p> <p><b>Kukusekana uthibitisho wa fedha zilizokusanya Sh.7,116,000</b> Wakati wa ukaguzi hatukuweza kujidhihirisha kama kiasi cha Sh.7,116,000 kilichotakiwa kiwe kimekusanywa kama gharama za kuchangiana zilikusanywa na kupelekwa benki.</p> <p><b>Malipo yenye nyaraka pungufu Sh.57,013,470</b> Ilibainika kuwa, Sekretarieti ilifanya malipo ya Sh.57,013,470 ambayo hayakuwa ya nyaraka za kuthibitisha uhalali wake kinyume na kanuni 95 (4) ya kanuni za fedha za umma za mwaka 2001.</p> <p><b>Mapungufu katika mali zisizoshikika Sh.265,687,412</b> Sekretarieti ya Mkoa ilionyesha katika taarifa mali zisizoshikika Sh.265,687,412. Maelezo ya ziada kuhusu mali hizo yalionesha kuwa mchanganuo hayakuwa na vigezo vya kuitwa mali zisizoshikakia kulingana na IPSAS 31 na hivyo kusababisha kilichoripotiwa kutokuwa sahihi</p>
<b>15</b>	<b>Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza</b>
	<p><b>Kukosekana kwa hati za malipo Sh.40,211,734</b> Wakati wa ukaguzi ilibainika kuwa, hati za malipo za Sh.17,431,634 hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi. Vilevile hati za malipo za Sh.22,780,100 zilikuwa hazina viambatanisho. Ni vigumu kuthibitisha uhalali wa malipo na matumizi yaliyofanyika.</p> <p><b>Mapungufu katika matumizi Sh.40,687,595</b> Matumizi ya Shs.40,687,595 yaliyofanyika kwa mwaka 2012/13 hayakuvingizwa kwenye hesabu zilizoandaliwa kama matumizi kinyume na aya ya saba (7) ya IPSAS 1. Hii imepelekea matumizi yaliyoonyeshwa kwenye taarifa kuwa pungufu kwa</p>

	<p>kiasi hicho.</p> <p><b>Kutokuandaa taarifa za usuluhisho wa benki</b> Sekretarieti haikufanya usuluhisho wa benki kinyume na mahitaji ya kanuni ya 162 ya fedha za umma ya mwaka 2001. Ni vigumu kuthibitisha usahihi wa kiasi cha Sh.1,758,249,684 kilichoonyeshwa kwenye mizania ya hesabu na taarifa ya mtiririko wa fedha kwa mwaka ulioishia Juni 2013.</p>
<b>16</b>	<b>Sekretarieti ya Mkoa wa Tabora</b>
	<p><b>Masurufu yaliyolipwa moja kwa moja kama matumizi Sh.99,876,016.30</b> Masurufu ya kiasi cha Sh.99, 876,016.30 yalilipwa moja kwa moja kama matumizi kinyume na kanuni ya 98 (2) ya sheria ya fedha za umma ya mwaka 2001.</p> <p><b>Malipo yenye nyaraka Sh. 52,347,385</b> Ilibainika kuwa, Sekretarieti ilifanya malipo ya Sh. 52,347,385 ambayo hayakuwa ya nyaraka za kuthibitisha uhalali wake kinyume na kanuni 95 (4) ya kanuni za fedha za umma ya mwaka 2001.</p> <p><b>Malipo yenye mashaka yaliyofanyika kutoka akaunti ya amana; Sh.287,032,941.717</b> Kiasi cha Sh.7,196,920 kililipwa kutoka kwenye akaunti ya amana ambapo Sh.5,000,000 zilitumika madeni miaka ya nyuma na ambayo hayakuwa kwenye daftari la madeni. Pia, kiasi cha Sh.2,196,920 kililipwa kutoka kwenye akaunti hiyo hiyo ambapo malipo hayo hayakuwa na nyaraka za kuthibitisha uhalali wake.</p> <p><b>Malipo ambayo hayakuidhinishwa, Sh.13,251,180</b> Hospitali ya Mkoa wa Tabora ilifanya malipo ya Sh.13,251,180 kwa ajili ya manunuzi ya bidhaa pamoja na huduma nyingine za miaka ya nyuma. Malipo haya yalikuwa hayajaidhinishwa kinyume na</p>

<b>B a l o z i</b>	<p>kanuni ya 85(3) ya fedha za umma ya mwaka 2001.</p> <p><b>Mapungufu katika taarifa ya matumizi</b> Sekretarieti ya mkoa wa Tabora ilionyesha kwenye hesabu zake matumizi ambayo fedha zake zililipwa tu ya Sh. 287,032,941.717. Matumizi ambayo fedha hazikuwa zimelipwa kufikia mwishoni mwa mwaka hayakuonyeshwa kinyume na mahitaji ya aya ya 7 ya IPSAS 1</p> <p><b>Mapato kuonyeshwa pungufu kwenye hesabu Sh. 518,885,778.50</b> Ilibainika kuwa kiasi cha Sh.518,885,778.50 kilikusanywa na hospitali ya mkoa kutokana na mauzo ya madawa na makusanyo kwa njia ya gharama za uchangiaji. Hata hivyo, kiasi hicho hakikuonyeshwa kwenye hesabu za Sekretarieti ya mkoa.</p>
	<p><b>Na. Jina la Ubalozi na sababu za kupata hati zenye mashaka</b></p>
<b>1</b>	<p><b>Ubalozi wa Tanzania nchini Zaire</b></p> <p><b>Kushindwa kuthibitisha bakaa la mwanzo Sh.31,817,025</b> Ubalozi ulionyesha kiasi cha Sh.31, 817,025 ikiwa ni malipo kabla ya kupata huduma ya pango kama bakaa iliyokuwepo mwanzoni mwa mwaka. Hata hivyo hatukuweza kuthibitisha uhalali na usahihi wake kwa kuwa nyaraka za malipo hazikuwasilishwa.</p>
<b>2</b>	<p><b>Ubalozi wa Tanzania nchini Uganda</b></p> <p>Ubalozi ulionyesha kiasi cha Sh.132, 596,735 kama bakaa iliyokuwepo mwanzoni mwa mwaka wa fedha iliyohusu madeni. Hata hivyo kiasi hiki kilitofautiana na kile kilichotumika katika kufikia bakaa ya mwisho wa mwaka ya Sh.87,494,585 na hivyo kusababisha tofauti ya Sh.48,893,168 ambayo haikurekebishwa.</p>

**Jedwali 7: Orodha ya taasisi ambazo zimepata hati isiyoridhisha pamoja na sababu zilizopelekea hati hiyo**

1	<b>Ubalozi wa Tanzania Muscat</b>
	<p>Ubalozi ulionyesha kiasi cha Sh. 150,681,699 kama bakaa ya mwisho ya fedha badala ya Sh.639,874,314 kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha. Hii ilitokana na kutoonyeha mapokezi ya fedha ya Sh.97,065,176 na kujumuisha hasara ambayo haikuwa na mchanganuo wa kuthibitisha uhalali wake ya Sh. 392,127,439 iliyotokana na kubadilisha fedha za kigeni na hivyo kupelekea kiasi hicho cha fedha kuonyeshwa pungufu kwa Sh.489,192,615.</p> <p><b>Mapato yaliyokusanywa kutopelekwa benki Sh.108,108,753</b></p> <p>Ubalozi ulikusanya kiasi cha Sh.564,194,173 ambapo kati ya kiasi hicho, ni Sh.456,085,421 tu ndizo zilipelekwa benki na Sh.108,108,753 zilikuwa hazijapelekwa benki.</p> <p><b>Kutokuandaa taarifa za usuluhisho wa benki</b></p> <p>Ubalozi haukuandaa usuluhisho wa benki kinyume na kanuni ya 162 ya fedha za umma ya mwaka 2001. Ni vigumu kuthibitisha usahihi wa kiasi cha fedhakilichoonyeshwa kwenye mizania ya hesabu na taarifa ya mtiririko wa fedha kwa mwaka ulioishia Juni 2013.</p>

## SURA YA TATU

### UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJIWA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI KWA MIAKA ILIYOPITA


#### 3.0 Utangulizi

Sura hiiinatoa matokeo yatathmini juu yautekelezaji wamapendekezo yaliyotolewa katika ripoti zangu za ukaguzi za miaka ya nyuma. Kifungu Na. 12 cha Sheria nambari 11 ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 inanipa mamlaka ya kutoa mapendekezona kufuatilia utekelezaji wake kwa lengo la kudhibitimatumizi yafedha za umma, kuongeza ukusanyaji wamapato nakuongezauwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za umma. Matokeoya tathminiya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi katika Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoailikuwakatika maeneo yafuatayo:

- (i) Majibu ya taarifa za kila fungu kutoka kwa Afisa Masuuli au Wakuu wa Idara/Wakala yaliyowasilishwa kwa Mdhibili na Mkuguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.
- (ii) Majibu kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) yaliyowasilishwa kuhusu ripoti jumuiifu ya Mdhibili na Mkuguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.
- (iii) Ufuatiliaji wa mapendekezo yaliotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali(PAC).

#### 3.1 Majibu ya taarifa za kila fungu kutoka kwa Afisa Masuuli/Wakuu wa vitengo yaliyowasilishwa kwa Mdhibili na Mkuguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.


Utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali unatokana na Sheria namba 11 ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008. Katika ukaguzi wa mwaka huu, Wizara 59 na Balizi 32 zilikuwa na jumla ya mapendekezo 960 ambayo yalikuwa yanatakiwa kutekelezwa kutokana na hoja za ukaguzi za miaka ya nyuma. Maafisa Masuuli wameteteleza baadhi ya mapendekezo hayo, na hali ya utekelezaji wa mapendekezo ni kama ilivyoelezwa katika chati hapa chini:



**Chati:** Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutoka Wizara 59 na Balizi 32.

Kama inavyoonyesha katika chati hapo juu, ni asilimia 42 tu ya mapendekezo ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambayo yametetelezwa kikamilifu. Ili Kuboresha shughuli za Serikali au wajibikaji, ni vyema Maafisa Masuuli wa Wizara na balizi kumalizia utekelezaji wa asilimia 29 ya mapendekezo ambayo hayajakamilika na pia kuanza kutekeleza asilimia nyingine 29 ya mapendekezo ambayo mpaka sasa hawajaanza kutekeleza. Kushindwa kutekeleza mapendekezoya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kinyume na Sheria ya Ukaguzi wa Umma namba 11 ya mwaka 2008.

Kwa upande wa Sekretarieti za Mikoa; mwaka huu wa fedha, Sekretarieti za Mikoa 21 zilikuwa na jumla ya mapendekezo 578 kutoka kwa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambayo yalihitaji utekelezaji kutoka kwa Makatibu Tawala wa Sekretarieti za Mikoa. Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) kupitia Makatibu Tawala alitekeleza baadhi ya mapendekezo yaliotolewa, kati ya mapendekezo 578 ni mapendekezo 272 tu sawa na asilimia 45 ndio yalitekelezwa kikamilifu. Hali ya Utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni kama inavyoonekana hapa chini:



**Chati:** Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutoka Sekretarieti za Mikoa 21.

Sekretarieti za Mikoa zinatakiwa kuongeza kasi ya utekelezaji wa mapendekezo yanayotolewa na Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kila Katibu Tawala wa Sekretarieti za Mikoa ambao ni Maafisa Masuulini wajibu waokuhakikisha kwamba mapendekezo ya Ukaguzi yanatekelezwa kwa lengo la kuboresha utendaji na kuleta ufanisi kwenye shughuli zao katika matumizi ya rasilimali za umma.

Kwa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutoa mapendekezo kutokana na mapungufu yaliobainishwa katika kaguzi lengoni kuboresha utendaji na kuongeza wajibikaji katika Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa. Si jukumula Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhakikisha kuwa utekelezaji wa mapendekezo hayo umefanyika. Jukumu hili ni la Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa kuhakikisha kuwa utekelezaji wa mapendekezo haya unafanyika kikamilifu.

Katika masuala ya Utawala Bora, kila Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa zinashauriwa kuwa nautaratibu maalumu ambao utakuwa unashughulikia utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, pia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) ina jukumu la kusimamia matokeo ya utekelezaji mapendekezo yataarifa za Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kupitia Bunge kuwataka Maafisa Masuulikuchukua hatua muhimuu ya utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Kwa kutotekeleza mapendekezo ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwaweza kusababisha kujirudiarudia kwa makosa yale yale yalio jitokeza katika miaka ya nyuma. Pia, hii inaonyesha kuwa hakuna usimamizi thabiti kutoka kwa maafisa masuuli wa Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa. Kwa mwaka huu wa fedha jumla kuu ya hoja zote za ukaguzi ambazo hazijajibiwa na zile ambazo zimejibiwa bila kukamilika ni Shilingi 636,849,769,109.34. Orodha kamili inayoonyesha kiasi halisi katika kila fungu imeambatanishwa katika Kiambatisho 'D'.

- 3.2 Majibu kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) yaliyowasilishwa katika ripoti jumuiifu kwa Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.**  
ya Ukaguzi wa Umma Namba 11 ya mwaka 2008 inamtaka Mlipaji Mkuu wa Serikali kuwasilishamajibu ya utekelezaji wa hoja za Mdhibili na Mkaguzi Mkuu Wa Hesabu za Serikali.

Katika kufuatilia utekelezaji huo, mwaka 2011/2012 kulikuwa na masuala 28 yaliyotokana na ripotiza miaka ya nyuma (yaani 2009/10, 2010/11 na 2011/2012). Mwaka huu wa fedha 2012/2013 PMG gameji buhoja zilizotolewa katika ripoti ya mwaka uliopita an idadi ya hoja hizo imepungua kwa hoja 6 kutoka hoja 28 mwaka jana mpaka hoja 22 mwaka huu.

Utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali ni kama inavyo onekana katika jedwali hapa chini.

**Jedwali 8: Ufuatiliaji wa Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali**

Na	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya Ukaguzi
1	Kutokufuata kikamilifu kwa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu Katika Sekta ya Umma (IPSAS)	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Serikali imeandaa muongozo wa uhasibu na sera za uhasibu na kuzisambaza kwa wadau mbalimbali kwa ajili ya kutoa maoni ya kuziboresha.</li> <li>• Serikali pia inaendelea kuandaa rejista ya rasilimali kama inavyo takiwa na Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu Katika Sekta ya Umma (IPSAS).</li> <li>• Na Serikali inategemea kuwa mtumiaji kamili wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu Katika Sekta ya Umma (IPSAS) mwaka 2016/17</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Mlipaji Mkuu wa Serikali anatakiwa kuhakikishak uwa rasimu ya sera za uhasibu na muongozo wa uhasibu unafanyika kama inavyo takiwa na viwango vya hesabu vya kimataifa (IPSAS) ili uweze kusaidia maadnalizi ya hesabu.</li> <li>• Daftari ya rasilimali inatakiwa kuwa imekamilika kabla mwaka wa fedha 2016/2017.</li> </ul>
2	Kutofuatwa kikamilifu kwa Sheria ya	Katika kuyakabili mapungufu yalitokana na sheria ya manunuzi	Kwa kuwa kuna Sheria mpya ya manunuzi ya

	Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 na kanuni zake za 2005	ya mwaka 2004, Serikali imefanya yafuatayo: <ul style="list-style-type: none"> <li>Serikali imechagua Mshauri ambaye ataainisha mapungufu katika nyanja muhimu zinazohitaji maboresho</li> <li>Serikali imejenga uwezo kwa kuwapatia mafunzo watumishi 735 kuhusu Sheria ya manunuzi ya 2004 na kanuni zake za mwaka 2005</li> </ul>	mwaka 2011 na kanunuzi za Manunuzi za mwaka 2013 ninaishauri Serikali kuanza kujenga uwezo kwa watumishi wake kwa kuzingatia Sheria mpya ya mwaka, 2011
<b>Mwaka wa fedha 2008/2009</b>			
3	Usimamiaji mbovu wa Mali za Serikali	Serikali imefanya mafunzo ya kuwajengea uwezo wafanyakazi wote wa Balozi juu ya namna ya kuendesha mashine za VISASTickernajinsi ya kutatua matatizo endapo zitaharibika na watatumia watumishi wa wizara katika kutengeneza Mashine hizo bila ya kumutumia Mafundi wa nje	Kwa kuzingatia umuhimu wa mashine hizi za VISA katika ukusanyaji wa mpato, uhakiki wa jibu la Mlipaji Mkuu wa Serikali litafuatiliwa katika ukaguzi ujao.
4	Umiliki wa ardhi na majengo ya ofisi za Balozi za Tanzania nchi za nje.	Ardhi na Majengo ya balozi yanamilikiwa na Wizara ya Mambo ya Nje na Uhusiano wa Kimataifa na Wakala wa Majengo kazi yake ni kusimamia ununuzi wa ardhi na ujenzi wa majengo hayo.	Lengo kuu la hoja hii ilikuwa ni kuitaka Serikali ipate Hati Miliki ya majengo yake na ardhi katika balozi zote nje ya nchi
5	Masuala ya Kodi:	Uongozi wa Mamlaka ya	PMG anashauriwa

	Hatua zilizo chukuliwa kutatua rufaa za kodi	Mapato tanzania umemwandika Mwanasheria Mkuu wa Serikali barua yenye Kumb. Na. TRA/SB/2.1/Vol.4 ya Tarehe 17/01/2012 katika kuomba misaada wa kisheria katika kufatilia kesi hizi. Pia Mamlaka hii imeandikia Wizara ya Fedha barua yenye Kumb. Na. TRA/CG/L.1/Vol III ya tarehe 11/09/2012 kuomba ushirikiano katika suala hili.	kuwasiliana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuweza kumaliza masuala haya ya kesi za kodi
<b>Mwaka wa fedha 2010/2011</b>			
6	Makusanyo pungufu ya mapato	<p>Ili kuongeza makusanyo ya mapato, Mamlaka ya Mapato ilifanya tafiti mwaka 2011 ili kuweza kupendekeza kuongeza sekta binafsi/sekta zisizo kuwa rasmi katika mfumo wa kodi.</p> <p>Pia Mamlaka ya Mapato imeandaa muhula wa pili wa mpango mkakati wa muda mrefu na mfupi wa kuongeza mapato pamoja na mpango mwingine wa kiutendaji kwa kipindi cha 2013/2014 mpaka 2017/2018.</p> <p>Mipango mingine muhimu iliyo andaliwa na Mamlaka ya Mapato ni kama ifuatavyo:</p> <ol style="list-style-type: none"> <li>I. Kuanzisha mfumo mpya wa ukusanyaji wa kodi</li> <li>II. Utekelezaji wa uhamasishaji wa ulipaji kodi kwa hiari kwa walipaji wote.</li> <li>III. Kuboresha viwango vya ulipaji kodi katika sekta ya mali asili (k.m Gesi, Madini, Mafuta n.k).</li> <li>IV. Kupitia upya misamaha</li> </ol>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Mapitio /ukaguzi wa kuona ufanisi wa mpango mwanachama wa kuongeza makusanyo ulioandaliwa na Mamlaka ya Mapato utafanyika katika ukaguzi ujao</li> <li>• Hata hivyo Mamlaka ya Mapato</li> </ul>

		<p>ya kodi kutoka kwa wawekezaji wanaozalisha nchini na kusafirisha nje.</p> <p>V. Kuongeza makusanyo kutoka katika sekta isiyo rasmi kwa kuweka kiwango kidogo kwa walipaji kodi wadogo</p> <p>VI. Kupunguza misamaha ya kodi kwa baadhi wa shughuli</p> <p>VII. Kuanzisha mchakato wa kuipitia Sheria ya Ongezeko la Thamani (VAT) ili kuongeza wigo wa ulipaji kodi</p> <p>VIII. Kuongeza wigo wa kulipa kodi kwa kuongeza baadhi ya bidhaa kama vile maji ya kunywa ya chupa.</p> <p>IX. Kuongeza idadi ya walipaji kodi kutoka 1,035,281 mwezi wa Juni 2012 mpaka 1,514,368 ifikapo mwezi Desemba 2012.</p> <p>X. Kuongeza uwiano wa mapato kwa kulinganisha na ongezeko wa pato la taifa kutoka asilimia 15.6 mwaka 2012 mpaka asilimia 17.8 ifikapo mwaka 2015</p>	<p>inashau riwa kuangalia na kuongeza wigo wa vyanzo vingine vya mapato .</p>
7	Hatua za kuboresha malengo ya kusanyaji wa mapato kilamwaka	<ul style="list-style-type: none"> <li>Mamlaka ya Mapato Tanzania imekua ikitoa elimu kwa walipa kodi wote kupitia luinga na radio ili kuwezesha kulipa Kodi kwa hiari na kuelewa umuhimu wa kutumia mashine za EFD katika biashara zao</li> <li>Pia Mamlaka imekua ikifanya ukaguzi wa kushtukiza kwa wafanya</li> </ul>	<p>Mlipaji Mkuu wa Serikali anatakiwa kuishauri Mamlaka ya Mapato katika kuweka mikakati ya kupanua wigo wa kodi kwa</p>

		biashara wote kuona kama kuna wafanyabiasha ambao hawalipi kodi na wale ambao hawatoi stakabadhi za mashine za EFD.	kuleta sekta zisizo rasmi katika mfumo wa kodi na kuondoa urasimu usio wa lazima ili kuhamasisha ulipaji kodi bila shuruti.
8	Malipo ya mishahara kwa watumishi ambao hawako kwenye utumishi wa umma	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Uhakiki wa wafanyakazi waliopo kazini uliofanyika katika kipindi cha mwezi Desemba 2011 and Machi 2012 Ulibaini wafanyakazi 10,164 ambao hawakuwepo kazini lakini walikuwa wanalipwa mishahara.</li> <li>• Baada ya zoezi hili ilipofika tarehe 30/6/2013 Serikali ilifanikiwa kukusanya kiasi cha Shilingi Bilioni 7.56 kutoka katika Halmashauri na Serikali kuu na pesa hizi zimeweka katika akaunti namba 9921141201 Benki Kuu.</li> </ul>	Ulipwaji wa mishahara hewa bado umeonekana katika ukaguzi wa mwaka 2012/2013 hivyo inatakiwa kuimarisha mifumo ya ndani ya udhibiti katika Halmashari, Wizara na ofisi nyingine za Serikali.
9	Madai mara mbili ya malipo ya uzeeni (pensheni na mafao ya mikataba) kinyume na sheria za pensheni	Jumla ya akaunti 124 za wastaafu zimesimamishwa kupisha uchunguzi zaidi, pia ukaguzi wa majalada ya wastaafu unaendelea ili kubaini wale wote ambao wanalipwa pensheni mara mbili	Uchunguzi huo unatakiwa kufanyika kwa umakini na matokeo ya uchunguzi huu yafikishwe ofisi ya Taifa ya ukaguzi kwa uhakiki zaidi
10	Usimamizi wa Dhamana za	Serikali inafanya mapitio ya Sera ya Mikopo, Dhamana na	Utekelezaji wa mikakati

	Serikali	Misaada ya mwaka 1974 iliyo fanyiwa marekebisho mwaka 2004. Pia Serikali inafanya mapitio ya sera ya deni la Taifa ili kufanya marekebisho katika baadhi ya vifungu katika sheria hiyo. Sheria hizi zinatakiwa kuwa zimekamilika ifikapo Agosti, 2013 na kuwasilishwa katika baraza la mawaziri mwezi Septemba 2013.	ya Serikali unasubiriwa kwa ajili ya uhakiki.
11	Fedha zilizotolewa kuagiza bidhaa nje yanchi ambazo hazijarudishwa Serikalini.	Hazina kupita mkusanyaji wa madeni ya Serikali amefanikiwa kukusanya kiasi cha JPY 70,621,810 sawa na Shilingi 776,839,920 na kiwango kilicho bakia ni JPY 16,628,878,047	Mlipaji Mkuu wa Serikali anatakiwa kuhakikisha kuwa mkusanyaji wa madeni anakusanya kiasi kilichobaki cha Sh.16,628,878,047
12	Madeni na Mihadi	Serikali imeongeza jitihada katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kuweza kuwa na uwezo wa kulipia matumizi yake. Hili limefanyika kwa kutoa elimu wa walipaji kodi ili kuweza kulipa kodi kwa ridhaa na pia Serikali imejitahidi kuziba mianya ya wakwepaji kulipa kodi ikiwa sambamba na kuongeza wigo kutoka sekta zisizo rasmi ili kukusanya mapato ya ndani.	Mamlaka ya mapato kushirikiana na Hazina wanatakiwa kuhakikisha kuwa fedha zinatolewa kwa wakati na kwa kuzingatia bajeti.
13	Mali zisizoingizwa katika daftari la mali	Zoezi la kuziwekea alama mali zote za Serikali kuu na Serikali za Mitaa utafanyika kwa awamu na mali zote zitaingizwa katika daftari ya mali na pia katika mfumo wa EPICOR 9.05	Mlipaji Mkuu wa Serikali anatakiwa kuonyesha hatua (ratiba) za utekelezaji wa ushauri huu.  Pia, daftari la mali za

			kudumu za Serikali linatakiwa kuwa tayari kabla ya mwaka 2017 ambapo Serikali itakuwa inatumia Viwango vya kufunga Hesabu vya kimataifa (IPSAS)
14	Misamaha ya kodi	<p>Serikali kupitia kwa Mamlaka ya Kodi na Wizara ya Fedha ilifanya tafiti kuhusu misamaha ya kodi na kuja na mapendekezo yafuatayo:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Kupunguza misamaha ya kodi ya thamani (VAT) kwa kupunguza idadi ya vitu vinavyo safirishwa nje tu ikiwa pia ni pamoja na kupunguza misamaha mingine ya kodi katika nyanja mbalimbali</li> <li>• Kutungwa kwa sheria ya uchambuzi wa kina na namna ya kutoa taarifa ya matumizi ya kodi kulinga na makundi tofauti ya walengwa hivyo kusaidia katika kutengeneza bajeti za mapato na matumizi</li> <li>• Pia misamaha ya kodi itakuwa ikitolewa pale tu ambapo itafahamika kuwa kuna chanzo kingine cha kupata kodi.</li> <li>• Kutunga Sheria ya kutoa misamaha ya kodi kwa kipindi maalumu tu.</li> <li>• Kukomesha msahama wa kodi uliokuwa ikitolewa katika uagizaji wa bidhaa kwa matumizi ya nyumbani</li> </ul>	Mlipaji Mkuu wa Serikali anatakiwa kuja na mpango mkakati wa kutekeleza mapendekezo yote hayo.

		<p>kwa sababu imethibitika kuwa mtumiaji wa bidhaa hizi hajapata unafuu wa bei licha ya kusamehewa kwa kodi katika bidhaa hizi</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Kuiwezesha Wizara ya fedha kuweza kufanya uchambuzi na kuaanda ripoti ya mwaka ya matumizi ya kodi na kuambatanisha katika riporti ya bajaeti ya Serikali.</li> </ul>	
15	Kutoandika kwa usahihi mikopo iliyotolewa na erikali kama dhamana	Serikali kupitia Mizara ya Fedha, Benki Kuu na benki ya Uwekezaji Tanzania (TIB) wanapitia mapendekezo kutoka kwa makampuni ya maua ili kuona uwezekano wa kuweka mikakati kwa makampuni hayo kuanza kulipa deni lao. Mpango huu unategemea kukamilika mwezi Juni 2013 na makampuni haya kuanza kulipa madeni yao mwezi Julai 2013	Makubaliano hayo yaliofikiwa baina ya Serikali na Makampuni hayo ya maua pamoja na vielelezo vingine vya msingi viwasilishwe ofisi ya ukaguzi kwa ajili ya uhakiki.
16	Kutojihusisha kikamilifu kwa Serikali katika makubaliano ya kutayarisha mikataba ya ujenzi mfanoChuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na mengine ya namna hiyo	Serikali itakapo pokea taarifa ya utekelezaji wa miradi hiyo ya ujenzi, Serikali itateua Mshauri kwa ajili ya kufanya ukaguzi kubaini kama ujenzi umezingatia thamani ya fedha pamoja na uhalali wa malalamiko kutoka kwa wanachama wa Mifuko ya Kijamii	Utekelezaji wa majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali unangojewa
<b>Mwaka wa fedha 2011/2012</b>			
17	Deni la Shirika la ndege (ATCL)	Serikali kupitia taasisi ya kuzuia na kupambana na rushwa (TAKUKURU) inachunguza wale wote walio ingia mkataba wa kukodisha ndege ya Airbus	Matokeo ya uchunguzi huu yanasubiriwa

		A320, na uchunguzi bado unaendelea	
18	Malipo ya matibabu nje ya nchi yasio na nyaraka za viambatanisho kiasi cha Sh. 448,144,343	<ul style="list-style-type: none"> <li>Mlipaji Mkuu wa Serikali amewaamru mabalozi wahusika kupitia barua yenye kumb Na CHA.466/564/01/06 ya mwezi Agosti, 2011 kuhakikisha kuwa nyaraka zote muhimu za malipo zinaambanishwa</li> <li>Pia Serikali itaendelea kuboresha udhhibiti wa ndani katika malipo yote kwa kuhakikisha nyaraka zote muhimu zinaambatanishwa katika malipo yote</li> </ul>	Nyaraka hizo pungufu zinasubiriwa kwa ajili ya uhakiki
19	Ulipwaji wa madeni ya miaka ya nyuma usio sahihi Sh 252,975,000,000	<p>Katika mwaka wa fedha ulioishia 30/06/2011, Serikali ilifunga mwaka ikiwa na deni la Sh.420 bilioni. Hivyo Serikali iliamua kuwa kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kutengeneza fungu kwa jina la mradi wenye namba 4168 kwa jina la Ujenzi maalumu wa barabara na kifungu hiki kupitishwa na Bunge.</p> <p>Lengo la kufanya hivi ilikuwa ni kulipa madeni yote ili kazi za ujenzi wa barabara ziendelee na kujenga mahusiano mazuri na wakandarasi na hata hivyo pesa hizi zilitumika kwa malengo hayo ili kuendeleza ujenzi wa barabara</p>	Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imeomba ukaguzi maalumu kufanyika, ukaguzi maalumu unaendelea.
20	Ulipwaji wa deni la PSPF na Serikali		Suala hili halijajibiwa na Mlipaji Mkuu wa

			Serikali
21	Fedha zilizo kaa muda mrefu katika akauti za Shule za sekondari Sh.1,551,005,412		Suala hili halijajibiwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali
22	Masurufu ambayo hayajarejeshwa kwa muda mrefu Sh.706,701,016		Suala hili halijajibiwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali

### 3.3 Ufuatiliaji wa mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Hesabu za Serikali Kuu (PAC)

Sehemu hii inaeleza namna ambavyo utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali(PAC) umefanyika kwa mujibu wa Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008.Sheria hii inamtakaMlipaji Mkuu wa Serikali kuandaa majibu ya hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na utekelezaji wake. Pia inamtaka Mlipaji Mkuu wa Serikalikutekeleza mapendekezo na maagizo ya Bunge kupitia kamati zake za Usimamizi. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali aliwasilisha taarifa yake yenye mapendekezo kwa Serikali katika Bunge mnamo tarehe 7/12/2013. Mapendekezo ya kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa mwaka ulioishia 30/6/2012 ni kama ifuatavyo:

#### Jedwali 9: Mapendekezo ya kamati ya hesabu za Serikali kuu

Aya kutoka katika ripoti ya kamati	Hoja	Mapendekezo ya kamati
4.2.1	Kutokukaguliwa kwa hesabu za vyama vya siasa kwa kipindi cha miaka minne mfululizo kwa kigezo cha	<ul style="list-style-type: none"> <li>Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliagizwa kuvikagua vyama vyote vya siasa kuanzia mwaka 2009/2010 mpaka</li> </ul>

Aya kutoka katika ripoti ya kamati	Hoja	Mapendekezo ya kamati
	kukosa fedha	<p>2011/2012 na taarifa ya ukaguzi iwe imakamilika ifikapo tarehe 31/01/2014 na msajili wa vyama vya siasi atangaze taarifa hizo katika magazeti kulingana na sheria ya vyama.</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Kwa miaka ijayo bunge litenge fedha kiasi cha kutosha kitakacho mwezesha Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuweza kukagua hesabu za vyama vya siasa bila ya kipingamizi chochote</li> </ul>
4.2.2	Kutozingatiwa kwa Sheria ya Manunuzi ya Umma na Kanuni zake	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Serikali iiwezesha Mamlaka ya Udhhibiti wa manunuzi ya Umma (PPRA) katika shughuli zake ili kuweza kuhakikisha kuwa ifikapo tarehe 30/6/2014 kila idara ya Serikali inakuwa na</li> </ul>

Aya kutoka katika ripoti ya kamati	Hoja	Mapendekezo ya kamati
		<p>Kitengo cha manunuzi (PMU) na pia kuhakikisha kuwa kila Ofisi ya Serikali inaweza kuandaa Mpango wa manunuzi wa mwaka wa fedha 2014/2015.</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Pia Serikali inatakiwa kuongeza Udhibiti katika kuzingatia Sheria ya Manunuzi katika wizara, idara na Sekretarieti za Mikoa kwa kuajili watu wenye weledi na wataalamu wa masuala ya manunuzi, kutoa elimu kwa nia ya kujengea uwezo watumishi wa idara ya manunuzi, pia kuzijengea uwezo Bodi za Zabuni na pia kitengo cha ukaguzi wa ndani.</li> <li>• Pia Serikali ihakikishe kuwa Kanuni Mpya za Manunuzi zinakamilika mapema ili zianze kutumika.</li> </ul>

Aya kutoka katika ripoti ya kamati	Hoja	Mapendekezo ya kamati
		<ul style="list-style-type: none"> <li>• Serikali pia inashauriwa kuhakikisha kuwa kabla haijatia saina makubaliano yoyote katika mikataba mikubwa inayohusu mustakabali wa maendeleo ya nchi, ni vyema basi mikataba hiyo iwe inapitiwa na PPRA kabla ya kutiwa saina.</li> <li>• Serikali pia inashauri kuiwezesha PPRA katika kuanzisha mfumo wa manunuzi wa kieletroniki (<i>Electronic Procurement System</i>)</li> </ul>
4.2.3	Kudhibiti ongezeko la misamaha ya Kodi	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Wizara ya Fedha inatakiwa kushirikiana na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kutoa taarifa sahihi za misamaha yote ya kodi ili Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za</li> </ul>

Aya kutoka katika ripoti ya kamati	Hoja	Mapendekezo ya kamati
		<p>Serikali aweze kufanya ukaguzi kuhusiana na misamaha hiyo ya kodi.</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>Pia inatakiwa Sheria ya Ukaguzi wa umma ya mwaka, 2008 irekebishwe ili kumwezesha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuweza kukagua misamaha yote ya kodi na kutoa taarifa ya ukaguzi.</li> </ul>
4.2.4	Uwepo wa kesi nyingi mahakamani za madai ya kodi ambazo hazijatolewa maamuzi.	Kama Serikali ina nia ya dhati ya kuepuka hasara za namna hii haina budi kupitia Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhakikisha inafanya kazi kwa uadilifu na kikamilifu katika kupata ushindi na kumaliza kesi mbalimbali zinazosubiri maamuzi hususan kesi zinazohusu madai ya kodi

Aya kutoka katika ripoti ya kamati	Hoja	Mapendekezo ya kamati
4.2.5	Kusitishwa kwa matumizi ya mita za kupima ujazo wa mafuta (Flow Meters) yanayoingia nchini kupitia kituo cha kupakulia mafuta Kurasini (KOJ)	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Serikali inatakiwa kulieleza Bunge ni kwa nini imeamua kuchukua uwamuzi wa kusitisha matumizi ya mita hizo.</li> <li>• Pia Mamlaka ya Mapato imetakiwa kuelezea ni kwa jinsi gani imeathirika katika ukusanyaji wake wa mapato kutokana na kusimamishwa kwa utumiaji wa mita hizo.</li> </ul>
4.2.6	Mkataba wenye utata wa kutengeneza Leseni za udereva Tanzania	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato ihakikishe inapitia upya mkataba huo na vipengele vyenye mapungufu virekebishwe.</li> <li>• Vilevile, TRA na Jeshi la Polisi wahakikishe mfumo wa leseni za udereva unatumika kwa</li> </ul>

Aya kutoka katika ripoti ya kamati	Hoja	Mapendekezo ya kamati
		<p>asilimia 100 ili kuongeza mapato ya Serikali.</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi maalum wa leseni hizi na kuwasilisha Taarifa yake kwenye Kamati.</li> <li>• Aidha, Kamati inapendekeza kuwa mikataba ambayo itahusisha utoaji wa misamaha ya kodi iwe inapitiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kabla ya kusainiwa</li> </ul>
4.2.7	Upotevu wa mapato ya kodi katika sekta ya mawasiliano	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Ili kuwa na taarifa sahihi za mapato ya makampuni, Mamlaka ya Mapato (TRA) na Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA) ziwe na uhusiano wa karibu katika kubadilishana</li> </ul>

Aya kutoka katika ripoti ya kamati	Hoja	Mapendekezo ya kamati
		<p>taarifa za miamala ya makampuni ya simu</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Serikali ikamilishe haraka majaribio ya mtambo huo ili uanze kutumika mapema kwa lengo la kuiwezesha TRA kukusanya kodi zaidi na vilevile Serikali kujiridhisha na mapato halisi ya makampuni ya simu husika.</li> <li>• Sheria ifanyiwe marekebisho ili gharama zinazoruhusiwa (<i>allowable deductions</i>) kuhusu gharama za matangazo ya biashara ziwekewe ukomo angalau asilimia tatu (3%) ya mapato ghafi.</li> </ul>
4.2.8	Mapungufu katika utekelezaji wa	Serikali itenge na kupeleka fedha REA kutoka vyanzo vya

Aya kutoka katika ripoti ya kamati	Hoja	Mapendekezo ya kamati
	mpango wa kupeleka umeme vijiji unaosimamiwa na REA chini ya Wizara ya Nishati na Madini;	ndani ambazo upatikanaji wake unaeleweka na hauchukui muda mrefu ukilinganisha fedha kutoka vyanzo vya nje kama vile wafadhili na wahisani kutoka nje.
4.2.9	Ulipaji usioridhisha wa deni ambalo Serikali inadaiwa na Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSPF)	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Serikali iendelee kutenga fedha na kulipa kila mwaka Sh. 71 bilioni kwenda PSPF ili kuwezesha mfuko huo kuendelea kutoa pensheni kwa wastaafu bila vikwazo;</li> <li>• PSPF ihakikishe inafanya uwekezaji na kutoa mikopo kwa Taasisi mbalimbali kwa kuzingatia uwezo wake wa kifedha ili isiendelee kuingia katika hatari ya mfuko kushindwa kujiendesha na kuathiri watumishi na wastaafu mbalimbali;</li> <li>• Mamlaka ya</li> </ul>

Aya kutoka katika ripoti ya kamati	Hoja	Mapendekezo ya kamati
		<p>Usimamizi na Udhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (SSRA) iwe makini katika kusimamia kiwango cha uwekezaji na mikopo inayotolewa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kiwe kinalingana na uwezo wa Mifuko hiyo hususan kutoathiri uwezo wa mifuko hiyo kulipa pensheni za wastaafu.</p>
4.2.10	Changamoto mbalimbali zinazoikabili Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya nje na Uhusiano wa Kimataifa inatakiwa kuhakikisha kuwa Mashine zote za kutolea Stika za VIZA zinafanya kazi na zinafanyiwa matengenezo kila mara.</li> <li>• Wizara hii pia inatakiwa</li> </ul>

Aya kutoka katika ripoti ya kamati	Hoja	Mapendekezo ya kamati
		<p>kuhakikisha kuwa Mfumo wa udhibiti matumizi ya fedha (IFMS-EPICOR) unafanya kazi kwa ufanisi wake ili kuepuka kuingia hasara</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Pia Wizara hii kwa kushirikiana na wizara ya Fedha kwa pamoja zinashauriwa kuangalia ni jinsi gani wanaweza kupunguza matumizi katika balozi zetu</li> <li>• Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuchagua baadhi ya Balozi (<i>sampling</i>) na kuzifanyia ukaguzi maalum (<i>Special Audit</i>) lengo likiwa kutafuta njia na namna bora zaidi ya kutatua matatizo na changamoto zinazokabili Balozi</li> </ul>

Aya kutoka katika ripoti ya kamati	Hoja	Mapendekezo ya kamati
		zetu ambazo kimsingi zinaathirika kwa kiasi kikubwa katika utendaji.
4.2.11	Mwenendo wa makusanyo ya maduhuli yanayofanywa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ihakikishe inaimarisha mfumo wa udhibiti wa ndani wa ukusanyaji wa maduhuli.</li> <li>• Kwa lengo la kuongeza ukusanyaji wa maduhuli, Wizara pamoja na kuwa na mfumo wa <i>Land Rent Management System (LRMS)</i>, ianze kutumia mfumo wa kieletroniki (EFD), katika kukusanya maduhuli ya Serikali.</li> <li>• Mfumo huo wa kieletroniki uambatane na namba ya</li> </ul>

Aya kutoka katika ripoti ya kamati	Hoja	Mapendekezo ya kamati
		<p>utambulisho wa mlipa kodi (TIN) ili kujua takwimu sahihi za walipa kodi pamoja na kupunguza migogoro ya ugawaji wa ardhi.</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Wizara itafute utaratibu maalum utakao hakikisha kuwa kodi ambazo hazijalipwa katika viwanja mbalimbali zinalipwa mapema iwezekanavyo.</li> </ul>

Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Hesabu za Serikali Kuu imekua mstari wa mbele katika kuhakikisha kwamba mapendekezo yote ninayo yapendekeza katika kukuza uwajibikaji, kuongeza makusanyo ya mapato ya ndani na kuleta nidhamu katika matumizi ya fedha za umma yanafanyiwa kazi. Kwa juhudi za kamati ya Bunge ya hesabu za Serikali imefanya majukumu yetu ya Kisheria ya kuitumikia Serikali yetu kuwa ya manufaa. Hivyo, Maafisa Masuuli wanashauriwa kuwa mstari wa mbele katika kutekeleza mapendekezo na maagizo ya Kamati ya Hesabu za Serikali pamoja na mapendekezo yanayotolewa na Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Za Serikali.

## SURA YA NNE

### MAKUSANYO YA MADUHILI NA MCHANGANUO WA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO

#### 4.1: Mapitio ya Ufanisi wa Mapato

Katika mwaka wa ukaguzi wa 2012/13 makadirio ya jumla ya Serikali yalikuwa Sh.15,191,944,300,000, wakati makusanyo halisi ni Sh.15,018,268,312,814 sawa na asilimia 98.86, hii inaonesha Serikali ilishindwa kufikia malengo kwa kiasi cha Sh.173,675,987,186 sawa na asilimia 1.1.

Vyanzo vya mapato kwa Serikali ni pato la ndani linalotokana na kodi, mapato ya vyanzo visivyo vya kodi, mikopo ya ndani na misaada kutoka kwa wahisani.

Katika mwaka wa fedha 2012/2013 mapato halisi yaliyokusanywa kutoka vyanzo vitokanavyo na kodi yalikuwa Sh.8,052,228,708,823 ikilinganishwa na lengo la Sh.8,432,361,000,003 hivyo kushindwa kufikia lengo kwa Sh.380,132,291,180 sawa na asilimia 4.5.

Mapato yasiyotokana na kodi kwa mwaka wa fedha 2012/13 yalikuwa Sh.419,561,845,673 ikilinganishwa na makadirio ya Sh.644,581,942,670; hivyo kutofikia lengo kwa kiasi cha Sh.225,020,096,997 sawa na asilimia 35.

Mapato kutoka vyanzo vya kifedha (finance income) yalikua Sh.61,594,970,635 ikilinganishwa na makadirio ya Sh.72,258,159,415; hivyo Serikali haikufikia malengo kwa kiasi cha Sh.10,663,188,780 sawa na asilimia 15.

Mikopo ya ndani ilikua Sh.2,492,710,243,677 wakati makadirio yalikuwa Sh.1,632,000,000,000, hivyo kusababisha ongezeko la mikopo kwa Sh.860,710,243,677 sawa na asilimia 35.

Mapato yatokanayo na misaada ya nje yalikua Shs.3,992,172,544,006 dhidi ya makadirio ya

Shs.4,410,810,197,912; hivyo kuonesha upungufu wa Shs.418,637,653,906 sawa na asilimia 9.

**Jedwali 10: Makadirio na mapato halisi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2012/2013 na 2011/2012**

Aina ya mapato	2012/2013		
	Makadirio yaliyo idhinishwa Sh.	Mapato Halisi Sh.	Tofauti kati ya Makadirio na Mapato Sh.
Mapato ya Ndani (Kodi)	8,432,294,000,003	8,052,228,708,823	-380,065,291,180
Mapato ya vyanzo visivyo vya kodi	644,581,942,670	419,561,845,673	-225,020,096,997
Vyanzo vya kifedha "Finance income"	72,258,159,415	61,594,970,635	-10,663,188,780
Mikopo ya Ndani	1,632,000,000,000	2,492,710,243,677	860,710,243,677
Misaada ya Wahisani wa nje	4,410,810,197,912	3,992,172,544,006	-418,637,653,906
<b>Jumla 2011/2012</b>	<b>15,191,944,300,000</b>	<b>15,018,268,312,814</b>	<b>-173,675,987,186</b>
Mapato ya Ndani (Kodi)	6,228,835,792,139	6,414,806,314,206	185,970,522,067
Mapato ya vyanzo visivyo Kodi	692,737,853,273	719,960,110,049	27,222,256,776
Vyanzo vya kifedha "Finance income"	204,874,736,788	208,132,532,126	3,257,795,338
Mikopo ya Ndani	1,204,262,000,000	1,639,365,483,932	435,103,483,932
Misaada ya Wahisani wa nje	5,195,184,967,800	3,168,234,333,111	-2,026,950,634,689
<b>Jumla</b>	<b>13,525,895,350,000</b>	<b>12,150,498,773,424</b>	<b>-1,375,396,576,576</b>

*Chanzo: Taarifa Jumuiifu ya Fedha ya mwaka 2012/2013 na 2011/2012*

Kulingana na jedwali hapo juu, kuna ongezeko la makisio ya mapato yatokanayo na kodi katika mwaka wa fedha 2012/2013 ya asilimia 35, ukilinganisha na mwaka 2011/12. Bajeti ya mapato yasiyotokana na kodi ilipungua kwa asilimia 7% mwaka wa fedha 2012/2013 ikilinganishwa na mwaka 2011/12. Pia kulikuwa na upungufu wa bajeti ya vyanzo vya kifedha (finance income) kwa asilima 65 ukilinganisha bajeti hiyo kwa mwaka wa fedha 2011/12.

Mapato halisi yatokanayo na vyanzo vya kodi kwa mwaka wa fedha 2012/2013 yaliongezeka kwa asilimia 26 ukilinganisha na makusanyo ya mwaka 2011/12. Ingawa, mapato yasiyotokana na vyanzo vya kodi yalipungua kwa asilimia 42 kwa mwaka wa fedha 2012/2013 ikilinganishwa na mwaka 2011/12. Pia mapato yatokanayo na vyanzo vya kifedha (finance income) kwa mwaka wa fedha 2012/2013 yalipungua kwa asilimia 70 ikilinganishwa na mwaka 2011/12.

Katika mwaka wa fedha 2012/2013, mikopo ya ndani na misaada kutoka nje iliongezeka kwa asilimia 52 na kwa mwaka 2011/2012 asilimia 26.

Licha ya hayo, kwa ujumla mwaka wa fedha 2012/13 kulikua na ongezeko la bajeti ya mapato kwa Sh.1,666,048,950,000 (sawa na asilimia 12) na mapato halisi yaliongezeka kwa Sh.2,867,769,539,390 (sawa na asilimia 24) ukilinganisha na mwaka wa fedha 2011/12. Ufanisi wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2012/13 ulikuwa na upungufu kwani malengo mengi ya makusanyo ya mapato hayakufikiwa, ukilinganisha na ilivyokua mwaka wa fedha 2011/12.

**4.1.1 Utekelezaji wa bajeti; uwiano wa fedha kutoka mfuko mkuu wa Serikali na matumizi kwa Serikali kuu (Fedha za Sekretarieti za Mikoa hazijumuishi Serikali za Mitaa)**

**4.1.2 Uwiano wa fedha za matumizi ya kawaida zilizotolewa kwa Wizara, idara za Serikali na Sekretarieti za Mikoa dhidi ya bajeti iliyoidhinishwa (isiyojumuisha Serikali za Mitaa)**

Mapitio ya taarifa za fedha za Wizara, idara za Serikali na Sekretarieti za mikoa kwa mwaka 2012/2013 zilionyesha kuwa bajeti ya matumizi ya kawaida ilipungua kwa kiasi cha Sh.615,003,216,505 sawa na asilimia 6.7 ikilinganishwa na Sh.9,214,885,955,263 za mwaka 2011/2012.

Pia, kulikuwa na upungufu wa Sh.402,811,133,083 kwa fedha zilizotolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ukilinganisha na mwaka 2011/2012.

Hata hivyo, katika mwaka wa fedha 2012/2013, kiasi cha Sh.8,284,419,655,467 kilitolewa kwa matumizi ya kawaida dhidi ya makadirio ya Sh.8,599,882,738,758, hii inaonyesha kuwa Sh.315,463,083,291 hazikutolewa ambazo ni sawa na asilimia 3.7.


Katika mwaka wa fedha uliopita, 2011/12 kiasi cha Sh.8,687,230,788,550 kilitolewa kwa matumizi ya kawaida dhidi ya makadirio ya Sh.9,214,885,955,263, hii inaonyesha kuwa Sh.527,655,166,713 hazikutolewa ambazo ni sawa na asilimia 5.7.

Muhtasari wa mchanganuo huu ni kama ifuatavyo:

**Jedwali 11: Uwiano wa bajeti ya matumizi wa kawaida, fedha zilizotolewa na matumizi halisi**

	2011/2012	2012/2013	Tofauti	Asilimia ya Ongezeko / (Punguzo)
Makadirio (Sh)	9,214,885,955,263	8,599,882,738,758	(615,003,216,505)	(6.7)
Fedha zilizotolewa (Sh)	8,687,230,788,550	8,284,419,655,467	(402,811,133,083)	(4.6)
Upungufu (Sh)	529,610,793,169	315,463,083,291		

Pia taarifa hii inaoneshwa katika chati mhimili hapa chini:



Kwa ujumla, upungufu wa fedha zilizotolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida katika mwaka wa fedha 2012/13 uliathiri utekelezaji wa shughuli za kawaida katika wizara, Idara za Serikali na Sekretarieti za Mikoa.

#### 4.1.3 Uwiano wa fedha za matumizi ya maendeleo zilizotolewa kwa Wizara, Idara za Serikali na Sekretarieti za Mikoa dhidi ya bajeti iliyoidhinishwa (hazijumuishi Fedha za Serikali za Mitaa)

Mapitio ya taarifa za fedha za Wizara, idara za Serikali na Sekretarieti za mikoa kwa mwaka 2012/2013 zilionyesha kuwa mwaka 2012/2013 bajeti ya matumizi ya maendeleo ilikuwa Sh.4,224,701,675,251, wakati katika mwaka 2011/2012 ilikuwa Sh.4,311,009,394,737 hivyo kuonesha upungufu wa bajeti kwa Sh.85,534,459,886, sawa na asilimia 2.

Pia, kuna upungufu wa fedha za maendeleo zilizotolewa mwaka 2012/2013 ambazo zilikuwa Sh.3,247,527,081,386; kiasi hiki ni pungufu kwa Sh.136,904,676,960 sawa na asilimia 4.1, kikilinganishwa na kiasi cha Sh.3,384,431,758,346 kilichotolewa mwaka 2011/2012.

Katika mwaka wa fedha 2012/2013, kiasi cha Sh.3,247,527,081,386 kilitolewa kwa matumizi ya maendeleo dhidi ya makadirio ya Sh.4,224,701,675,251,

hii inaonyesha kuwa Sh.977,940,092,853 hazikutolewa ambazo ni sawa na asilimia 23.1.

Muhtasari wa mchanganuo huu ni kama ifuatavyo:

**Jedwali 12: Uwiano wa bajeti ya matumizi ya maendeleo, fedha zilizotolewa na matumizi halisi**

	2011/2012	2012/2013	Tofauti	Asilimia ya ongezeko/ (Punguzo)
Makadirio (Sh)	4,311,009,394,737	4,225,474,934,851	(85,534,459,886)	-2.0
Fedha zilizotolewa (Sh)	3,384,431,758,346	3,247,527,081,386	(136,904,676,960)	-4.1
Upungufu (Sh)	934,713,248,551	977,940,092,853		

Kwa ujumla, upungufu wa fedha zilizotolewa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2012/13 uliathiri utekelezaji wa shughuli za kimaendeleo katika Idara za Serikali na Sekretarieti za Mikoa.

**4.1.4 Ulinganisho wa fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na matumizi halisi ya Kawaida katika Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa (hazijumuishi fedha za Serikali za Mitaa)**

Mwaka 2012/2013, fedha zilizotumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida zilikuwa Sh.8,249,278,491,861 wakati fedha zilizotolewa na Hazina zilikuwa Sh.8,687,230,788,550; hii inaonesha kwamba kiasi cha Sh.35,141,163,606 hakikutumika ambacho ni sawa na asilimia 0.42.

Katika mwaka wa fedha 2012/2013 matumizi halisi yalipungua kwa Sh.435,996,670,233; ikilinganishwa na matumizi katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, sawa na asilimia 4.64.

Muhtasari wa mchanganuo huu ni kama ifuatavyo:

**Jedwali 13: Ulinganisho wa fedha zilizotolewa kwa matumizi ya kawaida na matumizi halisi**

Mwaka wa fedha	2011/2012	2012/2013	Tofauti	Asilimia ya Ongezeko/ (Punguzo)
Fedha zilizotolewa (Sh)	8,687,230,788,550	8,284,419,655,467	(402,811,133,083)	-4.64
Matumizi halisi (Sh)	8,685,275,162,094	8,249,278,491,861	(435,996,670,233)	-5.02
Fedha zilizotumika (Sh)	1,955,626,456	35,141,163,606		

Kwa ujumla kwa mwaka wa fedha 2012/13, matumizi ya kawaida yalipungua ukilinganisha na matumizi hayo katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/12.

**4.1.5 Ulinganisho wa fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na matumizi halisi ya maendeleo katika Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa (Isipokuwa Fedha za Serikali za Mitaa)**

Katika mwaka wa fedha 2012/2013, fedha zilizotumika kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ni Sh.3,203,098,332,184 wakati fedha zilizotolewa na Hazina zilikuwa Sh.3,247,527,081,386; hii inaonesha kwamba kiasi cha Sh.44,428,749,202 hakikutumika, ambacho ni sawa na asilimia 1.4.

Katika mwaka wa fedha 2012/2013 matumizi halisi ya maendeleo yalipungua kwa Sh.173,197,814,002 sawa na asilimia 5.1; ikilinganishwa na matumizi yalivyokuwa katika mwaka wa fedha wa 2011/2012.

Muhtasari wa mchanganuo huu ni kama ifuatavyo:

## Jedwali 14: Ulinganisho wa fedha zilizotolewa kwa matumizi ya maendeleo na matumizi halisi

Mwaka wa fedha	2011/2012	2012/2013	Tofauti	Asilimia ya Ongezeko/ (Punguzo)
Fedha zilizotolewa (Sh)	3,384,431,758,346	3,247,527,081,386	(136,904,676,960)	-4.1
Matumizi halisi (Sh)	3,376,296,146,186	3,203,098,332,184	(173,197,814,002)	-5.1
Fedha zisizotumika (Sh)	8,135,612,160	44,428,749,202		

Kwa ujumla kwa mwaka wa fedha 2012/13, matumizi ya maendeleo yalipungua ukilinganisha na matumizi hayo katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/12.

### Mapendekezo

Ukaguzi wa mwaka wa fedha 2012/13 umebaini kwamba, utekelezaji wa bajeti ya Serikali kuu katika upande wa mapato na matumizi ulikua wa kuridhisha kwa wastani. Kilikua na uboreshaji wa mifumo ya uchumi (macro-control) ili kupata tija na ukuaji wa uchumi na maendeleo. Serikali ilifuata sheria, taratibu na miongozo mbalimbali ambayo ilisaidia kuongezeka kwa mapato japokua yalikua chini ya bajeti zilizo idhinishwa.

Ufanisi wa bajeti na mapato halisi ya ndani kwa miaka mitatu iliyopita umeonesha ongezeko la wastani. Serikali inatakiwa kuchukua hatua madhubuti katika eneo hili, ikiwemo; kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani na kurekebisha mifumo ya bajeti ili iweze kutekelezwa na kufikia malengo.

Serikali inashauriwa kuandaa bajeti yenye uwiano halisi na sawia (realistic budget), na Hazina ipeleke fedha kwenye Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa kama zilivyoidhinishwa na bunge. Kwa njia hii utekelezaji wa bajeti utafikiwa, na kiasi kikubwa na kupunguza uhamisho wa fedha wa mara kwa mara kati ya mafungu mbalimbali.

Pia, Serikali iboresha viashiria vya mapato ya ndani na ya nje, pamoja na kuwasiliana kwa karibu na wadau wa

maendeleo ili watimize kwa wakati ahadi zao katika kutoa fedha za misaada kwa Serikali.


**4.1.6 Uwiano wa Mapato yasiyotokana na Kodi dhidi ya bajeti**  
 Bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya mapato yasiyotokana na kodi katika Wizara na Idara (MDA), Balozi za nje na Sekretarieti za Mikoa (RS) kwa mwaka wa fedha 2012/2013 ilikuwa Sh.644,514,571,682, Sh.15,967,759,508, na Sh.65,245,988 kwa mtiririko huo. Makusanyo halisi ya mapato yalikuwa Sh.461,138,111,562, Sh.19,918,065,207, na Sh.2,127,827,139 kwa Wizara na Idara, Balozi na Sekretarieti za Mikoa. Kulikuwa na mapungufu katika ukusanyaji wa Wizara na idara zake wa Shs.183,376,460,120 sawa na asilimia 28 ya makisio, Balozi zilivuka viwango vya makusanyo kwa Sh.3,950,305,700, na sawa na asilimia 28, na Sekretarieti za Mikoa nazo zilivuka malengo kwa Sh.2,060,456,151 sawa na asilimia 3,157 ya makisio ya bajeti.

Aidha, bajeti iliyoidhinishwa ya mwaka 2011/2012 kwa ajili ya mapato yasiyotokana na kodi katika Wizara na idara, Balozi za nje na Sekretarieti za Mikoa kwa mwaka wa fedha 2012/2013 ilikuwa Sh.342,176,244,002, Sh.13,502,649,717, na Sh.65,091,271 kwa mtiririko huo. Makusanyo halisi ya mapato yalikuwa Sh.361,334,264,994, Sh.21,413,335,285, na Sh.8,129,873,913 kwa Wizara na Idara, Balozi na Sekretarieti za Mikoa. Kujumla mapato halisi yalikuwa Sh.483,184,003,908 sawa na asilimia 73.1 ikilinganishwa na lengo la mwaka la Sh.660,547,577,178.

**Jedwali 15: Muhtasari wa mapato yasiyotokana na kodi (Kiasi kwa Sh.Milioni)**

	MDA	Balozi	RS	Jumla	MDA	Balozi	RS	Jumla
Makisio idhinishwa	644,515	15,968	65	660,548	342,176	13,503	65	355,744
Makusanyo halisi	461,138	19,918	2,128	483,184	361,334	21,413	8,130	390,877
Ziada/ (Pungufu)	(183,376)	3,950	2,063	-(177,363)	19,158	7,911	8,065	35,134

## Vielelezo Na. 5: Mwenendo wa ukusanyaji wa mapato ya Wizara, Sekretarieti za mikoa na Balozi za Nje



### Pendekezo

Serikali inashauriwa kuandaa bajeti halisia ili kuweza kuongeza ufanisi katika makusanyo ya mapato yasiyotokana na kodi kutoka kwenye Wizara na Idara zake.

#### 4.1.7 Kushindwa kurejesha pesa za Mpango wa Mabakizo, Sh.3,501.5 billioni

Serikali ina makubaliano na Wizara pamoja na idara zake 5 ya kuweka kiwango maalum cha makusanyo yao kwenye mfuko mkuu na kisha kiwango maalum kitolewe kama fidia kwa Wizara na idara husika chini ya mfuko wa Mabakizo.

Zoezi la ukaguzi katika Wizara na idara husika limebaini kwamba Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto pamoja na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi hazikurejeshewa Sh.225,408,501 na Sh.3,276,065,574 sawa na jumla ya Sh.3,501,474,075 kinyume na makubaliano ya mpango wa mabakizo.

## **Pendekezo**

Serikali inashauriwa kutekeleza sera ya mpango wa mabakizo kwa kurejesha fedha kwa wizara pamoja na idara zake kulingana na makubaliano ya makusanyo yao. Marejesho/ fidia hizi zitasaidia wizara pamoja na idara zake kufikia malengo yao na hasa kuongeza tija katika makusanyo.

### **4.1.8 Masuala mengine yanayohusu bajeti**

Katika ukaguzi wa mwaka wa fedha 2012/13, masuala mengineyo yaliyojitokeza yamewekwa kwenye barua za ukaguzi zilizoenda kwa uongozi husika wa Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa. Kwa ufupi masuala yaliyojitokeza ni haya yafuatayo:

- Baadhi ya Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa hazikukusanya mapato yasiyotokana na kodi kama yalivyo katika bajeti. Athari zake ni kupungua kwa makusanyo kwa Sh.177,363,000,000. Pia, kuna baadhi ya Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa zilizoweka chini sana viwango vyao vya bajeti kiasi cha kuathiri uwezo wao wa ufanisi kwani malengo ya makusanyo yalifikwa kwa urahisi sana.
- Baadhi ya Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa zilitumia fedha zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa na matumizi yalilipiwa kwa kutumia vifungu visivyo sahihi kiuhasibu.
- Hazina ilitoa pesa pungufu za matumizi ya kawaida na za maendeleo ukilinganisha na kiasi kilichoidhinishwa na bunge. Kwa ujumla tatizo hili limeonekana kwenye kila Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa.
- Japokua kulikua na upungufu wa fedha zilizopelekwa kwenye Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa, kwa baadhi ya taasisi upungufu ulikuwa mkubwa sana kiasi cha kushindwa kulipia gharama za muhimu na msingi. Mfano, baadhi ya Ofisi za Balozi zilishindwa kulipia huduma za maji na umeme.
- Fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwenda kwenye Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa zilitumwa mwishoni mwa mwaka wa Serikali 30 Juni 2013. Katika

baadhi ya taasisi fedha zilipokelewa wiki ya mwisho ya mwezi Juni 2013. Kwa upungufu huu haitakua rahisi kwa Taasisi husika kupata muda wa kutosha wa kutumia fedha hizo kutekeleza mipango mbalimbali iliyopangwa na kuidhinishwa. Pia, taasisi zinashindwa kufuata taratibu za fedha na manunuzi kwani muda huwa ni mfupi kuelekea mwisho wa mwaka wa Serikali.

- Ni vigumu kwa Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa kufikia malengo yaliyowekwa endapo mapungufu haya hayatapatiwa ufumbuzi.

### Mapendekezo

Serikali iboreshe na kuimarisha mifumo ya fedha na ya kibajeti katika Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa, ili kuifanya bajeti iwe chombo halisi cha udhibiti wa matumizi Serikalini.

#### 4.1.9 Ulinganisho wa madai yanayodaiwa katika Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa dhidi ya bajeti


Katika mwaka wa fedha 2012/13 jumla ya madai (liabilities) katika Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa yalikuwa Sh.595,568,566,057. Uwiano wa madai hayo na bajeti ulikuwa ni asilimia 3.9 kwa mwaka wa fedha 2012/13 ukilinganisha na ilivyokuwa mwaka wa fedha 2011/12 (asilimia 6.6) na mwaka wa fedha 2010/11 (asilimia 9.1).

jedwali hapa chini.

#### Jedwali 16: Uwiano wa madai na bajeti kutoka mwaka 2010/11 hadi 2012/13 unaoneshwa kwenye

Mwaka	Madai (Sh)	Bajeti (Sh)	Uwiano wa madai na bajeti (asilimia)
2012/2013	595,568,566,057	15,191,944,300,000	3.9
2011/2012	899,000,000,000	13,525,895,350,000	6.6
2010/2011	1,058,000,000,000	11,609,557,584,000	9.1

**Kielelezo Na. 6: Pia taarifa hii inaoneshwa katika chati mhimili hapa chini:**



Madhara ya madai endapo yanapokuwa makubwa ni kutumia kiasi kikubwa cha bajeti ya mwaka husika ili kulipa madai ya miaka iliyopita, fedha hizo zinazolipa madai ya miaka ya nyuma zingeweza kutumika kulipia gharama za shughuli mbalimbali zilizoidhinishwa na kuwa katika bajeti kwa mwaka wa fedha husika. Ulipaji wa madai ya miaka ya nyuma imekua ni miongoni mwa sababu zinazochangia uhamishaji wa fedha kati ya mafungu ya Serikali wakati wa utekelezaji wa bajeti.

**Mapendekezo**

Serikali ipitie upya mfumo mzima wa bajeti taslim (cash budget system), ili pamoja na mambo mengine iweze kubadilisha muda/vipindi vya kutoa fedha kwa Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa kutegemea na aina ya shughuli inayohitaji kutekelezwa na taasisi hizi.

**4.2 HESABU ZA TAIFA**

**4.2.1 Utangulizi**

Sura hii ya Hesabu za Taifa inajumuisha Hazina, Ukaguzi wa awali wa mafao ya wasitaafu na Mamlaka ya Mapato

Tanzania. Hazina inajumuisha Deni la Taifa, Bajeti na Hesabu za Majumuisho.

#### **4.2.2 Deni la Taifa**

Deni la taifa ni jumla ya madeni yaliyopo hadi 30 Juni 2013 ambayo Serikali na taasisi zake inawajibika kulipa. Sheria ya Madeni, Dhamana na Misaada ya Serikali ya mwaka 1974 (iliyorekebishwa 2004) ndio sheria inayoongoza uendeshaji wa shughuli za deni la taifa. Kulingana na vifungu namba 3 na 6 vya sheria hii, Waziri wa Fedha ndiye mwenye dhamana ya kusimamia madeni ya ndani pamoja na madeni ya nje kwa niaba ya Serikali.

Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 deni la taifa lililotolewa taarifa kuwa kiasi cha Sh. 21,202.4 bilioni ikilinganishwa na kiasi cha Sh. 16,976 bilioni kwa mwaka 2011/2012 ikiwa ni ongezeko la Sh.4,226.4 bilioni sawa na asilimia 24.9. Ufutao ni mtirriko wa deni la taifa likijumuisha deni la ndani na deni la nje ya nchi.

##### **(a) Deni la ndani**

Deni la ndani ni dhamana za Serikali za muda mfupi, dhamana Serikali za muda mrefu na madeni mengine yasiyowekewa dhamana. Hadi mwisho wa mwaka wa fedha 2012/2013 deni la ndani lilikuwa kiasi cha Sh. 5,775 bilioni ikilinganishwa na kiasi cha Sh. 4,546 bilioni kwa mwaka 2011/2012 ikiwa ni ongezeko la asilimia 27.

Uchambuzi wangu umebaini kwamba kuongezeka kwa deni la ndani kumesababishwa zaidi na kubadilishwa kwa hati za ukwasi (conversion of liquidity paper into financing) kugharamia bajeti ya Serikali, Sh.339.5 bilioni pamoja na kubadilisha deni la muda mfupi katika akaunti ya benki, Sh.469.5 bilioni. Jumla ya Sh.809 bilioni sawa na asilimia 65.82 zilibadilishwa na hivyo kupelekea deni kuongezeka kwa kiasi hicho. Uchambuzi huu unajaribu kuonyesha mapungufu yatokanayo na kusimamia fedha pamoja na ukwasi kuhusiana na ukubwa wa deni.


### (b) Deni la nje

Deni la nje ni madeni kutoka taasisi za kimataifa, nchi na washirika wengine wa maendeleo. Hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha 2012/2013 deni la nje lilikuwa kiasi cha Sh. 15,427 bilioni ikilinganishwa na kiasi cha Sh. 12,430 bilioni kilichokuwa mwaka 2011/2012; Ikiwa ni ongezeko la Shs.2,997 billion sawa na asilimia 24.1.

Uchambuzi wangu umebaini kwamba ongezeko la deni limesababishwa na mikopo kutoka kwa mabanki na wafadhili wa nje kwa ajili ya kusaidia miradi mikubwa ya maendeleo ikiwemo bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam, na uboreshwaji wa miundo mbinu katika nyanja za usafirishaji, maji safi, na mkongo wa mawasiliano wa taifa. Maoni yangu ni kwamba Serikali inahitaji kuwa angalifu zaidi kabla ya kukopa madeni yenye masharti kwani yamekuwa ghali sana kiuendeshaji.

Kielelezo Na. 7: Mchoro ufuatao unaonyesha jumla ya Deni la Taifa kama lilivyohakikiwa tarehe 30/06/2013;

**Kielelezo Na. 3: Ukuaji wa Deni la Taifa**



Kutokana na umuhimu pamoja na unyeti wa deni la taifa katika uchumi wa nchi, nimeagiza iundwe timu ya kuangalia mwenendo wa deni. Timu imeshaanza kufanya kazi na mara kazi ikikamilika taarifa itatolewa.

#### **4.2.2.1 Akaunti zilizodumaa za wadeni**

Uhakiki wa mseto wa deni la taifa umebaini akaunti 7 (saba) za wafadhili wanaodai Serikali zenye thamani ya Sh.1,247,429,775,458 ambazo hazikufanyiwa malipo yoyote tokea mwaka 1998. Ofisi ya Ukaguzi ilifahamishwa na Serikali kwamba malipo katika akaunti hizo yamesimama kwa sababu mazungumzo kati ya Serikali na wafadhili yanaendelea kwa nia ya kuipatia Serikali nafuu ya madeni, na hata pengine yanaweza kufutwa .

Hata hivyo, pamoja na kuomba vielelezo, ikiwa ni pamoja na hadidu za rejea juu ya kuwepo kwa mazungumzo na wafadhili ambao akaunti zao zimedumaa, bado Ofisi ya Ukaguzi haikuweza kupata vielelezo vya kutosha kuweza kujiridhisha uwepo wa mazungumzo hayo.

#### **Pendekezo**

Naishauri Serikali kufanya jitihada za makusudi na kuzungumza na wafadhili wenye akaunti zilizodumaa na pia kuwasilisha ofisini kwangu taarifa za juhudi zao kwa uhakiki.

#### **4.2.2.2 Kukosekana kwa Ofisi ya Deni la Taifa**

Chini ya muundo wa sasa wa usimamizi wa deni la taifa, kuna taasisi na idara kadhaa zinazoshughulika na masuala ya deni la taifa kama vile Wizara ya Fedha, Tume ya Mipango, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, na Benki Kuu ya Tanzania. Muundo huu sio mzuri kwa shughuli za kusimamia deni kwani utakuta kila idara, au taasisi inayosimamia deni tayari ina shughuli zake kuu tofauti na usimamizi wa deni la taifa. Kwa mtindo huo basi, inakuwa vigumu kwa watendaji kufanya kazi zao kwa pamoja katika kusimamia masuala ya deni la taifa.

Kuendelea kukosekana kwa Ofisi moja inayoshughulikia masuala ya Deni la Taifa (Debt Management Office -DMO)

imeendelea kuwa changamoto kubwa katika uendeshaji na usimamizi wa shughuli za denila taifa. Pia, imepelekea taarifa za kumbukumbu za madeni kushughulikiwa na idara tofauti, na wakati mwingine inakuwa vigumu kupata taarifa sahihi za deni kutoka kwenye ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali na kulazimika kulinganisha taarifa hizo na zile za Msajili wa Hazina (TR) wa Serikali. Hivyo, kwa hali ya muundo wa sasa, usimamizi na uendeshaji wa deni la taifa unakuwa hauko wazi katika suala zima la uwajibikaji.

### **Pendekezo**

Naishauri Serikali kuharakisha uanzishwaji wa Ofisi ya kusimamia Deni la taifa ili kuweza kuongeza ufanisi katika usimamizi na uendeshaji wake.

#### **4.2.2.3 Mkataba baina ya Serikali na Mfuko wa Pansheni wa Mashirika ya Uma (PPF).**

Serikali iliingia mkataba wa uwakala na PPF kwa ajili ya kutoa huduma ya malipo ya pensheni kwa wastaafu wa Serikali kuanzia tarehe 01/07/2008. Katika kupitia makubaliano hayo ilibainika kwamba kuna mapungufu ya taarifa za msingi kama vile kifungu juu ya usiri, uwajibikaji kwa upande wa wakala pale atakapokiuka makubaliano na uhai wa makubaliano yenyewe.

Pia, mkataba huo hauelezi muda halisi Serikali inaotakiwa kuwasilisha fedha kwa PPF, kwani makubaliano bado yanaeleza kuwa kipindi cha kulipia pensheni ni baada ya miezi sita, wakati sasa utaratibu ni ndani ya miezi mitatu na mabadiliko hayo hayajafanyika mpaka sasa.

Zaidi ya hayo, kifungu cha 4.1.16 cha mkataba wa uwakala kinaitaka Serikali kufanya mikutano ya kujadili utendaji wa PPF katika kila nusu ya mwaka au mahitaji yanapojitokeza. Lengo la mikutano hiyo ni kujadili masuala ya utendaji pamoja na masuala mengine yanayohusu mkataba. Hata hivyo, mpaka kufikia wakati wa uandishi wa taarifa hii Serikali haijawahi kufanya mikutano ya namna hiyo.

Ilibainika pia kwamba, kulingana na kifungu cha 4.2.7 cha mkataba, Serikali kwa kushirikiana na Wakala wanapaswa kuhakikisha wastaafu wanasaini vyeti vya kuthibitisha uwepo wao kila baada ya miaka miwili. Hata hivyo, Serikali haikuweza kuthibitisha kufanyika kwa zoezi hilo.

Mapungufu katika usimamizi wa mkataba huu wa uwakala yamesababisha Serikali kushindwa kufuatilia na kupima ufanisi wa PPF kama ambavyo ilivyobainishwa kwenye Mkataba wa Uwakala. Isitoshe, ukomo wa uwakala hauko wazi ndani ya mkataba na hivyo kujenga dhana ya kuwa na mkataba hauna ukomo/mwisho.

#### **Mapendekezo**

Serikali inashauriwa kupitia upya mkataba na kujumuisha ndani yake vipengele muhimu vinavyokosekana kama ilivyoainishwa hapo juu.

Kwa yale mambo yaliyopo ndani ya mkataba na kuhitaji utekelezaji, Serikali inashauriwa kuyatekeleza ipasavyo.

#### **4.2.2.4 Mfumo wa Jumuiya ya Madola wa Kurekodi na Kusimamia Madeni (CS-DRMS)**

CS-DRMS ni mfumo wa Jumuiya ya Madola wa Kurekodi na Kusimamia Madeni; ni mfumo jumuishi unaotunza taarifa za madeni ya ndani na nje, misaada na ukopeshaji wa Serikali kwa ajili ya usimamizi wa kila siku. Mfumo huu unasimamiwa na Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ambae ndio mtunza taarifa za madeni.

Niliweza kuona kwamba, utunzaji wa kumbukumbu mbadala na taratibu za kuokoa taarifa za madeni hautoshelezi endapo majanga yanayoathiri utunzaji wa kumbukumbu yatajitokeza.

Zaidi ya hayo, hakuna utaratibu wa kufanya majaribio ya utunzaji wa kumbukumbu mbadala ili kuona kwamba kumbukumbu za deni ziko salama kiasi gani endapo utunzaji wa kawaida wa kumbukumbu utaathirika.

### **Pendekezo**

Vilevile naishauri Serikali kuanzisha taratibu zitakazoleta ufanisi katika kusimamia na kutunza utunzaji wa taarifa mbadala na uokoaji wa taarifa hizo.

#### **4.2.2.5 Kubadilisha Hati za Ukwasi kugharamia nakisi ya bajeti (Conversion of liquidity paper into financing paper)**

Ukaguzi wa Deni la Taifa umebaini upungufu wa mapato ukilinganishwa na matumizi na kusababisha Serikali kubadilisha hati za ukwasi za muda mfupi zenye thamani ya Sh.339,490,810,000 na kuwa hati za kugharamia uendeshaji wa bajeti. Kubadilishwa kwa hati za ukwasi kulisababisha Serikali kutozwa riba ya Sh.21,543,703,100.

Istoshe, Hati za Ukwasi za muda mfupi hutolewa na Serikali kwa lengo la kudhibiti mfumuko wa bei. Serikali huuza hati za ukwasi ili kuondoa pesa kwenye uchumi wa ndani kwa lengo la kupunguza mzunguko wa fedha na hivyo kudhibiti mfumuko wa bei.

Hata hivyo, pamoja na nia njema ya Serikali ya kudhibiti mfumuko wa bei kwa kutumia sera za kifedha, lakini bado kumekuwa na utaratibu wa sasa wa kubadilisha hati za ukwasi kila inapokabiliwa na nakisi ya bajeti. Hali hii inapelekea kuongezeka kwa Deni la Taifa mara hati hizo zinapobadilishwa. Isitoshe, utaratibu huu wa kubadilisha hati za ukwasi za muda mfupi unakinzana na sera ya Serikali ya kudhibiti mfumuko wa bei kwa maana ya kupunguza wingi wa fedha katika soko la ndani.

### **Pendekezo**

Naishauri Serikali kuepuka kubadilisha hati za ukwasi za muda mfupi.

#### **4.2.2.6 Nakisi ya muda mrefu ya Serikali**

Kifungu cha 34 (2)(a) cha Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, 2006 kinaagiza kwamba: “Kila malipo ya awali yatolewayo kwa Serikali chini ya kifungu hiki yatakuwa kwa ajili ya sababu ya kuisitiri Serikali kifedha kwa muda mfupi na

hivyo yatapaswa yalipwe ipaswavyo ndani ya siku mia moja na themanini”

Wakati wa zoezi la ukaguzi, niligundua kwamba akaunti za Serikali zilizoko Benki Kuu zimekuwa na nakisi katika kipindi chote cha miaka ya fedha ya 2011/2012, na 2012/2013 kwa kiwango cha Sh.469,484,405,012 na Shs.263,866,358,436 kwa mtiririko huo. Vilevile nakisi zilisababisha tozo ya riba ya Sh.42,288,317,341 kwa kipindi cha mwaka 2011/2012 na Sh.53,223,549,921 kwa kipindi cha mwaka 2012/2013. Uendeleaji wa nakisi ya akaunti za Serikali unachangiwa na mapungufu katika usimamizi wa fedha taslimu pamoja na makusanyo yasiyotosheleza.

Zaidi ya hayo, katika kipindi cha fedha cha mwaka 2011/2012, Serikali ilibadilisha deni lake benki kuu lenye thamani ya Shs.469,484,405,012 na kuwa Hati funganiMaalum (Special bond) za muda mrefu itakayokombolewa mwezi Oktoba, 2022 kwa makubaliano ya riba ya asilimia 11.4 na hivyo kusababisha tozo ya Sh bilioni 27 ambayo haikutengewa fedha wakati wa bajeti.


### **Pendekezo**

Naishauri Serikali kuimarisha usimamizi wa fedha taslimu na kutumia fursa ya deni la kibenki pale tu inapotokea dharura

#### **4.2.2.7 Ushiriki mkubwa wa Benki za Biashara katika Soko la Hisa za Serikali**

Mchanganuo wa wamiliki wa hisa na hati za Serikali za muda mrefu na mfupi pamoja na dhamana zilizoko sokoni kwa mwaka wa fedha ulioisha tarehe 30 mwezi Juni, 2013 ulikuwa na thamani ya Sh.5,765,404,222,296. Upembuzi wa muundo wa wamiliki unaonyesha kwamba Benki za Biashara zinaongoza kwa kumiliki sehemu kubwa ya hisa kwa asilimia 48 kama inavyoonyeshwa hapa chini:

### Mchoro Na. 8: Mchanganuo wa Hisa za Serikali



Umiliki wa asilimia 48 ya hati na dhamana za Serikali unapelekea kudumaza soko la wawekezaji kwani mtaji mkubwa wa taasisi za kibenki tayari umewekezwa katika soko la awali. Tabia ya mabenki kuwekeza mtaji mkubwa kwenye hati na dhamana za Serikali, unapelekea makampuni na wananchi kushindwa kupata mikopo nafuu kutoka kwenye mabenki na hivyo kuikoshesha Serikali mapato ambayo yangetokana na shughuli za kiuzalishaji za wananchi. Mwisho Serikali inajikuta ikiendelea kukopa ili iweze kuendesha shughuli zake za kimaendeleo na kiutendaji.

Ifahamike kwamba wingi wa benki za biashara katika kumiliki hati na dhamana za Serikali katika Soko la awali unachochea na kukosekana kwa mikakati madhubuti ya kuboresha Soko la pili. Japokuwa natambua kwamba Serikali imefanya kazi kubwa katika kushirikisha soko la awali kuhusiana na utoaji wa dhamana za Serikali sokoni, lakini bado Serikali inao wajibu wa kutengeneza mazingira rafiki katika soko la mitaji. Ushiriki wa taasisi za kifedha katika soko la mitaji utapelekea hati na dhamana za Serikali kuuzwa na kununuliwa pasipo shaka au hofu na wadau wote, tofauti na ilivyo sasa. Wadau, kwa maana ya

wananchi na makampuni binafsi wanapenda kuwekeza katika soko lenye uhakika na ambalo wanaweza kununua na kuuza hati pasipo shaka.

Hivyo basi, kukosekana kwa soko la mitaji lililochangamka inapelekea dhamana za Serikali kukosa mvuto wa kibiashara sokoni na kuuzwa kwa bei isiyo na ushindani. Wanunuzi wachache waliopo sokoni, kwa maana ya mabenki, ndio wanunuzi wenye utashi wa kuzimiliki hati hadi zifikapo ukomo katika soko la awali. Hivyo mabenki yanajikuta hayawezi tena kununua hati na dhamana kwenye soko la upili. Wadau nao wanashindwa kuingia katika soko la upili na hivyo kuzifanya hati ziendelee kununuliwa katika soko la awali kwa bei isiyotosheleza na hivyo kupelekea mahitaji ya Serikali kifedha kuendelea kukua.

Kwa mantiki hiyo basi, hati na dhamana za Serikali zinapouzwa kwa bei pungufu katika soko la awali inaongeza gharama na ukuaji wa deni la taifa kwani tayari hizo hati zinazwa chini ya thamani yake (face value) na hivyo kuilazimu Serikali kuuza hati nyingi zaidi ili kufikia malengo yake; vilevile kuna malipo ya riba na kuponi, na mwisho kuna athari hatarishi ya mwendelezo wa kumiliki hati ili kukidhi mahitaji ya Serikali.

### **Pendekezo**

Naishauri Serikali ihamasishe taasisi za kifedha nchini kama vile mabenki ya kibiashara, Pensheni, na Mifuko ya Bima kushiriki katika soko la Upili ambapo hisa za Serikali zitaweza kuuzwa na kununuliwa pasipo kuathiri mwenendo wa deni la taifa.

#### **4.2.2.8 Kutofanyika kwa uthamini wa Mfuko wa Mafao ya Uzeeni**

Mafao ya uzeeni ya watumishi wa Umma waliostaafu yanayolipwa kupitia katika Mfuko Mkuu wa Serikali, yanatakiwa kutambuliwa na Serikali kama Mpango wa Mafao Uliotafsiriwa (defined benefit plan) hii ni kwa mujibu wa mwongozo Na. 25 wa IPSAS (IPSAS Accrual no. 25).

Baada ya kuhakiki mfuko wa mafao ya wastaafu wa Serikali (Mafao ya Wastaafu Waajiriwa wa muda mrefu) nimebaini kwamba uendeshwaji wake unakinzana na Aya ya 166 ya mwongozo na. 25 wa Viwango vya kimataifa wa kuandaa hesabu katika sekta ya umma (IPSAS 25 para 166), ambapo Serikali ilishindwa kufanya tathmini sahihi ya mpango wa mafao uliotafsiriwa ili kuiwezesha Serikali kufahamu madai ya mwanzo ya mafao kufuatia kuanza kutumia rasmi mwongozo wa kimataifa wa kihasibu wa kuandaa heasabu katika sekta ya umma (IPSAS Accrual) na hivyo, Serikali haiwezi kufahamu takwimu sahihi kuhusu manufaa/ faida au hasara, na hata pengine gharama pamoja na riba za mfuko.

### **Pendekezo**

Naishauri Serikali inapoandaa hesabu zake kuzingatia mwongozo namba 25 Kimataifa wa Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS Accrual) na tathimini ya mafao ya uzeeni ifanyike.

#### **4.2.3 Mamlaka ya Mapato Tanzania**

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Na.11 ya mwaka 1995 kama ilivyorekebisha na Sheria Na.8 ya mwaka 1996 ikiwa na majukumu ya kusimamia ukusanyaji wa kodi za Serikali Kuu pamoja na ukusanyaji wa mapato mbalimbali ya Serikali. Mamlaka inatengeneza aina mbili za Taarifa za Hesabu ambazo ni zile za Mapato na Taarifa ya Hesabu za Matumizi. Taarifa ya Hesabu za Matumizi inaandaliwa kwa kutumia Viwango vya Kimataifa vya Tarifa za Fedha (IFRS) wakati zile za Mapato huandaliwa kwa kutumia Viwango vya Kimataifa vya kihasibu katika Sekta ya Umma kwa misingi ya fedha taslimu.

##### **4.2.3.1 Bakaa ya mapendekezo ya ukaguzi hayajashughulikiwa na TRA;**

Hadi tarehe Januari 08, 2013 nilipotoa ripoti ya ukaguzi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania(TRA) kulikuwa na bakaa ya mapendekezo ya ukaguzi hayajashughulikiwa jumla ya

Sh.765,761,469,666 na Dola za Kimarekani 65,206,108.82 yakisubiri kujibiwa na TRA kutokana na ripoti za miaka ya nyuma ukilinganisha na Sh. 545,273,124,808 na Dola za Kimarekani 210,072,760 zilizokuwa hazijajibiwa wakati wa kutoa ripoti ya TRA ya mwaka 2011/2012 kama inavyoonekana hapa chini:

**Jedwali 17: Masuala ya Mamlaka ya Mapato yaliyosalia**

Mwaka	2012/2013		2011/2012	
	Kiasi(Sh.)	Kiasi (Dola za Kimarekani)	Kiasi (Sh.)	Kiasi (Dola za Kimarekani)
<b>(i) Maduhuli</b>				
Idara ya Forodha	37,969,095,172	163,000	25,019,207,641	-
Idara ya Kodi za Ndani	16,975,679,331	-	16,955,384,161	-
Idara ya Walipakodi Wakubwa	661,727,408,695	65,043,109	503,166,532,902	105,036,380
<b>Jumla Ndogo</b>	<b>716,672,183,198</b>	<b>65,043,109</b>	<b>545,141,124,704</b>	<b>105,036,380</b>
<b>(ii) Matumizi</b>				
TRA Makao Makuu	49,089,286,468	-	132,000,104	-
<b>Jumla Ndogo</b>	<b>49,089,286,468</b>	<b>-</b>	<b>132,000,104</b>	<b>-</b>
<b>Jumla</b>	<b>765,761,469,666</b>	<b>65,206,109</b>	<b>545,273,124,808</b>	<b>105,036,380</b>

Baadhi ya masuala yaliyoainishwa kwenye jedwali hayakujibiwa kikamilifu tangu mwaka 2001/2002 na mengi ya hayo yanasubiri maamuzi ya Mahakama na kibali cha kufutwa kutoka bungeni.

**Pendekezo**

Serikali inashauriwa kuhakikisha kuwa hatua zinachukuliwa haraka iwezekanavyo kutekeleza mapendekezo ya ukaguzi ili kumaliza masuala yote yaliyosalia.

#### 4.2.3.2 Ukusanyaji wa Mapato

Hesabu za Mapato zinaonyesha kuwa kiasi cha Sh.8,117,588,095,662 kilikusanywa Tanzania Bara ikilinganishwa na makisio ya Sh.8,370,728,200,000 na kufanya makusanyo pungufu ya Sh.253,140,104,338 sawa na asilimia 3 ya makisio ya mapato ya mwaka.

Wakati huo huo makusanyo ya Zanzibar, yalikuwa Sh.103,866,495,532 ikilinganishwa na makisio ya Sh.106,730,400,000 na kufanya makusanyo pungufu kwa Sh. 2,863,904,468 sawa na asilimia 2.7 ya makisio ya Mapato ya mwaka.

Mchanganuo wa makusanyo ya mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa idara ni kama ifuatavyo katika jedwali namba 17 hapa chini:-

#### Jedwali 18: Mapato yaliyokusanywa - Tanzania Bara

Idara	Makisio Sh.	Makusanyo halisi Sh.	Ziada/Pungufu ya makusanyo Sh.	Asilimia
Idara ya Kodi za Ndani	1,411,645,400,000	1,520,625,330,860	108,979,930,860	7.7
Idara ya Walipakodi Wakubwa	3,747,622,500,000	3,533,067,632,720	(214,554,867,280)	-5.7
Idara ya Forodha	3,173,605,000,000	3,042,375,952,125	(131,229,047,875)	-4.1
<b>Jumla ndogo</b>	<b>8,332,872,900,000</b>	<b>8,096,068,915,705</b>	<b>(236,803,984,295)</b>	<b>-2.8</b>
Ongeza: Vocha za Hazina	37,855,300,000	21,519,179,957	(16,336,120,043)	-43.2
<b>Jumla</b>	<b>8,370,728,200,000</b>	<b>8,117,588,095,662</b>	<b>(253,140,104,338)</b>	<b>-3</b>

### Jedwali 19: Mapato yaliyokusanywa - Zanzibar

Idara	Lengo Sh.	Makusanyo halisi Sh.	Ziada/Pungufu ya Makusanyo Sh.	Asilimia
Idara ya Kodi za ndani	39,653,400,000	40,043,848,826	390,448,826	0.98
Idara ya Forodha	67,077,000,000	63,822,646,706	(3,254,353,294)	(4.9)
<b>Jumla</b>	<b>106,730,400,000</b>	<b>103,866,495,532</b>	<b>(2,863,904,468)</b>	<b>(2.7)</b>

#### 4.2.3.3 Uchambuzi wa mwelekeo wa makusanyo

Mtiririko wa ukusanyaji wa mapato kwa kipindi cha miaka mitatu kwa upande wa Tanzania bara umeonyesha kuwa kuna ongezeko la makisio ya makusanyo sambamba na ongezeko la makusanyo halisi. Makusanyo katika mwaka huu wa fedha yamekuwa pungufu ya malengo kwa asilimia 3 ukilinganisha na makusanyo ya asilimia 4 juu ya lengo kwa mwaka 2011/2012.

Kwa upande mwingine makadirio na makusanyo ya kodi kwa Zanzibar yameendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka. Hata hivyo, kwa mwaka huu wa fedha kumekuwa na ongezeko dogo la makisio ikilinganishwa na mwaka uliyopita na kusababisha makusanyo pungufu kwa asilimia 2.7 ikilinganishwa na asilimia 8.9 ya mwaka 2011/2012.


Mwelekeo wa makusanyo ya mapato Tanzania Bara na Zanzibar kwa miaka mitatu mfululizo ni kama ifuatavyo katika jedwali namba 19 hapa chini:-

#### Jedwali 20: Makusanyo ya mapato Tanzania bara

Mwaka	Lengo Sh.	Makusanyo halisi Sh.	Tofauti Sh.	Asilimia
2010/11	5,849,093,700,000	5,550,203,244,379	(298,890,455,621)	-5.1
2011/12	6,456,832,630,000	6,703,229,704,888	246,397,074,888	3.8

2012/13	8,370,728,200,000	8,117,588,095,662	(253,140,104,338)	-3
---------	-------------------	-------------------	-------------------	----


### Kielelezo Na 9: Mwelekeo wa Makusanyo ya Mapato - Tanzania Bara



### Jedwali 21: Mwelekeo wa Makusanyo ya Mapato - Zanzibar

Mwaka	Lengo Sh.	Makusanyo Halisi Sh.	Tofauti Sh.	Asilimia
2010/11	69,240,800,000	76,357,574,602	7,116,774,602	10.3
2011/12	100,581,100,000	91,652,054,954	(8,929,045,046)	-8.9
2012/13	106,730,400,000	103,866,495,532	(2,863,904,468)	-2.7

### Mwelekeo wa makusanyo kama unavyoonekana katika chati mhimili (Tanzania Zanzibar)



#### 4.2.3.4 Misamaha ya Kodi Sh. bilioni 1,515.6

Serikali ya Tanzania kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inatoa misamaha ya kodi kwa walengwa mbalimbali kwa lengo la kukuza biashara na sababu za kibinadamu kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zilizopo. Taarifa za Mapato kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2013 zimeonyesha kuwa kiasi cha Sh.1,515,607,377,799 ni misamaha ya jedwali Na.21 hapa chini;

#### Jedwali 22: Muhtasari wa misamaha ya kodi kwa Taasisi mbalimbali

Na	Taasisi	Idara ya Forodha na Ushuru wa Bidhaa (Sh)	Idara ya Kodi za Ndani (Sh)	Jumla (Sh) 2012/2013	Jumla (Sh) 2011/12	Misamaha iliyo ongezeko / (kupungua) (Sh)	Asilimia ya ongezeko/ (punguzo)	Asilimia ya misamaha kwa Taasisi 2012/13
1	Sekta ya madini	351,926,383,883	-	351,926,383,883	140,637,400,000	211,288,983,883	150%	23.2
2	Mashirika ya Umma	25,290,046,478	-	25,290,046,478	15,699,616,106	9,590,430,372	61%	1.7
3	Balozi za Nje/Umoja wa Mataifa	15,144,779,702	-	15,144,779,702	10,194,000,000	4,950,779,702	49%	1
4	Misamaha ya Kodi katika Maduka yasiyotozwa kodi	-	9,801,420,712	9,801,420,712	7,726,106,679	2,075,314,033	27%	0.6
5	Taasisi za Kidini	513,729,447	-	513,729,447	438,967,358	74,762,089	17%	0
6	Kituo cha Uwekezaji	300,398,017,045	-	300,398,017,045	280,961,890,898	19,436,126,147	7%	19.8
7	Misamaha ya kodi kwenye maduka ya jeshi	2,200,383,324	-	2,200,383,324	2,454,600,000	(254,216,676)	-10%	0.1
8	Misamaha ya Kodi za Ongezeko la Thamani	-	571,733,155,336	571,733,155,336	801,859,518,440	(230,126,363,104)	-29%	37.7
9	Taasisi za Serikali	6,680,711,987	-	6,680,711,987	9,603,414,035	(2,922,702,048)	-30%	0.4
10	Miradi ya Wafadhili	122,461,951,497	-	122,461,951,497	225,039,689,862	(102,577,738,365)	-46%	8.1

Na	Taasisi	Idara ya Forodha na Ushuru wa Bidhaa (Sh)	Idara ya Kodi za Ndani (Sh)	Jumla (Sh) 2012/2013	Jumla (Sh) 2011/12	Misamaha iliyo ongezeko / (kupungua) (Sh)	Asilimia ya ongezeko/ (punguzo)	Asilimia ya misamaha kwa Taasisi 2012/13
11	Makampuni na watu binafsi	72,237,968,263	-	72,237,968,263	304,045,656,449	(231,807,688,186)	-76%	4.8
12	Taasisi zisizo za kiSerikali	1,409,421,040	-	1,409,421,040	7,542,700,000	(6,133,278,960)	-81%	0.1
13	Uchimbaji wa mafuta/gesi	35,809,409,085	-	35,809,409,085	Introduced in FY2012/13	35,809,409,085	100%	2.4
	<b>Jumla</b>	<b>934,072,801,751</b>	<b>581,534,576,048</b>	<b>1,515,607,377,799</b>	<b>1,806,203,559,827</b>	<b>(290,596,182,028)</b>	<b>-16%</b>	<b>100</b>

Mwenendo umeonyesha kuwa misamaha ya kodi kwa Tanzania Bara mwaka huu wa fedha imepungua ikilinganishwa na mwaka uliopita lakini bado ina athari katika makusanyo ya mapato. Mwenendo unaonyesha pungufu ya Sh. 290,596,182,028 sawa na asilimia 16 kutoka Sh. 1,806,203,559,827 zilizosamehewa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012 hadi Sh. 1,515,607,377,799 katika mwaka wa fedha 2012/2013. Endapo kiasi hiki cha Sh. 1,515,607,377,799 kingekusanywa, ambacho ni sawa na asilimia 19 ya makusanyo yote, makusanyo yote yangukuwa Sh. 9,633,195,473,461 badala ya Sh. 8,117,588,095,662. Misamaha ya kodi iliyotolewa kwa mwaka huu ni sawa na asilimia 10 ya bajeti yote ya mwaka 2012/2013 ya Sh. 15,191,944,300,000.

### Jedwali 23: Mwelekeo wa Misamaha ya Kodi kwa miaka, 2011/12-2012/2013

Maelezo	2012/2013 (Sh)	2011/2012 (Sh)
Lengo	8,370,728,200,000	6,456,832,630,000
Makusanyo Halisi	8,117,588,095,662	6,703,229,704,887
Misamaha	1,515,607,377,799	1,806,203,559,827
Asilimia ya Misamaha kwa makusanyo Halisi	19	27
Ziada/(Pungufu) la Makusanyo	(253,140,104,338)	246,397,074,887
Ziada kama misamaha isingetolewa	1,262,467,273,461	2,052,600,634,714

#### 4.2.3.5 Uwiano Kati ya Misamaha ya Kodi, Makusanyo na Pato la Taifa

Mwelekeo unaonyesha kuwa wakati kumekuwa na ongezeko la makusanyo kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita kutoka Sh.bilioni 4,052 mwaka 2008/09 hadi shilingi bilioni 8,117.6 billioni kwa mwaka 2012/2013, misamaha ya kodi imeongezeka kutoka asilimia 2.7 kwa mwaka 2008/2009 hadi asilimia 4.3 mwaka 2011/2012 na baadaye kushuka hadi asilimia 3.1 ya pato la taifa mwaka 2012/2013.

Kiwango cha misamaha ya kodi kimekuwa kwenye wastani wa asilimia 2.6 ya pato la taifa kati ya mwaka 2008/2009 na 2010/2011 kama inavyoonekana kwenye jedwali Na. 23 hapa chini.

**Jedwali 24: Uwiano wa mapato baada ya misamaha ya kodi dhidi ya pato la taifa (Shilingi katika milioni)**

Maelezo	2008/09	2009/10	2010/2011	2011/2012	2012/2013
Pato la Taifa	26,868,213.4	31,316,223.9	35,026,679	41,125,313	48,385,100
Makusanyo	4,051,963.8	4,437,933.4	5,315,148	6,703,230	8,117,588
Asilimia ya makusanyo dhidi ya pato la taifa	15.1	14.2	15.2	16.3	16.8
Jumla ya misamaha ya kodi	731,267.7	653,652.5	1,016,320.3	1,806,203.6	1,515,607.4
Asilimia ya misamaha ya kodi dhidi ya pato la taifa	2.7	2.1	2.9	4.3	3.1
Asilimia ya misamaha ya kodi dhidi ya makusanyo	18	14.7	19	27	19

**Chanzo:** *Ripoti Jumuiifu ya CAG ya mwaka 2011/2012, Taarifa za fedha za TRA za mwaka 2012/2013 na Mpango Mkakati wa Nne wa TRA kuanzia 2013/2014 hadi 2017/2018*

Uchambuzi wa misamaha ya kodi unaonyesha kuwa misamaha ya kodi inaonyesha kiwango cha juu, hasa ikizingatiwa kuwa Serikali inajitahidi kuongeza mapato. Pamoja na jitihada zinazochukuliwa kupunguza misamaha ya kodi, imeonekana kuwa hakuna viwango na miongozo iliyowekwa kuonyesha ukomo wa misamaha ya kodi ambapo haitakiwi kuzidi hapo.

**Pendekezo**

Serikali inashauriwa kuweka ukomo wa misamaha ya kodi na kuhakikisha kuwa misamaha haitolewi zaidi ya ukomo uliyowekwa, kwa mfano asilimia moja ya pato la taifa.

#### **4.2.3.6 Usimamizi wa Bohari za Forodha (Customs bonded Warehouse)**

Sehemu ya Nne ya Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na ya Kati (EACCMA) ya mwaka 2004, inaeleza kuwa mali zilizoingizwa nchini zinaweza kuhifadhiwa katika Bohari za Forodha za Serikali au Bohari za Forodha zilizodhaminiwa na watu binafsi zikisubiri kulipiwa kodi husika na walioziingiza nchini. Sheria hii pia imeainisha matakwa muhimu katika kuhakikisha usimamizi mzuri wa Bohari za Forodha zinazomilikiwa na Serikali na zile zinazodhaminiwa na watu binafsi ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa mali zinaondolewa kutoka kwenye Bohari hizo ndani ya wakati ulioanishwa kisheria.

Nimekagua uendeshaji wa baadhi ya Bohari za forodha hizo katika kipindi cha ukaguzi kwa madhumuni ya kupima kiwango cha utekelezaji wa taratibu za kisheria zilizoanishwa. Ukaguzi umebaini mapungufu yafuatayo ambayo yanaweza kuathiri ukusanyaji wa mapato ya Serikali:

- (c) Mali/bidhaa mbalimbali zenye ushuru jumla ya Sh.1,102,640,257 zilikuwepo ndani ya bohari zaidi ya muda uliokubalika kisheria na hakuna hatua zozote zilizochukuliwa za kukusanya mapato hayo.
- (d) Mamlaka ya Mapato Tanzania ilisimamisha na hatimaye kusitisha uendeshaji wa Bohari za Forodha kumi na tatu zinazosimamiwa na watu binafsi kabla ya kukusanya ushuru ya forodha mali zilizokuwemo ndani yake zenye jumla ya Shs. 1,803,910,991.
- (e) Bohari za Forodha 27 zilikutwa zikiendeshwa pasipo kibali halali kutoka kwa Kamishna wa Forodha na Ushuru wa Bidhaa. Hakuna hatua zozote za kisheria zilizochukuliwa kwa wamiliki wa bohari hizo ambao walikuwa wakiziendesha bila ya kuwa na leseni halali.

## **Pendekezo**

Serikali inashauriwa kuwa na usimamizi wa kutosha katika uendeshaji wa Bohari za Forodha za Serikali na zile zinazomilikiwa na watu binafsi ambazo kwa ujumla wake zipo chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Mapato. Sheria ichukue mkondo wake kwa ushuru wa forodha ambao haukukusanywa.

### **4.2.4 Hesabu Jumuifu za Taifa**

#### **4.2.4.1 Ufanisi wa makisio na matumizi ya fedha**

Uchambuzi wa Hesabu Jumuifu katika kipindi husika Serikali ilipanga kutumia kiasi cha Sh.11,026,416,297,537 kwa matumizi ya kawaida ikilinganishwa na kiasi halisi kilichotolewa cha Sh.10,672,471,478,499 na kupelekea kuwepo kwa kiasi cha Sh. 353,944,819,038 ambazo hazikutolewa sawa na asilimia tatu ya bajeti ya matumizi ya kawaida. Serikali ilitumia kiasi cha Sh.10,640,607,414,988. hivyo kupelekewa kuwepo kwa Sh.31,864,063,511 ambacho hakikutumika.

Mapitio yangu kwenye vifungu vya fedha za maendeleo yalibaini kwamba Serikali iliidhinisha kutumia kiasi cha Sh. 4,165,528,002,463 ukilinganisha na kiasi cha Sh.3,656,297,898,562 zilizopokelewa kutoka hazina na hivyo kiasi cha Sh 509,230,103,901 cha bajeti hakitolewa sawa na asilimia 12 ya bajeti ya matumizi ya maendeleo iliyopitishwa. Licha ya kutoa fedha pungufu za maendeleo, akaunti ya fedha za maendeleo ilikuwa na salio la fedha ambayo haikutumika kiasi cha Sh.40,066,146,199 kutokana na matumizi ya kiasi cha. Sh.3,616,231,752,363.

Serikalihaikuweza kutoa kiasi cha Sh.863.2 bilioni sawa na asilimia 6 ya bajeti nzima kwa mwaka. Kiasi hiki ni kikubwa na kina athari katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Serikali. Pia, nilibaini kuna ucheleweshwaji katika kupeleka fedha kwenda kwenye Wizara na idara zake na hivyo kuchangia kuwepo kwa bakaa lisilotumika mwishoni mwa mwaka.

#### 4.2.4.2 Matumizi ya fedha za miradi ya maendeleo

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2013 taarifa jumuiifu za taifa zilionyesha kiasi cha Sh.bilioni 3,616.2 zilitumika katika miradi ya maendeleo ya taifa. Kati ya kiasi kilichotumika cha Sh.2218,908,035,033 kilitokana na mapato ya ndani na Sh 1397,323,717,329 ikiwa sawa na asilimia 39 ya fedha ya maendeleo iliyotumika ilikuwa nia misaada toka kwa washirika wa maendeleo. Mchanganuo wa fedha za miradi ya maendeleo kwa kipindi cha miaka mitatu ni kama inavyoonekana hapa chini:

Mwaka	2010/11	%	2011/12	%	2012/13	%
Mapato ya ndani	1,308,351,876,622	59	2,095,412,910,757	62	2,218,908,035,033	61
Mapato toka nje	909,680,949,735	41	1,280,883,235,429	38	1,397,323,717,329	39
Jumla	2,218,032,826,357	100	3,376,296,146,186	100	3,616,231,752,362	100

Kulingana na mchanganuo hapo juu, mseto wa fedha kwa mwaka 2010/2011 ulikuwa ni asilimia 59 mapato ya fedha za ndani kwa asilimia 41 mapato kutokana na fedha za nje. Kwa mwaka 2011/2012 fedha za ndani ilikuwa ni asilimia 62 fedha za ndani na asilimia 38 fedha za nje; na 2012/2013 ilikuwa asilimia 61 fedha za ndani na asilimia 39 fedha za nje-misaada.

Tumebaini kuwa kuna mabadiliko madogo katika mseto wa vyanzo vya fedha za miradi ya maendeleo kwa kipindi cha miaka mitatu. Kwa ujumla, serikali imechangia fedha za miradi ya maendeleo kwa wastani wa asilimia 61 kwa kipindi chote cha miaka mitatu ambapo misaada toka nje imechangia kwa wastani wa asilimia 39 ya fedha yote ya miradi ya maendeleo.

#### 4.2.4.3 Makusanyo ya maduhuli Sh. 15,018.3 bilioni

Taarifa Jumuiifu ya mapato iliyoishia tarehe 30 Juni, 2013 inaonyesha makusanyo halisi ya kiasi cha Sh.15,018,268,312,814 ikilinganishwa na makadirio ya Sh. 15,191,944,300,000 hivyo kuleta upungufu wa makusanyo ya Sh.173,675,987,186 sawa na asilimia moja ya makisio

ya bajeti yaliyoidhinishwa. Vyanzo vya mapato ya Serikali kwa ajili ya matumizi ya kawaida ni pamoja na kodi na mapato yasiyokuwa ya kodi wakati mapato kwa ajili ya shughuli za maendeleo hutokana na ruzuku, na ukopaji wa nje na ndani ya nchi.

**Pendekezo:**

Serikali inashauriwa kuongeza jitihada kuhakikisha inafikia malengo ya ukusanyaji ili kuweza kutekeleza malengo yaliyokusudiwa.

**4.2.4.4 Taarifa ya Matumizi ya Serikali Sh.14,256.8 bilioni**

Matumizi ya Serikali yaliongezeka na kufikia kiasi cha Sh.14,328,769,377,061 kwa mwaka 2012/2013 ikilinganishwa na kiasi cha Sh.12,061,571,308,279 kwa mwaka wa fedha 2011/2012 hivyo kupelekea kuwepo kwa ongezeko la Sh.2,267,198,068,782 sawa na asilimia 15 ya matumizi yote ya Serikali.

Matumizi ya kawaida yalikuwa kiasi cha Sh. 10,672,471,478,499 ukilinganishwa na Sh.8,685,275,162,094 kwa mwaka wa fedha 2011/2012 sawa na ongezeko la asilimia 23 ya jumla ya matumizi ya kawaida. Matumizi ya maendeleo yalikuwa kiasi cha Sh.3,656,297,898,562 ukilinganisha na kiasi cha Sh.3,376,296,146,186 zilizotumika mwaka 2011/2012 sawa na asilimia 7 kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini:

**Jedwali 25: Taarifa ya Matumizi ya Serikali**

Aina ya Akaunti	2011/12 (Sh.)	2012/13 (Sh.)	Tofauti	Asilimia
Kawaida	8,685,275,162,094	10,672,471,478,499	1,987,196,316,406	23
Maendeleo	3,376,296,146,186	3,656,297,898,562	280,001,752,376	7
Jumla	12,061,571,308,280	14,328,769,377,061	2,267,198,068,782	15

**4.2.4.5 Utoaji wa fedha za matumizi mwisho wa mwaka**

Ukaguzi umebaini kuwa fedha za matumizi kutoka Hazina hazitolewa kwa wakati kulingana na mahitaji ya kibajeti. Imebainika kuwa kiasi cha Sh.1,066,315,820,918 sawa na asilimia 7.4 ya fedha iliyotolewa, kilitolewa wiki ya mwisho ya mwaka wa fedha. Vilevile, kiasi cha Sh.4,494,546,936,669 sawa na asilimia 31.4 ya fedha zilizotolewa, kilitolewa katika robo ya mwisho ya mwaka wa fedha kama ilivyoainishwa kwenye jedwali Na. 25 hapa chini:

**Jedwali 26: Fedha iliyotolewa kwa kila robo ya mwaka**

Robo	Fedha zilizotolewa (Sh.)	Asilimia (%)
1	3,953,903,730,993.16	27.6
2	2,710,184,285,943.08	18.9
3	3,170,134,423,153.47	22.1
4	4,494,546,936,669.63	31.4
	<b>14,328,769,376,759</b>	<b>100%</b>

**Pendekezo:**

Serikali inashauriwa kulinganisha mapato, bajeti na utoaji wa fedha ili kutekeleza shughuli zake kwa wakati. Vilevile, Serikali iache mtindo wa kutoa fedha wiki ya mwisho ya mwaka wa fedha ili kuepusha ushawishi wa matumizi mabaya ya fedha za Umma kwa mantiki ya kumaliza fedha iliyopokelewa.

**4.2.4.6 Taarifa ya upotevu Sh. 13,231,354,196**

Taarifa ya hesabu jumuiifu ilionyesha malimbikizo ya upotevu wa mali na vifaa vya kiasi cha Sh. 13,231,354,196 ikilinganishwa na Sh. 13,024,783,230 katika mwaka wa fedha 2011/2012 ikiwa ni ongezeko la Sh. 206,570,924 sawa na asilimia mbili. Serikali haijachukua juhudi madhubuti ili kupunguza matukio ya upotevu wa mali na vifaa au kuanzisha mchakato kwa ajili ya Bunge kufuta upotevu/hasara hizi. Kutokuwepo udhibiti imara wa mali na vifaa vya Serikali kunaweza kusababisha hasara nyingi siku za usoni.

**Pendekezo:**

Serikali inashauriwa kuchukua hatua za kupunguza hasara zinanzojitokeza ikiwa ni pamoja na kuliomba Bunge kufuta hasara zilizopo kwenye vitabu.

#### **4.2.4.7 Kutojumuishwa kwa hesabu za Mashirika ya umma na Mamlaka za Serikali za mitaa kwenye hesabu za Taifa**

Taarifa ya hesabu jumuiifu haikujumuisha hesabu za mamlaka za Serikali za mitaa na mashirika ya umma yanayotumia mwongozo wa kimataifa wa kuandaa hesabu (IPSASs accrual). Mwongozo wa IPSASs 6 unazitaka taasisi zote zilizo chini ya udhibiti wa Serikali kujumuisha hesabu za taasisi na mashirika yote yalioko ndani na nje ya nchi.

#### **4.2.4.8 Utekelezaji wa Viwango vya kimataifa vya Uhasibu.**

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliamua kutumia viwango vya kimataifa vya uhasibu kuanzia mwaka wa fedha ulioanzia 1 Julai, 2012. Ninatambua hatua ambazo Serikali imezichukuwa ikiwa ni pamoja na kuweka mpango kazi kwa ajili ya kutekeleza jukumu hilo ikiwa ni pamoja na kufanya mafunzo kwa watumishi wa kada mbalimbali wakiwemo wahasibu na watumishi wa kada zingine ili kuweza kufanikisha lengo. Pamoja na Serikali kuanza kutekeleza jukumu hilo, kuna changamoto zimejitokeza ambazo Serikali inahitaji kuzifanyia kazi ili kufanikisha utekelezaji wa zoezi kwa ufanisi. Changamoto hizo ni kama vile kukosekana kwa kamati ya kitaifa kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi, Changamoto kwenye thamani ya mali na vifaa vya Serikali na baadhi ya kazi zilizopo kwenye mpango kazi kutokamilika kwa wakati. Undani wa changamoto hizi umeainishwa kwa kirefu kama ifutavyo:-

##### **a) Mpango kazi kutotekelezwa kwa wakati**

Uchambuzi wa mpango kazi kwa ajili ya utekelezaji wa Viwango vya ukaguzi uligundua kuwepo kwa kazi ambazo hazijatekelezwa kwa wakati kama vile kutenganisha ruzuku na mikopo, kuandaa miongozo na chati za kiasibu hivyo kuchangia kutokamilika kwa mpango kazi.

### **b) Kutokuwepo kwa kamati ya kitaifa**

Serikali haijaweza kuanzisha kamati inayoweza kusimamia utekelezaji wa shughuli zilizobaki ili kufikia malengo kwenye mpango kazi. Na pia jukumu la IPSAS limeachwa kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali. Kwa mtazamo wa kikaguzi, suala la IPSAS ni suala mtambuka ambapo linahusisha wadau wengi ambao wana majukumu ya umiliki, kuthamini mali zinazo milikiwa na Serikali, kutambua mali zote.

### **c) Mali, Majengo, na Vifaa (PPE)**

Serikali imeingia katika kipindi cha mpito cha miaka mitano kuhusu taarifa za mali na vifaa vya Serikali (PPE). Nimeona kwamba Ofisi ya Mhakiki Mali Mkuu wa Serikali (DGAM) ina mpango kazi wa miaka 5 unaoonyesha shughuli za uhakiki mali za Serikali (kuanzia mwaka 2012/13 hadi 2016/17). Hata hivyo, Serikali haina budi kufanyia kazi changamoto zifuatazo:

- Japokuwa zoezi la kuthaminisha mali za Serikali limefanyika katika kipindi cha mwaka wa fedha 2005/06, bado Serikali haijaweza kuboresha taarifa za mali na vifaa (PPE) katika kumbukumbu zake zikiwemo utambuzi wa vifaa kwa namba maalum (bar code), ratiba ya kufuta mali katika daftari la mali, na mpangilio wa mali za kifedha
- Hakuna mpango kazi wa kuthaminisha mali zainazomilikiwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Pia, hakuna mkakati wa kielekroniki wa kuingiza Mali na vifaa vya Serikali za Mitaa (LGA Asset module)
- Mpango kazi wa miaka mitano wa idara haujatilia maanani kuwajengea uwezo watumishi kwa njia ya mafunzo ya namna ya kutumia mfumo wa Epicor-hasa mali na vifaa vya Serikali.

### **(d) Ardhi na majengo kutotenganishwa kulingana na mwongozo IPSASs 17**

Aya ya 74 IPSAS 17 inasema ardhi na majengo ni mali tofauti na hivyo zinatakiwa kuhesabiwa, kuthaminiwa na kuweka kumbukumbu tofauti hata kama zitakuwa

zimenunuliwa pamoja. Ukaguzi wa Hesabu jumuiifu umebaini kuwa ardhi na majengo ya Serikali havijatenganishwa kinyume na mahitaji ya mwongozo wa kimataifa wa kuandaa hesabu (IPSAs 17).

(e) Mfumo wa kompyuta wa Epicor na ule wa Bajeti bado haurekebishwa ili uweze kuandaa taarifa za hesabu zilizoendana na IPSAS zilizo katika msingi wa taslimu.

(f) Mfumo wa bajeti wa Serikali bado upo chini ya msingi usio wa pesa taslimu (Cash Basis) japokuwa Serikali kuu imeshaamua kujiunga na IPSAS ya msingi usio taslimu kuanzia tarehe 1 Julai, 2012. Hali hii imepelekea ugumu wa kazi kwa watumiaji.

(g) Mafunzo kuhusu mfumo wa bajeti, Epicor, na IPSAS ya msingi usio taslimu (accrual basis) hayakuratibiwa ipasavyo kwa wadau husika katika Wizara, Idara, Wakala wa Serikali, hasa ukitilia maanan changamoto za kuhama kutoka Epicor 7 kwenda Epicor 9.05 na sasa kuhama kutoka 'IPSAS cash' kwenda 'IPSAS accrual'.

#### **4.2.4.9 Mapungufu katika usimamizi wa fedha**

Ukaguzi wa hesabu jumuiifu za taifa umebaini kuwepo kwa fedha kiasi cha Sh.18,152,597,859 ambazo mlipaji mkuu alirudisha kwenye mfuko mkuu wa Serikali. Hata hivyo, kwa kipindi hicho, Serikali ilikuwa na nakisi ya kiasi cha Sh.263,866,358,436 kwenye akaunti zake zilizopo Benki Kuu ambapo Serikali ililipia riba kiasi cha Sh.53,223,549,921.

Ni maoni yetu kuwa kiasi Sh.18,152 billioni alizokuwa nazo Mlipaji Mkuu zingesaidea kupunguza nakisi kwenye akaunti kwa asilimia 9.3 (kutoka Sh263 billioni hadi Sh.244.9 billioni) na hivyo kusaidia kupunguza nakisi na riba iliyolipwa ambayo ni gharama kwa Serikali. Hayo yote ni kwa sababu ya ukosefu wa usimamizi thabiti wa fedha katika akaunti za Serikali zilizopo Benki Kuu na pamoja na kutokuwepo kamati ya kitaifa inayosimamia fedha na pia ukosefu wa uratibu wa fedha na utekelezaji wa bajeti.

### **Mapendekezo**

Serikali inashauriwa kuanzisha Kamati ya kitaifa itakayosimamia na kuboresha usimamizi wa fedha za Serikali na pia Serikali iepuke kukopa fedha wakati kuna fedha taslimu kwenye akaunti zinginezo.

#### **4.2.4.10 Ufuatiliaji na tathmini ya miradi inayotekelezwa kwa fedha za mikopo**

Katika kupitia Mkakati wa Taifa wa Madeni wa mwaka 2002, niliweza kutambua juhudi za Serikali katika kuboresha uwezo wa kujimudu kifedha. Namna moja wapo ya kufikia uwezo huo ni kuboresha matumizi ya fedha zinazoelekezwa kwenye miradi ya maendeleo ili kuleta ukuaji endelevu wa uchumi.

Pamoja na hayo, Kanuni ya 23 ya Sheria ya Madeni, Dhamana na Misaada ya Serikali ya mwaka 1974 inawataka waratibu wa miradi ya maendeleo na wakala wa utekelezaji miradi husika kuwasilisha Wizara ya Fedha kila mwezi taarifa za matumizi ya fedha za mikopo na misaada kwa ajili ya ufuatiliaji. Mahojiano na wahusika katika Wizara ya Fedha yalidhihirisha kuwa jambo hilo linahitaji msukumo zaidi.

Hata hivyo, mpaka sasa hakuna kitengo kilichoanzishwa kwa lengo la ufuatiliaji na kufanya tahmini ya miradi inayotekelezwa kwa kutumia fedha za mikopo. Jambo hili linaweza kupelekea matumizi ya fedha za madeni yasifikie malengo na hivyo kuathiri uwezo wa uchumi kulipa mikopo hayo.

### **Pendekezo**

Serikali inashauriwa kuanzisha utaratibu wa ufuatiliaji na kutathmini miradi ya maendeleo ambayo imetekelezwa na inayotekelezwa kwa kutumia fedha za mikopo. Hali hii itasaidia kufanya tathmini ya matokeo ya miradi kadiri inavyoendelea.

### 4.3 USIMAMIZI WA MATUMIZI

#### 4.3.1 Utangulizi

Sura hii inahusu matokeo muhimu ya ukaguzi yaliyojitokeza katika ukaguzi wa matumizi kwa Wizara, Balizi na Sekretarieti za mikoa katika mwaka wa fedha 2012/13 kama ilivyo hapa chini:

#### 4.3.2 Masurufu yaliyokaa muda mrefu bila kurejeshwa - Sh. 319,423,337

Wakati wa mapitio ya udhibiti juu ya usimamizi wa masurufu, ilithibitika kwamba masurufu ya Sh. 319,423,337 yalikuwa bado hayajarejeshwa hadi wakati ukaguzi ukifanyika katika Wizara mbalimbali na ofisi za Sekretarieti za Mikoa kama jedwali na. 27 linavyoonesha, hii ni kinyume na Kanuni Na. 103 (1) ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka, 2001. Masurufu yasiyorejeshwa yanaweza kutumiwa vibaya na kusababisha kutofikia malengo yaliyokusudiwa.

#### Jedwali 27: Masurufu yaliyokaa muda mrefu bila kurejeshwa

s/n	Fun gu	Maelezo	Kiasi (Sh.)
1	27	Msajili wa Vyama vya Siasa	11,905,250
2	32	Ofisi ya Rais-Menejimenti ya utumishi	84,003,578
3	98	Wizara ya Ujenzi-TBA	31,410,000
4	82	Sekretarieti ya mkoa -Ruvuma	4,244,200
5	79	Sekretarieti ya mkoa -Morogoro	1,194,000
6	56	Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za mitaa	21,417,669
7	46	Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi	145,158,500
8	42	Bunge	9,240,000
9	36	Sekretarieti ya mkoa - Katavi	10,850,140
		<b>Jumla</b>	<b>319,423,337</b>

Hali ya usimamizi wa masurufu yasiyorejeshwa kwa miaka 3 iliyopita ni kama inavyoonekana kwenye jedwali Na. 28 hapa chini:

## Jedwali 28: Masurufu yasiyorejeshwa kwa ufupi

Mwaka	Kiasi (Sh.)	Wizara, Idara na sekretarieti za mikoa zilizohusika
2010/2011	436,398,424	8 <sup>16</sup>
K 2011/2012	806,437,464	4 <sup>17</sup>
u 2012/2013	154,174,697	9 <sup>18</sup>

ingana na jedwali hapo juu, mwenendo wa masurufu ambayo hayakurejeshwa ikilinganishwa na mwaka jana, kunaonesha tatizo kupungua kwa asilimia 81% kutoka Sh. 806,437,464 mwaka jana hadi Sh. 154,174,697 kwa mwaka huu. Hata hivyo ninashauri uzingatiaji wa Kanuni Na. 103 (1) ya kanuni za fedha za Umma, 2001 inayohimiza kwamba masurufu ya safari yanarejeshwa ndani ya siku kumi na nne, na kuwa masurufu maalum, baada ya kumaliza shughuli husika. Aidha, kwa wasiozingatia kanuni hii, inapaswa maafisa masuuli kuhakikisha wanarejesha kwa makato ya mishahara ya watumishi husika.

### 4.3.3 Malipo yaliyolipwa katika vifungu visivyostahili Sh. 2,394,834,855

Ukaguzi umebaini kuwa baadhi ya Wizara na Sekretarieti za Mikoa walitumia vifungu visivyostahili kulipa kiasi cha Sh.2,394,834,855 kinyume na kanuni Namba 51 (1-8) ya kanuni za Fedha za umma ya mwaka, 2001. Mchanganuo wa malipo ya fedha za Umma yako katika kiambatisho Na.1 yalilipwa kutoka katika mafungu yasiyostahili kwa makosa bila kupata idhini ya mamlaka husika. Kwa kutumia kasma/vifungu ambavyo matumizi ya fedha hayakuidhinishwa na Bunge kunaweza kuathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa katika bajeti. Muhtasari wa miaka mitatu (3) wa mwenendo wa malipo katika vifungu visivyostahili ni kama inavyoonekana katika jedwali Na.29 hapa chini:

<sup>16</sup> Fungu 27, 34, 42, 18, 74, 27, 34 & 42

<sup>17</sup> Fungu 40, 91, 74 & 34

<sup>18</sup> Rejea jedwali 27

**Jedwali 29: Mwenendo wa malipo katika vifungu visivyostahili**

Mwaka	Kiasi (Sh.)	Wizara, Balozi, Idara na Sekretarieti za mikoa zilizohusika
2009/2010	5,296,243,598	9 <sup>19</sup>
2010/2011	340,756,701	13 <sup>20</sup>
2011/2012	6,027,429,643	
2012/2013	2,394,834,855	25*

*\*Angalia Mchanganuo kwenye Kiambatisho 'E'*

Kwa ujumla mwenendo wa ulipaji wa malipo katika vifungu visivyostahili unaonekana kupungua kwa miaka mitatu iliyopita, hata hivyo ninaendelea kusisitiza kuzingatia vifungu katika bajeti na endapo ni lazima kubadili matumizi, nasisitiza kuzingatia utaratibu wa kupata kibali husika kwa mujibu wa kanuni ya 51 (1-8) ya kanuni za Fedha za Umma, 2001.

**4.3.4 Malipo yaliyozidi kiwango stahiki Sh. 68,089,906**

Wakati wa ukaguzi nilibaini mapungufu katika mifumo ya udhibiti wa ndani ya baadhi ya Wizara na Sekretarieti za Mikoa ambao ulisababisha kiasi cha Sh. 68,089,906 kulipwa zaidi ya kiwango stahiki kama inavyoonekana katika jedwali na. 30 hapa chini:

**Jedwali 30: Malipo yaliyozidi kiwango stahiki**

S/N	Kifungu na.	Maelezo	Kiasi (Sh.)
1	Fungu 40	Mahakama ya Tanzania	3,949,176
2	Fungu 36	RS-Katavi	22,614,478
3	Fungu 56	Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za mitaa	22,784,500
4	Fungu 63	RS-Geita	1,215,500
5	Fungu 91	Tume ya kudhibiti madawa ya kulevya	17,526,252
		<b>Jumla</b>	<b>68,089,906</b>

<sup>19</sup>FunguNa. 39, 44, 46, 52, 56, 61, 75, 86 & 94

<sup>20</sup>Fungu Na. 38, 42, 82, 59, 92, 33, 12, 91, 52, 27, 69, 29, & 85

Mtiririko wa mwenendo wa malipo zaidi ya kiwango stahiki kwa miaka mitatu (3) iliyopita uko katika jedwali na. 31 hapa chini:

**Jedwali 31: Malipo ya zaidi ya kiwango stahiki**

Mwaka	Kiasi (Sh.)	Wizara idara, Balozi na Sekretarieti za mikoa zilizohusika
2010/2011	126,495,025	7 <sup>21</sup>
2011/2012	90,392,726	2 <sup>22</sup>
2012/2013	68,089,906	5

Ingawa mwenendo wa Malipo zaidi ya kiwango stahiki unaonekana kushuka kutoka miaka ya nyuma, Menejimenti za Wizara, Idara, Balozi, na Sekretarieti za Mikoa wanashauriwa kuendelea kuboresha na kuimarisha mfumo wa udhibiti wa ndani ili kuepusha upotevu wa fedha za wananchi kupitia mwanya huu, pia watakao thibitika kusababisha hasara hizi, hatua sitahiki zichukuliwa ikiwa ni pamoja na fidia ya upotevu wa fedha.

#### 4.3.5 Matumizi yaliyofanywa nje ya bajeti iliyoidhinishwa Sh. 15,785,285,943

Ukaguzi wa hesabu za mwaka huu, umebaini kwamba, baadhi ya Balozi, Wizara na Sekretarieti za mikoa zililipa kiasi cha Sh. 15,785,285,943 kwa ajili ya shughuli mbalimbali. Hata hivyo, tumebaini kwamba matumizi haya aidha yalitumika zaidi ya kiwango cha bajeti kilichoidhinishwa ama kwa matumizi ambayo hayakuwa kwenye bajeti kabisa kinyume na kifungu cha 46 (3) cha Sheria ya Fedha za Umma mwaka 2001.

**Jedwali 32: Matumizi nje ya bajeti iliyoidhinishwa**

Mwaka	Kiasi (Sh.)	Balozi, Wizara na Sekretarieti za
-------	-------------	-----------------------------------

<sup>21</sup> Fungu Na. 34, 39, 18, 44, 42, 52, & 18

<sup>22</sup> Fungu Na. 46 & 56

		<b>mikoa zilizohusika</b>
2011/2012	2,292,796,070	10 <sup>23</sup>
2012/2013	15,785,285,943	29*

**\*Angalia kiambatisho ‘F’**

Uchambuzi kutokana na jedwali hapo juu, unaonesha kwamba, idadi ya Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Balizi ambazo zilifanya malipo yaliyozidi bajeti iliyo dhinishwa ziliongezeka kutoka 10 mwaka 2011/12 hadi 29 katika mwaka 2012/13. Hii inaonesha kwamba kuna udhaifu na kutokuwa makini katika kutekeleza bajeti na udhibiti wa matumizi. Ninashauri Balizi, Wizara na Sekretarieti za mikoa husika kuhakikisha wanaandaa bajeti halisia na kuifuata ipasavyo.

**4.3.6 Malipo yenye nyaraka pungufu Sh. 14,498,110,341**

Ukaguzi wa mwaka huu umebaini malipo ya kiasi cha Sh.14,498,110,341 ambayo yalikuwa na nyaraka pungufu katika Wizara na Sekretarieti za mikoa kinyume na kifungu namba 95 (4) kanuni za Fedha ya Umma za mwaka, 2001. Kukosekana kwa nyaraka za malipo kuna kwaza mawanda ya ukaguzi na hivyo inakuwa vigumu kuthibitisha uhalali wa malipo. Mwenendo wa malipo yenye nyaraka pungufu kwa miaka mitatu (3) iliyopita ni kama inavyoonekana katika jedwali Na. 33 hapa chini:

**Jedwali 33: Mtiririko wa malipo yenye nyaraka pungufu kwa miaka mitatu**

<b>Mwaka</b>	<b>Kiasi (Sh.)</b>	<b>MDA/RS zilizohusika</b>
2009/2010	362,026,933,382	18 <sup>24</sup>
2010/2011	8,076,574,791	23 <sup>25</sup>
2011/2012	2,122,925,171	8 <sup>26</sup>
2012/2013	14,498,110,341	29*

<sup>23</sup> Kasma (SV) 2003, SV 2020, SV 2006, SV 2016, SV 2017, SV 2014, SV 2005, SV 2010, SV 2032, SV 2007

<sup>24</sup> Fungu Na. 18, 19, 21, 22, 29, 32, 40, 42, 46, 50, 52, 69, 82, 85, 92, 94, & 95

<sup>25</sup> Fungu Na. 18, 19, 42, 58, 60, 39, 92, 93, 61, 52, 32, 24, 43, 94, 29, 46, 70, 72, 78, 79, 84, 88, & 95

<sup>26</sup> Fungu Na. 57, 85, 37, 38, 39, 51, 52, & 81

**\*Tazama kiambatisho ‘G’ kwa ufafanuzi.**

Ukirejea jedwali hapo juu, inaonekana kwamba mwaka jana, 2011/12 kiasi cha malipo yenye nyaraka pungufu imeongezeka kutoka Sh. 2.1 billioni hadi Sh. 14.4 bilioni, wakati taasisi zilizohusika zikiongezeka toka 8 hadi 29, hii inaonesha kwamba udhibiti wa ndani bado ni dhaifu katika kutunza nyaraka za malipo.

Lkumbukwe kuwa hati ya malipo yenye nyaraka pungufu ni sawa na kutokuwepo kwa hati hiyo na kukosekana kwa hati ya malipo ni sawa na upotevu wa fedha, rejea kanuni 95(4) & 18(f), ya kanuni za fedha ya umma ya mwaka, 2001, nashauri maafisa masuuli kuimarisha udhibiti wa mfumo wa ndani, na pia utunzaji wa nyaraka za malipo unaboreshwa katika taasisi husika.

#### **4.3.7 Malipo yasiyo na stakabadhi za kukiri malipo Sh. 47,935,509,285**

Serikali imekuwa ikipoteza fedha nyingi kwa kutokukusanya kodi kutokana na ukwepaji kodi wa makusudi unaofanywa na wafanyabiashara. Ninatambua juhudi za Serikali kuanzisha EFD ambazo hutunza kumbukumbu za miamala yote kwa ajili ya kurahisisha ukadiriaji wa kodi, pia juhudi za kuelimisha kupitia kauli mbiu mbalimbali kama ile ya “toa risiti, dai risiti”. Hata hivyo, kauli mbiu hii haioneshi kuzingatiwa na vyombo vya Serikali wenyewe katika kudai risiti za EFD na za kawaida (ERV) kutoka kwa watoa huduma mbalimbali Serikalini.

Kwa kutodai risiti za EFD maana yake ni kwamba wauzaji hawa wanakusanya kodi ikiwa ni pamoja na VAT na kutoiwasilisha TRA hivyo Serikali inakosa mapato. Ili kuongeza mapato ya Serikali, taasisi zote za Serikali zinahimizwa kudai risiti pindi zifanyapo manunuzi yake kutoka kwa wafanyabiashara wote wa huduma na bidhaa. Malipo yalifanywa bila kudai EFD / ERV risiti ni kama inavyonekana kwenye jedwali jedwali hapa chini:

**Jedwali 34: Malipo yasiyo na stakabadhi za kawaida na kielektroniki (EFR)**

S/n	Fungu na.	Maelezo	Aina ya Risiti	Kiasi (Sh.)
1	38	Ulinzi (Ngome)	EFR	45,248,767,272
2	93	Idara ya Uhamiaji	ERV	6,990,000
3	89	RS-RUKWA	ERV	4,345,000
4	83	RS-Shinyanga	ERV	32,100,000
5	58	Wizara ya Nishati na Madini	EFR	306,000,000
6	71	RS-Coast	ERV	7,155,419
7	43	Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika	EFD	127,297,755
8	69	Wizara ya Maliasili na Utalii	ERV	424,677,980 + 4,705,000
9	2031	Ubalozi wa Tanzania-Brasilia	ERV	2,744,371
10	46	Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi	ERV	1,029,990,000
11	51	Wizara ya Mambo ya Ndani	EFD	268,658,738
12	29	Huduma za Magereza	ERV	308,058,820
13	56	Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mkoa na Serikali za Mitaa	EFR	164,018,930
<b>Jumla</b>				<b>47,935,509,285</b>

Nimekuwa nikipendekeza kwa Serikali kuongeza mapato yake kwa kuchunguza vyanzo vipya vya mapato na kuisitiza elimu juu ya ulipaji kodi wa hiari. Nasisitiza juu ya Serikali kuongeza juhudi zaidi ya kutoa elimu ya ulipaji Kodi wa hiari na matumizi mashine za EFD bila shuruti. Mashine ambazo moja kwa moja zitapelekea kuongeza

mapato endapo kila manunuzi yataambatana na risiti za EFD.

Pia ninashauri menejimenti za Wizara na Sekretarieti za mikoa kuimarisha udhibiti wa ndani katika kudai na kufuatilia risiti za ERV kwa malipo yote kutoka kwa walipwaji ili kuthibitisha kwamba malipo hayo yamemfika mlengwa na amekiri kupokea.

#### **4.3.8 Malipo yasiyokuwa na mchanganuo wa matumizi Sh. 3,288,257,291**

Ukaguzi umebaini malipo ya kiasi cha Sh.3,288,257,291 yasiyokuwa na mchanganuo wa matumizi katika Wizara tatu (3) na Sekretarieti za mikoa mbili (2) kwa ajili ya shughuli mbalimbali. Malipo haya yalikosa maelezo na viambatanisho vinavyothibitisha uhalali wa kustahili kuwa malipo sahihi ya fedha za umma. Uchambuzi wa mafungu na kiasi cha fedha ni kama inavyonekana katika jedwali 35 hapa chini:

**Jedwali 35: Kukosekana kwa mchanaganuo wa matumizi**

s/n	Fungu	Maelezo	Kiasi (Sh.)
1	85	Sekretarieti ya mkoa -Tabora	14,079,710
2	39	Jeshi la Kujenga Taifa	1,419,608,750
3	38	Jeshi la Wananchi Tanzania	1,082,728,526
4	50	Wizara ya Fedha	259,266,000
5	87	Sekretarieti ya mkoa -Kagera	12,460,000
6	52	Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii	500,114,305
		<b>Jumla</b>	<b>3,288,257,291</b>

Maafisa Masuuli lazima watekeleze wajibu wao kwa makini katika kusimamia rasilimali za umma walizokabidhiwa kwa niaba ya wananchi kwa kuhakikisha kwamba wanazitumia kwa uangalifu. Halikadhalika, ufafanuzi wa kina wa uhalali wa malipo na faida inayopatikana kutokana na matumizi yake unapaswa kutolewa kwa wakati.

#### **4.3.9 Matumizi yasiyokuwa na manufaa Sh.620,002,236**

Matumizi yasiyokuwa na manufaa ni matumizi ambayo yamefanyika bila kupata thamani ya fedha na yasingeweza kufanyika endapo tahadhari ingechuliwa mapema. Malipo

ya kiasi cha Sh.620,002,236 yanahusu wizara mbili, balozi tatu na Sekretarieti za mikoa tano kama inavyoonekana kwenye kiambatisho 'H'.

Ninashauri menejimenti za Wizara, Balozi na Sekretarieti za Mikoa kuhakikisha zinaboresha mifumo yake ya udhibiti wa ndani ili kukabiliana na upotevu unaosababisha mianya ya upotevu uliotajwa hapo juu.

#### **4.3.10 Fedha kutumika kwa shughuli zisizotarajiwa - Sh. 1,770,390,504**

Uchunguzi wa hati za malipo na viambatanisho vyake umebaini kuwa malipo ya jumla ya Sh. 1,770,390,504 yalikuwa yamelipwa kwa shughuli zisizotarajiwa kinyume na Kanuni. No. 115 ya kanuni za Fedha ya Umma, 2001 ambayo inahitaji fedha zilizo katika bajeti kutumika tu kwa malengo yaliyokusudiwa, vinginevyo inaweza kusababisha matumizi mabaya ya fedha hizo na kufanya malengo yaliyokusudiwa yasifikwiwe. **Angalia Kiambatisho 'I'.**

Ili kuhakikisha kwamba fedha zote kama zilivyo idhinishwa na Bunge zinatumiwa kwa matumizi yaliyokusudiwa pekee na kwa mujibu wa sheria, ninashauri menejimenti ya taasisi zilizokaguliwa kuimarisha mfumo wa udhibiti wa matumizi kwa mujibu wa bajeti kuanzia maandalizi yake mpaka utekelezaji wake, ukiukwaji wowote utambuliwe na ushughulikiwe ipasavyo. Hata hivyo, ili shughuli zilizokuwa zimepangwa zifanyike, ninapendekeza kwamba fedha zote zilizotumiwa kwa ajili ya shughuli zisizotarajiwa zirejeshwe na kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa na kuidhinishwa na bunge.

#### **4.3.11 Kukosekana kwa hati za malipo za kiasi cha Sh. 70,195,394**

Hati za malipo ya kiasi cha Sh. 70,195,394 pamoja na nyaraka hazikuwasilishwa zilipohitajika kwa ajili ya ukaguzi. Hii ni kinyume na Kanuni ya 86 (1) ya kanuni za Fedha ya Umma ya mwaka, 2001 ambayo inahitaji malipo

yote ya fedha za umma kulipwa kwa kutumia hati maalum za malipo zikiwa na viambatanisho vyake vyote.

Kukosekana kwa hati za malipo pamoja na nyaraka zake ni dalili tosha kwamba mfumo wa udhibiti wa ndani ni dhaifu, pia mawanda ya ukaguzi yanakwazwa, hivyo ni vigumu kuthibitisha uhalali wa malipo na matumizi ya fedha ya umma.

**Jedwali 36: Orodha ya Wizara na idara ambazo hati za malipo zilikosekana**

S/N	Fungu na.	Maelezo	Kiasi (Sh.)
1	10	Joint Finance Commission	6,501,200
2	81	Sekretarieti ya Mwanza	17,431,634
3	29	Idara ya Magereza	46,262,560
<b>Jumla</b>			<b>70,195,394</b>

**Jedwali 37: Mwenendo wa miaka mitatu (3) wa matumizi yasiyo na hati za malipo**

Mwaka	Kiasi (Sh.)	Wizara idara na Sekretarieti za Mikoa zilizohusika
2010/11	250,796,986	3 <sup>27</sup>
2011/12	922,974,797	2 <sup>28</sup>
2012/13	70,195,394	3 <sup>29</sup>

Jedwali hapo juu linaonesha kwamba tatizo la kukosekana hati za malipo limekuwa likijirudia mwaka hadi mwaka pamoja na kwamba kiasi cha fedha kimepungua mwaka 2012/13 (Sh. 70milioni) ikilinganishwa na mwaka wa fedha uliopita 2011/12 (Sh. 922 milioni), wakati idadi ya taasisi

<sup>27</sup> Fungu no. 42, 52, & 54

<sup>28</sup> Fungu 81 & 34

<sup>29</sup> Anagalia jedwali 36

zilizoshiriki zimeongezeka kufikia 3 mwaka huu kutoka 2 mwaka jana.

Hata hivyo, kuendelea kwa tatizo hili ni kielelezo tosha cha udhaifu katika udhibiti wa mfumo wa ndani, kwa hiyo napenda kuwakumbusha watendaji wa Wizara / Sekretarieti / Balozi kwamba ni wajibu wao kimsingi kuimarisha udhibiti wa ndani ili kuhakikisha hati zote za malipo na viambatanisho vyake zinahifadhiwa barabara .Kwa mujibu wa Kanuni na. 18(f) na 95(4) ya kanuni za Fedha ya umma ya mwaka, 2001, hati za malipo zisizo na viambatanisho na hati zilizokosekana kwa sababu yeyote zinaashiria ni upotevu wa fedha za umma.

#### 4.3.12 Fedha kiasi cha Sh. 371,879,693 imetumika kulipa madeni ya mwaka uliopita.

Ukaguzi umebaini fedha kiasi cha Sh. 371,879,693 imetumika kulipa madeni ya mwaka uliopita. Kiasi hiki cha fedha kilikuwa kimeidhinishwa na bunge kwa ajili ya shughuli za mwaka 2012/2013 na hakuna ushahidi wa madeni hayo kutengewa fedha katika bajeti ya mwaka huu wa fedha. Hivyo, kuna uwezekano wa kutofikia malengo ya awali yaliyokuwa yamekusudiwa. Hii ni kinyume na kanuni ya 85 ya Fedha za Umma ya mwaka 2001.Orodha ya taasisi zilizohusika ni kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini:

#### Jedwali 38: Orodha ya malipo ya madeni ya miaka ya nyuma

S/N	Fungu Na.	Maelezo	Kiasi (Sh.)
1	32	Ofisi ya Raisi Menejimenti ya Utumishi Wa Umma	84,417,208
2	82	Sekretarieti ya mkoa-Ruvuma	3,950,270
3	70	Sekretarieti ya mkoa -Arusha	34,557,000
4	85	Sekretarieti ya mkoa -Tabora	15,151,180
5	56	Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa	13,960,208
6	91	Tume ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya	3,752,000
7	52	Wizara ya Afya na Maendeleo ya	184,522,474

S/N	Fungu Na.	Maelezo	Kiasi (Sh.)
		Jamii	
8	81	Sekretarieti ya mkoa -Mwanza	17,543,300
9	34	Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa	14,026,053
	<b>Jumla</b>		<b>371,879,693</b>

Ninatambua kwamba, kwa sasa Serikali kuu inaandaa hesabu zake kwa sheria za viwango vya kimataifa kwa msingi usio taslimu (IPSAS Accrual) ambao tofauti na ule wa awali wa fedha taslimu (Cash basis) huu hutambua Serikali kupokea huduma au bidhaa japo fedha taslimu hazijalipwa, hata hivyo, bajeti yenyewe bado inaandaliwa kwa msingi wa fedha taslimu (cash basis), kwa hiyo, umakini unatakiwa kuhakikisha madeni yanayovuka mwaka wa fedha yanarekodiwa kwa umakini na kutengewa fedha na kisha kuingizwa katika bajeti ya mwaka unaofuata. Ni muhimu kufanya hivyo ili kuepuka kulipa madeni kwa kutumia fedha zilizokasimiwa na kuidhinishiwa kwa kazi za mwaka husika.

Kwa ujumla, mapungufu niliyoainisha katika usimamizi wa matumizi ya fedha za umma yanasababishwa na kutofanyika kwa tathmini ya mara kwa mara ya viatarishi/mianya ya upotevu wa fedha, daftari la kuorodhesha viatarishi/mianya hiyo na mfumo dhaifu wa namna ya kudhibiti mianya hiyo. Pia, hatua stahiki kutochukuliwa kwa wakati inapotokea udhaifu katika kusimamia matumizi ya fedha ya umma. Juhudi zaidi zinapaswa kufanyika kwa kutathmini mianya ya upotevu wa fedha kwa ngazi ya taasisi husika, kuanzishwa daftari la kurekodi mianya (risk register) na kisha kuundwa kwa sera za udhibiti wa mianya hiyo. Ni kwa kufanya hivyo tu, kutaleta udhibiti madhubuti wa fedha za umma na kuhakikisha malipo yanafanyika kwa matumizi yaliyo sahihi na yenye tija kwa taifa.



## SURA YA TANO

### TATHMINI YA UDHIBITI WA NDANI NA UTAWALA BORA

#### 5.0 Utangulizi

Udhibiti wa ndani ni mchakato muhimu unaoandaliwa na kutekelezwa na uongozi wa taasisi pamoja na watumishi wake ukiwa na lengo la kupambana na vihatarishi na kuhakikisha ufanisi katika kufanikisha malengo ya kiutendaji, taarifa za fedha na utekelezaji wa kanuni na sheria zilizopo. Kwa madhumuni ya ripoti hii, udhibiti wa ndani ni namna Serikali Kuu pamoja na Sekretarieti za Mikoa zinavyojihakikishia kuwa taarifa zao za fedha ni za kuaminika, kuwepo kwa mpango madhubuti wa utendaji kazi wenye maadili na kuzingatia gharama za uendeshaji, sheria na kanuni ikiwemo viwango husika na miongozo mbalimbali.

Sehemu hii ina ainisha matokeo ya ukaguzi yatokanayo na baadhi ya vipengele vya udhibiti wa ndani katika Serikali Kuu na Sekretarieti za Mikoa ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa vitengo vya ukaguzi wa ndani na kamati zake, usimamizi na udhibiti wa vihatarishi, teknolojia ya habari na mawasiliano, mifumo ya kihesabu na udhibiti wa udanganyifu.

#### 5.1 Mapungufu ya Kiutendaji katika Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani

Kanuni ya 28(1) ya Kanuni ya Fedha za Umma, 2001 inawataka maafisa masuuli wote wa Serikali Kuu ikiwemo Sekretarieti za Mikoa kuanzisha na kusimamia vitengo vya ukaguzi wa ndani. Kitengo cha ukaguzi wa ndani madhubuti kinatakiwa kutathmini ubora wa mfumo wa kihesabu, fedha na usimamizi wa utendaji ndani ya Serikali Kuu kwa kufanya mapitio juu ya utendaji na uandaaji wa taarifa za fedha na udhibiti wa bajeti. Mapungufu yafuatayo juu ya tathmini ya utendaji wa kitengo cha ukaguzi wa ndani yamebainika katika Wizara/Idara/Wakala na Sekretarieti za Mikoa 22 kama inavyo onyeshwa katika kiambatisho 'J' kinyume na matakwa ya kanuni:

- i. Vitengo vya ukaguzi wa ndani vimeendelea kuwa na watumishi wachache, baadhi kuwa na mtumishi mmoja mpaka wawili. Kwa kuzingatia shughuli mbalimbali za taasisi za Serikali Kuu na mawanda ya ukaguzi, mkaguzi mmoja au wawili hawatoshi kwa utendaji madhubuti.
- ii. Mawanda ya ukaguzi hayakujitosheleza kutokana na upungufu wa rasilimali mbalimbali zikiwepo fedha na vitendea kazi. Hivyo tathmini ya udhibiti na usimamizi wa fedha pamoja na utendaji kwa ujumla haikufanyika ipasavyo hali iliyonilazimu kutopunguza mawanda yangu ya ukaguzi kwa kutegemea kazi ya mkaguzi wa ndani.
- iii. Nafasi ya ukaguzi wa ndani katika mfumo wa utawala pamoja na majukumu na wajibu wake hayakubainishwa wazi katika mkataba kwa wateja wa ukaguzi wa ndani.

Naendelea kusisitiza kwamba, menejimenti za Wizara/Idara/Wakala pamoja na Sekretarieti za Mikoa zishirikiane na ofisi ya Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani, kuimarisha kitengo cha ukaguzi wa ndani kwa kuongeza idadi ya watumishi wenye sifa na fedha.

## **5.2 Mapungufu katika Kamati za Ukaguzi**

Maendeleo makubwa ya hivi karibuni katika mfumo wa uendeshaji wa sekta ya umma imekuwa ni uanzishwaji wa kamati za ukaguzi. Kamati za ukaguzi zinachangia kwa kiasi kikubwa katika usimamizi wa fedha, maadili na uadilifu wa watumishi wa umma na utawala bora. Kamati ya ukaguzi ina wajibu wa kusimamia maendeleo na utekelezaji wa sera, mfumo wa udhibiti wa ndani, taarifa za fedha na udhibiti wa vihatarishi. Kanuni ya 30 ya Kanuni ya Fedha za Umma, 2001 inahitaji kila Wizara/Idara/Wakala na Sekretarieti za Mikoa kuwa na kamati za ukaguzi.

Matokeo ya kaguzi zilizofanyika katika kipindi cha mwaka 2012/2013 kwa kupitia utendaji wa Kamati za Ukaguzi

yanaonyesha kuwa, Wizara/Idara/Wakala na Sekretarieti za Mikoa zipatazo 28 zilikuwa na mapungufu yafuatayo:

- i. Utendaji usioridhisha wa Kamati za Ukaguzi uliopelekea kushindwa kusimamia utekelezaji wa majukumu ya wakaguzi wa ndani.
- ii. Katika baadhi ya maeneo, muundo wa Kamati ya Ukaguzi haukuwa kama ulivyoainishwa katika Kanuni ya 31(1) ya Kanuni ya Fedha za Umma, 2001 ambayo inamtaka Afisa Massuli kuteuwa wajumbe ambao ni maafisa waandamizi na angalau mjumbe mmoja ateuliwe na Katibu Mkuu kutoka nje.
- iii. Kamati za Ukaguzi hazikupitia taarifa za fedha na ripoti za kaguzi za ndani na nje za maeneo husika.
- iv. Katika baadhi ya maeneo hakukuwa na ushahidi wa kuandaliwa kwa ripoti za mwaka za kamati na kuwasilishwa kwa Maafisa Masuuli kwa ajili ya hatua stahiki juu ya mapendekezo ya Kamati;

Mapungufu katika utendaji wa Kamati za Ukaguzi yanaathiri mfumo mzima wa usimamizi wa utendaji na utawala bora. Ni muhimu kwa kamati za ukaguzi za Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa kuwa na hadidu za rejea zinazoainisha bayana jinsi ya kuwa mwanachama, ratiba na idadi ya mikutano, wajibu na majukumu ya kila mjumbe pamoja na uandaji na utoaji wa taarifa.

### **5.3 Mapungufu katika Udhhibiti wa Vihatarishi**

Usimamizi wa vihatarishi ni sehemu muhimu ya mfumo wa udhibiti wa vihatarishi kwani unahusisha uelewa wa malengo ya taasisi, kutambua, na kutathmini vihatarishi vitokanavyo na utekelezaji wa malengo hayo na mara kwa mara, kuandaa na kutekeleza mipango madhubuti ya kudhibiti vihatarishi hivyo.

Ukaguzi ya Wizara/Idara/Wakala na Sekretarieti za Mikoa ulibaini kuwa, Wizara 11 na Sekretarieti za Mikoa 14 kama inavyoonekana katika Kiambatisho 'J'; hazikuwa na Sera inayotambulika ya Usimamizi wa Vihatarishi na hakukuwa

na tathmini rasmi ya vihatarishi iliyofanyika hivi karibuni kutabaini vihatarishi vilivyopo na vinavyojitokeza ikiwa ni matokeo ya mabadiliko ya mazingira ya utendaji na utoaji wa huduma.

Uongozi wa Wizara/Idara/Wakala na Sekretarieti za Mikoa unatakiwa kuandaa na kuratibu utekelezaji wa Sera ya Usimamizi wa Vihatarishi na kuhakikisha kwamba taarifa za vihatarishi na namna ya kukabiliana nazo zinapitiwa mara kwa mara ili kubaini mabadiliko yoyote na kuhakikisha njia madhubuti za kudhibiti vihatarishi zinakuwepo wakati wote.

#### **5.4 Mapungufu katika Mazingira ya Usimamizi wa Teknolojia ya Habari**

Ofisi nyingi za Serikali zinatumia mifumo ya kompyuta katika utendaji kazi wake ikiwa ni pamoja na uandaaji wa taarifa za fedha. Hali hii inaleta changamoto kwetu sisi wakaguzi ya kuelewa uhusiano uliopo baina ya mifumo hii na uandaaji wa taarifa za fedha. Kama hatua moja wapo ya kuelewa shughuli za mkaguliwa, ni muhimu kufanya tathmini ya mazingira ya Teknolojia ya Mawasiliano.

Wakati wa kufanya tathmini katika mazingira ya udhibiti wa teknolojia ya habari, mapungufu yafuatayo yalibainika katika jumla ya Wizara 10 na Sekretarieti za Mikoa 13 kama inavyooneshwa katika **kiambatisho 'J'**

- i. Ukosekanaji wa sera ya Teknolojia ya Habari, jambo linaloweza kupelekea udhaifu katika usimamizi na utumiaji wa vifaa vya teknolojia ya habari ikiwa ni pamoja na programu za kompyuta.
- ii. Hakukuwa na udhibiti wa kutosha kwa rasilimali za kompyuta ikiwemo taarifa, mipango, vifaa na vyumba kwa ajili ya ulinzi wa rasilimali hizo dhidi ya ubadilishwaji, upoteaji na uvujaji wa taarifa. Aidha seva zimekuwa zikiwekwa katika vyumba ambavyo shughuli nyingine za ofisi zinafanyika kinyume na sera bora za usimamizi wa mifumo ya teknolojia ya

mawasiliano zinazotaka kuwepo kwa chumba maalum, chenye ulinzi na kisichoingia vumbi kwa urahisi.

iii. Hakukuwa na mpango wa kujikinga na majanga pindi yanapotokea hali inayoleta ugumu katika urejeshaji wa mfumo kwa wakati pindi panapotokea majanga. Aidha hakukuwa na vyanzo vya taarifa vilivyokwisha fanyiwa majaribio kwa ajili ya kurejesha taarifa hizo sambamba na mtu mwenye jukumu la kusimamia mchakato mzima wa urejeshwaji wa taarifa.

## **5.5 Mapungufu katika kuzuia udanganyifu**

Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISSAI 1240) vinafafanua udanganyifu kama ni "kitendo cha makusudi kinachofanywa na mtu mmoja au zaidi ndani ya menejimenti na wale wanaohusika na uongozi, wafanyakazi, au watu wa nje, wakishiriki kwa njia ya udanganyifu ili kujinufaisha kwa njia zisiyo halali au haramu." Jukumu la kubaini na kuzuia udanganyifu wowote unaoweza jitokeza linabakia kwa menejimenti husika ikishirikiana na watumishi wake.

Hata hivyo, nilipanga ukaguzi wangu katika namna ambayo ingeniwezesha kubaini makosa makubwa katika taarifa za fedha yatokanayo na ukiukwaji wa taratibu ikiwa ni pamoja na udanganyifu.

Ukaguzi wa 2012/2013 umebaini kuwa Sekretarieti za Mikoa mitano (Dodoma, Mbeya, Morogoro, Tanga na Manyara) hazikuwa na mfumo uliondikwa na kuidhinishwa na menejimenti kwa ajili ya kubaini, kuzuia na kupambana na udanganyifu. Hakukuwa na utaratibu kwa ajili ya kubaini na kuzuia vihatarishi vinavyoweza pelekea kuwepo kwa udanganyifu katika mazingira ya kazi.

Vifuatavyo ni viashiria ambavyo vilibainika katika baadhi ya ripoti za mwaka huu ambavyo kimtazamo ni kama dalili za udanganyifu:

- Malipo yaliyofanyika bila nyaraka,
- makosa katika taarifa za fedha,
- mapungufu katika utunzaji na usimamizi wa mali za Serikali ikiwemo majengo na magari,

- Kutokuwepo kwa muundo wa kazi unaozingatia mtumishi mmoja kutofanya kazi zisizoshabihiana na hasa wakati wa kufanya malipo.

Wajibu wa kubaini na kuzuia udanganyifu bado unabakia mikononi mwa menejimenti za Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa husika. Mianya ya udanganyifu iliyoainishwa hapo juu haina budi kufanyiwa kazi sambamba na uandaaji wa sera ya kuzuia udanganyifu itakayokuwa na mipango iliyoidhinishwa ya kuzuia udanganyifu na kufanya tathimini za vihatarishi mara kwa mara.

#### 5.6 Mapungufu katika matumizi ya mfumo wa kihasibu (IFMS/Epicor)

Shughuli zote za kihasibu za Serikali zinapaswa kufanyika katika Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha (IFMS). Toleo jipya la Epicor 9.05 lina baadhi ya vipengele vinavyoshughulika na malipo ya madai, wadaiwa, usimamizi wa fedha, leja, manunuzi na vinginevyo.

Katika mwaka wa ukaguzi ilibainika kuwa, mfumo wa kihasibu wa Epicor 9.05 hautumiki kikamilifu kama jinsi ilivyokusudiwa. Uandaaji wa hundi na uchapishaji wake umekuwa ukifanyika nje ya mfumo. Na taarifa za mwezi za benki zimekuwa zikiandaliwa nje ya mfumo kinyume na matarajio. Mapungufu zaidi yameonekana katika Wizara/Idara/Wakala na Sekretarieti za Mikoa 8 kama inavyoonyeshwa katika **kiambatisho 'J'**. Mapungufu haya yamechangiwa na mambo yafuatayo:

- Baadhi ya vipendelele havikuwa na muundo unaokidhi matakwa ya watumiaji na hivyo kushindwa kutumika kikamilifu.
- Kukosekana kwa mafunzo ya kutosha juu ya mfumo mpya wa Epicor 9.05

Napendekeza kuwa, uongozi wa Wizara/Idara/Wakala kwa kushirikiana na Hazina uhakakikishe kuwa vipengele vyote vya Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha vinaboreshwa kuendana na mazingira ili mfumo uweze

kutumika kikamilifu. Aidha nashauri kuwepo kwa mafunzo ya mara kwa mara hasa panapokuwa na toleo jipya la mfumo pamoja na waajiriwa wanya.

#### **5.6.1 Taarifa ya Uhasibu kuandaliwa nje ya Mfumo Funganifu**

Wakati wa ukaguzi ilibainika kuwa, kati ya balozi 32, ubalozi mmoja tu (Pretoria) ndio ulioanza kutumia Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha katika kuandaa taarifa za fedha.

Balozi sita ambazo ni; Paris, Washington, New York, London, Ottawa na Brussels zimejaribu kutumia mfumo wa bila mafanikio na hivyo kuendelea kuandaa taarifa zake za fedha nje ya Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha.

Mtazamo wangu ni kuwa, kutotumia Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha kunapelekea kuwepo kwa uwezekano mkubwa wa uandaaji wa taarifa za fedha zenye makosa na zinazoweza kufanyiwa mabadiliko kirahisi hali inayosababisha watumiaji kupunguza imani juu ya usahihi wa taarifa hizo na pia kuathiri upatikanaji wa taarifa kwa wakati.

Ni muhimu kwa uongozi wa balozi zote kuhakikisha Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha unakuwepo na unatumika ipasavyo katika shughuli zote za kiasibu ikiwemo uandaaji wa taarifa za fedha na kwamba watumishi wote wanapewa mafunzo ya jinsi ya kuutumia.

Kwa kuongezea, Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ina jukumu la kusimamia kwa karibu na kuhakikisha Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha unatumika kikamilifu katika balozi zote.

## SURA YA SITA

### USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU NA MISHAHARA

#### 6.0 UTANGULIZI

##### **Usimamizi wa rasilimali watu**

Ukaguzi wa rasilimali watu unahusu kuainisha masuala mbalimbali na kuyatafutia ufumbuzi mapema kabla hayajasabibisha madhara. Ni nafasi ya kupima mambo mazuri ya taasisi, na pia jinsi gani mambo yanaweza kufanyika tofauti na ilivyo zoeleka, kwa ufanisi zaidi au kwa kupunguza gharama.

Ukaguzi wa rasilimali watu unahusisha kutumia muda na rasilimali katika kutilia mkazo malengo, kuangalia sera za rasilimali watu, taratibu na mikakati ya kulinda taasisi, kuanzisha njia bora na kutambua fursa kwa ajili ya kuboresha. Lengo la mapitio ya rasilimali watu ni kuweza kusaidia kutathmini kama maeneo maalum yanajitosheleza kulingana na sheria na kwa ufanisi. Matokeo yanaweza kutoa taarifa muhimu zinazoweza kusaidia kujua ni maeneo yapi yanahitaji uboreshaji. Ukaguzi wa rasilimali watu kwa ujumla unajumuisha yafuatayo:

- (i) Tathmini ya sera za kazi katika utumishi na taratibu zilizopo, kwa kulenga maeneo muhimu katika idara ya utumishi (kwa mfano, kuajiri wafanyakazi ndani na nje, malipo ya mishahara, usimamizi katika utendaji wa kazi, nk).
- (ii) Mapitio ya viashiria vyarasilimali watu katika utumishi (kwa mfano, idadi ya nafasi za kazi zilizowazi, muda wa kujaza nafasi mpya, viwango vya watumishi kuacha kazi, upimaji wa watumishi, nk).

##### **Usimamizi wa mishahara**

Katika ukaguzi wa mishahara, mkaguzi hukagua nyaraka zote kuhusumishahara, kuhakiki usahihi wake na kuangalia masuala yanayoweza kujitokeza kama vile mtumishi kuwa na kumbukumbu za utumishi ambazo hazijakamilika, makato ambayo hayaendani na michango

na kadhalika. Udhibiti wa ndani wa ulipaji mishahara ni lazima uwe wa kutosha ili kuhakikisha usahihi wa taarifa na kuzuia udanganyifu.

## 6.1 Masuala muhimu yaliyojitokeza katika ukaguzi wa rasilimali watu katika Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa

Ufuatao ni muhtasari wa masuala yaliyojitokeza katika ukaguzi wa Wizara na Sekretarieti za Mikoa. Maelezo ya kina katika ukaguzi huu yanapatikana katika ripoti zilizotolewa kwa kila Wizara, IdaraWakala na Sekretarieti za Mikoa.

### 6.1.1 Mishahara isiyolipwa ambayo haikurejeshwa HazinaSh.269,312,496

Ukaguzi wa mishahara katika mwaka ulioishia 30 Juni, 2013ulibaini kuwepo mishahara ambayo haikulipwa kiasi cha Sh.269,312,496 kutokana na kuwa watumishi waliopaswa kulipwa kutokuwapo tena katika ajira ya Serikalikwa sababu mbalimbali ikiwemo vifo, kuacha kazi na kustaafu.Hata hivyo, kiasi hiki kilikuwa bado hakijarejeshwa Hazina kama inavyoonekana katika jedwali Na.39 hapa chini;

#### Jedwali 39: Orodha ya Wizara,Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa yenye Mishahara isiyolipwa na kurejeshwa hazina

Na.	Fungu	Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa	Kiasi (Sh)
1.	10	Tume ya pamoja ya Fedha (Joint Finance Commission)	12,818,737
2.	37	Ofisi ya Waziri Mkuu	16,183,592
3.	63	Sekretarieti ya Mkoa wa Geita	3,668,079
4.	65	Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana	22, 466,761
5.	74	Sekretarieti ya Mkoa wa Kigoma	27,136,507
6.	76	Sekretarieti ya Mkoa wa Lindi	157,364,863
7.	82	Sekretarieti ya Mkoa wa Ruvuma	2,843,275
8.	89	Sekretarieti ya Mkoa wa Rukwa	3,879,907
9.	75	Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro	15,197,151.70
10.	79	Sekretarieti ya Mkoa wa Morogoro	7,753,623
<b>Jumla</b>			<b>269,312,495.7</b>

*Chanzo: Ripoti za ukaguzi kwa menejimenti kwa mwaka wa fedha 2012/2013*

Mishahara isiyolipwa ambayo haikurejeshwaa Hazina ina hatari ya kutumiwa kinyume na makusudio ya matumizi ya fedha hizo. Menejimenti za Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa husika wahakikishe kwamba fedha hizo zinarudishwa Hazina.

#### 6.1.2 Malipo kwa watumishi ambao hawapo kwenye utumishi Sh.793,283,755

Ukaguzi ulibaini malipo ya kiasi cha Sh.779,329,181 kwa watumishi waliostaafu, waliofukuzwa na walioacha kazi ambao hawakuondolewa katika orodha ya mishahara kwa wakati kinyume na kifungu No.17 cha Sheria ya Umma kwa wastaafu (Public Service Retirement Benefit Act No.2) ya mwaka 1999. Malipo yalikusishwa Wizara nne(4), Sekretarieti za Mikoa nne (4) na balozi tatu(3) kama inavyoonekana katika jedwali hapo chini.

Mbali na hayo, Sekretarieti za Mikoa mitatu(3) zilikuwa na makato ya mishahara ya kiasi cha Sh.13,954,573 ambayo yalifanyika hazina na kupelekwa katika taasisi mbalimbali za fedha. Makato haya yalifanyika kwa watumishi ambao hawapo tena katika utumishi wa umma kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kustaafu, kufariki au kuacha kazi.

#### Jedwali 40: Malipo kwa watumishi ambao hawapo kwenye utumishi wa Umma

Na.	Fungu	Wizara, idara na Sekretarieti za Mikoa	Kiasi (Sh)
1.	34	Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa	7,904,151
2.	40	Idara ya Mahakama	26,724,156
3.	70	Sekretarieti ya Mkoa Arusha	28,696,726
4.	52	Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii	87,157,948
5.	69	Wizara ya Maliasili na Utalii	32,394,926
6.	81	Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza	5,873,645
7.	85	Sekretarieti ya Mkoa wa Tabora	14,512,701
8.	87	Sekretarieti ya Mkoa wa Kagera	591,600
9.	2005	Ubalozi wa Tanzania - Abuja	157,814,844
10.	2013	Ubalozi wa Tanzania -Paris	289,666,694.21
11.	2021	Ubalozi wa Tanzania -Kampala	127,991,790
		<b>Jumla</b>	<b>779,329,181.21</b>

*Chanzo: Ripoti za ukaguzi kwa menejimenti kwa mwaka wa fedha 2012/2013*

**Jedwali 41: Makato yasiyoruhusiwa kisheria kutoka kwa waliokuwa watumishi wa Serikali Sh.13,954,573.40**

No.	Fungu	Sekretarieti ya Mkoa	Kiasi(Sh)
1.	73	Sekretarieti ya Mkoa wa Iringa	2,166,974.40
2.	81	Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza	10,340,527.00
3.	85	Sekretarieti ya Mkoa wa Tabora	12,507,501.4
<b>Jumla</b>			<b>25,015,002.80</b>


*Chanzo: Ripoti za ukaguzi kwa menejimenti kwa mwaka wa fedha 2012/2013*

Uchambuzi wa malipo ya watumishi ambao hawapo tena katika utumishi wa umma kwa Serikali kuu kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo kutoka mwaka 2010/2011 mpaka 2012/2013 ni kama inavyoonekana hapa chini:

Mwaka wa fedha	2010/2011	2011/2012	2012/2013
Malipo yasiyostaili (Sh.)	142,715,828	55,917,338	779,329,181
Idadi ya Wizara na Sekretariati zilizohusika	7	3	8

*Chanzo: Ripoti za ukaguzi kwa menejimenti kwa mwaka wa fedha 2012/2013*

Taarifa hii inaweza kuonekana katika mchoro ufuatao:



Hali hiyo hapo juu inaonyesha kwamba kuna mapungufu katika mfumo wa udhibiti wa ndani katika malipo ya

mishahara ambayo yanaisababishia Serikali hasara. Menejimenti inapaswa kuwa na mfumo wa udhibiti wa ndani ulio imara na kuhakikisha kwamba mishahara iliyolipwa kwa wasio watumishi inarejeshwa na pia udhibiti unawekwa ili kuhakikisha kwamba mishahara inalipwa kwa watumishi waliohakikiwa.

## 6.2 Kukosekana au kuwepo kwa mfumo duni wa kupima utendaji wa watumishi wa umma

Kanuni Na.22(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma ya mwaka 2003 zinataka kila taasisi katika utumishi wa umma kuwa na mfumo wa kupima utendaji wa watumishi wake; mahitaji haya ni sambamba na kifungu D.63(1) cha Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za mwaka 2009.

Zaidi ya hayo, Kanuni Na 22 (2) ya Kanuni ya Utumishi wa Umma, 2003 inaeleza madhumuni ya tathmini ya utendaji wa watumishi wa umma kwa lengo la kugundua, kutathmini na kuweka kumbukumbu ya uwezo na mapungufu ya watumishi ili kuweza kuchukua hatua stahiki kwa ajili ya kuendelea kuboresha ufanisi katika utumishi wa umma.

Hata hivyo, wakati wa ukaguzi wa malipo na kumbukumbu za rasilimali watu kwa mwaka 2012/2013 ilibainika kuwa, baadhi ya ofisi zilikuwa hazifanyi tathmini ya utendaji wa watumishi wake kama inavyoonekana hapa chini.

### Jedwali 42: Kukosekana au kuwepo kwa mfumo duni wa kupima utendaji wa watumishi wa umma

Na	Fungu	Wizara/idara/ Sekretarieti ya Mkoa
1.	34	Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa
2.	35	Kurugenzi ya mashitaka ya umma
3.	72	Sekretarieti ya Mkoa- Dodoma
4.	F75	Sekretarieti ya Mkoa- Kilimanjaro

*Chanzo: Ripoti za ukaguzi kwa menejimenti kwa mwaka wa fedha 2012/2013*

Kwa ajiri ya kuboresha utendaji, ni muhimu kwa menejimenti ya Wizara/idara na Sekretarieti ya Mikoa husika kufuata kanuni pamoja na kusimamia zoezi la kupima utendaji wa watumishi wake.

### 6.3 Madai ya watumishi Sh. 1,116,040,060

Mapitio ya Wizara/idara/ Sekretarieti za Mikoailibaini madai ya watumishi wa muda mrefu yanayofikia kiasi cha Sh. 1,116,040,060. Hali hii inaathiri motisha na utendaji wa watumishi. Hii imejitokeza katika Wizara mbili(2) na Ubalozi mmoja kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini:

**Jedwali 43: Madai ya watumishi**

Na.	Fungu	Wizara/idara	Kiasi (Sh)	maoni
1.	49	Wizara ya Maji	929,139,870	Madai ya watumishi waliopandishwa vyeo, mishahara ambayo haikulipwa na posho ambazo hazijalipwa wakati wa uteuzi wa watumishi katika vyeo vipya.
2.	58	Wizara ya Nishati na Madini	34,618,822	Madai ya watumishi 20 waliopandishwa vyeo, tangu mwaka 2008 hadi 2009.
3.	2032	Ubalozi wa Tanzania - Kuala Lumpur	152,281,368	Madai kuhusu gharama ambazo zilitakiwa kulipwa na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Madai haya ni pamoja na: - Gharama za matibabu, ada za shule, gharama za Umeme, gesi asilia, Kodi za nyumba, gharama za maji na gharama za mtandao wa mawasiliano(Internet)
Jumla			1,116,040,060	

*Chanzo: Ripoti za ukaguzi kwa menejimenti kwa mwaka wa fedha 2012/2013*

Kama nilivyotangulia kusema hapo juu, madai ya watumishi wa umma yana madhara katika suala la motisha. Hivyo, inaweza kuathiri kiwango cha utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa umma. Menejimenti katika Wizara/idara husika wahakikishe madai halali yanalipwa kulingana na sitahili za watumishi.

#### **6.4 Uhaba wa rasilimali watu**

Rasilimali watu ni sehemu muhimu ya utendaji bora wa taasisi yoyote. Katika kipindi cha mwaka 2012/2013, ukaguzi umebaini kuwepo kwa uhaba mkubwa wa watumishi katika Wizara na Sekretarieti za Mikoa jambo ambalolinaweza kuathiri ufanisi wa utendaji kazi. Upungufu huu wa watumishi umebainika katika Wizara/Idara na Sekretarieti ya Mikoa zilizokaguliwa kama inavyoonekana katika **kiambatisho 'K'**.

Kuna upungufu wa idadi ya watumishi ikilinganishwa na ikama iliyoidhinishwa ambayo ni changamoto kubwa katika utendaji. Serikali inatakiwa kuboresha uwezo wake kifedha ili kuwa na uwezo wa kuajiri watumishi wa kutosha kwa ajili ya kuboresha utendaji.

#### **6.5 Mikopo kwa watumishi isiyodhibitiwa**

Kifungu cha 3 katika Sheria ya Kurejesha Madeni Na.7 ya mwaka 1970 (Debt Recovery Act) inataka makato yote kwa ujumla kwa watumishi wa umma kutozidi theluthi mbili (2/3) ya mshahara yao.

Aidha, waraka wa utumishi Na. C/CE.45/271/01/1/87 wa tarehe 19 Machi 2009 unaelekeza na kusesitiza kwamba, makato katika mishahara yasizidi 2/3 ya mishahara. Ukaguzi wa malipo ya mishahara katika mwaka wa fedha wa 2012/2013 ulibaini kuwepo kwa watumishi wanaopokea mishahara chini ya theluthi moja ya mishahara yao kabla ya makato katika Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoakama ifuatavyo:

**Jedwali 44: Makato yaliyofanyika kwa watumishi zaidi ya theluthi mbili (2/3) pato la mshahara**

No	Fungu	Wizara/idara/ Sekretarieti ya Mkoa
1.	24	Tume ya Maendeleo ya Ushirika
2.	39	Jeshi la Kujenga Taifa
3.	58	Wizara ya Madini na Nishati
4.	70	Sekretarieti ya Mkoa-Arusha
5.	72	Sekretarieti ya Mkoa- Dodoma
6.	74	Sekretarieti ya Mkoa- Kigoma
7.	78	Sekretarieti ya Mkoa- Mbeya
8.	81	Sekretarieti ya Mkoa- Mwanza
9.	84	Sekretarieti ya Mkoa-Singida
10.	86	Sekretarieti ya Mkoa- Tanga
11.	91	Tume ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya
12.	F75	Sekretarieti ya Mkoa-Kilimanjaro

*Chanzo: Ripoti za ukaguzi kwa menejimenti kwa mwaka wa fedha 2012/2013*

Mikopo isiyodhibitiwa inaweza kuleta madhara makubwa kwa watumishi husika katika ufanisi wa kazi na taasisi kwa ujumla. Menejimenti ya Wizara/idara/ Sekretarieti ya Mkoa husika zinapaswa kuchukua hatua kudhibiti ukopaji uliozidi kiwango kilichowekwa ili kulinda maslahi ya watumishi wake.

**6.6 Matatizo yanayohusiana na matumizi ya mfumo wa taarifa za watumishi wa umma**

Serikali imewekeza katika mfumo wa habari wa rasilimali watu katika taarifa za watumishiwa umma (Human Capital Management Information System), unaoitwa LAWSON ili kudhibiti mishahara ya watumishi wa Serikali.

Matumizi ya mfumo huu mpya ni utekelezaji wa Waraka Na.1 wa mwaka 2010 uliotolewa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais ambapo Serikali ilionyesha nia yake katika eneo hili la rasilimali watu, mishahara na usimamizi wa mafao.

Licha ya maboresho haya katikaeneo la kusimamia rasilimali watu na mishahara ya watumishi bado kumeendelea kuwa na matatizo katika baadhi ya taasisi ikiwemo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Sekretarieti ya Mkoa- Singidajambo ambalo linakwamisha ufanisi katika utendaji wa mfumo:

- Matatizo ya mtandao yamekuwa yakiathiri utendaji wa mfumo
- ukiritimba katika kuidhinisha taarifa za watumishi wa umma zilizowasilishwa kwa njia ya mfumo
- Kuchelewa kutoa mrejesho juu ya taarifa zilizohamishwa kwa njia ya mfumo
- Maafisa wanaoendesha mfumo kutokuwa na ujuzi wa kutosha wa jinsi mfumo unavyofanya kazi na uhaba wa idadi ya Maafisa katika ngazi ya juu ya kutoa maamuzi.

Natoa wito kwa uongozi wa Wizara na Sekretarieti za Mikoa zinazo pambana na changamoto hizi zishirikiane na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na Wizara ya Fedha ili kuhakikisha mfumo huu unafanya kazi ipasavyo katika uandaaji wa taarifa za watumishi.

## **6.7 Kuchelewa kurejesha mishahara isiyolipwa Hazina na makato ya mishahara kwa taasisi za fedha Sh.73,672,288**

(i) **Kuchelewa kurejesha mishahara isiyolipwa Hazina** Kanuni Na.113 (3) ya Kanuni za Fedha za Umma 2001 na waraka wa Serikali namba EB/AG/5/03/01VOL.VI/136 wa Agosti 31, 2007 kutoka Wizara ya Fedha, inazitaka Sekretarieti za mikoakurejesha mishahara isiyolipwa Hazina bila kuchelewa na kwamba fedha haipaswi kutumika kwa shughuli nyingine yoyote hata kama matumizi ni halali.Kinyume na utaratibuhuu, mishahara kwa mwaka wa fedha 2007/08, 2008/09, mwaka 2009/10 na 2011/12 (yaani Kuanzia Oktoba 2007 hadi Mei 2012) katika Sekretarieti ya Mkoa wa Iringa (Vote 73) iliwasilishwa Hazina tarehe 2 Mei 2013 kupitiahati ya malipo Na. 1/5 na hundi Na.322885 ya tarehe 2 Mei 2013.

Aidha, kulikuwa hakuna risiti ya kukiri kupokelewa kwa kiasi hicho na Hazina.

**(ii) Kuchelewa kuwasilisha makato ya mishahara kwa taasisi za fedha**

Mapitio ya makato ya mishahara yaliyowasilishwa kwa taasisi mbalimbali za fedha zilizotoa mikopo mwaka wa fedha 2012/2013, inaonyesha kwamba Sekretarieti ya Mkoa wa Iringa iliwasilisha kiasi cha Sh.48,060,982.02 ikiwa imechelewesha makato hayo kwa muda wa miezi mitano kwa taasisi mbalimbali za fedha.

Pia, Ukaguzi ulibaini malipo ya adhabu kwaTume ya Taifa ya Uchaguzi (Fungu 61) kwa kuchelewa kuwasilisha makato kwa wakati ya kiasi cha Sh.5,656,393 kwa Mkurugenzi Mkuu Mfuko wa pensheni kwa watumishi wa Umma (PSPF) kama inavyoonekana hapa chini;

**Jedwali 45: Adhabu kwa kuchelewa kupeleka makato ya watumishi**

Hati za malipo	Tarehe	Maelezo	Kiasi(Sh.)
061VC12000253	29/10/2012	2822163 tangu Julai 1999 hadi Machi, 2000	5,270,000
061VC12001253	7/5/2013	3165452	386,393
<b>Jumla</b>			<b>5, 656,393</b>

*Chanzo: taarifa za malipo ya mishahara ya Tume ya Uchaguzi ya Taifa kwa mwaka 2012/13*

Ukiachilia mbali uwezekano wa kupewa adhabu kwa kuchelewa kupeleka kwa wakati makato ya watumishi kwa taasisi za fedha,kiasi cha fedha za mishahara ambacho hakikulipwa pamoja na makato mbalimbali ambacho hakijawasilishwa kinaweza tumika kwa shughuli nyinginezo. Ni wajibu wa menejimenti husika kuhakikisha uwasilishwaji wa fedha sehemu husika kwa wakati.

## **6.8 Kukosekana Afisa utalii katika ubalozi wa Tanzania-Berlin**

Ubalozi wa Tanzania- Berlin ni kati ya ubalozi kubwa wenye kazi mbalimbali katika maeneo ya utalii, biashara na uwekezaji.

Ubalozi wa Berlin unahudumia nchi nyingine ambazo ni Poland, Austria, Hungary, Frankfurt, Uswisi, Jamhuri ya Czech, Romania, Bulgaria na Slovakia. Fursa za kiuchumi katika maeneo yaliotajwaimeendelea kuongezekamwaka hadi mwaka. Hivyo, uwepo wa wataalamu katika sekta ya utalii na masuala ya ulinzi ni jambo muhimu sana kwa ajili ya kukuza utalii na kuimarisha shughuli za diplomasia ya uchumi katika nchi hizo.

Ukaguzi ulibaini kuwa, watumishi waliopo hawatoshi kuhudumia maeneo hayo yote makubwa yaliyo chini ya Ubalozi. Uongozi wa ubalozi uliomba mtaalam wa masuala ya utalii, biashara na uwekezaji Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Hata hivyo, wataalamu hao hawajapatikana ili kujaza nafasi hizo.

Uongozi wa ubalozi wa Tanzania uendeleo kuikumbusha Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kuhusu upatikanaji wa watumishi hawa ambao wataleta mabadiliko yenye tija katika maeneo mbalimbali ikiwemo yaliyotajwa hapo juu.

## SURA YA SABA

### MAPITIO YA TARATIBU ZA MANUNUZI

#### 7.0 UTANGULIZI

Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya 2008 katika kifungu cha 26 (c) and (d) Pamoja na Kifungu Na. 44(2) cha Sheria ya Manunuzi ya umma ya mwaka 2004, na Kanuni ya 31 ya kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka,2005 (GN 97), kwa pamoja vinaeleza bayana kumtaka Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya tathmini na uzingatiaji wa taratibu za manunuzi katika kaguzi zake za kawaida. Sura hii inaonyesha mapitio ya taratibu za manunuzi ya umma kama zilivyozingatiwana wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa.

Ukaguzi wa mwaka huu ulifanyika pia ili kuona kama taratibu za manunuzi zinafuatwa. Hii inajumuisha utunzaji wa nyaraka muhimu za manunuzi, taratibu za uingiaji wa mikataba, na manunuzi yanayofuata thamani ya fedha na ubora wa bidhaa. Ukaguzi huu umefanyika kwa kuzingatia Sheria ya Manunuzi ya umma ya Mwaka 2004 na Kanuni zake, pia, maagizo mengineyo yatolewayo na Mamlaka ya Kudhibiti Manunuzi ya Umma (PPRA).

#### 7.1 Mapungufu yaliobainika katika ukaguzi wa Manunuzi

Ukilinganisha na ukaguzi wa mwaka jana, inaonekana kuwa manunuzi ya umma yameendelea kuwa ni eneo muhimu sana la kuzingatiwa ili kupata thamani halisi ya fedha za umma. Hata hivyo, Serikalikwa kupitia ripoti zangu na za PPRA za miaka ya nyuma imezingatia ushauri uliotolewa katika sekta ya manunuzi ya umma, imeendelea kuwekeza katika kuimarisha sheria na taratibu za manunuzi katika ofisi zote za umma. Pamoja na juhudi hizo, lakini bado kuna baadhi ya ofisi za Serikali ambazo hazifuati sheria za manunuzi kwa umakini na uweledi. Kwa mwaka huu nimegundua kuwa kuna baadhi ya taratibu za manunuzi ambazo hazikufuata uwazi, ushindani na thamani ya fedha.

Baadhi ya mapungufu hayo yaliyobainika katika ukaguzi wa manunuzi ya umma ni kama inavyo elezwa hapa chini:

## 7.2 Manunuzi yaliyofanyika bila ushindani Sh. 235,855,610

Kanuni Na. 63 ya kanuni ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2005, pamoja na jedwali la kwanza la kanuni hii vyote kwa pamoja vinatoa msisitizo wa kuzingatia thamani ya fedha na ubora wa bidhaa katika manunuzi yote ya fedha za umma. Ili upate manunuzi yenye tija, ni muhimu sana kuzingatia ushindani wa bei na ubora wa bidhaa na huduma hizo kutoka kwa wazabuni. Serikali kupitia baadhi ya Wizara, Idara na Sekretarieti za Mkoa zilifanya manunuzi yenye thamani ya Sh. 235,855,610 bila ya kufuata kanuni ya kushindanisha wazabuni, na jambo hili linaweza kuruhusu kufanya manunuzi kwa gharama kubwa na pia kupata bidhaa zisizo kuwa na ubora. Tazama jedwali 46 hapa chini.

### Jedwali 46: Manunuzi yasiyo kuwa na ushindani

Fungu	Jina la Wizara/Sekretarieti ya Mkoa	Hoja	Kiasi (Sh)
94	Ofisi ya Rais Tume ya utumishi wa Umma	Manunuzi ya huduma za kiushauri bila kufuata ushindani	50,000,000
56	TAMISEMI	Manunuzi ya bidhaa bila ushindani	13,413,380
2031	Ubalozi wa Tanzania Brasilia	Manunuzi kwa kutumia fedha taslimu bila ya kufuata ushindani	42,016,072
86	Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga	Manunuzi yaliyofanywa kwa kutumia chanzo kimoja; yaani bila ushindani.	25,000,000
76	Sekretarieti ya Mkoa wa Lindi	Matengenezo ya magari yasiofuata ushindani	22,368,110
70	Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha	Manunuzi ya bidhaa yasiofuata ushindani wa bei	20,334,500

Fungu	Jina la Wizara/Sekretariati ya Mkoa	Hoja	Kiasi (Sh)
75	Sekretariati ya Mkoa wa Kilimanjaro	Manunuzi ya bidhaa yasiofuata ushindani bei	47,091,190
63	Sekretariati ya Mkoa wa Geita	Manunuzi bila kushindanisha wazabuni	6,500,000
77	Sekretariati ya Mkoa wa Mara	Matengenezo ya magari yasiofuata ushindani	9,132,358
	<b>Jumla</b>		<b>235,855,610</b>

*Chanzo: Ripoti ya ukaguzi kwa Menejimenti.*

Tatizo hili la kununua bidhaa/vifaa/huduma bila kuzingatia ushindani wa bei kwa wazabuni lipo pia katika taarifa zangu za ukaguzi za miaka ya nyuma. Mwaka jana manunuzi yasiofuata ushinda wa bei yalikuwa ni Sh.530,386,985 mwaka huu wa fedha tatizo hili limeonekana katika idara tisa (9) na kuwa na jumla ya Sh. 235,855,610. Hii inaonyesha kuwa Serikali imetatia tatizo hili kwa kiasi kidogo sana na tatizo hili bado lipo na linahitaji kufanyiwa kazi ili kuleta tija katika manunuzi na kupata thamani ya fedha katika manunuzi ya umma.

### **7.3 Mali zilionunuliwa na kuachwa bila ya kutumika Sh. 239,908,449**

Ni muhimu sana kwa Serikali kupanga manunuzi yake yote kwa kuzingatia manufaa na matumizi ya mali hizo. Ili kupata thamani ya fedha kutokana na manunuzi ya mali, ni muhimu kununua mali ambazo zitatumika kufanya shughuli zilizo kusudiwa. Kama Serikali itanunua Mali na kuziacha bila ya kuzitumia, kutakuwa hakuna tija wala thamani ya fedha ya umma katika ununuzi huo. Mwaka huu Serikali imefanya manunuzi yenye jumla ya Sh.239,908,449 mali hizo zilipokelewa, lakini hazijawahi kutumika. Tazama jedwali '47'hapa chini.

## Jedwali 47: Mali ambazo hazijatumika

Fungu	Jina la wizara/Secretariati ya Mkoa	Hoja	Kiasi (Sh.)
72	Secretarieti ya Mkoa wa Dodoma	Ununuzi wa bidhaa uliofanyika miaka mitatu nyuma lakini mali hazitumiki	220,136,665
30	Ofisi ya Rais Secretarieti ya baraza la Mawaziri	Manunuzi ya ya software yaliufanyika tangu mwaka 2011 lakini hajatumika	19,771,784
	<b>Jumla</b>		<b>239,908,449</b>

*Chanzo: Ripoti ya ukaguzi kwa Menejimenti.*

Kwa kutumia fedha za umma kununua mali zisizo leta tija na manufaa kwa Serikali sio jambo zuri na ni ukiukwaji wa sheria za manunuzi ya Umma. Kama Afisa masuuli hana matumizi ya lazima ya mali zinazotakiwa kununuliwa basi ni bora mali hizo zisinunuliwe. Manunuzi yafanyike pale tu ambapo kutakuwa na matumizi ya mali hizo.

### 7.4 Malipo yaliyozidi Kiwango cha Mkataba/ bei Sh.674,331,273

KanuniNa. 122 ya kanuni za Manunuzi ya umma ya mwaka, 2005, kinahitaji mnunuzi kupata taarifa za manunuzi (kama ankara na taarifa za upokeaji bidhaa) baada ya kuwa bidhaa hizo zimekaguliwa, zimekubalika na zimepokelewa, na kama hakuna tatizo lolote katika bidhaa hizo ndipo waanze taratibu za kumlipa mzabuni.

Katika ukaguzi wa mwaka huu imegundulika kuwa kuna baadhi ya Wizara, Idara na Sekretarieti za mikoa ambazo zimeingizia hasara Serikali kiasi cha Sh. 674,331,273 kwa kulipia bidhaa zaidi ya kile kilichodaiwa na mzabuni kupitia ankara. Tazama jedwali Na'48' hapa chini.

#### Jedwali 48: Malipo yaliyozidi bei tajwa kwenye Ankara

Fungu	Jina la Wizara/Sekretarieti ya Mkoa	Hoja	Kiasi (Sh)
40	Mahakama ya Tanzania	Ulipaji wa gharama za kukunua magari uliozidi gharama zilizoonyeshwa kwenye ankara	609,523,267
36	Sekretarieti ya Mkoa wa Katavi	Malipo kwa kampuni ya Toyota zaidi ya ankara	21,334,478
37	Ofisi ya Waziri Mkuu	Mkandarasi aliyelipwa zaidi kwenye ujenzi wa ofisi	25,947,276
91	Tume ya Kudhibiti Madawa ya kulevyu	Mkandarasi aliyelipwa zaidi ya anachodai	17,526,252
	<b>Jumla</b>		<b>674,331,273</b>

*Chanzo: ripoti ya ukaguzi kwa Menejimenti.*

Hii inaonyesha kuwa hakuna usimamizi thabiti katika malipo ya manunuzi, kwa kuwalipa wazabuni zaidi ya walichokidai ni matumizi mabaya ya fedha za umma. Tatizo hili linatakiwa litazamwe na kutatuliwa mapema kwa kuzihusisha idara za uhasibu na idara za manunuzi kwa kushirikiana kwa ukaribu katika kupata nyaraka sahihi kabla ya malipo kufanyika.

#### 7.5 Manunuzi kinyume na Mpango wa Manunuzi wa Mwaka Sh. 2,748,885,871

Kila ofisi inatakiwa kuandaa Mpango wa Manunuzi wa mwaka mzima na kutangaza mpango huo katika magazeti kwa ajili ya matumizi ya Umma, hii imeelezwa katika Kanuni Na 46(9) sheria ya manunuzi ya umma ya mwaka 2005. Jambo hili husaidia Serikali kuwa na taarifa ya kuwa ni kitu gani taasisi inapanga kununua kwa mwaka husika, pia mpango huu kwa kuwa unajumuisha mahitaji ya ofisi nzima, ni rahisi kwa kitengo cha manunuzi kuamua kununua vitu kwa wingi kwa wakati mmoja na kuvisambaza kwa idara zote, hii inasaidia kuweza kupata vitu kwa bei rahisi kama utanunua vingi kwa wakati mmoja.

Kwa kushindwa kuweka mahitaji yote katika mpango wa manunuzi wa mwaka inaweza kuruhusu kufanya manunuzi holela. Mwaka huu Serikalikupitia kwa maafisa masuuli imetumia kiasi cha Sh. 2,748,885,871 kufanya manunuzi ambayo hayakuwa katika mpango wa manunuzi wa mwaka katika idara husika. Tazama jedwali Na. '49' hapa chini

**Jedwali 49: Orodha ya Wizara, Idara na sekretarieti za mikoa zilizo fanya Manunuzi nje ya mpango wa manunuzi wa mwaka**

Fungu	Jina la Wizara/Sekretariati ya mkoa	Hoja	Kiasi (Sh.)
38	Jeshi la Wananchi la Tanzania	Manunuzi yaliofanya nje ya mpango wa manunuzi wa mwaka	2,477,842,091
82	Secretariaeti ya mkoa wa Ruvuma	Manunuzi yaliofanya nje ya mpango wa manunuzi wa mwaka	26,320,000
79	Secretarieti ya mkoa wa Morogoro	Manunuzi yaliofanya nje ya mpango wa manunuzi wa mwaka	244,723,780
	<b>Jumla</b>		<b>2,748,885,871</b>

*Chanzo: ripoti ya ukaguzi kwa Menejimenti.*

Katika mwaka 2012/2013 na 2011/2012 ni asilimia 68% ya Ofisi za Serikali hazikuandaa mpango wa mwaka wa manunuzi, hii ilikua ni ongezeko la asimilia 14 kutoka mwaka 2010/2011. Hii inaonyesha kuwa Serikali inatakiwa kuweka msisitizo katika kuandaa mpango wa manunuzi kwa mwaka na kuhakikisha kuwa kila ofisi inazingatia mpango huo.

**7.6 Manunuzi yaliyofanyika bila idhini ya Bodi ya Zabuni Sh.480,000,000,000**

Kanuni Na. 41 ya kanuniza Manunuzi ya umma ya mwaka 2005 inazitaka Bodi za Zabuni kuzipitia rasimu zote za zabuni kabla ya kuzipitisha. Kabla zabuni yoyote kupitishwa Bodi ya Zabuni inatakiwa kuhakikisha kuwa mahitaji yote ya muhimu katika zabuni husika yamejumuishwa kwa lengo la kupata thamani halisi ya fedha.

Pia, Bodi ya Zabuni ndiyo inayo husika katika kufungua zabuni na katika kuamuanani apewe zabuni hiyo. Kutoa zabuni kwa wauzaji wa bidhaa au huduma bila idhini ya Bodi ya zabuni kunaweza sababisha idara kutoa zabuni kwa wasiostaili na hivyo Serikali kushindwa kupata thamani halisi ya fedha.

Ukaguzi umebaini kuwa Serikali kupitia kwa maafisa masuuli iliingia mikataba yenye kiasi cha Sh.480,000,000,000 kwa mzabuni bila idhini ya Bodi ya Zabuni. Tazama jedwali Na. '50' hapo chini.

**Jedwali 50: Manunuzi yaliyofanyika bila idhini ya Bodi ya Zabuni**

Fungu	Jina la Wizara	Hoja	Kiasi (Sh)
57	Jeshi La Wananchi wa Tanzania	Manunuzi bila kupata idhini ya Bodi ya zabuni	480,000,000,000
	<b>Jumla</b>		<b>480,000,000,000</b>

*Chanzo: ripoti ya ukaguzi kwa Menejimenti.*

Katika taarifa yangu ya mwaka 2011/2012 nilitoa taarifa kuhusu tatizo hili, lakini ilikua imetokea katika Sekretarieti moja tu ya Mkoa wa Kilimanjaro ambayo ilikuwa ni Kiasi cha Sh. 107,171,592. Mwaka huu kiasi kimeongezeka kufikia Sh. 480,000,000,000. Hii inaonyesha kuwa Bodi ya Zabuni katika Wizara kwa mwaka huu haikutimiza majukumu yao vizuri kama sheria ya manunuzi inavyo wataka. Serikali inatakiwa kuchukua hatua katika kuziwezesha Bodi zote za manunuzi kuweza kufanya kazi kwa uhuru na ufanisi mkubwa.

**7.7 Manunuzi kwa kutumia Masurufu Sh.470,907,577**

Kifungu cha 58 (2) cha Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004 kinaelekeza manunuzi kufanyika katika namna ambayo itaongeza uashindani kuleta tija, uwazi na kupata thamani ya fedha.

Kutumia fedhatastimu kununua bidhaa au hudumabila ya kuitangaza kazi hiyo kama zabuniaubilaushindani wabeikwa wauzaji angalau watatu itakuwani ukiukwaji wakifungu namba.58 (2) cha Sheria ya Manunuzi ya mwaka, 2004. Kwa kukiukasehemu ya Sheria hii, Serikali inaweza kuwainanunua kwa bei kubwa bidhaa/vifaa visivyo na ubora na visivyo leta tija kama ambavyo ingetangazwa na kupata bei tofauti kutoka kwa wazabuni tofauti.

Serikali kupitia Wizarazake kwa mwaka huu imenunua bidhaa mbalimbali kwa kutumia fedha taslimu, hii inamaanisha kuwa sheria ya manunuzi imekiukwa na Maafisa masuuli wa wizara/idara hizi. Tazama Jedwali Na.51 Hapa chini.

**Jedwali 51: Manunuzi kwa kutumia Masurufu**

Fungu	Jina la Wizara/Sekretariate ya Mkoa	Hoja	Kiasi (Sh.)
38	Jeshi La Wananchi wa Tanzania)	Manunuzi kwa kutumia masurufu	410,808,973
36	Sekretariate ya Mkoa wa Katavi	Manunuzi kwa kutumia masurufu	9,000,750
74	Sekretariate ya Mkoa wa Kigoma	Manunuzi kwa kutumia masurufu	2,797,685
95	Sekretarieti ya Mkoa wa Manyara	Manunuzi kwa kutumia masurufu	10,727,600
47	Sekretarieti ya Mkoa wa Simiyu	Manunuzi kwa kutumia masurufu	3,830,000
86	Sekretariate ya Mkoa wa Tanga	Manunuzi kwa kutumia masurufu	6,067,400
63	Sekretariate ya Mkoa wa Geita	Manunuzi kwa kutumia masurufu	15,275,169
85	Sekretariate ya Mkoa wa Tabora	Manunuzi kwa kutumia masurufu	12,400,000
	<b>Jumla</b>		<b>470,907,577</b>

*Chanzo: ripoti ya ukaguzi kwa Menejimenti.*

Kwa Serikalikufanya manunuziyenye tija na kwa nia yakupatathamani halisi yafedha, manunuzi yote makubwa yanatakiwa kufanywa kwa njia yazabuni na kwa ushindani bei kutoka kwa wazabuni tofauti. Hii itawezesha Serikali kupata vifaa na huduma kwa bei nafuunakupunguza uwezekano wa kutumiafedha za Serikalikununuavituambayo havinakiwango cha uborakwa bei ya juu.

## 7.8 Vifaa vilivyonunuliwa havikuingizwa vitabuni Sh. 147,691,351

Kanuni Na. 198 ya sheria ya fedha za Umma inaagiza kuwa vifaa vyote vikisha pokelewa viingizwe kwenye regista ya vifaa bila ya kuchelewa, pia bidhaa hizo zinatakiwa ziwe na stakabadhi ya kukiri mapokezi, ankara pamoja na taarifa ya kukaguliwa na kupokelewa. Sheria hii imewekwa ili kudhibiti upotevu wa vifaa vilivyo nunuliwa, hivyo kutokuifuata sheria hii kunaweza sababisha upotevu wa vifaa au kufanya malipo kwa vifaa ambavyo havijapokelewa.

Baadhi ya Wizara na Sekretarieti za Mkoa mwaka huu zimefanya manunuzi yenye jumla ya Sh.147,691,351 kununua vifaa mbalimbali lakini vifaa hivyo vyote havikuingizwa kwenye vitabu vinavyotunza kumbukumbu na hivyo imekuwa vigumu kujua uhalali wa malipo na matumizi ya vifaa. Tazama jedwali Na. '52' hapa chini

### Jedwali 52: Vifaa havikuingizwa vitabuni

Fungu	Wizara/Sekretarieti ya Mkoa	Hoja	Kiasi (Shs.)
51	Wizara ya Mambo ya Ndani	Matumizi ya mafuta ambayo yana utata	83,000,000
47	Sekretarieti ya Mkoa wa Simiyu	Vifaa havikuingizwa vitabuni	12,807,900
82	Sekretarieti ya Mkoa wa Ruvuma	Vifaa havikuingizwa vitabuni	2,316,500
71	Sekretarieti ya Mkoa wa Coast	Vifaa havikuingizwa	5,500,000

Fungu	Wizara/Sekretarieti ya Mkoa	Hoja	Kiasi (Shs.)
		vitabuni	
87	Sekretarieti ya Mkoa wa Kagera	Vifaa havikuingizwa vitabuni	23,854,778
85	Sekretarieti ya Mkoa wa Tabora	Vifaa havikuingizwa vitabuni	20,212,173
	<b>Jumla Sh.</b>		<b>147,691,351</b>

*Chanzo: ripoti ya ukaguzi kwa Menejimenti.*

Tatizo hili nimekuwa nikilitolea ushauri katika ripoti zangu nyingi za miaka ya nyuma, lakini ushauri wangu umekuwa haufanyiwi kazi. Mwaka huu pia tatizo hili limejitokeza, hivyo inaonyesha kuwa vitengo vya manunuzi katika wizara na sekretarieti za mkoa hazitekelezi vizuri wajibu wao. Serikali inatakiwa kuwajengea uwezo maboharia/maafisa ugavi wote ili waweze kutimiza wajibu wao ipasavyo.

### **7.9 Mapungufu yaliyobainishwa na PPRA**

Mamlaka ya Udhhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) ni Mamlaka iliyo anzishwa chini ya Sheria ya Manunuzi ya umma ya Mwaka, 2004. Mamlaka hii imepewa nguvu ya kisheria ya kusimamia shughuli zote za manunuzi yanayo tumia fedha za umma. Mamlaka hii lengo lake kuu nikufuatilia utekelezajimanunuziyanayofanywa na taasisi za Serikalikwa kutumia fedha za umma, ili kuhakikishamanunuzi yanafanyika kwatija, ushindani na uwazi kwa kuzingatia thamani ya fedha.

Yafuatayo ni baadhi ya mapungufu ambayo PPRA imeyabainisha katika ripoti ya mwaka, na mimi pia nimeona niyajumuishe katika ripoti yangu ya mwaka kwa Serikali:

### **7.10 Ufuatiliaji wa Sheria ya Manunuzi ya umma ya mwaka, 2004 na Kanuni zake za mwaka, 2005.**

Mwaka huu PPRA ilifanya ukaguzi katika Wizara na Idara za Serikali zipatazo 32 kwa lengo la kuona ni kwa asilimia

ngapi Serikali inafanya manunuzi kwa kufuata sheria. Imegundulika kwamba kwa mwaka huu Sheria ya manunuzi imefuatwa kwa asilimia 66% kulinganisha na asilimia 69% iliyotolewa taarifa mwaka jana. Hivyo basi kwa kuwa mwaka huu ufuatiliaji wa sheria hii ni kwa asilimia 66% inamaanisha kuwa ufuatiliaji umepungua kwa asilimia 3% kulinganisha na mwaka jana. Matatizo makubwa yamegundulika katika (i) ufuatiliaji wa mikataba asilimia (66%), (ii) Utunzaji wa kumbukumbu za manunuzi asilimia (56%) (iii) kutumia mfumo wa manunuzi wa PPRA (23%), (iv) kutatua malalamiko ya wazabuni (-5%).

#### **7.11 Usimamizi Dhaifu wa Mikataba**

Ukaguzi uliofanywa na PPRA umebaini kuwa kuna mapungufu makubwa katika uandaaji wa mikataba na hivyo kusababisha Serikali kupata huduma isiyoridhisha kama vile kuchelewa kupata mali kwa muda uliokubaliwa kwenye mkataba, ongezeko la gharama, pamoja na kupata bidhaa, huduma ambazo zipo chini ya kiwango. Usimamizi wa mikataba kwa ujumla imeonekana kuwa ni asilimia 60% kwa wizara na idara zote asilimia 32% zilizo kaguliwa.

#### **7.12 Utunzaji wa kumbukumbu za Manunuzi.**

Katika suala la utunzaji wa kumbukumbu, imeonekana kwamba ni asilimia 45% tu ya taarifa zote muhimu za mikataba ndiyo zinazotunzwa vizuri katika wizara na idara. Kukosekana kwa nyaraka muhimu za mikataba kunasababisha mawanda ya ukaguzi kukwazwa.

#### **7.13 Tathimini ya Mfumo wa Utunzaji wa taarifa za Manunuzi (PIMS)**

Mfumo wa utunzaji wa taarifa za manunuzi, ni mfumo ambao PPRA wameuanzisha kwa malengo ya kuwa na mfumo mmoja dhabiti ambao taarifa zote za manunuzi kwa wizara, idara, sekretarieti na Serikali za mitaa wanakuwa wakiutumia kwa ajili ya kutunza taarifa za manunuzi. Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa ni asilimia 57% tu ya ofisi zote zilizokaguliwa kwa mwaka huu ndizo zinatumia mfumo huu kwa kuweza kuaanda mpango wa mwaka wa manunuzi na kuweka katika mfumo huu.

Pia,asilimia 5% ya ofisi zote wamefanikiwa kuweka taarifa za zabuni zao, asilimia 8% taarifa za ukamilifu wa mikataba, asilimia 3% taarifa za manunuzi za kila mwezi, asilimia 18% taarifa za manunuzi za robo mwaka na asilimia 34% taarifa ya manunuzi ya mwaka.

Uchunguzi zaidi ulibaini kuwa idadi ndogo kutumia mfumo huo inatokana na ugumu wa mfumo huo, kwani watumishi wengi wa idara za manunuzi hawawezi kutumia mfumo huu kutokana na kukosekanakwa mafunzo ya kutosha, miundombinu isiyo imara kama vile kukatika kwa umeme kusikotarajiwa na kukosekanakwa mtandao.

#### **7.14 Mapendekezo yaliyotolewa na PPRA**

Katika kutatua matatizo ya kutokufuata Sheria na kanuni za manunuzi, PPRA imetoa mapendekezo yafuatayo:-

- I. Kwa zile taasisi zote za manunuzi ambazo zimefanya vizuri, zinatakiwa kupongezwa kwa kazi zao nzuri na kwa wale ambao hawakufanya vizuri wanatakiwa watoe maelezo ni kwa nini hawajafanya kazi zao vizuri na kujadiliana nao namna ya kutatua matatizo yao ambayo yameonekana
- II. Taasisi zote za manunuzi ambazo zimepata chini ya wastani wa 68% iliyo pangwa kufikiwa na taasisi zote, wanatakiwa kujipanga na kuomba kupatiwa mafunzo ya jinsi ya kufanya kazi kulingana na Sheria na Kanuni za manunuzi na mafunzo hayo yafanyike kulingana na mahitaji ya taasisi husika.

Kwa matatizo ambayo yamejitokeza wakati wa ukaguzi wa Mikataba, PPRA imeshauri yafuatayo:

- I. Kukagua sehemu zote za mikataba na kutoa ushauri, PPRA inatakiwa iwezeshe kwa kuongezewa watumishi pamoja na vitendea kazi kama vile magari ili Mamlaka iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi.
- II. Mamalaka itaandaa muongozo wa usimamizi wa mikataba ambao utakuwa unatoa muongozo wa namna ya kutunza mikataba.

- III. Mamlaka pia imeshauri kuwa, Kitengo cha ukaguzi wa ndani kiimarishwe katika masuala ya manunuzi ili wawe na uwezo wa kukagua mikataba yote.

Ili kuufanya mfumo wa kutunza taarifa za manunuzi kuwa ni mfumo rafiki kwa watumiaji, PPRA inatakiwa kufanya uchunguzi na kujua ni vitu gani vya kuongeza katika mfumo huo ili watumiaji wawe na uwezo wa kuutumia mfumo huo.

**7.15 Mapungufu katika manunuzi na utunzaji wa bohari/stoo katika taarifa ya Kurugenzi ya Uhakiki mali zaSerikali.**

Jedwali la kumi na tano katika Kanuni za fedha za Umma inaeleza umuhimu wa kuwepo Mhakiki Mali ambaye atakuwa akifanya kazi zake kwa uhuru bila ya kuingiliwa. Kwa kuzingatia hili, nimepokea taarifa ya Mhakiki Mali wa Serikali kama ilivyoelezwa kwenye Kanuni Na. 245 (3) ya kanuni za Fedha za Umma ya mwaka, 2001 kwamba; Mhakiki Mali anatakiwa kuwasilisha nakala moja ya taarifa ya uhakika mali kwa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kumbukumbu zake, na pia kumpatia nakala Afisa Masuuli, katibu Mkuu na Mhasibu Mkuu.

Katika kutekeleza yale yalioelezwa kutoka kwenye Kanuni za fedha hapo Juu, kwa mwaka wa fedha ulioishia 30/06/2013, Idara yaSerikaliya usimamizi wa Malichini yaWizara ya Fedha ilihakikimali katikaWizarambalimbalinaofisiza Sekretarieti za Mikoa na kutoa taarifa ifuatayo:

**Jedwali 53: Taarifa ya Mhakiki Mali**

Na.	Mapungufu	Kiasi (Sh)
1)	Ugawaji wa Vifaa na mafuta usio na nyaraka za kutosha	926,306,813
2)	Upekeaji wa Vifaa vya Bohari wenye mapungufu ya nyaraka	2,726,633,911
3)	Mapokezi ya Vifaa vya Bohari bila kuhesabiwa	732,686,791
4)	Kukosekana kwa regista ya mikopo	46,326,412

Na.	Mapungufu	Kiasi (Sh)
5)	Utoaji Mkubwa wa Mafuta	4,362,065
6)	Kazi za ziada ambazo hazikupewa kibali	37,128,000
7)	Uandishi wa taarifa za Manunuzi wenye makosa	1,910,000
8)	Kazi za ujenzi ambazo hazijakamilika	242,100,440
9)	Malipo kwa mkandarasi bila ya kumaliza kazi	44,857,928
10)	Vifaa vyenye mapungufu	436,713,066
11)	Ununuzi wa bidhaa bila ya kuhesabu	5,342,194,700
12)	Vifaa vimetolewa lakini havijapokelewa	3,779,659,039
13)	Utowaji wa bidhaa wenye bakaa sifuri	41,363,200
14)	Manunuzi yasiofuata Sheria	1,115,000
15)	Manunuzi bila ushindani wa bei	237,754,344
16)	Vifaa ambavyo havijaingizwa kwenye daftari la Mali	570,887,400
17)	Malipo ya mkandarasi yaliofanywa bila ruhusa	3,240,000
18)	Ugawaji wa vifaa vya bohari wenye mapungufu	3,625,000
19)	Uandishi wa taarifa za Manunuzi wenye makosa	7,500,000
20)	Bakaa ya vifaa ambayo haijahamishwa	1,160,934,158
21)	Vifaa ambavyo vimekopeshwa	133,509,210
22)	Mafuta ambayo hayakingizwa katika kitabu cha matumizi	216,789,901
23)	Mafuta ambayo hayajaingizwa katika leja	433,858,166
24)	Utoaji wa bidhaa za bohari bila ya kuzihesabu	110,066,640
25)	Ukarabati na matengenezo ya magari ya Serikali kwa Karakana Binafsibila kibali kutokaldara ya	94,922,669

<b>Na.</b>	<b>Mapungufu</b>	<b>Kiasi (Sh)</b>
	matengenezo	
26)	Vifaa ambavyo havijapokelewa	1,773,377,965
27)	Mapokezi ya vifaa bila ya kuviandika kwenye leja	93,015,600
28)	Utoaji wa vifaa bila ya kuandika kwenye leja	866,525,065
29)	Vizibiti ambavyo havijarudishwa kwa wamiliki	2,614,000
30)	Madawa ambayo yamekwisha muda wake	31,312,095
		<b>20,103,289,577</b>

Kwa maelezo zaidi angalia kiambatisho 'L'

Ninapendekeza wizara, idara na Sekretarieti za mikoa kuimarisha udhibiti wa mfumo wa ndani katika manunuzi ili kupunguza mapungufu yaliyo ainishwa na Mhakiki Mali wa Serikali.

## SURA YA NANE


### USIMAMIZI MALI NA MADENI

#### 8.0 UTANGULIZI

##### **Mchakato katika Usimamizi wa Mali**

Mchakato wa Usimamizi wa Mali unafafanua mtiririko wa kazi, taratibu na mbinu kwa ajili ya usimamizi wa mali katika kufikia malengo ya Wizara, Wakala, Idara na Sekretariati za Mikoa kwa kufuata sheria na kanuni za Umma zilizopo.

Inahusisha usimamizi wa kila hatua katika mzunguko wa mali: kupata mali, kupokea na kutunza na mwishouondoaji wa mali kwa njia mbalimbali ikiwemo uuzaji kama inavyoonywesha hapa chini:



Madhumuni ya ukaguzi yalikuwa ni kutathmini uwezo,ufanisi wa taratibu za usimamizi wa mali na vifaa hasa manunuzi, utunzaji na uwekaji kumbukumbu, uandaaji taarifa, uuzaji na ukokotoaji wa uchakavu bila kusahau kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS),sheria na kanuni zilizopo. Ili kulinda na kuhifadhi mali na vifaa, ni lazima kuwepo na udhibiti wa kutosha dhidi ya wizi na matumizi mabaya.Matokeo ya ukaguzi kwa upande wa Serikal Kuu yameonyeshwa kwa muhtasari katika aya zifuatazo hapa chini. Maelezo ya kina yanapatikana katika ripoti za ukaguzi zilizotolewa kwa Maafisa Masuuli.

#### 8.1 Mapungufu katika utunzaji wa taarifa sahihi za mali katika rejista ya mali za kudumu

Rejista ya mali za kudumu ni rejista inayotunza kumbukumbu sahihi za mali zinazomilikiwa na taasisi na ambayo inafanyiwa maboresho mara kwa mara ili kuweka

mabadiliko yaliyojitokeza na kuhakikisha usahihi wa kilicho orodheshwa. Rejista pia inaonyesha kumbukumbu ya mali zilizopo wakati wa kuanza mwaka na mwisho wa mwaka na taarifa zake hutumika katika uandaaji wa taarifa za fedha.

Rejista ya mali za kudumu ni sehemu muhimu ya mfumo wa usimamizi wa taarifa za mali. Ukubwa wa rejista ya mali za kudumu unategemea idadi na aina ya mali zilizopo katika taasisi (kama, kuongeza mali, kuuza au kuhamisha). Rejista ya mali za kudumu ni lazima kusuluhishwa mara kwa mara na vitabu vya majumuisho.

Rejista ya mali za kudumu iliyojitosheleza ni lazima iwe na maelezo yafuatayo: Jina la mali; maelezo ya kina; Namba, utambulisho wa pekee, au utambulisho mwingine wa mali; tarehe ya kununuliwa; eneo mali ilipo; watu wenye dhamana ya mali husika; inatarajiwa kudumu kwa muda gani; na tathmini ya muda wa kutumika; gharama ya kununulia mali; njia ya uchakavu, thamani ya sasa; na tarehe ya kuiondoa/kuiuza. Kumbukumbu ya mali zote ni lazima ziwekwe katika rejista ya mali za kudumu kwa ajili ya kurahisisha marejeo.

Ukaguzi ulibaini kuwepo kwa mapungufu katika usimamizi wa rejista ya mali za kudumu kama ifuatavyo:

- (i) Taarifa muhimu zilizojadiliwa hapo juu hazikuonyeshwa
- (ii) Mali hazikuingizwa katika rejista ya mali za kudumu
- (iii) Utambulisho wa pekee haukuonyeshwa katika rejista ya mali za kudumu
- (iv) Kiasi cha mali kilicho orodheshwa katika rejista ya mali za kudumu ni tofauti na kiasi kilichoonyeshwa katika taarifa za fedha.
- (v) Mali zilizoondolewa/kuuzwa kuendelea kuonekana katika rejista ya mali za kudumu.

Zifuatazo ni sampuli za Wizara, Idara Wakala, na Sekretarieti za Mikoa ambazo zimekuwa na mapungufu

katika utunzaji wa rejista ya mali za kudumu kama ilivyoainishwa hapo juu:

**Jedwali 54: Wizara, Wakala, idara na Sekretarieti za Mikoa zilizobainika kuwa na mapungufu katika utunzaji wa rejista ya mali za kudumu**

Na	Fungu	Wizara/Idara/Wakala na Sekretarieti za Mikoa
1.	10	Tume ya Pamoja ya Fedha
2.	13	Kitengo cha Kudhiti Biashara ya Fedha Haramu
3.	35	Kurugenzi ya Mashitaka ya Umma
4.	37	Ofisi ya Waziri Mkuu
5.	38	Jeshi la Wananchi wa Tanzania
6.	52	Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii
7.	61	Tume ya Taifa ya Uchaguzi
8.	65	Wizara ya Kazi na Ajira
9.	73	Sekretarieti ya Mkoa wa Iringa
10.	75	Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro
11.	78	Sekretarieti ya Mkoa wa Mbeya
12.	80	Sekretarieti ya Mkoa wa Mtwara
13.	81	Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza
14.	82	Sekretarieti ya Mkoa wa Ruvuma
15.	85	Sekretarieti ya Mkoa wa Tabora
16.	91	Tume ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya
17.	98	Wizara ya Ujenzi
18.	99	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi
19.	2005	Ubalози wa Tanzania -Abuja
20.	2021	Ubalози wa Tanzania -Kampala
21.	2023	Ubalози wa Tanzania- Bujumbura
22.	2004	Ubalози wa Tanzania -Kinshasa
23.	2024	Ubalози wa Tanzania - Riyadh

*Chanzo: Ripoti za ukaguzi kwa menejimenti kwa mwaka wa fedha 2012/2013*

Mapitio ya usimamizi wa mali yalibainisha Wizara, Wakala, idara na Sekretarieti za Mikoa 23 ambayo ni sawa na asilimia 27% ya Wizara, Wakala, idara na Sekretarieti za Mikoa zilizokaguliwa kuwa na mapungufu katika utunzaji wa rejista ya mali za kudumu. Katika mwaka wa fedha ulioishia 30 June 2013, Serikali Kuu ilianza kutumia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS) katika misingi isiyo ya fedha taslimu katika uandaaji wa taarifa za fedha, ingawa kuna kipindi cha miaka mitano ya mpito kabla ya kuanza kutumia IPSAS

kikamilifu, naishauri Serikali kuainisha mali zake zote na kurekodi katika rejista ya mali za kudumu taarifa zinazojitosheleza na pia kuondoa mali zote zilizokwishauzwa kwenye rejista.

## **8.2 Mali ambazo zimeegeshwa bila matengenezo**

Kulingana na Kanuni Na.254 (1) ya Kanuni za Fedha za Umma 2001 inataka vifaa, magari, mashine au mitambo ambayo imefikia muda wake wa mwisho au haziwezi tena kufanyiwa matengenezo au kwa sababu nyingine yeyote hazitumiki, ni lazima kubakia mpaka zifikie wingi wa kutosha kustahili kuitisha Bodi ya kuzifuta na kutoa taarifa juu ya mali hizo. Hata hivyo, katika kipindi cha mwaka wa ukaguzi, nilibaini kuwa mali mbalimbali ziliachwa na kuegeshwa bila matengenezo kwa muda mrefu na bila kufanya taratibu ya kuzifuta kama inavyoonyeshwa kwenye Kiambatisho 'M'. Nasisitiza kuwa kitengo kinachosimamia mali za Serikali kilichopo Hazina kishughulikiyekuondoa mali zilizochakaa kupitia taratibu stahiki. Mchanganuo wa aina ya mali na mkaguliwa husika ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho 'M'**

Mali ambazo zimeachwa bila matengenezo na ziko katika hali nzuri zinapaswa kufanyiwa matengenezo ili ziendelee kutumika. Naishauri Serikali kupitia kwa maafisa masuuli, kuziua na kuziondoa katika rejista ya mali za kudumu mali ambazo zimechakaa.

## **8.3 Kutothaminishwa kwa baadhi ya Majengo, Mitambo na Vifaa**

Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu Katika Sekta ya Umma (IPSAS) Na.17 aya ya 53 inahitaji "vitu ambavyo vipo kwenye daraja moja la mali kama vile majengo, mitambo na vifaa vifanyiwe tathmini kwa pamoja. Baadhi ya Wizara, Wakala, Idara na Sekretarieti za Mikoa zilifanya tathmini kwa sehemu ya mali na kuacha mali zingine bila kufanya tathmini na hivyo kusababisha kiasi cha fedha kilichoonyeshwa kwenye taarifa ya hesabu kuwa na mkanganyiko wa gharama na thamani kwa tarehe tofauti.

Mapitio ya majedwali ya mchanganuo wa majengo, mitambo na vifaa ikiwemo magari na pikipiki za Wizara, Wakala, Idara na Sekretarieti za Mikoa ilibainika kuwa taarifa za mali katika madaraja hayo hazikuonyesha thamani ya mali kinyume na aya 49 ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu Katika Sekta ya Umma Na.17. Kutokuonyeshwa kwa thamani ya mali ni dalili tosha kuwa uthamini wa majengo, mitambo na vifaa haukufanyika inavyopaswa. Vifungu ambavyo vina changamoto hii ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho 'N'**

Pamoja na kwamba Serikali Kuu imeanza kutumia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu Katika Sekta ya Umma (IPSAS) katika misingi isiyo ya fedha taslimu katika uandaaji wa taarifa za fedha. Katika kipindi cha mpitowa miaka mitano naishauri Serikali kufanya tathmini ya mali zake zote zitakazoonyeshwa katika hesabu na zile ambazo bado kufanyiwa tathmini zijulikane.

#### 8.4 Ukosefu wa nyaraka za umiliki wa Majengo, Mitambo na Vifaa (PPE)

Wakati wa mapitio ya taarifa za fedha kwa mwaka uliomalizika tarehe 30 Juni 2013, nilibaini kuwa ardhi na majengo ya Wizara, Wakala, Idara na Sekretarieti za Mikoa hayakuwa na hati miliki kuthibitisha umiliki halali wa kisheria. Hivyo, endapo litatokea tatizo hasa la kisheria kuhusiana na mali za Wizara, Wakala, Idara na Sekretarieti za Mikoa hiyo, kuna uwezekano mkubwa wa kupoteza mali hizo. Orodha ya Wizara, Wakala, Idara na Sekretarieti za Mikoa ambazo hazina nyaraka za umiliki wa mali ni kama zinavyoonekana katika jedwali Na 55 hapa chini:

#### Jedwali 55: Orodha ya Wizara, Wakala, Idara na Sekretarieti za Mikoa ambazo hazina nyaraka za umiliki

Na.	Fungu	Wizara/Idara na Sekretarieti Mikoa	Maelezo
1.	68	Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia	Jengo lililopo katika kiwanja Na. 1168/19 mtaa wa Jamhuri halina hati miliki
2.	72	Sekretarieti ya	Kutokuwepo kwa hati miliki

		Mkoawa Dodoma	katika majengo yafuatayo: Ofisi ya Halmashauri ya Mpwapwa; Kitalu A; Bahi Nyumba Na.30 Kitalu H; nyumba ya DC -Bahi; Nyumba Na.4 Kitalu H, ofisi ya DC Chamwino Nyumba Na.902 Kitalu D; ofisi ya DC Chamwino nyumba na.997 Kitalu D; RC nyumba na. 42-43 Mlimani.
3.	88	Sekretarieti ya Mkoawa Dar Es Salaam	Sekretarieti ya Mkoawa Dar Es Salaam ina kiwanja hakina hati miliki
4.	93	Idara ya Uhamiaji	Kutokuwepo kwa hati miliki katika majengo yaliyopo katika viwanja vyenye Na. 28,29,30,31,32,45,46,112,113, 114,115,116,117 na 118 eneo la Kilimatinde -Manispaa ya Tabora
5.	F75	Sekretarieti ya Mkoawa Kilimanjaro	Majengo ya ofisi yaliyopo katika ofisi ya DAS Rombo(Mashati), ofisi ya DAS Rombo (Usseri) na ofisi ya DC -Mwanga yaliyonunuliwa mwaka 1971,1972 na 1988

*Chanzo: Ripoti za ukaguzi kwa menejimenti kwa mwaka wa fedha 2012/2013*

Hati miliki ni uthibitisho wa umiliki kisheria. Naishauri Serikaliihakikishe kuwa ina chukua hatua za makusudi kufuata taratibu za kupata hati miliki za ardhi na majengo yanayomilikiwa na Wizara, Wakala, Idara na Sekretarieti za Mikoa.

## **8.5 Utambuzi usiofaa wa mali zisizoshikika Sh.31,681,109,927.58**

Taarifa za fedha za baadhi ya Wizara, Wakala, Idara na Sekretariati za Mikoa zimeainisha kiasi cha Sh.31,681,109,928 kama mali zisizoshikika (intangible assets) kinyume na matakwa ya viwango vya kimataifa vya uhasibu. Taarifa za fedha zimejumuisha kimakosa mali zisizoshikika kuwa ni pamoja na ripoti, nyaraka na gharama ya kufanya tathmini kama inavyonekana kwenye sampuli ya mafungu yaliyoko katika **Kiambatisho 'O'**.

Taarifa ya mali zisizoshikika si sahihi na inaweza kupotosha watumiaji wa taarifa hiyo.

Tatizo la mfumo wa fedha kuonyesha gharama za mali, vifaa na huduma zilizonunuliwa na taasisi za Serikali zilizotajwa hapo juu kama mali zisizoshikika linapaswa kutatuliwa na Wizara ya Fedha. Thamani halisi ya mali isiyoshikika inapaswa kuonekana katika taarifa za fedha hivyo Serikali ihakikishe kuwa thamani ya mali isiyoshikika inatolewa taarifa kulingana mahitaji ya IPSAS 31.

#### **8.6 Ukosefu wa vifaa vya ufuatiliaji (CCTV kamera) katika vituo vya mizani**

CCTV Camera na vifaa vingine vya ufuatiliaji ni muhimu kuwepo katika mizani katika barabara ili kuongeza uwazi na uwajibikaji katika uendeshaji wa vituo sambamba na kuondokana na malalamiko yasiyo ya lazima kutoka kwa wasafirishaji pamoja na kuzingatia sheria za wakala wa vipimo. Kwa kuzingatia hilo, Mkurugenzi Mtendaji wa wakala wa barabara (TANROADS) kupitia barua aliyoandika tarehe 06/07/2011 kwenda kwa Wasimamizi wa Mkoa wa TANROADS iliwataka watendaji hao kuhakikisha ukarabati wa haraka wa vifaa vya ufuatiliaji ikiwemo CCTV kamera na mfumo wa uchapishaji tiketi baada ya kupima mizigo katika mizani. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa CCTV Kamera zilikuwa bado hazijawekwa katika baadhi ya vituo kama inavyoonekana hapa chini:

- a) Namanga na Makuyuni (Arusha)
- b) Mikese, Kihonda na Mikumi (Morogoro)
- c) Uyole na Mpemba (Mbeya)
- d) Makambako (Iringa)

Vifaa vya ufuatiliaji utendaji vinatakiwa kuwepo katika mizani yote ili kuboresha uwazi na uwajibikaji katika utendaji. Serikalihaina budi kuhakikisha vifaa vya kufuatilia utendaji vinawekwa katika vituo vyote vya mizani nchini.

**8.7 Uhamisho wa fedha za maendeleo kwenda katika taasisi zilizo chini ya wizara kuonyeshwa kama mali za wizara katika taarifa za fedha za wizara Sh.696,991,606,941**

Kulingana na aya 13 ya IPSAS 17 inaeleza majengo, mitambo na vifaa kuwa ni mali ambazo zinatumiwa katika uzalishaji au usambazaji wa bidhaa na huduma, ukodishaji kwa wengine au kwa ajili ya shughuli za utawala na zinazoweza kutumiwa kwa zaidi ya mwaka mmoja wa fedha. Pia aya ya 14 ya IPSAS 17 inaonyesha sifa zinazofanya mali, mitambo na vifaa kutambulika kuwa ni pamoja na kuwepo na manufaa yatokanayo na mali husika kwa sasa na kwa siku za usoni, na kwamba thamani na gharama ya mali iwe inaweza kufahamika kwa uhakika.

Mapitio ya michanganuo ya hesabu za fedha umebaini kuwa wizara mbili zilihamisha fedha kiasi cha Sh.696,991,606,941 ikiwa ni ruzuku kwenda katika taasisi zilizo chini yake kwa ajili ya shughuli za maendeleo kama mali (majengo, mitambo na vifaa) za wizara husika.

Kimsingi uhamisho la fedha hauna sifa ya kuitwa mali (majengo, mitambo na vifaa) kwa mujibu wa muongozo tajwa hapo juu. Taarifa za fedha katika wizara hizi mbili si sahihi katika upande wa taarifa za mali na inaweza potosha watumiaji wa taarifa. Wizara zilizokuwa na mapungufu katika eneo hili ni kama inavyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 56: Uhamisho wa fedha za maendeleo kwenda katika taasisi zilizo chini ya wizara**

Na	Fungu	Wizara	Kiasi kilichohamishwa (Sh)	maelezo
1	46	Wizara ya Elimu na Mafunzo	26,797,695,648	Hamisho la fedha kwenda katika vyuo vikuu
2	98	Wizara ya Ujenzi	670,193,911,293	Hamisho la fedha kwenda TANROADS, TBA na TEMESA kwa ajiri ya shughuli

Na	Fungu	Wizara	Kiasi kilichohamishwa (Sh)	maelezo
				za maendeleo kama ujenzi na matengenezo ya barabara, ujenzi wa nyumba za Serikali na ununuzi wa vivuko
Jumla			696,991,606,941	

*Chanzo: Ripoti za ukaguzi kwa menejimenti kwa mwaka wa fedha 2012/2013*

Marekebisho katika chati ya akaunti yanatakiwa kufanyiwa kazi na Wizara ya Fedha kupitia kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali ili kutofautisha fedha za matumizi na uhamisho wa fedha za maendeleo katika mfumo wa Epicor.

#### **8.8 Mapungufu katika usimamizi wa meno ya tembo na nyara nyingine za taifa**

Wakati wa ukaguzi na uhakiki wa orodha za mali zilizoko stoo katika chumba cha pembe za ndovu (Ivory room)-Dar es salaam na vituo vya mikoani vilivyo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii, tulibainikutokuwepo kwa rejistainayoonyesha orodha ya mali zote zilizoko katika chumba cha pembe za ndovu (Ivory room) makao makuu ya wizara -Dar es Salaam. Kwa upande wa vituo vya mikoani, ukaguzi ulibaini kuwa kiasi kikubwa cha nyara za Serikali zinahifadhiwa katika vituo kwa zaidi ya mwaka mmoja bila kusafirishwa kwenda katika chumba cha pembe za ndovu kilichopo makao makuu ya wizara kwa ajili ulinzi na usalama. Pia, mapungufu yafuatayo yalibainika:

(i) **Meno makubwa 108 ya tembo na kilo 20 za pembe za ndovu yalitoweka katika kituo cha polisi Kilwa -Lindi** Mapitio ya nyaraka na kumbukumbu katika pori tengefu la Miguruwe yalibaini kuwa, katika kipindi cha kuanzia tarehe 5 Juni 2012 mpakatarehe 8 Juni 2012, meno makubwa ya tembo 108 yalikuwa ni miongoni mwa vielelezo (ushahidi)

vilivyokuwa katika kituo cha polisi Kilwa. Kati ya meno 108 yaliyokamatwa, 74<sup>30</sup> yalitoweka kituo cha polisi wakati meno makubwa 34 yalibadilishwa na meno madogo tofauti na yale yaliyokamatwa (kesi Na. ECO 3/09/2009 na kesi Na. KLM /IR/43/2010 (ECO 2/2010). Aidha, ukaguzi ulibaini kutoweka kwa kilo 20 za pembe za ndovu ambazo zilikamatwa na kuhifadhiwa kama kielelezo/ushahidi (kesi Na.KLM/IR/184/2009 (kilo 7), Na. KLM/IR/235/2009 (kilo3) na KLM /567/2010 (kilo10)).

**(ii) Meno makubwa ya tembo yalibadilishwa kinyume cha sheria na meno madogo na kusababisha hasara ya kilo 203.66 katika kituo cha Polisi Kilwa**

Meno makubwa ya tembo yenye jumla ya kilo 498.3 yalikamatwa kwa nyakati tofauti na kuhifadhiwa kwenye kituo cha polisi Kilwa kama kielelezo/ushahidi . Hata hivyo, mapitio ya nyarakazinazohusiana na meno hayo ya tembo ulibaini kuwa,menomakubwa yalibadilishwa na meno madogo ya tembo na kusababisha hasara ya kilo 203.66.

**(iii) Meno ya tembo 103 yaliyohifadhiwa kituo cha polisi Liwale bila Mkurugenzi wa wanyamapori kuwa na taarifa**

Wakati wa ukaguzi tulitembelea pori tengefu la Liwale na kubainikuwa meno ya tembo 103 yalikuwa yamehifadhiwa katika kituo cha polisi Liwale. Hata hivyo, hakukuwa na kumbukumbu yoyote katika ofisi ya pori tengefu la Liwale kuhusu meno hayo.

**(iv) Kuondolewa kwa gari kituoni**

Ukaguzi ulibaini kuwa gari No.T903 AGF lililokamatwa kama kielelezo/ushahidi liliondolewa katika kituo cha Polisi Kilwa baada ya kukamatwa na kilo 26 za meno ya tembo yenye thamani ya Sh.135,000,000 ambalo kesi yake bado inaendelea kusikilizwa mahakamani.

---

<sup>30</sup> Rejea kesi No. KLM/IR/144/2009 (4 PCS), KLM/498/2008(4 PCS), KLM/501/2008(10 PCS) KGS 15, KLM/4/2007(46 PCS), KLM/IR/277/2007(10 PCS)

Kutokana na kukosekana kwa kumbukumbu sahihi, meno ya tembo yanaweza kuibiwa au kupotea bila menejimenti kuwa na taarifa yoyote. Aidha naishauri Serikali ihakikishe kunakuwa na udhibiti wa kutosha katika usimamizi wa nyara za Serikali nchi nzima.

**8.9 Masurufu ya kiasi cha. Sh. 288,923,451 hayakuonyeshwa katika taarifa ya fedha kama ni wadaiwa**

Kulingana na Kanuni 103 (1) ya Kanuni za Fedha za Umma ya mwaka 2001 inaeleza kuwa masurufu yanatakiwa kurejeshwa maratu baada shughuli iliyokusudiwakukamilika. Ukaguzi wa kumbukumbuzinazohusu masurufu, ulibaini kuwa masurufu ya kiasi cha Sh.283,322,462 hayakurejeshwa kinyume na matakwa ya sheria. Aidha, kiasi cha masurufu yasiyorejeshwa mpaka mwishoni mwa mwaka kwa kiasi cha Sh.283,322,462 hakikuoneshwa katika taarifa za fedha kama wadaiwa kinyume na maelezo ya Waraka Na.11 wa mwaka 2012/2013 na IPSAS Na.1.Mapungufu haya yalibainika katika sampuli ya Wizara/Idara na Sekretarieti za Mkoa ifuatayo katika jedwali Na 56:

**Jedwali 57: Masurufu yasioonyeshwa katika taarifa ya wadaiwa**

Na.	Fungu	Wizara / Idara na Sekretarieti ya Mkoa	Kiasi(Sh.)
1.	44	Wizara ya Viwanda na Biashara	4,931,300
2.	49	Wizara ya Maji	158,875,201
3.	51	Wizara ya Mambo ya Ndani	119,515,961
4.	95	Sekretarieti ya Mkoa wa Manyara	1,800,000
5.	2007	Ubalozi wa Tanzania Lusaka, Zambia	3,800,989
	<b>Jumla</b>		<b>288,923,451</b>

*Chanzo: Ripoti za ukaguzi kwa menejimenti kwa mwaka wa fedha 2012/2013*

Serikali ihakikishe maafisa masuuli wanafanya kazi zao ipasavyo katika kuandaa taarifa za fedha zinazokubalika na kuzingatia miongozo ya kihasibu.Wadaiwa wote waonyeshwe katika taarifa za fedha kama Waraka Na.11 wa mwaka 2012/2013 na IPSAS Na. 1. Serikali inashauriwa

kuwa na udhibiti wa ndani ulio imara ili kuwezesha kukusanya fedha kwa wakati kutoka kwa wadaiwa mbalimbali.

#### **8.10 Madeni ambayo hayajalipwa Sh.277,728,051,810**

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2013, Wizara, Wakala, Idara na Sekretarieti za Mikoa zilikuwa na deni la kiasi cha Sh.277,728,051,810 ambalo lilikuwa bado halijalipwa. Uchambuzi wa taarifa ulionyesha kuwa deni hilo limekuwepo kwa zaidi ya miezi 12 katika Wizara, Wakala, Idara na Sekretarieti za Mikoa.

Mchanganuo wa madeni ya Wizara ya maji ulionyesha kwamba kulikuwa na madeni ya kiasi cha Sh. 6,152,485,146 kwa mwaka ulioishia 30/6/2013. Kati ya hayomadeni, Sh. 5,152,376,652 ambazo ni sawa na asilimia 80 ni madeni ya gharama za umeme ambayo miradi mbalimbali na Mamlaka za Maji wanadaiwa na TANESCO. Pia, kati ya deni lililoonyeshwa la Wizara ya Mambo ya Ndani- idara ya Polisi katika taarifa yake ya fedha, Sh.13,333,345,895.96 sawa na asilimia 11 ya deni lote, ilikuwa ni riba na adhabu kwa kushindwa kulipa mkopo wa kununulia magari uliotolewa na Mfuko wa taifa wa bima ya afya (NHIF) na Mfuko wa Taifa wa hifadhi za jamii (NSSF) katika mwaka 2010 na 2012.

Kwa kutokutenga fedha ya kulipia madeni katika bajeti kumekuwepo changamoto katika kulipia madeni ambayo yalipaswa kulipwa siku za nyuma kwani kunaweza kuathiri utekelezaji wa mipango ya siku za mbeleni pindi itakapofikia. Wizara, Wakala, Idara na Sekretarieti za Mikoa ambazo madeni yake yana zaidi ya mwaka mmoja ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho 'P'**

Serikalikwa kupitia Mlipaji Mkuu wa Serikali ihakikishe maafisa masuuli wa Wizara, Idara, Wakala, na Sekretarieti za Mikoa wanasimamiamatumiziya fedha kulingana na bajeti zao na kuhakikisha kuwa fedha zinatengwa katika bajeti ya mwaka ujao kwa ajili ya kulipia madeni ya muda mrefu.

Aidha, nashauri upande wa Serikali kuongeza bajeti sambamba na utoaji wa fedha zote zilizoidhinishwa kwenye bajeti ili kuwawezesha Maafisa Masuuli kulipa madeni kwa wakati na kuondokana na adhabu zitokanazo na ucheleweshaji wa malipo.

## SURA YA TISA

### 9.0 UKAGUZI MAALUM

#### 9.1 Utangulizi

Kwa mujibu wa kifungu cha 29 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Mdhidhibiti na Mkaguzi Mkuu anaweza kufanya ukaguzi maalum. Pia, kanuni ya 79(1) ya Kanuni za ukaguzi wa Umma za mwaka 2009 zinaeleza kwamba “Ukaguzi maalum unaweza kufanyika endapo Afisa Masuuli au mtu yeyote, Taasisi, Mamlaka ya Umma, Wizara, Idara, Wakala, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na vyombo vingine vyovyote, kuomba kwa maandishi kwa Mdhidhibiti na Mkaguzi Mkuu; ilimradi Mdhidhibiti na Mkaguzi Mkuu halazimiki kukubali ombi hilo”

Mawanda ya ukaguzi yatatolewa na mtu aliyeomba ukaguzi maalum, ijapokuwa Kanuni ya 80(2) ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009 inampa mamlaka Mdhidhibiti na Mkaguzi Mkuu kurekebishamawanda ya ukaguzi atakapoona kuna umuhimu wa kufanya hivyo.

Katika mwaka huu wa Ukaguzi, nilifanya ukaguzi maalum nne (4). Ripoti za ukaguzi maalum zilitolewa kwa Maafisa Masuuli husika. Muhtasari wa masuala yaliyojitokeza katika ukaguzi maalum ni kama ifuatavyo:

#### 9.2 Ukaguzi maalum uliofanywa kwenye hospitali teule za rufaa, za Wilaya na hospitali binafsi kwa mwaka wa fedha 2010/2011 na 2011/2012

Matokeoya ukaguzimaalum uli husu hospitali Teule 4 za rufaa, 48 za Wilaya na hospitali 39 binafsi juu ya malipo ya mishahara na matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2010/2011 na 2011/2012. Mapungufu yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi maalum ni kama ifuatavyo:-

## **Mishahara**

**Malipo ya mishahara kwa watumishi hewa Shilingi 754,992,183**

- Mishahara iliyolipwa kwa wastaafu, watoro na wasiostahili kulipwa kupitia akaunti zao binafsi kiasi cha Shilingi 754,992,183. Hii ilibainika kwa hospitali 10 kati ya 91 zilizokaguliwa.
- **Mishahara ambayo haijalipwa katika hospitali Shilingi 3,047,574,792**  
Mishahara ambayo haijalipwa shilingi 3,047,574,792 inayohusu wastaafu, watoro na maafisa wasiostahili katika hospitali mbalimbali. Mishahara hiyo haikurejeshwa Hazina badala yake menejimenti ilizitumia fedha hizo kuwalipa wafanyakazi ambao hawapo kwenye utaratibu wa mishahara ya Serikali na fedha nyingine kulipa matumizi ya kawaida ya hospitali.
- **Malimbikizo ya mishahara ambayo hayajalipwa shilingi 2,323,084,860.** Malimbikizo ya mishahara ambayo haijalipwa kwa muda mrefu yalifikia kiasi cha shilingi 2,323,084,860.

## **Malipo ya kawaida**

- **Hospitali kutotenganisha akaunti za fedha wanazopokea toka Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na mapato ya vyanzo vingine.**  
Baadhi ya hospitali zinachanganya ruzuku toka Serikalini pamoja na mapato mengine ya hospitali kwenye akaunti moja. Pia, kuna hospitali ambazo hazitenganishi vitabu vya fedha (Vote book) vya ruzuku toka Serikalini kupitia wizarani na mapato ya vyanzo vingine vya hospitali.
- **Madeni na miadi ambayo haijalipwa Shilingi 2,511,881,024**  
Ukaguzi ulibaini madeni yatokanayo na malimbikizo ya mishahara, posho za likizo na madeni ya wafanyabiashara kiasi cha shilingi 2,511,881,024.

Kutokulipa madeni kwa wakatikunahatarisha kwa kiasi kikubwa matumizi ya bajeti ambapo fedha itakapotumika kulipa madeni na miadi na kupelekea kutofikiwa malengo yaliyopangwa kwa mwaka husika.

- **Hospitali hazijathibitisha kupokea Shilingi 304,075,145**  
Kiasi cha shilingi 304,075,145 fedha ambazo zilitolewa kwaajili ya matumizi ya hospitali hazijathibitishwa kupokelewa.
- **Tofauti kati ya fedha iliyotumwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na fedha halisi iliyopokelewa na hospitali zilizokaguliwa Sh.84,996,355**  
Kiasi cha shilingi 823,870,474 kilipelekwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwenye hospitali teule za wilaya na hospitali binafsi. Ukaguzi maalum ulibaini kuwa kati ya Sh. 823,870,474 zilizopelekwa na Wizara ni kiasi cha shilingi 738,874,119 ndicho kilipokelewa na kusababisha tofauti ya Shilingi 84,996,355 ambazo zimekosa usuluhisho.
- **Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kutuma fedha kwenye hospitali bila mchanganuo wa matumizi.**  
Ilionekana kuwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii hutumafedha kwendakwenye hospitali bila mchanganuo wa matumizi.

### **9.3 Ukaguzi maalum wa Wizara ya Ujenzi kuhusu ununuzi wa kivuko cha Misungwi**

Wizara ya Ujenzi inawajibika kupitia Wakala wa Umeme na Ufundi (TEMESA) kusimamia vivuko hapa nchini ikiwa ni pamoja na kivuko cha Misungwi. Katika mwaka wa fedha 2004/2005, Wizara iliingia Mkataba na kampuni ya Sinnautic International ya Uholanzi kwa ajili ya kununua kivuko cha kufanya kazi kati ya kigongo - Busisi kwa gharama ya €2,483,441 CIP - Mwanza. Gharama hii ilijumuisha gharama ya vipuri.

Ukaguzi maalumu ulibaini mapungufu yafuatayo:-

- Injini moja kubwa aina ya Caterpillar No.1 inafanya kazi baada ya kuunganishwa moja kwa moja na (propulsion unit) bila ya kupitia kwenye 'clutch' ambayo kazi yake kubwa ni kuunganisha mzunguko ya injini. Uunganishaji huo unaweza kusababisha injini kuharibika mapema kwani injini itakapowashwa italazimika kuzunguka moja kwa moja na kusukuma Kivuko upande wowote utakaoelekezwa na Nahodha.
- Uongozi wa Wizara ya Ujenzi kutosimamia kwa karibu mkataba wa ununuzi wa kivuko. Mtendaji mkuu wa Wizara ambaye ndiye Afisa Masuuli hakuwa anafuatilia mwenendo na maendeleo ya taratibu za ununuzi wa kivuko.
- Kulikuwepo mabadiliko katika mkataba bila idhini ya Afisa Masuuli ambaye ndiye mtendaji Mkuu wa Wizara na wala idhini ya bodi ya ununuzi (Tender Board) ambayo ndio ingeruhusu mabadiliko katika mkataba.
- Mzabuni bado hajakabidhi rasmi kivuko kwa Wizara ya Ujenzi kulingana na mkataba Na. 10014/2004/05 wa ununuzi wa kivuko cha Misungwi, ingawaje kivuko hiki kimeshaanza kutumika.
- Upotevu wa kiasi cha Sh. 29,402,371.80 zilizotumika kugomboa vipuri hewa uliotokana na kuhamisha jukumu la ugomboaji wa vipuri kutoka kwa mzabuni kwenda Wizara ya Ujenzi kinyemela na kinyume na mkataba.
- Mzabuni alishindwa kuleta kivuko kwa wakati kulingana na masharti ya mkataba.
- Katibu Mkuu hakuteua kamati ya mapokezi ya kivuko kulingana na sheria na kanuni za manunuzi ya umma.
- Utata katika kupokea vipuri uliohusisha; mabadiliko ya sehemu ya kupokelea vipuri Dar es salaam badala ya Mwanza, kubadilisha mgomboaji wa vipuri kuwa Wakala wa Serikali wa kugomboa shehena bandarini badala ya mzabuni mwenyewe kama ilivyo kwenye mkataba.
- Kampuni ya Sinnautic International haikuzingatia masharti ya mkataba, kwa kuwa hadi leo hii hajamaliza kazi zote zilizokuwa zimeainishwa kwenye mkataba kama vile kuleta vipuri vya thamani ya Euro 41,140,

mashine ya kubana hewa au gesi, mashine ya kufanyia majaribio ya utemaji wa dizeli havijakamilishwa.

- Udhafu katika sheria ya MerchantShippingAct,2003imesababishausajili waMVMisungwikwanamba za usajiliMZ/ P032katika bandari yaMwanzamwaka 2008bilakuwa na cheti cha usalama majini na cheti cha ubora na umahiri wa wafanyakazi.

#### **9.4 Ukaguzi maalum wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kuhusu Mfumo wa Pembejeo za kilimo wa Taifa**

Mfumo wa pembejeo za kilimo wa taifa ulianzishwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2008 kwa ajili ya utekelezaji mradi wa kuongeza kasi ya uzalishaji wa chakula. Dhumuni la mradi ni kuchangia katika kuongeza uzalishaji wa vyakula na tija katika kilimo kwenye maeneo yaliyokusudiwa kwa kuboresha upatikanaji wa pembejeo muhimu za kilimo kwa wakulima. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatekeleza mradi huu kupitia Wizara ya Kilimo, Chakulana Ushirika. Ukaguzi maalumu ulibaini mapungufu yafuatayo:

##### **9.4.1 Ngazi ya Wizara**

- Wizara kuchelewa kufanya manunuzi ya vocha za pembejeo za kilimo na hivyo kusababisha vocha za kilimo kuwafikia walengwa baada ya majira ya mvua.
- Utunzaji na uandaaji mbaya wa taarifa za vocha za pembejeo za kilimo. Hii imesababisha Wizara kukosa taarifa ya vocha za pembejeo za kilimo zilizosalia na kurejeshwa wizarani kwa mwaka wa fedha 2010/11 na 2011/12. Vitabu vya kumbukumbu za vocha za pembejeo za kilimo ambazo hazijatumika na kurejeshwa kutoka Wilayani havionyeshi namba ya vocha za pembejeo za kilimo zilizotumika.
- Ukosefu wataarifa za kutoshajuu yausambazaji wa mbolea na mbegunchini. Uagizaji kutoka nje ya nchi na usambazaji wa pembejeo za kilimo upo chini ya sekta binafsi zinazojishughulisha na pembejeo za kilimo.

- Ukosefu wamwongozowa uendeshaji wamfumo wa Pembejeo za kilimo wa Taifa.

#### 9.4.2 Ngazi ya Mkoa

- Ukosefu wa kumbukumbu za kutosha wa vocha katika mikoa ya Arusha na Mbeya.
- Mikoa ya Arusha, Lindi na Rukwa kuchelewa kusambaza vocha za pembejeo wilayani.

#### 9.4.3 Ngazi ya Wilaya

- Utunzaji mbaya wa taarifa za wasambazaji/wauzaji wa pembejeo za kilimo katika wilaya za Karatu, Meru, Karagwe, Lindi na Mpanda.
- Kukosekana kwa vigezo vya kuteua wazambazaji/wauzaji wa pembejeo za kilimo katika wilaya za Karatu, Lindi, Nkasina Mpanda.
- Utunzaji mbaya wa taarifa za vocha za pembejeo katika wilaya za Karatu, Chato, Ruangwa, Meru na Kilosa.
- Wilaya za Karatu, Meru, Lindi, Ruangwa na Kilosa kuchelewa kusambaza pembejeo za Kilimo vijijini.
- Kutofanyika kwa ukaguzi wa mbolea na mbegu kwa mujibu wa kifungu cha 5(i) cha sheria ya mbolea ya mwaka 2009 katika wilaya za Karagwe na Mpanda.
- Kuchelewa kufika vocha za pembejeo katika wilaya za Ulanga na Nkasi.
- Tuhuma za wizi wa vocha za pembejeo ambazo hazikupelekwa kwa walengwa katika wilaya ya Chato.
- Vocha za pembejeo zenye thamani ya shilingi 1,159,834,000 ambazo hazikutumika katika wilaya ya Chato hazikurejeshwa Wizarani.

#### 9.4.4 Ngazi ya Vijiji

- Wilaya kushindwa kusimamia mradi ipasavyo
- Katika kijiji cha Laghangareri wilayani Karatu, walengwa 300 kati ya 900 hawakupewa vocha za pembejeo za kilimo kwa mwaka 2010/2011.
- Muuzaji wa pembejeo za kilimo katika kijiji cha Jobaj wilayani Karatu, EagleAgrovet alikabidhiwa vocha za

pembejeo za kilimo na Afisa mtendaji wa kijiji, kinyume na waraka uliotolewa na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

- Walengwa katika kijiji cha Jobaj wilayani Karatu walipewa mbegu bora kati ya kilo kumi hadi kumi na mbili au mbolea ya kupandia kwa mwaka 2010/11 na mwaka 2011/12 wakibadilishana na vocha za pembejeo za kilimo za mbolea, ijapokuwa thamani ya vocha za kilimo za mbolea ni kubwa ukilinganisha na pembejeo walizopewa walengwa.
- Wananchi ambao hawamo katika orodha ya walengwa katika vijiji vya Nyabishenge na Kaisho wilaya ya Karagwe na Vijiji vya Ngaibara, Jobaj na Kilimamoja wilayani Karatu walipokea vocha za pembejeo za kilimo bila kufuata utaratibu.
- Ukosefu wakumbukumbu zawalengwakatika kijijicha MawiloWilaya ya Lindi.
- Walengwa kutokuwa na uwezo wa kifedha kuchangia gharama za pembejeo za kilimo ambazo ni ghali.
- Katika vijiji vya InchankimanaMsilale wilayani Chato vocha za pembejeo za kilimo zilikua zinanunuliwa na Wauzaji wa pembejeo kwa shilingi 10,000 kila moja mwaka 2010/11.
- Walengwa katika wilaya za Ulanga na Karagwe kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mfumo wa pembejeo wa taifa.
- Mbegu bandia zilisambazwa kwa walengwa katika vijiji vya Mpanda, Kaisho na Nyabishenge wilaya ya Karagwe na kijiji cha Idunda wilaya ya ulanga.
- Wasimamizi wa mradi kuchelewa kuwapelekea walengwa vocha za pembejeo katika mwaka 2011/12.
- Mjumbe wa kamati ya vocha ya kijiji cha Ntene wilayani Lindi aliteuliwa na muuzaji wa pembejeo za kilimo kuwa wakala wake.
- Walengwa waliopo vijiji vya chinongwe na Litima katika wilaya ya Ruangwa hawakupata vocha cha pembejeo za kilimo kutoka wilayani.
- Katikakijiji cha Mamba wilaya ya Mpanda walengwa wamelalamikia juu ya ubora wambegu za

mahindinambolea. Mbegu na mbolea hizo hazina ubora na hivyo mavuno hayakuwa kama walivyotarajia.

#### **9.5 Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuhusu matumizi mabaya ya fedha za ada katika Chuo cha Uuguzi Mkomaindo**

Katika mwaka wa fedha 2012/2013, ukaguzi maalum ulifanyika kwenye makusanyo ya ada za mafunzo na matumizi yake katika Chuo cha Uuguzi Mkomaindo na mapungufu yafuatayo ndiyo yaliyojitokeza katika ukaguzi huo:-

- Kukosekana kwa daftari la fedha la kurekodi makusanyo ya ada za mafunzo; na kutofanyika kwa usuluhisho wa benki kinyume cha kanuni ya 162(1) ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 inayotaka kufanyika usuluhisho kati ya daftari la fedha na benki kufanyika kila mwezi.
- Kulikuwa na udhaifu katika utunzaji wa daftari la kupokea na kutoa nyaraka za fedha(counterfoil register) uliosababisha kuwapo kwa tofauti kati ya tarehe halisi ya kupokea kitabu cha stakabadhi kutoka Hazina Ndogo Mtwara na tarehe ambayo imeingizwa kwenye daftari la kupokea nyaraka za fedha (counterfoil register), stakabadhi nane (8) na nyaraka mbili (2) za kupeleka fedha benki havikuingizwa kwenye daftari la kupokea nyaraka za fedha pamoja na kuwa vilitumika kukusanya fedha za ada za wanachuo.
- Ukaguzi ulibaini ada ya mafunzo iliyopokelewa kwa fedha taslimu kiasi cha Sh.31,056,000 ambazo hazikupelekwa benki kwenye akaunti ya Chuo ya Makusanyo ya ada za mafunzo wala haikuwepo kwenye ofisi ya kuhifadhia fedha taslim, kinyume na kanuni ya 60 ya Kanuni za fedha za umma.
- Kulikuwa na barua za udahili wa wanachuo za kughushi katika mwaka wa masomo 2010/2011.

## SURA YA KUMI

### MASUALAMENGINE

#### 10.0 UTANGULIZI

Kulingana na Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 na Kanuni 34 ya kanuni za ukaguzi wa umma za mwaka 2009, inamwezesha Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu kutoa mapendekezo kwa Serikali kwa ajili ya jambo lolote ikiwa ni pamoja na usimamizi bora wa fedha za umma, maghala ya Serikali, dhamana, mihuri na masuala mengine ya rasilimali za umma. Katika sura hii nimetoa mapendekezo yangu juu ya masuala yafuatayo:

- Uendeshaji wa Wakala wa Serikali
- Malipo ya kodi ya pango kwa wamiliki wa majengo kwa ajili ya ofisi za Wizara, Wakala na Idara mbalimbali
- Masuala yanayohusu Usimamizi wa Magereza.
- Jukumu la Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu katika ukaguzi wa hesabu za miradi inayosimamiwa kwa Ushirikiano bainaya Serikali na Sekta Binafsi (PPP)
- Masuala ya yaliyojitokeza katika ukaguzi wa vyama vya siasa.

#### 10.1.0 Tathmini ya Wakala wa Serikali

Wakala wa Serikali ni taasisi za umma zilizoanzishwa chini ya Sheria ya Wakala ya mwaka 1997, na hufanya kazi chini ya wizara. Kabla ya kuanzishwa kwa Wakala zilikuwepo kama idara chini ya Wizara lakini Serikali iliamua kuzibadilisha kuwa wakala. Miongoni mwa malengo mengi ni; (a) Kuboresha utoaji wa huduma za umma (b) kuboresha ubora wa huduma (c) kukuza na kuendelea kuboresha huduma.

Ili kufikia malengo yaliyotajwa hapo juu, Serikali ilitoa uhuru zaidi kwa wakala wa Serikali, kama kuajili nje ya masharti ya utumishi wa umma na kuwa na uwezo wa kumiliki mapatowanayozalisha. Haya yote yalifanyika ili kuwahamasisha watumishi wa wakala kufanya kazi kwa bidii, kitaaluma, na kwa uadilifu mkubwa ili kufikia malengo ya kutoa huduma za umma kwa ufanisi zaidi.

Ukilinganisha wakala na idara za Serikali, unaweza kuona wazi kwamba:

- (i) Kiwango cha huduma kinachotolewa kimekuwa bora sasa ikilinganishwa na wakati ambapo wakala walipokuwa idara katika wizara.
- (ii) Ubora wa huduma zinazotolewa kwa umma umeongezeka, wakala wa Serikali wamekuwa wakitoa huduma bora ikilinganishwa na huduma walizokuwa wakitoa walipokua idara chini ya wizara.
- (iii) Ikilinganishwa na idara, ukusanyaji wa mapato umeboreka.
- (iv) Gharama za utawala kwawakala wa Serikali zimeongezeka ikilinganishwa na gharama za utawala wakati wakala zikiwa idara chini ya wizara.

Licha ya kulinganisha kati ya Wakala za Serikali na idara za Serikali, kwa kipindi kirefu wakala wa Serikali zimekuwa zikikabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zinahitaji Serikali kuingilia kati ili kuzitatua. Zifuatazo ni baadhi ya changamoto ambazo wakala nyingi za Serikali zimepitia.

#### **10.1.1 Utegemezi wa fedha toka Serikalini**

Wakala wa Serikali nyingi bado zinategemea ruzuku kutoka Serikalini. Vyombo hivi vilianzishwa vikiwa na mtazamo wa kuweza kujitegemea kifedha kama ilivyoelezwa katika kifungu Na. 12 cha Sheria ya uwakala ya mwaka 1997 (Sura ya 245 iliyofanyiwa marekebisho mwaka, 2009). Sehemu hii inasema wazi kwamba fedha za wakala zinatokana na fedha zilizopatikana kutokana na utoaji wa bidhaa na huduma na malipo ya ada ambayo yataziwezesha wakala kukidhi matumizi yao. Lakini imebainika kwamba Wakala wa Serikali kwa kiasikikubwa wamekua tegemezi kwenye fedha za Serikali ili kufidia gharama zao za uendeshaji ikiwa ni pamoja na kulipa mishahara ya watumishi na baadhi ya shughuli zao za maendeleo. Hii inaonyesha hatari kubwa juu ya uwezekano wa wakala kuweza kuwa na huduma endelevu kutokana na utegemezi wao.

### 10.1.2 Ukosefu wa fedha za kutosha kuziwezesha wakala

Wakala wa Serikali bado zinategemea ruzuku toka Serikali. Imeonekana kwamba fedha za kuendesha wakala hazitoshi. Pamoja na ukweli kwamba vyombo hivi awali vilianzishwa kwa lengo la kutoa huduma bora kwa umma kwa kutumia fedha zao wenyewe zinazopatikana kutokana na malipo ya ada, tozo mbalimbali, mauzo ya bidhaa au huduma, wakala bado zinapata ruzuku toka Serikalini. Imebainika kuwa fedha inayopatikana bado ni chini ya bajeti zao. Jedwali hapa chini linaonyesha baadhi ya wakala, makadirio yao na fedha halisi walizopata kwa mwaka 2012/2013.

#### Jedwali 58: Upungufu wa fedha

Jina la wakala	Makadirio (Sh.) (A)	Fedha Halisi iliyopokelewa (Sh.) (B)	Kiasi Kisichotolewa (Sh) C=(A-B)	Asilimia $D=C/A*100$
Wakala wa Umeme vijijini	139,608,473,000	43,832,473,000	(95,776,000,000)	(69%)
Wakala za mbegu za kilimo	3,905,348,918	688,472,050	(3,216,876,868)	(82%)
Wakala wa Umeme na Ufundi	16,517,804,783	5,212,086,776	(11,305,718,007)	(68%)
Wakala wa Majengo Tanzania	7,854,766,677	2,500,848,001	(5,353,918,676)	(68%)

*Chanzo: Ripoti ya ukaguzi kwa menejimenti*

Kutokana na jedwali hapo juu tunaweza kuona wazi kwamba kuna uhaba wa fedha kutoka Serikalini kuwezeshawakala za Serikali. Pia, kwa kiwango kikubwa hililinaathiri mafanikio tarajiwa ya kuanzishwa kwa wakala. Ni vigumu sana kwa wakala kutoa huduma bora kama asipowezeshwa kifedha kama inavyoonekana hapo juu. Ili kufikia lengo kuu la kuanzisha wakala wa Serikali la kutoa huduma za kutosha na ubora, ni muhimu kwa Serikali kutoa fedha kwa wakala kama zilivyoidhinishwa katika makadirio.

### 10.1.3 Serikali Kuchelewa kupeleka fedha

Pamoja na kuwepo kwa upungufu wa fedha, pia fedha zinazotolewa zimekuwa kwa kiasi kikubwa zinatolewa kwa

kuchelewa. Fedha isipotolewa kwa wakati kuna athari kubwa kwa walengwa kutofikia malengo yao. Kwa huduma kuwabora na kamilifu inatakiwafedha itolewe kwa wakati. Kama Serikali haiwezi kutoa fedha kwa wakati hakuna jinsi ambavyo wakala anaweza kutoa huduma bora. Wakala wamekuwa wakipokea fedha si kwa mujibu wa mipango yao ya utekelezaji na hili linaathiri utekelezaji wa shughuli za wakala.

#### 10.1.4 Upungufu wa idadi ya watumishi na vitendea kazi

Nimebaini kuna upungufu wa watumishi wenye sifa stahiki na vitendea kazi kwa wakala wa Serikali. Wakala zilianzishwa kwa ajili ya kuboresha huduma za umma. Uboru wa huduma huenda pamoja na idadi nzuri ya watumishi na vitendea kazi kama magari. Ni vigumu wakala kutoa huduma bora kama hawana idadi ya kutosha ya watumishi wenye ujuzi na vitendea kazi. Ili wakala ziweze kutoa huduma bora na kuboresha upatikanaji wa huduma, ni muhimu sana kwa kuwa na idadi nzuri ya watumishi wenye sifa ikiwa ni pamoja na vitendea kazi vyote muhimu.

#### 10.1.5 Kutofikia Lengo kwenye ukusanyaji wa mapato

Kulingana na kifungu cha 12 (2) (a) cha Sheria ya uwakala ya mwaka 1997 (Sura ya 245 iliyofanyiwa marekebisha mwaka 2009) kinasomeka, Wakalaitatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa kanuni zakibiashara na itahakikisha kwamba, mapato yake yanatosha kukidhi matumizi yake. Ukaguzi wa mwaka huu umebainisha kwamba, baadhi ya wakala zimeshindwa kukusanya mapato kufikia makisio yaliyopitishwa. Hali hii inaonyesha ni vigumu kwa wakala kuweza kukidhi mahitaji yao wenyewe bila kutegemea fedha kutoka wizarani. Angalia jedwali hapa chini likionyesha mapato na makisio.

#### Jedwali 59: Upungufu katika makusanyo

Jina la wakala	Makadirio (Sh.)	Mapato Halisi (Sh.)	Kiasi Kisichokusanywa (Sh)	Asili mia
Wakala wa Mbegu za kilimo	4,031,144,000	3,243,186,175	787,957,825	20%
Wakala wa Umeme	27,922,064,400	22,732,726,218	5,189,338,182	19%

na Ufundi				
Wakala wa huduma za misitu Tanzania	74,628,558,879	62,668,602,055	11,959,956,823	16%

*Chanzo: Ripoti ya ukaguzi kwa menejimenti*

Moja ya majukumu ya wakala ni kutoa huduma bora kwa umma na kupata mapato kutoka kwa wale wanaotumia huduma hizo. Hivyo basi ni muhimu mapato yaendane na huduma iliyotolewa. Kama ukikadiria kukusanya kiasi fulani cha mapato kutokana na huduma unayoitoa, kushindwa kufikia lengo inaweza kuashiria kuwa huduma zinazotolewa hazitolewi kwa ubora uliokusudiwa. Wakala kujitegemea kifedha wanapaswa kuwa na uwezo wa kutoa huduma bora kwa umma ambayo itawawezesha kupata mapato ya kutosha kulipa madeni yao na sehemu ya mapato kuisaidia Serikali.

#### **10.1.6 Mapendekezo**

Kutokana na changamoto nilizoeleza hapo juu, napendekeza Serikali kufanya yafuatayo kwa wakala wa Serikali:-

- Wakala zote za Serikali zilizoanzishwa kwa lengo la kutoa huduma kwa umma na kupata mapato kutokana na huduma wanazozitoa, ni wakati muafaka kwao kushindana katika dunia ya kibiashara kwa kuwa wabunifu zaidi na kuongeza ubora wa viwango vya huduma vinavyohitajika. Hili litaboresha makusanyo yao na kupunguza utegemeziwa fedha kutoka Serikali kuu.
- Wakala ambazo zilianzishwa kwa lengo la kupeleka huduma kwa idadi kubwa ya wateja, zinatakiwa kufanya hivyo. Ili kuwa na idadi kubwa ya wateja, itawawezesha kuwa chanzo kizuri cha mapato na hivyo kuweza kukidhi matumizi yao.
- Ili kutoa huduma bora ni muhimu wakala zikawa na watumishi wenye ujuzi wa kutosha na vitendea kazi. Wizara husika kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-Utumishi zinatakiwa kuhakikisha kwamba wakala zina watumishi wa kutosha wenye sifa stahiki pamoja na vitendea kazi muhimu ambavyo vitawawezesha

kuongeza kiwango cha huduma na kuboresha huduma wanazotoa kwa wananchi.

## 10.2 Ulipaji wa kodi ya kupanga ofisi Sh. 7,895,872,337

Serikali ya Tanzania ina Wizara, Idara, Wakala na Tume zilizo chini ya wizara zilizokaguliwa, na katika ukaguzi wa mwaka huu wa fedha, nimegundua kuwa kuna baadhi ya Wizara, Idara na wakala wa Serikali ambazo hazina majengo ya ofisi zao binafsi. Wizara, Idarana wakala wa Serikali hizi zimekuwa zikipanga katika majengo mbalimbali na kulipa pesa nyingi kama kodi ya pango kwa matumizi ya ofisi. Ukaguzi uliofanyika katika sampuli za wizara, idara na wakala umebaini kuwa jumla ya wizara/idara na wakala 14 kwa mwaka wa fedha 2012/2013 zimelepa kiasi cha Sh.7,895,872,337 kwa ajili ya kodi ya pango. Ukaguzi umebaini kuwa baadhi ya majengo haya yanamilikiwa na makampuni binafsi. Jedwali hapa chini linaonyesha mchanganuo wa sampuli.

### Jedwali 60: Ulipaji wa kodi ya pango katika Wizara na Idara za Serikali

Fungu	Wizara, Idara na Wakala wa Serikali	Kiasi(Sh.)
96	Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo	1,038,809,034
	Idara ya huduma za habari (Department of Information Service)	216,000,000
98	Wizara ya Ujenzi	482,219,184
	Wakala wa barabara Tanzania (TANROADS)	1,432,616,640
	Bodi ya mfuko wa barabara (Roads Fund Board)	531,300,000
10	Tume ya pamoja ya fedha	159,264,127
61	Tume ya Uchaguzi ya Taifa	937,200,000
35	Kurugenzi ya mashitaka ya umma	654,506,859
43	Mkulima wa kisasa (Modern Farmer) - Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika	81,120,000

Fungu	Wizara, Idara na Wakala wa Serikali	Kiasi(Sh.)
	Mamlaka ya vitambulisho vya Taifa ( NIDA)	1,423,142,893
97	Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki	435,585,600
12	Tume ya Utumishi wa Mahakama	129,708,000
40	Mahakama ya kazi (Labour court)	116,400,000
40	Mahakama ya ardhi (Land court)	258,000,000
	<b>Jumla</b>	<b>7,895,872,337</b>

*Chanzo: Taarifa za Fedha kwa mwaka 2012/2013*

Mchanguo hapo juu unaonyesha gharama kwa wizara, idara na wakala wa Serikali zilizochaguliwa kukakuliwa kama sampuli. Hivyo Serikali imekuwa ikilipa kiasi kikubwa kwa makampuni na watu binafsi kwa ajili ya kodi ya pango kwaajili ya Wizara, Idara na wakala zake. Kama Serikali ingekuwa na majengo yake kwa ajili ya Wizara. Idara na wakala kiasi tajwa hapo juu kingeweza pelekwa katika shughuli nyingine muhimu za kimaendeleo. Kwa kuziweka ofisi za Serikali kwenye majengo ya Makampuni na watu binafsi kunaiingiza Serikali katika gharama kubwa inayotokana na ulipaji kodi. Kwa dunia ya sasa hivi, gharama za kodi ya pango inapanda kila siku, na hii inatokana na ukweli kwamba mahitaji ya nyumba yanaongezeka sana, hivyo inategemewa kuwa Serikali itaendelea kuingia katika gharama kubwa kwa ajili ya kulipia kodi ya kupangajengo la ofisi kwa wizara, idara na wakala za Serikali.

Kunaumuhimu wa Serikali kuwekeza katika ujenzi wa majengo yakeenyewe. Ninaishauri Serikali kuwa na mpango endelevu wa kujenga majengo kwa ajili ya ofisi za Serikali. Serikali inaweza kufanya yafuatayo ili kufanikisha jambo hili.

- Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, nyumba na maendeleo ya makazikwa kushirikiana na Wakala wa majengo Tanzania (TBA) watafute maeneo ambayo Serikali inaweza kujenga ofisi za wizara, idara na wakala wake.

- Serikali ifanye majadiliano na Mifuko ya hifadhi ya Jamii ili waweze kupata mkopo kwa ajili ya kugharamia miradi yaujenzi wa majengo ya Serikali.
- Serikali pia ifanye mazungumzo na washirika wa maendeleo kama vile Benki ya Maendeleo ya Africa (AfDB) na Benki ya Dunia ili waweze kupata mikopo/misaada kwa ajili ya miradi ya ujenzi wa Ofisi hizo.
- Kwa zile wizara, idara na wakala za Serikali ambazo zinakusanya mapato kutokana na shughuli zao, nashauri watumie mapato ya ndani ya wizara kuanza kujenga ofisi zao binafsi.

### **10.3 Changamoto zilizopo huduma ya magereza Tanzania**

Idara ya magereza ni idara muhimu inayoshughulikia maisha ya watazania. Kwa kawaida, magereza ina kazi tatu za msingi, moja ikiwa ni usalama na udhibiti wa wahalifu, pili ni kuwaadhibu wahalifu na tatu ni kuwabadilisha waharifu na kuwa raia wema.

Kwa sasa kuna magereza 122 yanayojumuisha magereza ya wanaume, wanawake na vijana. Magereza yote 122 yana wajibu wa kuwatunza na kuwaangalia wafungwa zaidi ya 45,000 wakati uwezo wake ni wafungwa 22,669. Hii inamaanisha kwamba magereza yamezidiwa na idadi ya watu kwa zaidi ya asilimia 100 na hii inasababisha ugumu katika kudhibiti na kufuatilia wafungwa katika magereza yenye msongamano.

Nilifanya ziara katika moja ya magereza na nikabaini masuala mengi ambayo yamenifanya nitoe mapendekezo yangu kwa Serikali ili ichukue hatua muhimu kuokoa hali ya sasa iliyopo katika magereza mengi nchini Tanzania. Kati ya masuala mengi niliyoyaona, yafuatayo yanawakilisha nilichokiona wakati wa ukaguzi na mapendekezo juu ya hali inayoendelea katika magereza nchini.

### 10.3.1 Bajeti finyu

Ni kweli kwamba idara nyingi zina matatizo ya kifedha, taasisi nyingi zinaendeshwa kwa ufinyu wa mgao wa bajeti. Lakini magereza na taasisi nyingine ambazo zinashughulika na maisha ya watu moja kwa moja kama hospitali na kadhalika zinahitaji kuangaliwa wakati wa kupitia bajeti zao. Magereza yanahitaji chakula cha kuwalisha wafungwa, kuwavisha na kutunza afya zao. Si tu kuhudumia wafungwa, taasisi hii inahitaji kununua mavazi/sare kwa ajiri ya maafisa wake, kulipa posho za likizo, kulipa posho ya uhamisho na mengine mengi.

Katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, idara ya magereza ili bajeti ya Sh.131.5 bil kwa matumizi ya kawaida na Sh.51.6 bil kwa miradi ya maendeleo. Kutokana na ufinyu wa bajeti, Idara ya magereza walipewa bajeti yenye ukomo ya Sh. 51.4 bil kwa matumizi ya kawaida na Sh.1.3 bil kwa shughuli za maendeleo.

Ukaguzi iliangalia mahitaji na bajeti iliyoidhinishwa katika sampuliya vifungu vya matumizi vilivyoathirika kutokana na kupungua kwa mgao wa bajeti kama vile mavazi ya wafungwa, chakula cha wafungwa na sare za wafanyakazi. Angalia jedwali hapa chini.

**Jedwali 61: Bajeti finyu**

Maelezo	Mahitaji halisi (Sh)	Bajeti iliyoidhinishwa (Sh)	Tofauti kati ya bajeti iliyoidhinishwa na mahitaji halisi	%
Chakula cha wafungwa	32,400,320,000	8,000,001,000	(24,400,319,000)	75%
Mavazi ya wafungwa	1,583,198,200	500,000,000	(1,083,198,200)	68%
Sare za wafanyakazi	3,707,888,000	350,000,000	(3,357,888,000)	91%

*Chanzo: Kitabu cha bajeti na mapendekezo ya bajeti kutoka kwa menejimenti*

Kutokana na jedwali hapo juu inaonekana kwamba maeneomatatu yaliathirika zaidi. Mahitaji halisi hayakufikiwa hata nusu yake. Mlinganisho huu unatoa picha kwamba wafungwa hawapati mgaounaohitajika wa

chakula, mavazi kwa wafanyakazi kama inavyotakiwa na hivyo kusababisha mazingira ya kazi kuwa magumu.

### 10.3.2 Upungufu wa fedha zilizotolewa

Pamoja na ukweli kwamba ukomo wa bajeti waliyopewa idara ya magereza ilikuwa nusu ya mahitaji, lakini bado fedha iliyoidhinishwaya taasisi hii haikutolewa kama ilivyoidhinishwa. Katika mwaka huu wa fedha kulikuwa na upungufu wa fedha wa kiasi cha Sh. 23,683,463,320 katika matumizi ya kawaida ambayo ni sawa na asilimia 16 ya bajeti; na kwa upande wa fedha za maendeleo kulikuwa na upungufu wa kiasi cha Sh. 525,485,285 sawa na asilimia 34 ya bajeti ya maendeleo. Uchambuzi wa bajeti dhidi ya kiasi cha fedha kilichotolewa ni kama kinavyoonekana katika jedwali hapa chini:

#### Jedwali 62: Upungufu wa fedha zilizotolewa

Maelezo	Bajeti iliyoidhinishwa (Sh)	Kiasi kilichotolewa (Sh)	Tofauti ya Kiasi kilichotolewa na Bajeti iliyoidhinishwa	%
Bajeti ya matumizi ya kawaida	143,414,319,789	119,730,856,469	(23,683,463,320)	(16%)
Bajeti ya maendeleo	1,535,655,285	1,010,170,000	(525,485,285)	(34%)

*Chanzo: Taarifa ya fedha ya idara ya magereza*

Jedwali hapo juu linaonyesha kwamba kuna changamoto kubwa kwa taasisi hii kwa kuhudumia zaidi ya wafungwa 45,000 na maafisa wake na hii inaathiri masuala ya chakula, sare kwa maafisa na wafungwa, likizo za watumishi, gharama za uhamisho na kwa kiwango kikubwa inaathiri malipo ya madeni kutoka kwa wauzaji.

### 10.3.3 Ongezeko la madeni kutoka kwa wauzaji na madai ya wafanyakazi

Huduma ya chakula kwa ajili ya magereza, sare za wafungwa na sare za maafisa, dawa na matibabu kwa wafungwakunahitaji kuwa na uhusiano mzuri na watoa huduma (wazabuni). Kuanzia mwaka 2009/2010 hadi 2012/2013 idara ya magereza imeshindwa kulipa deni la

jumla ya Sh.46,559,702,987 lililotokana na gharama za matengenezo, sare, huduma ya maji na umeme, bidhaa na huduma nyingine kutoka kwa wauzaji mbalimbali. Angalia mchanganuo wa deni hili kwenye jedwali hapa chini:

**Jedwali 63: Ongezeko la madeni kutoka kwa wauzaji na madai ya wafanyakazi**

Maelezo	Kiasi (Sh.)	%
Ugavi wa bidhaa na huduma	25,997,391,544	56%
Madai ya wafanyakazi	16,010,580,484	34%
Huduma ya maji na umeme	4,540,930,958	10%
<b>Jumla</b>	<b>46,559,702,987</b>	

*Chanzo: Taarifa za fedha za idara ya magereza*

Asilimia 56 ya deni lote linatokana na wauzaji /wasambazaji wa huduma na bidhaa kwa magereza. Hii inaonyesha kwamba magereza ina hali mbaya ya kifedha na haikopesheki.

**10.3.4 Miundombinu hafifu na msongamano katika magereza**

Majengo ya magereza yaliyo mengi yamejengwa kwa zaidi ya miaka 50 iliyopita, miundombinu ya magereza (kama mifumo ya maji taka) ilikuwa ni kwa ajili ya idadi ndogo ya wafungwa. Magereza kwa sasa yana wafungwa zaidi ya 45,000 wakati miundombinu iliyopo ni kwa ajili ya wafungwa 22,669 tu.

Hii ina maana kwamba kuna umuhimu wa kuwa na magereza ambayo yatakuwa na uwezo wa kubeba wafungwa wengi zaidi ili kuepukana na msongamano. Na nilibaini kwamba msongamano unasababishwa na kesi zinazosubiri uamuzi wa mahakama.

**10.3.5 Mapendekezo juu ya hali iliyopo katika magereza**

Kutokana na changamoto inayoikabili idara ya huduma ya magereza ya Tanzania ninapendekeza yafuatayo kwa Serikali na kwa idara ya huduma ya Magereza yenyewe.

### **Idadi ya mahabusu kuwa juu katika magereza**

- Mahakama ya Tanzania iharakishe kutoa maamuzi juu ya kesi zilizopo. Kuna idadi kubwa ya mahabusu katika magereza ambao wanasubiri kesi zao kusikilizwa na haki kutolewa na mahakama. Kwa kukamilisha kesi zinazowakabili mahabusu kutasaidia kupunguza idadi ya mahabusu katika magereza.
- Serikali inaweza kuchagua kutumia njia nyingine ya kuwaadhibu wafungwa baada ya kupatikana na hatia. Serikali inaweza kuchagua kutumia njia mbadala kama wafungwa kutumikia kifungo cha nje cha kuanzia mwaka mmoja mpaka miwili chini ya uangalizi wa mkuu wa wilaya au mkoa huku akijushughulisha na shughuli za jamii kama usafi maofisini bila malipo (extra Mural labour), kifungo cha nje chini ya uangalizi cha miaka minne na kuendelea kutokana na makosa madogo madogo kwa wafungwa ambao tayari wametumikia theluthi moja(1/3) ya kifungo chao gerezani huku wakishughulika na huduma za jamii bila malipo(Parole). Hii kwa kiasi kikubwa itapunguza idadi ya mahabusu na wafungwa katika magereza.
- Kwa ajili ya wahalifu wadogo na wanaokiuka sheria ni bora kulipa faini na kama wao wakishindwa kulipa faini, wanapaswa kupelekwa kwa uongozi wa miji yao, au wilaya na kupewa kazi za jamii (communal based labour).

### **Masuala yatokanayo na ufinyu wa bajeti**

- Kuwahudumia mahabusu na wafungwa kunasababisha gharama kubwa kwa Serikali. Kuwalisha, kuwapa mavazi na matibabu ni ghali. Uongozi wa idara ya huduma ya magereza unashauriwa kuboresha shughuli zao za uzalishaji kama useremala, shughuli za kilimo, ushonaji, ujenzi wa nyumba na mafundi mitambo na magari. Baada ya hapo watafute soko la bidhaa zao na hii itawawezesha kuwa na uwezo wa kujilisha na kujinunulia mavazi wenyewe.

- Idara ya huduma ya Magereza inahamasishwa kuandika juu ya mapendekezo kadhaa ya maendeleo na kutafuta wahisani mbalimbali kama Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Shirika la Misaada la Marekani (USAID), nk ambayo watatoa fedha kwa ajiri ya kupanua na kuboresha magereza.
- Uongozi wa idara ya huduma ya magereza unashauriwa kutoa wito kwa wajumbe wa kamati ya bunge ya Serikali kuu (PAC) na viongozi wengine wa Serikali kutembelea magereza na kuona hali halisi katika magereza. Hii itawasaidia kufanya maamuzi sahihi juu ya mgao wa rasilimali.

#### **10.4 Jukumu la Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali katika kukagua miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP)**

Mipangoya ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP) ni mbinu mpya zinazotumiwa na sekta ya umma kwa kushirikiana na makampuni katika sekta binafsi ili kuleta mitaji na uwezo wao wa kutoa miradi ya umma kwa wakati, wakati sekta ya umma inabaki na wajibu wa kutoa huduma hizo kwa umma katika njia ambayo itanufaisha umma.

Baada ya kutambua haja ya kuwa na mbia na kujenga mahusiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, Serikali ilikuja na sera ya taifa ya ubia kati ya sekta ya umma na binafsi mwezi Novemba, 2009 na ilitunga sheria ya ubia kati ya sekta ya umma na binafsi Namba 18 ya mwaka 2010. Hata hivyo, kwa kiasi kikubwa jukumu la Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali kwa upande wa ukaguzi wa miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP) umekuwa mdogo; na kwamba unaleta hatari kubwa katika rasilimali za umma ambayo ingeweza kupungua kama Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali angehusishwa katika ukaguzi.

#### **10.4.1 Hatari iliyopo katika mipangilio ya ubia kati ya sekta ya umma na binafsi**

Sheria yaubia kati ya sekta ya umma na binafsini miongoni mwa sheria muhimu ambayo ilianzishwa Tanzania katika kuleta mageuzi mbalimbali yenye lengo la kuleta mabadiliko ya kiuchumi kutoka uchumi unaoendeshwa na kumilikiwa na umma kuelekea katika uchumi unaoendeshwa na karatibiwa na masoko pamoja na mashirika binafsi. Ubia kati ya sekta ya umma na binafsi kwa kiasi kikubwa unasaidia Serikali kuondokana na vikwazo vya bajeti, ambapo sekta ya umma na binafsi wanaweza kufanya kazi kwa pamoja ili kupata thamani bora ya fedha kwa ajili ya walipa kodi katika kutoa huduma za umma kupitia faida inayoongezeka kwa sekta binafsi na utoaji wa huduma bora kwa sekta ya umma.

Miradi muhimu ya maendeleo kama vile ujenzi wa benki ya damu katika Kanda ya Ziwa katika Hospitali ya Bugando kwa upande wa sekta ya afya, Songas kwa upande wa viwanda vya nishati, na maduka ya Mlimani City kwa upande wa sekta ya kijamii na kiuchumi ni baadhi ya mifano michache ambayo imetokana na ubia kati ya sekta ya umma na binafsi. Ushirikiano umeimarisha uwezo mdogo wa sekta ya umma kukidhi mahitaji ya maendeleo ya miundombinu, kupatikana kwa thamani ya fedha kwa njia sahihi ya kudhibiti hatari kwa kushirikiana na sekta binafsi kwa muda wote wa maisha ya mradi kuanzia ubunifu/ujenzi mpaka matengenezo nk.

Pamoja na faida ambayo inaweza kupatikana kutokana na mipango ya ubia kati ya sekta ya umma na binafsi, kuna baadhi ya hatari zinazohusiana na ubia ambayo ni muhimu zaidi kwa Serikali kuingilia kati. Ubia unaweza kuongeza gharama za uendeshaji, kutoa huduma chini ya kiwango, madhara katika maslahi ya umma, na kuanzisha fursa mpya kwa udanganyifu, kula njama, na rushwa.

Ili kukabiliana na hatari hizi, viwango vya kimataifa vya Taasisi Kuu za Ukaguzi ISSAI 5220 na ISSAI 5240 hutoa mwongozo wa jinsi ya Taasisi Kuu za Ukaguzi wanapaswa

kushiriki katika mapitio ya mchakato unaohusiana na ubia kati ya sekta ya umma na binafsi. Ninapendekeza kwa Serikali kuhakikisha hatua zinachukuliwa ili kupunguza kiwango cha hatari ambacho Serikali inaweza kupata kupitia makubaliano hayo. Miongoni mwa hatari ambazo ubia unaweza kusababisha ni pamoja na;

- Michakato hafifu katika utoaji wa maamuzi inaweza kusababisha kuchaguliwa kwa mbia asiye sahihi, au ushirikiano usiofaa kutumika kwa ajili ya mradi huo. Katika baadhi ya matukio washirika binafsi wanachaguliwa bila kufanya mchakato wa ushindani wa zabuni hivyo kupunguza faida ya Serikali ambayo ingepata kutokana na bei bora ya kiuchumi.

Serikali inapaswa kubuni kupitia mchakato wa manunuzi na tathmini ambao utapima utegemezi na uadilifu wa washirika wenye uwezo. Tathmini hiyo inapaswa kuzingatia uchaguzi wa mshirika mwenye rekodi zilizothibitishwa katika maendeleo ya mradi kwa njia ya mchakato wa ushindani wa zabuni.

- Ukosefu wa hali ya fedha katika kufanya utafiti wa upembuzi yakinifu unaweza kuwa gharama kubwa kwa pande zote mbili. Miradi muhimu ya maendeleo husimamiwa kwa njia imara ya utafiti wa upembuzi yakinifu ambapo gharama zinazohitajika hupatikana na kuchambuliwa. Hata hivyo, ukosefu wa mfuko wa uwezesaji na ufahamu unazuia njia ya kweli kuamua kufanya uchambuzi wa faida na gharama inayohusu mradi fulani.

Kwa kutambua umuhimu wa upembuzi yakinifu ili maslahi kwa pande zote mbili yaweze kutumika na mafanikio kupatikana, Serikali inapaswa kuunda mfuko wa fedha za uwezesaji wa ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP) ili kuwezesha upembuzi yakinifu juu ya miradi muhimu ya utekelezaji. Pamoja na hayo, Serikali inahimizwa kuzindua juhudi kamili za uhamasishaji ili kushirikisha kikamilifu sekta binafsi katika miradi ya taifa yenye vipaumbele

vinavyotambulika. Kuendelea kukosekana kwa fedha katika kufanya utafiti wa upembuzi yakinifu kunaweza kusababisha jambo lenye gharama kubwa sana.

- Kuna wakati ambapo mbia binafsi huamua kiasi cha faida kitakachogawiwa kutokana na matumizi ya mali yasiyotarajiwa au gharama ambazo si halali kulingana na mkataba.

Serikali inapaswa kuhakikisha kuwa masuala ya kugawana faida (ikiwa ni pamoja na uwezekano wa faida kwa siku zijazo kutokana na mauzo ya mali au uwekezeshaji) yanawekwa wazi katika makubaliano ya ushirikiano. Ni lazima pia kuhakikisha kwamba maslahi ya nchi yanalindwa wakati mali zilizochangiwa zinaondolewa katika ushirikiano (kwa mfano kuhakikisha Serikali inapata sehemu ya mapato). Serikali pia inapaswa kuwa na uwezo wa kuthibitisha jumla ya gharama zilizolingizwa katika mradi ambayo zinatarajiwa kurudi wakati wa uhai wa mradi huo.

- Chini ya utaratibu wa sasa, kuna uwezekano wa Serikali kupoteza udhibiti wa mali yake. Serikali au chombo cha umma kinaweza kukubaliana kuhamisha baadhi ya mali zake kwa umiliki wa mbia binafsi, kama ilivyo kwa Shirika la utangazaji Tanzania (TBC) na StarMedia Tanzania. Ni vyema kutambua kwamba mara mali inapokuwa imehamishwa kwenda kwa sekta binafsi, sekta ya umma ina uwezekano wa kupoteza umiliki juu ya hizo mali.

Nina ishauri Serikali kwamba inapaswa kufikiria kama mali zenye umuhimu wa kitaifa zinaweza kukodishwa kwa sekta binafsi badala ya kuhamishwa kabisa. Makubaliano ya ushirikiano wana namna hii yanaweza kutoa fursa kwa sekta ya umma kuingilia kati katika tukio kubwa la kushindwa katika utoaji wa huduma au kufilisika kwa mbia.

- Maendeleo ya mradi, zabuni na gharama za miradi wa ubia kati ya sekta ya umma na binafsi unaoendelea una

uwezekano wa kuwa mkubwa zaidi ya ilivyokuwa katika taratibu za jadi za manunuzi Serikalini. Katika ubia kati ya sekta ya umma na binafsi kunagharama zinazoambatana na madeni kutokana na ukweli kwamba sekta binafsi inaweza kupata fedha na kuzitumia kwa ufanisi ili kuongeza uwekezaji wao. Dhamana aliyopewa mbia wa sekta binafsi inaweza isiwe ya bei kamilifu kwenye makubaliano ambayo inaweza kusababisha hali ya kupoteza thamani ya uwekezaji katika nchi.

Serikali inatakiwa kujihakikishia kama gharama zote na ya kushiriki ni halali. Uchambuzi makinini lazima ulenge kushughulikia mgao sahihi wa athari zinazoweza kutokea katika mradi huo kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kuhusiana na mradi huo. Katika mipangilioyote ya ubia (PPP), chombo cha umma kinapaswa kuangalia athari zinazoweza kutokea na kuhakikisha kwamba zinaweza kudhibitiwa ipasavyo.

- Kutokana na miradi hii kuwa ni ya muda mrefu na ugumu unaohusiana nayo, ni vigumu kutambua dharura zozote zinazoweza kutokea wakati wa kuendelea mradi na matukio au masuala huweza kutokea bila kutarajiwa na pande zote wakati wa kuingia mkataba. Ni dhahiri kwamba pande zote zitahitaji kujadili upya mkataba ili kuzingatia hizo dharura.

Serikali inapaswa kuwa makini katika ubunifu wa mkataba na majadiliano ili kuhakikisha kwamba athari yoyote kutokana na matukio yasiyoonekana inagawanywa kati ya pande zote mbili na kwa mujibu wa viwango vya athari hiyo kulingana na makubaliano.

- Mbia wa sekta ya umma anaweza kuzuiwa kupata taarifa za kutosha kuhusu utendaji wa mbia mwenzie kwa sababu ya makubaliano au sheria ya ujumla ambayo hairuhusu habari kutolewa kwa mbia mmoja kulingana na mahitaji ambayo hayakutolewa kwa wadau wote.

Serikali inapaswa kuhakikisha kuwa makubalianoyanaruhusu habari ya utendaji kuwa zinatolewa, kulingana na mahitaji, kwa mbia wa sekta ya umma. Wakati Serikali inakuwa kama taasisi ya kutoa mkopo au mdhamini ni lazima kuomba taarifa za ziada kutoka kwenye upande inayoshirikiana nayo ili kuhakikisha usalama wa mkopo wake.

- Kuna nyakati ushirikiano/ubia unaweza kufirisika au Serikali inataka kujitoa katika makubaliano. Kama Serikali haikutambua uwezekano wa mazingira hayo kabla ya kuingia katika mkataba, kuna hatari ya Serikali kushindwa kujitoa isipokua kwa kulipa fidia kama adhabu.

Katika uchambuzi wa vihatarishi kabla ya kuingia katika ushirikiano, Serikali inapaswa kufikiria kwa makini na kuweka vifungu kwenye masharti ya mkataba (mfano kifungu kinachohusu uwezo wa kujitoa inapotokea utendaji mbovu bila upotevu wa fedha kama fidia) au kifungu kinachoruhusu kuwepo kwa mipango ya dharura (mfano kuuza hisa).

- Inapotokea Serikali/ chombo cha umma kinapofanya malipo ya awali makubwa kulingana na mkataba, ambayo yanaweza kumwezesha mbia binafsi kifedha. Kama asilimia kubwa ya bei ya mkataba italipwa awali, mbia binafsi atakosa motisha ya kutoa huduma kwa haraka au ya kiwango bora. Serikali pia inaweza kupoteza rasilimali zake chache endapo kutatokea mabadiliko.

Serikali inapaswa kuhusianisha malipo ya mikataba na mafanikio ambayo yalikubalika kufikiwa na kiwango chahuduma zinazotolewa.

- Sheria ya ubia kati ya sekta ya umma na binafsi haimwezeshi Mdhimiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali kupata rekodi na taarifa za ubia kati ya sekta

ya umma na binafsi. Sheria haisemi kama mbia binafsi anapaswa kuweka rekodi sahihi ya vitabu vya hesabu na za mradi na kama vitabu vitakua wazi kwa ajili ya uchunguzi na mamlaka iliyompa mkataba au Serikali. Sheria haimhitaji mbia binafsi kuwasilisha taarifa za hesabu zilizokaguliwa na taarifa nyingine yeyote ambayo kwa kiasi fulani inaweza kuhitajika na mamlaka iliyompa mkataba.

Sheria inapaswa kuhakikisha kuwa mkataba wa ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP) na makubalianao ya kushirikiana katika uzalishaji (PSAs) yanamwezesha Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kupata rekodi za fedha na taarifa nyingine za mbia binafsi au kampuni iliyo katika mpango wa ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP).

Pamoja na hayo, Serikali inapaswa kusaidia na kumpatia Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu taarifa zote muhimu za mkataba wa ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP) katika maisha yote ya mradi tokea mchakato wa zabuni, kupewa rasmi mkataba na awamu ya uendeshaji wa mradi. Mwongozo Na. 3 wa Viwango vya Shirika la Kimataifa la Asasi Kuu za Ukaguzi (ISSAIs) 5220 inasema kwamba, kuchunguza mradi na Taasisi kuu ya Ukaguzi (SAI) katika hatua zote za mradi inafaida zake endapo udhaifu wowote ukigundulika unaweza kurekebishwa kabla ya mkataba haujasainiwa na matatizomabayazaidikuepukwakatika hatua ya baadaye.

Serikali pia inapaswakutoa taarifamara kwa marajuu yautendaji wa mradi kuonyesha wazi wazikamambiabinafsianatekelezamajukumu yake kwa mbia wa sekta ya ummailihatari yoyote yahasara itambulike mapema iwezekanavyo, kuwezesha Serikali/mbia wa sekta ya ummakufikiranamna bora yakulinda maslahi yake.

## 10.5 Masuala yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi wa hesabu za Vyama vya Siasa

Kwa mara ya kwanza, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ameanza kufanya ukaguzi wa Vyama vya Siasa hapa nchini kwa mujibu wa kifungu cha 14(1) cha sheria ya Vyama vya Siasa Na. 5 ya mwaka 1992. Wakati tunaandaa taarifa ya fedha ya mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali kuu, zoezi hili lilikua bado linaendelea, hivyo taarifa hii fupi ni juu ya mambo ya jumla yaliyojitokeza hadi sasa.

Nitakapokamilisha zoezi zima la ukaguzi, nitakua katika nafasi ya kutoa ripoti ya kina zaidi juu ya ukaguzi wa Vyama vya Siasa nchini kwa lengo la kutoa ushauri kwa Msajili wa vyama vya siasa juu ya namna bora ya kusimamia vyama hivi na kuhakikisha kuwepo kwa uwajibikaji na uwazi katika usimamizi wa fedha za umma walizokabidhiwa.

Katika ukaguzi wa vyama tisa (9) vya siasa uliokwishafanyika hadi sasa tumeona yafuatayo:

- a) Taarifa za hesabu zilizowasilishwa zinatofautiana na misingi ya uhasibu na mfumo wa utoaji taarifa za fedha. Muundo na mwaka wa fedha wa vyama vya siasa upo tofauti na hauonyeshi taarifa muhimu zinazohusu misingi ya uandaaji wa taarifa za fedha, pia sera za uhasibu na maelezo ya taarifa za fedha hayakuwepo hivyo kuathiri mawada ya ukaguzi.
- b) Tumeshindwa kuelewa mfumo wa taarifa za fedha wa vyama vinne (4) vya siasa kwasababu taarifa ya fedha zilizowasilishwa zinaonesha kiasi kilichopokelewa na kilichotumika na taarifa hiyo haikuwa na taarifa za jumla za chama na maelezo ya taarifa za fedha. Mfumo mzuri wa uhasibu ni kiungo muhimu kwa ajili ya kukuza uwajibikaji na uwazi.
- c) Vyama vya siasa kumi na moja (11) kati ya ishirini na moja (21) vyenye usajili wa kudumu havikuwasilisha taarifa za hesabu za mwaka kwa mujibu wa Kifungu cha 14(1)(i) cha sheria ya vyama vya siasa na 5 ya mwaka 1992.

- d) Vyama vya siasa saba (7) kati ya tisa (9) vilivyokaguliwa havitunzi vitabu vya hesabu sahihi vinavyoonyesha fedha na mali za chama kwa mujibu wa kifungu cha 14(1) cha sheria ya Vyama vya Siasa Na. 5 ya mwaka 1992. Badala yake vyama vya siasa vinarekodi kiasi kilichopokelewa na kilichotumika.
- e) Vyama vya siasa vinne (4) kati ya tisa vilivyokaguliwa havina akaunti ya banki kwa mujibu wa kifungu cha 15(1) cha sheria ya vyama vya siasa Na. 5 ya mwaka 1992.
- f) Tulibaini kuwa hakuna chama cha siasa hadi sasa kilichowasilisha kwa Msajili wa vyama vya siasa tamko la mali zote zinazomilikiwa na chama husika kwa mujibu wa kifungu cha 14(b)(ii) cha sheria ya vyama vya siasa Na. 5 ya mwaka 1992. Sheria haijataja tarehe kamili ya kuwasilisha tamko hilo.

#### **10.5.1 Mapendekezo**

Ili kuboresha utoaji wa taarifa, uwasilishwaji na ulinganifu wa utendaji wa vyama vya siasa, vyama vinatakiwa kuandaa taarifa za hesabu kwa mujibu wa viwango vya uhasibu vya kimataifa. Kuanza kutumika kwa mfumo mmoja wa taarifaza kijasibu utasababisha kufanana kwa taarifa za hesabu za vyama vya siasa. Hii inawezekana pale ambapo Msajili wa vyama vya siasa akishirikiana na Mhasibu Mkuu wakitoa mwongozo wa aina ya muundo wa taarifa za fedha utakaotumiwa na vyama vya siasa.

#### **10.5.2 Changamoto**

Kwa mujibu wa kifungu cha 14(1)(i) cha sheria ya Vyama vya Siasa Na. 5 ya mwaka 1992 inanihitaji nikague vyama vya siasa. Hata hivyo, wakati wa ukaguzi nimekutana na changamoto katika ukaguzi wa hesabu za fedha ambazo si za umma. Kwa mujibu wa katiba kwenye Ibara 143(2)(c) ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nataka kukagua fedha na rasilimali za umma. Katika hali hiyo kuna utata kama ibara hiyo inakidhi haja ya mimi kufanya ukaguzi wa fedha za vyama ambazo sio za umma.

Kifungu cha 14(1)(i) cha sheria ya vyama vya siasa Na. 5 ya mwaka 1992 inahitaji kila chama vya siasa chenye usajili wa kudumu kuwasilisha taarifa za hesabu zilizokaguliwa tarehe 30 Octoba bila kujali mwisho wa mwaka wa fedha wa chama hicho. Sheria imechukulia kuwa vyama vya siasa vina mwaka wa fedha unaofanana ambavyo si sahihi. Kwa upande mwingine Sheria ya ukaguzi wa umma ya mwaka 2008 inawataka maafisa Masuuli kuwasilisha taarifa ya hesabu kwaajili ya ukaguzi miezi mitatu baada ya kufunga mahesabu yaani 30 Septemba kila mwaka.

Napendekeza Serikali irekebishe sheria ya vyama vya siasa Na. 5 ya mwaka 1992 ili kutatua changamoto zilizopo.

## SURA YA KUMI NA MOJA

### 11.0 MAJUMUISHONAMAPENDEKEZO

Matokeo ya ukaguzi katika taarifa hii yaliwasilishwa kwa Maafisa Masuuli wote kwa ajili ya utekelezaji. Kwa mujibu wa Sheria na. 11 ya ukaguzi wa umma ya mwaka 2008, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuandaa taarifa ya utekelezaji wa mapendekezo na kuyawasilisha kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali-Wizara ya Fedha.

Katika taarifa hii nimebainisha dosari na mapungufu kadhaa katika mifumo ya udhibiti wa ndani ikiwemo mianya ya upotevu wa fedha na usimamizi dhaifu wa mifumo hiyo. Masuala haya yanatakiwa kushughulikiwa na Maafisa Masuuli kwa kuweka mifumo thabiti ya udhibiti wa ndani itakayolenga kuzuia kabisa kutokea tena kwa mapungufu haya. Ili kukabili mapungufu haya, nimetoa mapendekezo kadhaa ambayo kama yatatekelezwa, nataraji kuwa yataongeza udhibiti katika usimamizi wa fedha ndani ya Serikali.

Baada ya kuwasilisha katika taarifai hii masuala muhimu niliyoyaona wakati wa ukaguzi wa Wizara, Idara za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, na Balozi kwa mwaka huu wa fedha 2012/2013, napenda nitoe hitimisho na mapendekezo ya jumla ambayo kama yatatekelezwa yataongeza ufanisi katika usimamizi wa mali ya umma na kuongeza ufanisi wa namna bora ya uendeshaji wa Serikali kama ifuatavyo:

#### 11.1 Kutotekelezwa kwa baadhi ya mapendekezo yangu ya mwaka uliopita

Ninatambua jitihada zinazooneshwa na Serikali kupitia Maafisa Masuuli katikakutekelezamapendekezoyaliyotolewakatikakaguziza miakayanyuma(2010/11, 2011/12 na 2012/13).Hata hivyo, k u n a baadhiyamapendekezoniliyotoakatikataarifahizo ambayo hadi sasa hayajafanyiwa kazi.

Katika ukaguzi wa mwaka huu, Wizara, Idara za Serikali, Sekretarieti za Mkoa 77 zilikuwa na hoja za miaka ya nyuma za kiasi cha Sh.636,849,749,109 ambapo, Wizara ya Ujenzi ikiwa na sehemu kubwa ya Shs.253,777,000,000 ikifuatiwa na Wizara ya Fedha (Fungu 50) ikiwa na Shs.244,919,408,265. Hazina (Fungu 21) ni ya tatu kwa kuwa na Sh.72,668,447,899 za hoja ambazo hazijajibiwa. Kama nilivyoshauri hapo awali, Utekelezaji hafifu wa mapendekezo ya Mkaguzi na kutoyafanyia kazi unaweza ukapelekea kujirudia kwa hoja za ukaguzi katika miaka ijayo.

### **Mapendekezo**

Serikali inapaswa kuweka juhudi za makusudi ili kuhakikisha kuwa mapendekezo ya mkaguzi yanafanyiwa kazi ipasavyo. Mlipaji Mkuu wa Serikali anatakiwa kutoa maagizo kwa Maafisa Masuuli kuchukua hatua muhimu ili kuboresha utunzaji wa nyaraka, ambayo ni moja ya sababu kuu zinazochangia kukosekana kwa nyaraka na kwa hiyo kushindwa kujibu baadhi ya hoja za ukaguzi.

Pia, Maafisa Masuuli wanatakiwa kutengeneza mpango kazi wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi. Mpango kazi huo wa utekelezaji uwe maalum kwa ajili ya masuala ambayo hayawezi kufanyika ndani ya kipindi cha muda mfupi.

Msisitizo wa kuwa na daftari kutunza taarifa za hoja za ukaguzi kwa kila Afisa Masuuli ni utaratibu mwingine muhimu litasaidia pia kufuatilia masuala ya ukaguzi yasiyojibiwa ikiwa ni pamoja na maendeleo yaliyopatikana hadi sasa katika kutekeleza mapendekezo hayo.

## **11.2 Usimamizi wa Manunuzi**

Utekelezaji wa Sheria ya manunuzi na Kanuni zake ni wa umuhimu mkubwa katika kupata thamani ya fedha katika manunuzi ya Serikali. Ofisi yangu pamoja na PPRa, tumekuwa tukitoa ushauri kwa Serikali kupitia Maafisa Masuuli juu ya njia bora ya kuendesha shughuli za manunuzi. PPRa wamekuwa wakitoa waraka (circulars)

mbalimbali kwa Wizara na Sekretarieti za Mikoa juu ya namna ya kuboresha utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi na Kanuni zake. Katika mwaka huu wa ukaguzi kuna kujirudia kwa baadhi ya hoja ambazo mapendekezo yake yalitolewa katika taarifa za ukaguzi za miaka iliyopita. Mapungufu hayo ni pamoja na manunuzi yaliyofanyika bila ya kuwako katika mpango wa manunuzi, Manunuzi bila kuzingatia ushindani wa bei, Mali zilionunuliwa lakini hazitumiki, manunuzi ya kawaida na malipo ya mikataba zaidi ya kiwango, manunuzi bila idhini ya Bodi ya Zabuni na manunuzi kwa kutumia Masurufu.

Kwa kutilia maanani kuwa Manunuzi yanachukua sehemu kubwa ya matumizi ya Serikali, hivyo basi, usimamizi duni katika shughuli za manunuzi kunaongeza hasara kubwa ya rasilimali za taifa.

### **Mapendekezo**

Kama nilivyosema awali, manunuzi yanachukua sehemu kubwa ya rasilimali za Serikali ili kutekeleza shughuli zake kama zilivyopangwa. Hivyo, Serikali inatakiwa kuboresha mfumo wa manunuzi kuwa wenye kuzingatia sheria ya manunuzi na kanuni zake ili kuepuka kujirudia kwa hoja. Yafuatayo yanahitaji kuzingatiwa ili kuboresha mfumo huo:

- Serikali kupitia PPRA inatakiwa kuendesha semina kadhaa kwa lengo la kujenga uwezo wa wasimamizi wa vitengo vya manunuzi (PMU), Bodi za Zabuni, Maafisa Masuuli na wakuu wa idara kuhusu umuhimu wa kutekeleza Sheria ya Manunuzi ya Umma na kanuni zake.
- Pia ni muhimu kuwa na Mfumo wa Kompyuta wa Usimamizi wa Manunuzi (PIMS) katika uendeshaji wenye ufanisi. Mfumo huu unamilikiwa na Mamlaka ya udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA). PPRA inatakiwa kuhakikisha kwamba mfumo huu ni mfumo rafiki kwa watumiaji wa Wizara/Idara za Serikali na Sekretarieti za Mikoa na unaweza kutumika kwa urahisi ili kuboresha shughuli za manunuzi ya umma.

### **11.3 Kutofanyiwa kazi kwa changamoto ya upungufu wa nguvukazi katika Wizara na Sekretarieti za Mikoa**

Rasilimaliwatu ni kigezo kikubwa katika kuongeza tija na ufanisi wa utendaji wa taasisiyeyote, hii ni pamoja na ufanisi wa utoaji wa huduma kwa jamii husika. Wakati wa ukaguzi wa 2012/2013 nilibaini uhaba mkubwa wa wafanyakazi ikilinganishwa na ikama. Katika sampuli ya Wizara na Sekretariati za Mikoa 28 zilizokaguliwa, nilibaini uhaba wa watumishi 12,646, sawa na asilimia 57 ya ikama inayopendekeza watumishi 22,159. Ninatatizwa na uhaba huu mkubwa wa watumishi ambao unaweza kuashiria ama ikama haiko sahihi au kuna upungufu mkubwa ambao unaweza kuathiri utoaji wa huduma kwa taasisi hizi za Serikali.

#### **Mapendekezo**

Kama nilivyoeleza hapo juu, upungufu wa watumishi 12,646 katika sampuli ya taasisi 28 zilizofanyiwa majaribio ni mkubwa mno ikilinganishwa na ikama ya watumishi 22,159 ambayo kwa kiasi kikubwa inaweza kuathiri utendaji kazi wa Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa husika. Nashauri Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma (PO- PSM) ipitie upya ikama za Wizara, Idara za Serikali na Tawala za Mikoa na kuja na mapendekezo halisi ya idadi ya watumishi wanaohitajika. Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara za Serikali na Tawala za Mikoa wanapaswa kuhakikisha kwamba wana idadi yakutosha ya watumishi na wenye sifa stahiki. Nashauri pia wawe na mpango unaotekelezeka kwa ajili ya motisha kwa watumishi na sera ya kuwafanya wadumu kazini. Uhaba wa watumishi unapojitokeza unapaswa kutolewa taarifa kwa mamlaka husika ikiwa ni pamoja na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma (PO- PSM).

### **11.4 Malipo ya mishahara kwa watumishi hewa**

Ninatambua juhudi za Serikali kupitia Ofisi ya Raisi-Menejimenti na Utumishi wa Umma ikishirikiana na Wizara ya Fedha kutatua changamoto ya malipo ya mishahara hewa. Juhudi hizo ni pamoja na kazi kubwa iliyofanyika ya uhakiki wa watumishi waliopo kazini na zile za kuwekeza

katika mfumo wa kusimamia rasilimali watu kwa kutumia kompyuta (LAWSON).

Mbali na juhudi hizo za Serikali, bado kuna changamoto ya kuendelea kuwepo kwa mishahara hewa ambapo kiasi cha Sh.779,329,181 kililipwa kwa watu wasio watumishi wa Serikali kwa mwaka huu wa fedha kutoka katika wizara, Idara na Sekretarieti za mikoa 11 zilizofanyiwa ukaguzi. Matokeo haya yanaonesha ya kwamba bado ipo changamoto ya kulipa mishahara kwa watumishi hewa, hivyo ni wito wangu kwa Serikali kuongeza juhudi ya kumaliza tatizo hili.

### **Mapendekezo**

Ili kuepuka upotevu kama huu katika siku zijazo, Maafisa Masuuli katika Wizara, Idara na Mikoa husika wanapaswa kuangalia taarifa za mishahara ya watumishi wao mara kwa mara na kuthibitisha uhalali wa watumishi wote kabla ya malipo. Mawasiliano pia lazima kuimarishwa ili kuhakikisha kwamba majina ya wastaafu, watoro/walioacha kazi au walioachishwa kazi yanafutwa katika taarifa za wafanyakazi mara moja. Mbali na hayo, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuhakikisha mishahara isiyolipwa kwa watumishi ambao muda wao wa utumishi umekoma kwa sababu moja au nyingine iwe inarudishwa Hazina kwa wakati. Zaidi ya hayo, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuhakikisha kuwa Mfumo wa kutunza taarifa za watumishi (HCMIS-LAWSON) unafanya kazi na unatumika kikamilifu ili kupata thamani ya fedha tarajiwa.

### **11.5 Usimamizi wa Matumizi**

Moja ya jukumu la msingi la menejimenti ni kuanzisha mfumo thabiti wa udhibiti wa ndani, kutokana na umuhimu wake nimekuwa nikisisitiza jukumu hili katika taarifa yangu kila mwaka. Baadhi ya wakaguliwa wameweza kutekeleza mapendekezo yangu na wameboresha utendaji wao wa kazi kwa kiasi kikubwalakini pia wapo ambao bado hawajayafanyia kazi mapendekezo hayo. Kwa sababu ya kuendelea kuwepo kwa mfumo ya udhibiti wa ndani dhaifu katika taasisi nilizozikagua, nimebaini madhaifu mbalimbali katika

usimamizi wa matumizi ya fedha za umma. Mapungufu hayo ni pamoja na hati za malipo zisizo na viambatanisho vya kutosha Sh.14,498,110,431 kutoka katika Wizara/Sekretarieti za Mikoa 29; Matumizi yaliyofanywa nje ya Bajeti kiasi cha Sh.15,785,285,943 yakihusisha Wizara/Sekretarieti za Mikoa 29, Malipo ambayo hati zake za malipo hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi Sh.70,195,394 yakihusisha Wizara/Sekretarieti za Mikoa 3. Mengine niliyobaini, pamoja na Wizara/Sekretarieti za Mikoa zilizohusika kwenye mabano ni kama ifuatavyo-Masurufu yaliyokaa muda mrefu bila kurejeshwa Sh.319,423,337 (9); Malipo yaliyolipwa kutoka katika vifungu visivyokasimiwa Sh.2,394,834,855 (25); Malipo yaliyozidi viwango stahiki-Shs.68,089,906 (5); Malipo yasiyo na stakabadhi za kawaida na kielektroniki (EFR)-Shs. 47,935,509,285 (13); malipo yasiyokuwa na mchanganuo wa matumizi-Sh.3,288,257,291 (6); Malipo yasiyo na tija/manufaa-Sh.687,169,796 (10); Fedha kutumika kwa shughuli zisizotarajiwa Sh.1,770,390,504 (17); Malipo ya madeni ya mwaka uliopita kwa kutumia fedha za mwaka 2012/2013 Shs.371,879,693 (9).

Kama nilivyoonesha hapo juu, mapungufu mengi yangeweza kuepukwa endapo mapendekezo yangu yangelitekelezwa. Madhaifu haya yamekua yakijitokeza mwaka hadi mwaka na nimekua nikitoa mapendekezo ya namna ya kuyatatua.

### **Mapendekezo**

Hili ni moja ya eneo ambalo lina changamoto nyingi. Zaidi sana, changamoto hizi husababishwa na kutokuwepo kwa mfumo thabiti wa udhibiti wa ndani, na kama katika taasisi husika upo, umekuwa aidha hausimamiwi kwa usahihi au maafisa wenye dhamana kukiuka taratibu kwa maksudi. Maafisa Masuuli wa Wizara/Idara, Mikoa na Balozi wanapaswa kuhakiki malipo yote na kuyathibitisha kuwa halali na yana nyaraka sahihi kama matakwa ya Kanuni za Fedha za Umma ya 2001, Kanuni ya 95 (4) inavyosema. Uangalizi wa ndani unahitaji kuboreshwa ikiwa ni pamoja na ukaguzi wa awali. (Pre-Audit)

## 11.6 Utendaji katika Balozi zetu.

